*TANZANIA OSAKA ALUMNI*

# Kitabu cha

# Mbinu Bora 3

**Ofisi ya Rais**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**P.O. Box 1923,**
**Dodoma.**

***Machi*, 2017**

# KITABU CHA MBINU BORA 3 (2017)

**Kimeandaliwa na Tanzania Osaka Alumni (TOA):**
**Paulo Faty,**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe;**
**Judicate Mwanga,**
**Mhadhiri, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo;**
**na**
**Michiyuki Shimoda,**
**Mshauri Mwandamizi, OR-TAMISEMI**

**na kuhaririwa na**
**Paulo Faty,**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe;**
**na**
**Honorina Ng’omba,**
**Mshauri wa Serikali za Mitaa – JICA-TANZANIA**

# Yaliyomo


| Yaliyomo | Ukurasa |
|---|---|
| Dibaji | 4 |
| Utangulizi (TOA) | 5 |
| Utangulizi (JICA) | 6 |
| Vifupisho | 7 |
| Sura ya Kwanza:Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani | 9 |
| Sura ya Pili; Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato | 27 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi : Ukusanyaji Bora wa Ushuru Kutoka Mazao ya Misitu | 29 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero : uboreshaji wa Ukusanyaji wa Mapato ya Vyanzo vya Ndani | 40 |
| Halmashauri ya Mji wa Korogwe:Ubunifu Katika mapato ya Ndani ili Kuboresha Utoaji Huduma | 49 |
| Sura ya Tatu: Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma | 59 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Handeni : Mpando wa Niache Nisome – Uondoaji wa Utoro wa Mtoto wa kike Katika Shule za Sekondari | 61 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto:Utumiaji wa Teknolojia Itumiayo Nguvukazi | 69 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi:Ujenzi wa Barabara ya Isipii – Mpanga TAZARA kwa Teknolojia Itumiayo Nguvukazi | 79 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Moshi: Jitihada za Jamii katika Kuboresha Barabara | 86 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Siha: Juhudi za Wananchi Kutunza Usafi wa mazingira | 95 |
| Mkoa wa Kilimanjaro: Matumizi Endelevu ya Ardhi | 105 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro: Uhamasishaji wa Utalii wa Utamaduni na Ushirikishwaji katika Uhifadhi wa misitu | 115 |
| Sura ya Nne: Maendeleo ya Kiuchumi ya Jamii | 127 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Iringa: Uhakika wa Chakula katika Kaya za Tarafa ya Pawaga | 137 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe: Kilimo cha Umwagiliaji na Uhakika wa Kuzalisha Mpunga | 145 |
| Mkoa wa Tanga: Juhudi za Wakulima Wadogo Kuzalisha Maziwa | 150 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Meru: Ushirikiswaji bora wa Wadau katika Mnyororo wa thamani | 164 |
| Marejeo | 180 |

# Dibaji

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yamelenga katika utoaji bora wa huduma wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa za Serikali Kuu. Maboresho yamekaribisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, washirika wa maendeleo na wadau wengine tangu awamu ya kwanza hadi sasa. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) iliwekwa dhahiri mwaka 1998 na utekelezaji wake wa maboresho ya Serikali za Mitaa ulianza mwaka 2000. Kupitia ushirikiano huu maboresho ya Serikali za Mitaa hapa Tanzania yamefanikiwa kuleta Serikali za Mitaa za kidemokrasia, matumizi bora ya raslimali watu, kuongozeka kwa ruzuku toka hazina, kuimarika kwa utawala bora katika Serikali za Mitaa, kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi na kwa ujumla kuongezeka kwa uhuru wa Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma.

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yametekelezwa kwa mkakati wa jumla ambao umejumuisha kujifunza jitihada za maboresho na utekelezaji wake katika nchi nyingine, Afrika na kwingineko na kuunda mkakati sahihi wa utekelezaji wake na mbinu mbadala kwa Tanzania. Tangu mwaka 2002 Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI – Wakati huo) na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) kwa pamoja wameendesha mafunzo kuhusu Ugatuaji nchini Japani kupitia mafunzo ya Osaka. Mafunzo haya yamehudhuriwa na Wakurugenzi na Watumishi wengine toka OR – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na wadau wengine wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Mafunzo haya pia yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na wakuu wa idara kupita mafunzo ya mikoa baada ya mafunzo ya Osaka (Reginal Post Osaka Training).

Mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa yametoa fursa kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kujifunza uzoefu wa ugatuaji madaraka wa Kijapani, kuchagua mbinu bora za ugatuaji wa Kijapani na kutekeleza mbinu hizo katika Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hili limeibua umuhimu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mbinu hizi bora kupitia kitabu, ili kuzifanya Sekretarieti za Mikoa na MSMkuona na kujifunza utekelezaji na siri zake humuhumu nchini.

Kitabu hiki cha tatu ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kati ya OR – TAMISEMI na JICA kuimarisha sera ya ugatuahi wa madaraka Tanzania. Kitabu hiki kinaanza kwa kuonyesha historia ya mafunzo ya Osaka na mbinu bora kama ifuatavyo; Sura ya Kwanza inaonyesha kwa ufupi Masuala mazuri yaliyoigwa toka Japani; Sura ya pili inahusu Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na uboreshaji wa mapato ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Mufindi na Kilombero na Halmashauri ya Mji wa Korogwe; Sura ya tatu inahusu Ushirikishwaji wa jamii katika Utoaji Huduma ambayo inawasilisha Mbinu bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Handeni, Lushoto, Mufindi, Moshi, Siha na Ngorongoro na Mkoa wa Kilimanjaro. Sura ya Mwisho inayohusu Maendeleo ya jamii Kiuchumi ikiwaisilisha Mbinu Bora toka Halmashauri za Wilaya za Iringa, Korogwe na Meru na Mkoa wa Tanga.

OR – TAMISEMI inashauri watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na wa MSM na wadau wote wa maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania kusoma kitabu hiki, kufahamu jitihada za ndani, kujifunza siri za mafanikio na kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kuonyesha utendaji mzuri katika mazingira ya ugatuaji wa madaraka.

**Mhandisi Mussa Iyombe**
**KATIBU MKUU**
**OR-TAMISEMI**

# Utangulizi (TOA)

Kitabu cha mbinu bora cha tatu ni matokeo ya jitihada za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OR – TAMISEMI na Serikali ya Japani kupitia JICA tangu mwaka 2002 kwa kuendesha mafunzo huko Osaka na mafunzo baada ya Osaka katika kila mkoa juu ya uzoefu wa Ugatuaji Madaraka huko Japani. Mafunzo haya yalitoa fursa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, MSM na wadau mbalimbali wa maboresho hapa Tanzania kujifunza uzoefu wa Kijapani kuhusu Ugatuaji katika maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Raslimali Watu, Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato, Upangaji na Utoaji Huduma Shirikishi na Maendeleo ya Kiuchumi katika MSM hasa kupitia wimbi la OVOP. Masuala mazuri yaliyoigwa yametekelezwa katika Sekretariati za Mikoa na MSM nyingi kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa jamii ndani ya sera ya ugatuaji, yaani "D by D". Mbinu Bora nyingi za utekelezaji zimeonyesha mafanikio na matokeo chanya kwa jamii. Kamati ya Utendaji ya TOA imeamua kutoa Mbinu Bora ambazo zimewasilishwa kwenye toleo hili la tatu. TOA itaendelea kutoa matoleo mengine ya kitabu hiki siku za mbele sambamba na utekelezaji unaondelea wa Masuala mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa.

Kukamilika kwa kitabu hiki cha tatu cha Mbinu Bora kumetokana na misaada kutoka taasisi na watu binafsi mbalimbali. TOA inapenda kutambua na kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufikia makubaliano na Serikali ya Japani, kufadhili na kuruhusu watumishi wa Tanzania kuhudhuria mafunzo ya Ugatuaji nchini Japani toka mwaka 2002 hadi sasa. Pili, TOA inaelekeza shukrani za dhati kwa Serikali ya Japani na JICA kwa kuandaa, kusaidia na kufadhili mafunzo ya Osaka na Mafunzo ya Mikoa na uzalishaji wa kitabu hiki. TOA pia inapenda kutambua na kushukuru juhudi za utekelezaji wa yale yaliyojifunzwa za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa MSM na utayari wao wa kuandika Mbinu Bora kamilifu kama zinavyoonekana kwenye kitabu hiki.

Uchambuzi na uunganishi wa Mbinu Bora zilizopo kwenye kitabu hiki ulifanywa na Bwana Paulo F. Faty (Mhadhiri - Chuo Kikuu Mzumbe) na Bwana Judicate Mwanga (Mhadhiri - Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo), pia Masuala yaliyoigwa Japani yamechambuliwa na Bwana Michiyuki Shimoda (Mshauri Mwandamizi, OR – TAMISEMI). TOA inapongeza kwa dhati mchango wao na inawashukuru sana. Mwisho TOA inapenda kuwashukuru watumishi wote wa OR – TAMISEMI, JICA na TOA kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali iliyoboresha na kuunda kitabu hiki. Siyo rahisi kutaja wote waliochangia katika kazi hii, hata hivyo TOA inaheshimu michango yote iliyotolewa na Taasisi na Watu mbalimabali. Mwisho kabisa, ingawa Watu na Taasisi nyingi zimechangia katika kitabu hiki, TOA na timu ya uchambuaji wanawajibika kwa makosa na mapungufu yanayoweza kuhisiwa na wasomaji wa kitabu hiki.

**Liana A. Hassan**
**MAKAMU MWENYEKITI - TOA**

# Utangulizi (JICA)

Wasomaji Wapendwa!

Utekelezaji wa sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) umechukua zaidi ya miaka 10 sasa ukiwa na lengo la kuboresha huduma kwa kugatua shughuli, majukumu na raslimali toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Kutokana na ukweli huu hapo juu Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) limejikita katika kusaidia utekelezaji wa sera hii hasa katika kuimarisha utoaji huduma katika ngazi za msingi kwa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sekta za afya, kilimo, maji na barabara.

Toka mwaka 2002, JICA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) imekuwa ikiendesha mafunzo kuhusu maboresho katika Serikali za Mitaa yanayoitwa "Osaka Training". Mafunzo haya yalilenga Maofisa wa juu wa Menejimenti katika maboresho ya Serikali za Mitaa, yaani Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi waMSM, Maofisa wa OR – TAMISEMI na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa malengo ya kujifunza uzoefu wa Kijapani katika maboresho ya Serikali za Mitaa. Katika kurudi kwao, waliwasilisha na kujadiliana uelewa na uzoefu walioupata kwenye warsha za mafunzo za mikoa (2003 – 2007). Matokeo yake Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa MSM (TOA) ulianzishwa ili kuwa na jukwaa ambalo wajumbe wa TOA wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu, mbinu bora na changamoto zilizopo. JICA imekuwa ikisaidia uimarishaji wa taasisi ya TOA.

Kutokana na utekelezaji wa Masuala yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka, mbinu bora nyingi ziliwasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika warsha za Mikoa zilizofanyika katika kanda sita mwaka 2011/12. Baada ya uhakiki na uchambuzi wa mbinu hizi bora, toleo la kwanza, la pili na hili la tatu la "kitabu cha mbinu bora" hatimaye limetoka. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa ***"tunatakiwa kujifunza siyo tu kutoka nchi nyingine bali katika jitihada nyingi zilizopo ndani ya nchi".***

Nitafurahi kama mtajifunza vipengele muhimu kutoka kitabu hiki na kuchukua hatua ndogo lakini za uhakika ili kuboresha utendaji katika eneo husika.

JICA ina mpango wa kuisaidia TOA kuendesha mafunzo ya Watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Wakuu wa Idara katika Mikoa yote kwa kutumia vitabu hivi. Tungependa kufuatilia na kujua mbinu bora zitakazofuata zilizotokana na kitabu hiki na mafunzo yake. Tunatarajia kuanzisha jukwaa la kujifunza wenyewe kwa wenyewe (Horizontal Learning) katika ngazi za Msingi.

**Toshio Nagase**
***Mwakilishi Mkuu – Ofisi ya JICA Tanzania***

# Orodha ya Vifupisho

| AMCOs | Agricultural Marketing Cooperatives |
|---|---|
| ALAT | Association of Local Authorities In Tanzania |
| ASDP | Agriculture Sector Development Programme |
| AMSDP | Agricultural Marketing Systems Development Programme |
| CAG | Controller and Auditor General |
| CAMA | Computer Assisted Mass Appraisal |
| CMD | Cassava Mosaic Disease |
| CBD | Central Business District |
| CBSD | Cassava Brown Streak Disease |
| CFO | Commercial Farmers Organisation |
| CMT | Council Management Team |
| CRB | Contractors Registration Board |
| CRDB | Cooperative and Rural Development Bank |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DADPs | District Agricultural Development Plans |
| DALDO | District Agricultural and Livestock Development Officer |
| DCDO | District Community Development Officer |
| DED | District Executive Director |
| DRC | Democratic Republic of Congo |
| FAO | Food and Agriculture Organisation |
| FBO | Faith Based Organization |
| FFS | Farmers Field School |
| HQ | Headquarters |
| ICT | Information Communication Technology |
| KCMC | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| LGA | Local Government Authority |
| LAs | Local Authorities |
| LGCBG | Local Government Capacity Building Grant |
| LGLB | Local Government Loans Board |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (A Network of Farmer Groups in Tanzania) |
| MEOs | Mtaa Executive Officers |
| MoUs | Memorandum of Understanding |
| OVOP | One Village One Product Movement |
| POT | Post Osaka Trainings |
| PPP | Public –Private- Partnership |
| PRA | Participatory Rural Appraisal |
| RCC | Regional Consultative Committee |
| RUBADA | Rufiji Basin Development Authority |
| SACCOs | Savings and Credit Cooperative Societies |
| SEDP | Secondary Education Development Programme |
| SGR | Strategic Grain Reserve |
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| SMEs | Small and medium Enterprises |

| | |
|---|---|
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| TANZAM | Tanzania Zambia Highway |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs regulatory Agency |
| TFNC | Tanzania Food and Nutrition Centre |
| TANROAD | Tanzania Road Agency |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railways |
| TOA | Tanzania Osaka Local Government Reform Alumni |
| TOSCI | Tanzani Official Seed certification Institute |
| TSCP | Tanzania Strategic Cities Project |
| TZS | Tanzanian Shillings |
| VAEOs | Village Agricultural Extension officer |
| VETA | Vocational Education Training Authority |
| WAEO | Ward Agricultural Extension Officer |
| WEO | Ward Executive Officer |
| WDC | Ward Development Committee |
| WPs | Ward Patrons |

# Sura ya Kwanza: Utangulizi; Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani

## 1.0 MAFUNZO YA OSAKA

Kitabu hiki kimeandaliwa na Umoja wa Washiriki wa Mafunzo ya Osaka kuhusu Serikali za Mitaa wanatoka Tanzania (TOA). TOA ni Umoja wa washiriki wa kozi inayotolewa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Mafunzo yenyewe yanaitwa "Mafunzo yenye Mrengo wa Nchi – Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania", lakini yajulikanayo sana kama "Mafunzo ya Osaka". Umoja una wanachama ambao ni Makatibu Tawala wote wa Sekretarieti za Mikoa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini.

Mafunzo ya Osaka yalianza mwaka 2002. Kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Makatibu Tawala wote kutoka Mikoa 21 (kipindi hicho) pamoja na Wakurugenzi wa Halmahauri wawili kutoka kila mkoa walihudhuria. Pia maofisa wa juu toka OWM – TAMISEMI (wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi)[1], Katibu Mkuu wa ALAT na baadhi ya wanataaluma mashuhuri walihudhuria kozi hii.

Kutokana na mafanikio na matokeo dhahiri, JICA iliamua kuendelea na mpango huu, kwa kupanua wigo wake kwa kuongeza nchi nyingine tatu za kiafrika ambazo zilikuwa zikipanga maboresho ya ugatuaji, yaani Kenya, Uganda na Zambia, pamoja na Tanzania. Mpaka leo zaidi ya viongozi 100 wa maboresho wanaojumuisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wamefaidika moja kwa moja na mafunzo ya Osaka. Pia washiriki hawa waliporudi katika mikoa yao waliendesha warsha za ndani zijulikanazo kama "mafunzo ya Post Osaka" ili kubadilishana uzoefu na uelewa walioupata Osaka kwa kuwaalika Wakurugenzi waliobaki pamoja na wakuu wa idara. Hivyo wafaidika wa mafunzo haya waliongezeka mpaka kufikia zaidi ya 1,500, ingawa uanachama wa TOA ulibakia kuwa wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kutoka katika Masuala mbalimbali yaliyoigwa Osaka na mafunzo ya Post Osaka, Halmashauri zilizohudhuria ziliandaa mipango kazi ya kuboresha utendaji wao. Kukiwa na zaidi ya miaka 10 ya utendaji, imethibitishwa kuwa kuna idadi kubwa ya mbinu bora zinajitokeza katika Halmashauri nyingi kwa kutekeleza ile mipango kazi ambayo ni vyema kuwashirikisha wengine. Kwa hiyo TOA iliamua kuhakiki na kuchambua kesi hizo za mbinu bora na kutengeneza kitabu hiki, ili viongozi wa Halmashauri waweze kuzirejea kesi hizi na kuzitumia pale wanapoona zinafaa na zina tija, katika kuboresha kazi zao.

[1] Pamoja na Makatibu wakuu wawili wa Zamani wa OWM-TAMISEMI, yaani, MS. Tarishi M.K. na Bwana H.A. Katanga

Kabla ya kuingia kwenye kesi zenyewe za mbinu bora, ni vyema katika sura hii tukaangalia kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya kwa viongozi wa maboresho wa kitanzania, nini ilikuwa maana ya mafunzo ya Osaka kwa Tanzania na Masuala gani yalijadiliwa kwenye mafunzo haya.

## 2.0 HISTORIA YA MAFUNZO YA OSAKA

Kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya? Na yalikuwa na maana gani kwa Tanzania?

### 2.1 Maoni ya JICA Kuhusu Msaada kwenye Ugatuaji

JICA ina maoni ya kipekee kuhusu misaada kwenye utawala ambayo yanaweza kutofautiana na maoni ya washirika wengine wa maendeleo. JICA imeshuhudia programu kubwa kubwa za maboresho zikifanywa katika nchi zinazoendelea na washirika wa maendeleo kama Programu wa kurekibisha Miundo ya Uchumi (SAPs) na maboresho ya utawala ikiwa ni pamoja na Ugatuaji wa madaraka. Inaweza kusemwa kuwa programu hizi na maboresho haya yaliyofanywa katika nchi zinazoendelea ni sawa kabisa na yale yanayojaribiwa sasa katika nchi zilizoendelea bila kujali tofauti iliyopo ya kihistoria na mazingira kati ya nchi hizi. Pia mara kwa mara inajidhihirisha kuwa maboresho haya yanatekelezwa kwa msukumo mkubwa toka kwa wafadhili, bila kuzingatia asili ya mchakato wa maendeleo na umiliki wa nchi husika.

Kutokana na machungu ya kushindwa kufikia malengo katika ushirikiano wa kimataifa wa aina hii, JICA imekuwa na msimamo ufuatazo katika kusaidia ugatuaji.

(i) Hakuna mfumo wowote unaoweza kutumika katika nchi zote.
(ii) Ugatuaji wenyewe siyo lengo bali ni njia ya kufikia lengo fulani.
(iii) Kuasilisha na kukuza mfumo ndani ya nchi kupitia majadiliano ya kitaifa ni muhimu.
(iv) Jinsi gani ya kuhakikisha viwango vya chini vya kitaifa vya huduma[2] vinafikiwa ni muhimu katika kuandaa maboresho ya Ugatuaji.
(v) Maboresho ya Ugatuaji ni mchakato mrefu, ambao hautakiwi kuchukuliwa kama Mradi au Programu tu.
(vi) Maboresho ya Ugatuaji ya haraka haraka yanaweza kuleta fujo. Katika kila maboresho ya Ugatuaji (d by d), ni lazima kuhakikisha kuna mazingira sahihi kwa upande wa Halmashauri na wanajamii kupokea majukumu makubwa yanayogatuliwa.

### 2.0 Changamoto Kubwa Iliyogunduliwa katika Programu ya Tanzania ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na Ujumbe wa Maandalizi ya Mafunzo wa Mwaka 2002

Baada ya maombi ya Serikali ya Tanzania kuhusu kuwepo kwa Mpango wa mafunzo wa maboresho katika serikali za mitaa mwaka 2001, JICA iliamua kutuma ujumbe kwenda kuchambua hali ilivyo ili kuunda kozi ya mafunzo yenye maudhui ya kumaliza Masuala muhimu. Ujumbe ule ulipofika Tanzania, Novemba mwaka 2002, uligundua kuwa Programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania ilikuwa na changamoto zifuatazo;

[2] Viwango vya chini vya kitaifa vya huduma ni nadharia kuwa kiwango fulani cha huduma lazima kifikiwe hata kama ni katika jamii maskini vijijini sawa na kwenye miji mikubwa.

(i) Jedwali kubwa na lenye hatua nyingi za utekelezaji (Zaidi ya kurasa 80)

(ii) Programu ya maboresho ilikuwa ukitekelezwa kwa jedwali zuri sana lakini halikuruhusu maboresho/mabadiliko zaidi. Ujumbe uliona kulikuwa na nafasi ndogo sana iliyoachwa ya kuweza kubadili lolote ili kuruhusu majaribio ya suala ambalo ni muhimu. Ujumbe uliona kuwa kila kitu kimeshadhamiriwa, na Serikali ya Tanzania ililazimika kufuata reli hiyo bila kwenda pembeni au kurudi vyuma.

(iii) Programu iliandaliwa kwa msaada mkubwa kutoka kundi la wafadhili.

(iv) Wafadhili wa kawaida waliopo kwenye mfuko “Basket funding” waliunda kamati ya msukumo pamoja na serikali. Kuandikwa kwa Programu yenyewe kulifanywa na wataalamu washauri wa nje na hata utekelezaji wenyewe. Ujumbe ulihofia kuwa Programu ya maboresho iliandaliwa bila kupitia mchakato stahiki wa kujenga uelewa ndani ya nchi na kupata makubaliano yanayohusu mahitaji ya mabadiliko.

(v) Hatari ya kukimbilia kwa haraka Ugatuaji wa Madaraka (D by D).

Sera ya ugatuaji (D by D) iliyokuwa ikihamasishwa na Serikali ilidhihirika kwenye ujumbe huo kuwa ni kama vile Tanzania ilikuwa inatekeleza ugatuaji wa madaraka sawa na ule wa nchi zilizoendelea. Swali likawa; Je ni kweli uwezo na mtazamo wa Halmashauri na Wizara zote ulikuwa tayari kwa mabadiliko haya ya haraka? Ujumbe huu uliaona changamoto zifuatazo katika hili;

- Upinzani kutoka Wizara za kisekta
- Ukosefu wa majadiliano ya kina kuhusu ugatuaji katika jamii
- Hakukuwa na uwezo kamilifu kwa upande wa Halmashauri kuchukua majukumu yote yaliyogatuliwa

**2.3 Uwezekano wa Umuhimu wa Uzoefu toka Japani katika Ujenzi wa Taifa na Maboresho ya Ugatuaji - Ujumbe kutoka Japan kwenda Tanzania kupitia Mafunzo ya Osaka.**

Baada ya kuona hali halisi ya Tanzania iliyoelezewa hapo juu, JICA iliamua kuwa uzoefu wa Japani kwenye ujenzi wa Taifa na Maboresho yaliyokuwa na mchakato wa muda mrefu ya Ugatuaji ungeweza kuwa unastahili na muhimu kwa viongozi wa maboresho wa Tanzania kujifunza na kupitia upya maboresho yao.

Japani ni nchi ndogo huko Bara la Asia isiyo na ustaarabu wa Magharibi, ambayo ilianza ujenzi wa taifa kama nchi iliyo nyuma kabisa lakini ikafikia maendeleo ya ajabu. Japani ina uzoefu mwingi wa aina yake wa kutumia mifano (models) ya nje (mfano wa Magharibi) ambayo wafadhili wengine hawana. (Mataifa ya Ulaya yamekuwa mara zote mstari wa mbele na katikati ya dunia na hujiona hayana sababu ya kujifunza toka nje). Kwa kweli, Japani ilianza Ujenzi wa taifa na maendeleo, kwa kujaribu kuiga mifano ya Magharibi lakini ikashindikana mwanzoni kabisa. Tokea hapo ikawa ni mchakato mrefu wa kujaribu na kushindwa mpaka hatimaye ilipofikia Japani ikaunda mfumo wake wa kipekee unaoitwa “Nusu kijapani nusu Magharibi”. Japani inaamini kuwa aina hii ya uanzishaji wa mfumo, pamoja na umiliki wake

thabiti kupitia kujaribu na kushindwa mara nyingi ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Mchakato huu ambao Japan ilitumia ili kuanzisha mfumo wake wa serikali za mitaa na maboresho ya Ugatuaji ni tofauti kabisa na mifano ya Ulaya ambayo nchi zinazoendelea zinajaribu kuanzisha kwa sasa. JICA ilifikiri kuwa kuwasilisha "mfumo huu tofauti" unaweza kuwa muhimu, kwani kuwa na mfano mmoja tu, inaonekana kama vile "ndio njia pekee" hakuna nyingine. Lakini kukiwa na mifano zaidi ya miwili, wanaweza wakaanza kulinganisha na kuona ni mfano upi unafaa zaidi katika mazingira yao, na ni hatua ipi iwe ya kwanza katika kuandaa mfumo wao wenyewe.

Ifuatayo ni mifano tu ya kuvutia ya vigezo vinavyoweza kuigwa toka mfumo wa kijapani kati ya mengi yaliyopo;

**(1) Mchakato wa Maboresho wa Polepole Sana Lakini wa Uhakika**

Japani ilitumia miaka 110 toka ilipoanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa na Ugatuaji; ingawa tunahesabu miaka 55 ya Maboresho Makuu baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia hadi kufika ugatuaji halisi (D by D) mwaka 2000. Serikali ilijaribu kuhakikisha kuwa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha kabla ya kugatua majukumu, na siyo kukimbilia kurekebisha taasisi za Ugatuaji (D by D). Uzoefu huu wa Japani unaipa Tanzania fursa ya kufikiria mara mbili kama mwendo wa maboresho siyo kasi sana, na kama nchi inataka kuendelea na mwendo kasi uliopo, basi haina budi kuhakikisha kuna ujenzi wa uwezo stahiki kwa upande wa Serikali za Mitaa.

**(2) Ukasimishaji wa Shughuli/Majukumu kwa Wakala (Agency Delegated Functions)**

Katika kipindi tajwa cha miaka 55, serikali ilichagua mfumo wa "kukasimu" unaoitwa ADF kama hatua ya mpito, badala ya kurukia Ugatuaji moja kwa moja. Kwa sababu ya mfumo huu Japani ilipingwa sana na nchi za Magharibi kwa kipindi kirefu kuwa haijafanya Ugatuaji sahihi, na mwishoni kabisa Serikali ikaamua kuingia katika Ugatuaji halisi mwaka 2000 na kuondokana na mfumo wa kukasimu (ADF). Hata hivyo sasa hivi imethibitika kuwa ADF ilichangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mfumo mzuri wa Serikali za Mitaa na kupelekea kufikiwa kwa ugatuaji halisi (D by D) nchini Japani; hasa katika vipengele vifuatavyo;

- Shukrani kwa ADF, Halmashauri zilifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara husika, na zikaweza kujenga uwezo wao kupitia mafunzo kazini (on the job training) kukiwa na usaidizi wa kitaalamu wa karibu toka wizarani. Kila walipopata changamoto, maofisa wa Serikali za Mitaa waliweza kuwasiliana na maofisa wa wizara husika kwa simu na maofisa wa wizara waliweza kusaidia kwa wema na kumaliza changamoto hizo pamoja. Haya yote yaliwezekana kwa sababu kimsingi shughuli zote zilikuwa ni wajibu wa Wizara na zilikasimishwa tu kwa Halmashauri. Hivyo hakukuwa na upinzani wowote toka wizarani, zaidi ya ushirikiano ilipofikia Ugatuaji wa shughuli; kinyume kabisa na yanayotokea katika nchi zinzoendelea zinapotekeleza ugatuaji.

- Hoja ya msingi ilikuwa ni kuhakikisha kuwa raslimali ambazo ni chache zilizopo ndani ya nchi zinaweza kutumika vizuri zaidi kuelekea upande mmoja yaani maendeleo ya nchi, badala ya kuzigawa na kutengeneza tofauti kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.
- Ilikuwa ni muhimu sana katika hatua za mwanzo ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na uwezo dhaifu. Bila mfumo wa kukasimu (ADF) kipindi hicho Halmashauri zisingeweza kufanya vizuri shughuli zao za kuhudumia watu wala uwezo wao usingejengeka.
- Sababu nyingine muhimu ilikuwa mafunzo kazini (OJT). Shukrani kwa mchakato wa mafunzo kazini (OJT), kwa miaka 55, watumishi wote wa Serikali za Mitaa pamoja na muundo wao kwa ujumla walijenga uwezo thabiti, kwa kupokea ufahamu na utaalamu kutoka wizarani, na kuwa tayari Serikali Kuu ilipoamua kugatua madaraka (D by D).

Uzoefu huu wa Japan unaleta swali moja la msingi kwa Tanzania juu ya namna gani nchi inaweza kujithibitishia uhakika na ubora wa mchakato wa kuzijengea uwezo Halmashauri ilihali Ugatuaji (D by D) ukiendelea; kuhakikisha matumizi mazuri ya raslimali chache zilizopo nchini na kukwepa kabisa upinzani toka Wizara za kisekta.

**(3) Mfumo wa Kubadilishana Watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**

Nchini Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za maboresho, mtindo wa kubadilishana watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ulitumika sana kama mbinu bora kabisa ya (a) kujaza upungufu wa watumishi hasa wenye sifa katika Halmashauri za pembezoni na (b) kuhakikisha uhamishaji wa ujuzi na utaalamu kutoka kwa wasomi wa Wizara kwenda kwa watumishi wa Halmashauri waliokuwa na ujuzi na uzoefu mdogo ili kujenga uwezo wa Halmshauri hizo.

Serikali iliunda jopo kubwa la maofisa wataalamu katika wizara ya Serikali za Mitaa na kuwapeleka kwenda kwenye Halmashauri zilizokuwa na uwezo mdogo huko pembezoni ili kuzisaidia. Hatua hii ya uhamisho wa muda ilidumu kwa muda wa miaka 4 - 5 na baadaya watumishi hawa walirudishwa kwenye nafasi zao za kawaida kwenye wizara zao. Kadri walivyokuwa na uwezo wa kitaalamu kuwezesha wengine ndivyo walivyopelekwa kwenye Halmashauri za mbali na zenye udhaifu mkubwa. Pale walipofaulu na kutenda vizuri katika vituo hivi vipya, waliahidiwa kupanda vyeo zaidi wanaporudi, ambayo iliwapa motisha wataalamu hawa waliobobea kwenda kwenye sehemu zisizovutia kwa hamasa ya juu kabisa. Pia Halmashauri nyingi zilipeleka watumishi wao kwenye wizara mbalimbali kufanya kazi, katika misingi ya mafunzo kazini kwenye maeneo ambayo Halmashauri husika ilihitaji.

Baada ya kurudia mizunguko kadhaa ya kubadilishana watumishi, ujuzi na utaalamu wa kutosha ulihamishwa kikamilifu toka Wizara kwenda Halmashauri, kitu ambacho kilisaidia sana kujenga uwezo wa Halmshauri nchini Japanni. Sasa Halmashauri zinajitegemea katika raslimali watu bila kuitegemea Serikali Kuu tena.

Nidhahiri kuwa ugatuaji wa raslimali watu ukifanyika kwa ukamilifu wake bila kuwa na mbinu za kutatua matatizo, hupelekea upungufu mkubwa wa watumishi kwenye

Halmashauri ambazo zipo katika maeneo maskini na pembezoni. Ni kwa sababu hii Tanzania iliamua kurudisha Masuala ya raslimali watu kwa sehemu kubwa Serikali Kuu. Hata hivyo haina mantiki kuendeleza Ugatuaji wa madaraka (D by D) bila Ugatuaji halisi wa raslimali watu. Badala ya "0 au 100", serikali inatakiwa kutafuta mkakati wa namna ya kugatua raslimali watu na wakati huohuo kukwepa kutengeneza upungufu katika maeneo ya vijijini, na kujiridhisha kuwa kuna mchakato wa kujenga uwezo wa baadaye wa Halmashauri.

## 3.0 MASUALA YALIYOJITOKEZA NA KUJADILIWA WAKATI WA MAFUNZO YA OSAKA

Kutokana na upungufu wa nafasi Masuala machache tu ya msingi yameweza kuwasilishwa kwenye sehemu hiyo hapo juu, kati ya mambo mengi yanayotokana na uzoefu wa Japani ambayo Tanzania imepewa. Hapa vipengele vingine vitatajwa na kuelezewa kwa kifupi.

### 3.1 Masuala ya Jumla

Masuala na Maswali yafuatayo yalijitokeza na kujadiliwa wakati wa mafunzo ya Osaka:

**(1) Umuhimu wa kukuza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama kigezo cha mafanikio ya Ugatuaji wenyewe**

- Je hakuna hatari ya kudidimiza utoaji huduma, kugatua wajibu mkubwa kiasi hiki ndani ya muda mfupi?
- Ni namna gani ya kukabiliana na hali halisi kuwa Halmashauri zinahitaji uwezo zaidi ili kutekeleza shughuli zilizogatuliwa?
    - Vipi kuhusu ajira? Namna gani itawezekana kupata watumishi wenye sifa katika Halmashauri zilizopo kwenye maeneo maskini na pembezoni?
    - Ni jinsi gani ya kuziba pengo kati ya ujuzi na utaalamu katika Serikali za Mitaa na kuziendeleza? Je siyo muhimu kwanza kuweka mbinu za kuhamisha ujuzi na utaalamu, pamoja na usaidizi wa kitaalamu kutoka serikali kuu kwenda Halmshauri? Siyo muhimu kwanza kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Halmashauri badala ya kutegemea misaada toka nje?

**(2) Ugatuaji na Maendeleo**

- Ili kuweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi na kwa raslimali chache zilizopo, ni muhimu kutafuta mbinu mkakati ya kuzitumia raslimali hizi (hivi ndivyo ambavyo Japani imekuwa ikifanya kujiletea maendeleo yake)
- Namna gani unaweza kusimamia maendeleo ya nchi na ugatuaji kwa pamoja wakati mara kadhaa hupingana? Unawezaje kujiridhisha kuwa hakutakuwa na utengano wa raslimali na tofauti (kutokuelewana) kati ya Serikali Kuu na Halmashauri au kati ya Halmashauri zenyewe?

**(3) Ugatuaji na Viwango vya chini vya kitaifa**

- Jinsi gani ya kusimamia ugatuaji na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa? Ni jinsi gani itahakikishwa kuwa Halmshauri zilizopo vijijini zitakuwa na uwezo wa kutosha kama zilivyo zile tajiri katika kigezo cha utoaji huduma kwa watu? (uwezo wa watumishi na fedha).

**(4) Ukweli Kuhusu Uwezo wa Halmashauri kuweza Kutoa Huduma**

- Swali liliulizwa; Ni Maofisa Ugani wangapi waliopo katika Halmashauri ukijumuisha na wale ambao wanatumikia katika kata na vijiji? Swali hili liliulizwa kwa washiriki ili kuwafanya waelewe hali ilivyo mbaya ambayo Halmashauri za Tanzania zinatakiwa kukabiliana nayo. Ukichukua Mkoa mmoja kama mfano, Mkoa wa Nagano nchini Japani, ni mkoa mdogo kabisa ulioko maeneo ya vijijini lakini una maofisa ugani wa kilimo wapatao 1500. Pia kuna Halmshauri 77 za ngazi za chini katika Mkoa huu ambazo kila moja inaajiri maofisa ugani kati ya 20 – 30. Maana yake kuwa wakulima katika Mkoa (prefecture)[3] wa Nagano wanafurahia huduma zinazotolewa na zaidi ya maofisa ugani 3,000 wa Halmshauri ikilinganishwa na wakulima wa Tanzania ambao wana maofisa ugani wasiozidi 100[4]. Pia nchini Japani kuna mashirika mengi ya binafsi yanayouza mashine za kilimo, mbolea, madawa, mbegu n.k pamoja na taasisi za ushirika zilizo imara; zote hizi hutoa huduma mbalimbali za ugani na ushauri wa kitaalamu.
- Ni vyema kutambua hali ngumu iliyoelezewa hapo juu na kuanzisha mkakati mpya. Hatutakiwi kuota ndoto kwamba Tanzania inaweza kufikia kutoa huduma nzuri kama za nchi zilizoendelea kwa idadi ndogo hivi ya watumishi kwenye eneo lote hata kama Serikali Kuu itaamuwa kufanya kila kitu peke yake.

**(5) Umuhimu wa Juhudi za Wananchi na Ushirikiano kati ya Halmashauri na Jamii**

- Kutokana na Ukweli ulioongelewa hapo juu, haikwepeki kutumia kwa kiasi kikubwa Uwezo wa watu na Juhudi za kujitegemea ili kutoa huduma zilizo bora.
- Ni imani ya JICA kuwa kama watu wataongozwa na kuwezeshwa vizuri, wana uwezo wa kufanya mambo mengi wenyewe, kama kujenga shule za msingi, zahanati, barabara zao na kuzitunza.
- Kwa Japani pia, kipindi cha hatua za mwanzo za Maendeleo, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga shule za msingi. Kwa mfano, ilikuwa ni watu katika jamii zao waliochangia kutoka mifukoni mwao na wakafanya kazi pamoja kujenga na zaidi wakatafuta watu wanaoweza kufundisha na wakawalipa mishahara yao. Ndiyo maana shule nyingi za

---

[3] Mkoa (prefecture) huko Japani ni karibu sawa na wilaya za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. (Ingawa Wilaya nyingine za Tanzania ni kubwa sana kuliko Mikoa ya Kijapani).

[4] Pia si kwamba Japani ina hali nzuri katika maana hii. Kinyume chake, Japani ni nchi ambayo ina idadi ndogo kabisa ya watumishi kwa idadi ya watu waliopo ikilinganishwa na nchi zilizoendelea. Maana yake ni kuwa Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia n.k wana watumishi wengi zaidi wa serikali.

kipindi hicho hazikuwa za "umma" bali "binafsi", kwa maana ya "shule zinazomilikiwa na jamii; ilikuwa ni baada ya miongo kadhaa, serikali ilipotajirika na ikaanza kuzimiliki na hatimaye kuwa shule za umma.

- Inahitaji mabadiliko ya mtazamo wa Serikali na Watu, kutoka fikra kuwa ni jukumu la Serikali kutoa huduma zote kwa watu kuelekea mtazamo kuwa watu wanaweza kufanya mengi sana kwa juhudi zao wenyewe na serikali ikawezesha tu mchakato huo badala ya Serikali kutekeleza peke yake.

**(6) Umuhimu wa Kuainisha Ukubwa Sahihi wa Sehemu za Serikali za Mitaa; na Kuunda Mbinu Mpya za Kuzifikia Jamii kutoka makao makuu ya Halmashauri**

- Kutokana na vigezo hivyo hapo juu ni lazima kuunda mbinu imara sana za Halmashauri kuzifikia jamii. Hapa Tanzania, Halmashauri za Wilaya ni kubwa mno, hivyo ni muhimu kufikiria jinsi ya kujenga daraja kati ya Halmashauri na jamii.
- Kutoka kwenye wazo la kukuza mtazamo wa watu kuwa na uhuru wao, eneo la Halmashauri linatakiwa kuwa dogo sana ili watu waweze kuona kuwa sehemu hiyo kweli ni yao. Kwa upande mwingine sehemu hii ndogo ya Serikali za Mitaa inatakiwa iwe na uimara wa kutosha kutoa huduma za kutosha ambayo inahitaji kiasi cha raslimali fedha na watu. Haya ni mahitaji muhimu mawili yanayopingana.
- Kuweza kutoa majibu kwa swali hili hapa juu linalojipanga lenyewe, sahihisho lililopo ni kuwa na mfumo wenye ngazi nyingi kutoka Halmashauri hadi jamii. Kwa Japani mfumo huu wa ngazi nyingi unafanya kazi vizuri. Lakini Tanzania pia ina mfumo mzuri wenye wilaya – kata – kijiji – kitongoji. Hii inasaidia sana kukuza uhuru wa jamii na jitihada shirikishi za maendeleo kati ya Halmashauri na jamii. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii (O&OD) unaweza kuwa jukwaa zuri zaidi la kuboresha mfumo huu na kuuwezesha kufanya kazi vizuri zaidi.

## 3.2 Usimamizi na Ugatuaji wa Raslimali Watu

Kama ilivyo kwenye sehemu iliyotangulia, mafunzo ya Osaka yalitoa tahadhari kwa Viongozi wa Tanzania katika miaka michache ya mwanzo kuwa waangalifu kuhusu kutoharakisha kugatua na kupeleka madaraka maarufu kama *D-by-D*. Hata hivyo, kuhusu ugatuaji wa masuala ya rasilimali watu, ujumbe ulikuwa tofauti kidogo kwa vile ilionekana kwamba madaraka haya yalikwisha anza kurudishwa Serikal Kuu; kwani uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmasahuri na Wakuu wa Idara unafanywa na Wizara pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuendesha mchakato wa ajira kwa kada nyingine za watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nchi ya Japani haikugatua madaraka na kuyapeleka Halamashauri kwa haraka, bali Serikali Kuu ilendelea kuhodhi baadhi ya shughuli. Kwa mantiki hii, ugatuaji nchini Japani haukuwa umekamilika kwa miaka mingi mpaka ilipofika mwaka 2000. Hata hivyo, kuhusiana na kugatua

masuala ya usimamizi wa rasilimali watu, Japan ilihakikisha kwamba madaraka haya yamegatuliwa na kupelekwa Halmashauri kikamilifu tangu mwanzo kabisa wa maboresho.

Hii ni kwa sababu kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu ndiyo jambo la muhimu sana na msingi wa ugatuaji. Kulingana na mfumo wa Serikali za Mitaa Japani, masuala yote huamuliwa na kutekelezwa ndani ya Mamlaka za Serikali Mitaa husika bila kuingiliwa na Serikali Kuu, yaani kuajiri na kufukuza, kuendesha mafunzo, kupanga ngazi za mishahara, kufanya uhamisho, kupandisha vyeo , mpaka kustaafu. Mamlaka za Serikali za Mitaa Japani huajiri wahitimu wapya kutoka vyuo vikuu kila inapofika mwezi Aprili kulingana na mahitaji yao. Wahitimu walioajiriwa na Mamlaka fulani ya Serikali za Mitaa, wataitumikia Mamlaka husika kwa maisha yao yote mpaka watakapostaafu. Hakuna kanuni ya uhamisho kutoka Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa kwenda mamlaka nyingine.

Zaidi ya hayo, Wenyeviti au Mameya ni wanasiasa na huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kura, na ndio wakuu wa Tawi la Utawala/Utendaji sambamba na Tawi la Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Watendaji wanawajibika kwa Meya/Mwenyekiti na siyo kwa Madiwani, kwa hiyo masuala ya watendaji hulindwa na huwakilishwa na Meya/Mwenyekiti katika Baraza la Madiwani.

Kwenye mafunzo ya Osaka, mambo matatu yafuatayo yalitiliwa mkazo kwamba ndivyo vitu muhimu katika kufikia uwezo wa juu wa rasilimali watu katika Halmashauri:

1) Kuajiri
   Kuajiri watumishi wenye sifa kuliko wote na wanaofaa katika kufikia dhima/malengo ya mamlaka husika; na
2) Mafunzo
   Baada ya kuajiri, kuwapa mafunzo yanayolenga na kuwezesha kufikiwa kwa dhima/malengo ya mamlaka husika (siyo malengo ya mtu binafsi); na
3) Kujipanga
   Kuhakikisha kuwa uwezo wote wa Raslimali watu katika Halmashauri unatumika kikamilifu ili kutimiza malengo ya mamlaka husika

Kwa minajili hiyo, Japani iliona kuwa ni jambo lisilokwepeka kutangulia kugatua madaraka yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu ili kila Halmashauri iweze kuchambua hali halisi, kupanga mipango, kuajiri, kutoa mafunzo, kupanga majukumu na kudhibiti watumishi. Mtumishi wa Halmashauri lazima awe mtu anayelipenda eneo husika na watu waliopo, anayefanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu, anayeelewa vizuri kuhusu hali ya eneo husika, anayewafahamu watu vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na wakazi wa eneo husika; hii ndiyo mantiki ya ugatuaji. Ni uzoefu wa nchi ya Japani kwamba, kwenye Halmashauri zenye mafanikio ya kuridhisha, kuna maofisa na watendaji wanaofanya kazi kwa kujituma hasa katika kuwahudumia watu, na kushirikiana na wakazi; na walio wengi wao ni wale watendaji waliozaliwa na kukulia katika maeneo hayo na wanayapenda makazi hayo, pamoja na uongozi thabiti wa Meya/Mwenyekiti ambaye naye ni mzawa.

Jambo jingine muhimu linalozifanya Halmashauri za Japani ziwe na nguvu ni juhudi waliyonayo katika kuwapa watumishi wao mafunzo. Halmashauri za Japani zinawekeza sana kwa watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo pamoja na mpango wa mafunzo kazini ambao uko kimkakati kulingana na mahitaji ya kitaasisi (siyo mahitaji binafsi) na kwa mtazamo wa mbali.

Hili linawezekana kule Japani kwa sababu hakuna uhamisho wa watumishi toka Halmashauri moja kwenda nyingine ya na kiwango cha kubakiza/kushikilia watumishi kazini ni kikubwa sana, hivyo Halmashauri huwekeza bila hofu kwamba baada ya kuwasomesha watakimbia.

Kinyume chake, Tanzania kuna uhamisho wa mara kwa mara wa watumishi muhimu kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine na hivyo ni vigumu sana kuwabakiza/kuwashikilia watumishi kwenye Halmashauri moja. Katika hali kama hii, changamoto kubwa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba matokeo yatokanayo na mafunzo ya watumishi yanabaki ili yalete maboresho katika utendaji kazi wa mamlaka husika, na kuzifanya Halmashauri ziwe na bidii katika kujenga uwezo wa watumishi licha ya uwezekano mkubwa wa kuwapoteza baada ya kuwasomesha. Swali moja liliulizwa kwenye mafunzo ya Osaka kama Tanzania inaweza kuandaa na kutekeleza mpango mkakati na thabiti wa muda mrefu wa mafunzo ya kuwajengea watumishi wake uwezo katika hali hii.

Kwa upande mwingine, mafunzo ya Osaka yaliibua suala la “kufanya kazi kama timu” ili kuweza kutumia asilimia 120 ya uwezo wa nguvu kazi iliyopo na kuyafikia malengo ya kitaasisi. Kule Japani, kuna mambo kadhaa kuhusu mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu ambayo yamefafanuliwa kwa uangalifu mkubwa kwa ajili hiyo, kama vile:

1) Ngazi za mishahara zimewekwa makusudi kwa lengo la kuondokana na rushwa na kuchochea watumishi wafanye kazi kwa bidii hadi watakapostaafu;
2) Mfumo wa kipekee wa Japani “kucheleweshа upandishaji vyeo” ili kumfanya kila mtu afanye kazi kwa bidii kwa miaka mingi kabla ya kupandishwa cheo (kukamua asilimia 120 ya uwezo wa kila mmoja);
3) Watumishi kufanya kazi kwa kuzunguka kila idara ya Halmashauri husika na mtindo wa kuweka kumbukumbu za kila mwaka za utendaji wa kila mtumishi ili kufanya za tathimini kwa haki na kwa malengo na kuchagua wale wenye uwezo mkubwa na wanaostahili kupandishwa vyeo kuwa Wakurugenzi;
4) Shughuli zote zinazohusu rasilimali watu ziko chini ya Idara ya Uendelezaji Rasilimali Watu ili iwezeshe namba 3) hapo juu;
5) Mazingira ya kipekee ya Japani yanawezesha “utendaji kazi kama timu”, usimamizi unaofanywa na wakuu/viongozi, na mafunzo kazini yanayoendeshwa na wasimamizi, mtindo unaojulikana kama mtindo wa “chumba kikubwa” yaani ofisi ya wazi mithili ya ofisi za benki.


Yote yaliyoelezwa kwenye sehemu hiyo hapo juu yamewekwa na kanuni zinazotawala Mamlaka za SM za Japani ili kuhakikisha mambo matatu yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu yanazingatiwa mfano 1) Kuajiri; 2) Mafunzo; na 3) Kushughulika kwa bidii. Swali liliulizwa, katika mazingira ya sasa ya Halmashauri za Tanzania, ni kwa jinsi gani zinaweza kutekeleza mambo haya matatu.

### 3.3 Fedha za Serikali za Mitaa na Ugatuaji wa Masuala ya Fedha

**a) <u>Misingi ya kifedha katika Halmashauri</u>**

Michoro (1) na (2) inaonyesha japo kwa ufupi hali ya Halmashauri za Japani kuhusu masuala ya fedha.

Mchoro (1) unaonyesha ukubwa wa majukumu ya Halmashauri katika matumizi ya kutoa huduma ndani ya kila sekta. Ukiangalia sekta ya afya, Halmashauri hutumia 94% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya afya ya taifa na Serikali Kuu hutumia 6% tu. Kwenye elimu uwiano kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ni 85% kwa 15%. Ukizingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uzito wa majukumu na matumizi,





**Mchoro (1) Uwiano wa Matumizi ya SK na SM kwa kila sekta**
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010
(Ministry of Home affairs of Government of Japan)

Halmashauri za Japani zinafanya sehemu kubwa zaidi ya majukumu ya Serikali ya kutoa Huduma. Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba kiasi kikubwa cha bajeti <u>hutengwa</u> kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu mazito yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao.

Je hali ikoje Tanzania? Ukweli ni huu, ukiangalia majukumu yote yaliyogatuliwa na kupelekwa kwenye ngazi za msingi katika Halmashauri Tanzania, ukubwa wa majukumu ni sawa tu yale ya Halmashauri za Japani. Lakini, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri Tanzania,
ilikuwa pungufu ya TZS trilioni 3 ya bajeti ya taifa ya zaidi ya TZS trilioni 11 ya mwaka 2011/12.


Ulinganisho unaofanywa, ni ule unaohusu bajeti za Halmashauri zenye kuwa na masharti au uhuru wa matumizi. Mchoro (2) unaonyesha viwango na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri za Japani. Kama ilivyothibitishwa na takwimu hizi, 51% ya mapato hutokana na vyanzo vya ndani ( kodi ushuru na malipo mbalimbali). Pia kuna <u>ruzuku ambazo hazina masharti yoyote ya matumizi</u> zinazoitwa “ruzuku toka SK kwenda SM ” (ruzuku za LAT). Ruzuku ya LAT ni <u>fedha nyingi inayotoka SK kwa mara moja</u> kwenda SM na serikali za mikoa. Fedha hii inahamishwa toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti kuu ya kila Halmashauri <u>siku ya kwanza ya kila robo mwaka</u>. Ukijumlisha mapato ya ndani na ruzuku za LAT toka SK, Halmashauri za Japani zina aslimia 75% ya bajeti yao isiyo na masharti na wanaweza kutumia kama wanavyoamua wenyewe.

Mchanganuo huu ni wa muhimu sana kwa Halmashauri SM za Japani katika kufikia malengo ya mipango yao ya maendeleo, kwani wana bajeti ya kutosha na ya uhakika kila mwaka. Washiriki toka Tanzania walipochunguza hali za Halmashauri za kwao, walithibitisha kwamba zina hali mbaya ya kifedha pia fedha nyingi wanayopokea ina masharti ya matumizi kama ilivyo kwenye Mchoro, (3).




Mchoro(2): Vyanzo na viwango vya mapato ya SM za Japani

Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010 (Ministry of Home Affairs of Government of Japan)




Mchoro (3): Muundo wa vyanzo mapato ya SM za Tanzania


Chanzo: Ni hesabu zilizofanywa na mwandishi toka tovuti ya serikali ya Tanzania

Ama kwa hakika, hata kwa hali hii ingelikuwa jambo la maana kama 94% ya ruzuku wanayopokea isingelikuwa na masharti ili Halmashauri ziwe na uhuru wa kuzitumia. Bahati mbaya, kuna ruzuku mbalimbali zinazokuja zikiambatana na masharti katika matumizi. Hivyo basi, hata kama Halmashauri itaanda mipango mizuri ya maendeleo, ni vigumu sana kutekeleza miradi yao ya vipaumbele kwa sababu ya ruzuku zenye masharti, ambazo husababisha mipango ya maendeleo isitekelezeke kirahisi.

Ikumbukwe kwamba kiasi cha fedha inayotengwa kwenye bajeti za Halmashauri ni kidogo mno cha Shilingi trilioni 3 kati ya trilioni 11 za bajeti ya taifa (2011/12). Hizi Shilingi trillioni 3 ni sawa na 94% ya bajeti nzima ya Halmashauri, na hii inathibitisha jinsi ambavyo hawana vyanzo vya ndani vya kutosha.

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Serikali ya Tanzania kutenga kiasi cha kutosha cha bajeti kutekeleza wingi wa majukumu ya Halmashauri yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao kama kweli wameazimia kufikia ugatuaji wa madaraka. Fedha hii inaweza kuwa zile kutoka vyanzo vya

ndani au katika ruzuku isiyo na masharti[5]. Kama hakuna bajeti ya kutosha inayotengwa, basi hakuna sababu ya kugatua majukumu kwenda ngazi za Halmashauri. Vinginevyo, shughuli hizo hazitatekelezwa na mwishowe jamii itateseka kwa kukosa huduma. Kama tulivyoona kwa Halmashauri za Japani, ikitokea kwamba 85% ya majukumu ya kutoa huduma za elimu yamegatuliwa na kupelekwa ngazi za Halmashauri, basi kiasi cha kutosha cha bajeti ya kutekeleza majukumu hayo hugatuliwa na kupelekwa Halmashauri ili kufikia malengo. Vinginevyo si haki hata kidogo kwa Halmashauri na hasa kwa watu wanaotegemea huduma.




**Mchoro (4): Aina za Kodi kwenye Majiji/Miji**
**Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010**
**(Ministry of Home Affairs of Government of Japan)**

**b) <u>Kodi za Ndani kwa ajili ya Uendelevu na ushamiri wa Serikali za Mitaa</u>**

Kule Japani, kuna sababu zilizo wazi kabisa kuhusu aina zote za kodi zinazotengwa kwenye ngazi zote mbili za SM. Prefectures(SM za Wilaya ndiyo ngazi ya juu za SM) na Municipalities (Miji na Majiji) ndiyo ngazi za chini za SM[6]). Japokuwa Wilaya (Prefecture) ndiyo ngazi ya juu ya SM ya Japani, zinaweza kulinganishwa na Halmashauri za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. Kuhusu majukumu, ngazi za chini za SM Japani (Municipalities) ndizo zinalinganishwa na ngazi za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa Tanzania. Hata hivyo kule Japani, huduma zote za muhimu kwa jamii hutolewa na Majiji/Miji (Municipalities) kwa sababu ndizo ngazi za msingi zilizo karibu na watu, huku Prefecture/Wilaya wanahusika hasahasa na maendeleo ya kiuchumi kwa vile majukumu haya yanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya mipango na kuyatekeleza kimkakati.

Kulingana na majukumu yalivyo na wajibu wa Majiji/Miji, zifuatazo ni kodi ambazo zinaweza kutozwa na Majiji :

Kama inavyoonekana katika mchoro (4), kodi za nyumba na mali zisizo hamishika ni sawa na 45.3% ya mapato yatokayo na kodi, ambayo ni karibu na nusu ya mapato yote yatokanayo na kodi. Ukijumlisha na "Kodi ya mkazi"(kodi ya Kichwa) pamoja na "kodi ya mipango miji", inakuwa ni zaidi ya 80% ya mapato yatokanayo na kodi. Kodi za nyumba na kodi ya mipango miji hutozwa kwenye ardhi na majengo na hizi ni kodi ambazo hakuna awezaye kuzikwepa. Kama ardhi yote na majengo yote yamesajiliwa na kuthaminiwa vizuri, basi hivi ni vyanzo vya uhakika kwa serikali za Mitaa.

[5] Kwa hatua zilipofikia kwa sasa, bado haishauriwi kugatua madaraka ya kifedha na kuwapa SM mamlaka makubwa ya kutoza kodi. Hii ni kwa sababu hali hii itaziumiza zile SM zilizo kwenye maeneo yenye ufukara ya vijijini, kwa vile hazina vyanzo vya uhakika vya kodi, huku zile SM tajiri za mijini zitakuwa na mapato mengi kutoka vyanzo vyao vya ndani . Kwa hiyo ni busara zaidi kuendelea kutoa ruzuku kutoka chanzo kimoja, lakini SM ziwe na uhuru na maamuzi wa kuzitumia kulingana na vipaumbele vyao kwa sasa.

[6] Kuna Prefecture/Wilaya 47 na (Munispaa) 1,742 hadi kufikia Octoba 2012. Manispaa za Japani zinajumuisha Majiji**<u>, Miji na Vijiji</u>**, na tofauti na mgawanyiko wa ngazi za SM za Tanzania.

“Kodi ya kila mkazi wa Halmashauri za Japani” ni “kodi ya kichwa” iliyofutwa hapa Tanzania ambayo ni “kodi ya maendeleo”[7]. Chanzo hiki cha kodi pia huwa ni chanzo cha kuaminika kwa sababu wakazi wote wameandikishwa na Halmashauri inajua wanapoishi. Tukiangalia hali ya Tanzania, vyanzo vingi vya mapato ni vile vinavyohusiana na shughuli za kiuchumi, mfano ushuru wa mazao (23%), ushuru wa huduma (18%), ushuru wa nyumba za kulala wageni(3%), leseni (10%), karo na malipo mbalimbali (17%), ambazo hubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa eneo husika, na cha kushangaza ni kwamba kodi ya majengo ni 8% tu ya mapato yatokanayo na kodi.

Mafunzo ya Osaka yaliwapa viongozi wa Tanzania changamoto kwamba ili Halmashauri ziweze kutoa huduma endelevu zinazohitajika kwa wakati na viwango vinavyotegemewa, ni lazima kujenga wigo mpana na mfumo wa uhakika wa kukusanya kodi ndani ya Halmasahuri zenyewe. Uzoefu wa Japani unaonyesha kwamba bila kuweka msisitizo kwenye vyanzo vyenye uhakika vya kodi/ushuru kama vile kodi za majengo, kodi ya kichwa/kodi ya maendeleo, siyo rahisi hata kidogo kwa Halmashauri kutekeleza majukumu yake. Kwa mazingira haya, ni muhimu kuwa na mfumo wa daftari la kuandikisha ardhi na mali zisizo hamishika pamoja na daftari la wakazi wote kwa kila Halmashauri, hii itasaidia nchi nzima siyo tu kwenye masuala ya kukusanya mapato, bali kwa matumizi mengine mengi.

Kuhusu utaratibu huu, inafaa kusema kwamba tayari Tanzania kuna mifano ya kufurahisha na inayotia moyo ya Halmashauri zinazotekeleza kile kinachopendekezwa hapa, rejea kisa mkasa cha Manispaa ya Mtwara Mikindani kwenye Sura ya Tatu.

### 3.4 Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa – Uzoefu wa kufurahisha wa dhana ya ki-Japani ya “Kijiji kimoja zao moja” au (OVOP)”

Hitaji la maendeleo ya kiuchumi ya Halmashauri limekuwa likisumbua vichwa vya Wakurugenzi wengi wa Tanzania. Kuhusiana na hili, kuna uzoefu maarufu nchini Japani wa dhana ijulikanayo kama “zao moja kwa kijiji kimoja” maarufu kama OVOP, iliyoanzia kwenye wilaya/ Prefecture ya Oita ambayo hapo awali ilikuwa moja ya wilaya fukara kuliko zote nchini humo. Uzoefu unaotokana na dhana hii unaweza kuwa muafaka kwa Tanzania kama utatafsiriwa na kutumika inavyostahili kulingana na mazingira ya Tanzania.

#### (a) Zao moja kwa kijiji kimoja (OVOP) ni nini?

Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” au OVOP ni mkusanyiko wa ubunifu wa shughuli za maendeleo ya jamii zilizobuniwa na kupata msukumo wa viongozi kutoka jamii husika katika Wilaya (Prefecture) ya Oita, ambao waliipenda jamii yao na wakahuzunishwa kutokana na hali ya ufukara uliokuwa umekithiri huko miaka ya nyuma. Japokuwa juhudi kama hizo za mtu mmoja mmoja zilikuwepo hapa na pale kwenye Wilaya (Prefecture)ya Oita tangu miaka ya

[7] Tofauti pekee ni kwamba kodi ya kichwaTanzania hutozwa kwa kiwango sawa kwa kila mtu, kwa Japani kodi ya mkazi hutozwa kulingana na viwango vya kipato cha kaya. Kama hakuna kipato cha kiasi fulani kinachokubalika, basi wanakaya wa kaya hiyo hawana sababu ya kulipa kodi ya mkazi.

1960, dhana yenyewe ya "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilianzishwa rasmi mwaka 1979 na Dr. Morihiko HIRAMATSU, akiwa Gavana[8] wa Wilaya hiyo kwa kuanza kuzitambua baadhi ya juhudi za jamii zilizokwisha anza na kuziendeleza.

Dr. HIRAMATSU, alikuwa ni msomi mwenye mafanikio makubwa akiwa mtumishi wa cheo cha juu kwenye Wizara ya Biashara za kimataifa na Viwanda yaani "Ministry of International Trade and Industry (MITI)". Hii ilikuwa Wizara yenye nguvu sana, lakini aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi kwenye Wilaya ya Oita yaani nyumbani kwao. Kilichomsukuma ni kwa sababu alihofia sana kuwa Wilaya ya nyumbani kwake iliendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuwa miongoni mwa Wilaya fukara kuliko zote nchini Japani kwa wakati huo.

Baada ya kurudi kwao, aligombea na kushinda cheo cha Ugavana wa Wilaya ya Oita. Alipoanza kazi hii jambo la kwanza alilolifanya ni kutembelea vijiji vyote kwenye Wilaya hiyo. Wakati akifanya matembezi haya, alikuta kuna miradi ya maendeleo na jitihada mbalimbali za watu wenyewe kujaribu kujinasua huko vijijini. Aliguswa sana na jitihada hizo za wananchi wakiongozwa na viongozi wao wenye mapenzi mema na juhudi hizi zilikuwa hazijulikani kwa serikali. Alithamini sana juhudi za jamii, na akawatia moyo waendelee na jitihada za kujikwamua. Kwa wanavijiji, wengi wao walikuwa hawajawahi kutoka nje ya vijiji vyao, kwa hiyo kwao ilikuwa ni faraja kubwa kutembelewa na mtu mkubwa kama Gavana na kusifiwa kwa kile walichokuwa wanakifanya!. Hawakuwahi kuwaza kwamba kile walichokuwa wanakifanya kilikuwa ni kitu cha kipekee na cha thamani machoni pa wengine. Tangu Gavana wao Dr. HIRAMATSU alipofanya matembezi haya, juhudi hizo za jamii zilipewa msukumo mkubwa na watu wakahamasika zaidi na kujisikia fahari wenyewe.

Kwa upande wake, Dr. HIRAMATSU alifikiri ni jukumu muhimu kwa Serikali ngazi ya Wilaya kuunga mkono na kuendeleza juhudi za thamani kubwa zilizoanzishwa na wananchi kutaka kuboresha maisha yao wenyewe, kuzieneza zaidi na kubadilisha uzoefu huu mzuri na viongozi wa vijiji vingine ndani ya Wilaya yao.

Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP ina mambo muhimu yanayolitofautisha na dhana nyingine kwani Vuguvugu hili hupelekea kuzalisha bidhaa za kipekee (ikijumuisha utalii), ili kupata maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii husika. Hata hivyo, jambo jingine la tofauti kwenye vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" ni kwamba: kuna uzoefu dhabiti wa jamii unaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi midogo ya maendeleo ya shughuli za kiuchumi ngazi za msingi. Wananchi husika huunganisha uwezo wao wa kujipanga na kutekeleza mustakabali wa maisha yao; jamii zimejijengea uwezo, zimeamka na zina ujasiri; Jamii zimeimarika na zimefikia uwezo wa kujitawala na kujiendesha wenyewe kama kijiji. Ukweli uliopo hapa ni kwamba wananchi wana uzoefu wa kufanikiwa na wakati mwingine kushindwa (lakini wamejijengea uwezo na tabia ya kujikwamua katika kushindwa huko), siyo tu kwamba jamii inategemea kupata mafanikio ya kiuchumi pekee, bali pia jamii inatarajia kujijengea uwezo, uzoefu na ujasiri na kupata nguvu zaidi katika mchakato huo. Ukweli huu ni muhimu ufahamike ili kulielewa vizuri vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja". Ikumbukwe

[8] Cheo cha Gavana wa Prefecture ni cheo cha juu zaidi kwenye SM za juu Japani ikilinganishwa na Meya wa kwenye SM za Tanzania (Ona "3.2. Usimamizi wa Rasilimali Watu na Ugatuzi wa madaraka" kwa Meya.)

kwamba ni rahisi sana kupata mafanikio au faida ya mara moja katika biashara au mradi fulani kutokana na msaada wa mara moja kutoka nje ya jamii, lakini kama jamii hiyo itakumbana na vikwazo fulani fulani baadaye, hawataweza kuvishinda kama watakuwa hawajajijengea uwezo kupitia michakato iliyotangulia ya kutatua matatizo yao kwa nguvu na jitihada zao wenyewe.

Kwa mantiki hii, ni vyema kutambua kwamba nyingi kati ya juhudi zilizojitokeza kwenye Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" kule Oita, zilipitia mchakato ufuatao:

- Kabla ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja"au OVOP, wanavijiji wa Oita walikuwa fukara sana, walikuwa wamekata tamaa kuhusu mabadiliko, wenye kijicho na kuoneana wivu wao kwa wao, kutokana na hali hii haikuwezekana kushirikiana baina yao ili kuboresha maisha kwa pamoja. Hata hivyo, kupitia Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" walianza kujitambua kwamba "Ndiyo, tunaweza kama tunataka!" Haya ni mafanikio makubwa katika mchakato wa kubadili fikra.
- Katika badiliko la fikra hapo juu, wanavijiji walianza kujijengea uzoefu wa kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali ndani ya jamii, wakizikabili changamoto wanazokutana nazo na kuzishinda kwa pamoja. Mchakato huu uliwafanya waweze kujipanga vizuri na vizuri zaidi.
- Kupitia mchakato huo huo, waliimarisha mahusiano na taasisi za nje zenye usaidizi ikijumuisha Halmashauri na Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Pamoja na ujenzi wa uwezo wa jamii ulioelezwa hapo juu, jamii husika zilifanikiwa kupata matokeo dhahiri ya maendeleo ya kiuchumi.

**(b) Dr. HIRAMATSU alifanya nini akiwa Gavana wa Wilaya?**

Kwanza kabisa, ieleweke vizuri kwamba vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" halikuwa ni programu ya lazima("maamrisho ya kutoka juu kwenda ngazi za msingi") iliyoandaliwa na Dr. HIRAMATSU na kwamba watu hawakuambiwa cha kufanya. Kwa bahati mbaya, baadhi ya nchi zinazoendelea ambazo zilivutiwa na Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja", waliuelewa vibaya ukweli huu. Walizingatia tuu zile faida za kiuchumi zinazotokana na OVOP na kujaribu kuendeleza vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" kama sera ya taifa na kutoa maamrisho kutoka juu kwamba kila kijiji kizalishe kitu ambacho kinaweza kuuzwa hapa nchini au nje ya nchi. Kinyume chake sasa, alichokifanya Dr. HIRAMATSU kwenye Wilaya ya Oita ilikuwa ni, kwanza, kutembelea vijiji vyote, kuzitambua juhudi za wananchi za thamani ambazo zilikwishaanza, akawasifia na kuwatia moyo.

Pili, alivishirikisha vijiji vingine na viongozi wao kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa ili habari hii iwe kichocheo, waanze na wao kufikiri kuhusu maendeleo yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo husika, badala ya kulalamika eti hawana chochote kwenye vijiji vyao na kukata tamaa.

Tatu, alipotambua bidhaa fulani za kipekee kwenye baadhi ya vijiji, alisaidia kutafuta soko la ndani na nje ya Wilaya ya Oita. Alitumia maarifa yake, uzoefu na mitandao ambayo alikwisha jijengea alipokuwa afisa wa ngazi za juu Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda. Alizitangaza bidhaa hizi nchi nzima.

Nne, aliwezesha suala zima la kubadilishana uzoefu baina ya viongozi wa vijiji mbalimbali ili wajifunze na kuhamasika kutokana na kujifunza kwa watu walio kwenye ngazi moja na siyo kujifunza kwa ngazi tofauti ya maendeleo. Alianzisha shule ya kuendeleza rasilimali watu[9]" iliyoitwa "*Toyonokuni*[10]. Juhudi hizi za Gavana, zilisaidia kuchochea ari ya viongozi na hii ikapelekea kuibuka kwa miradi mingi yenye sura ya "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP.

Kama inavyoonekana hapo juu, dhamira ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilikuwa ni Halmashauri kuzitambua, kuzisifia, kutia moyo juhudi za kimaendeleo zinazojitokeza kwa jamii. Jukumu la Halmashauri ni "uwezeshaji" na siyo "utekelezaji" au "uelekezaji". Dr. HIRAMATSU hakuwaambia wanavijiji jambo la kufanya katika kuendeleza vuguvugu hili, bali aliheshimu juhudi zao na umiliki wao, pamoja na nguvu zao. Mafunzo ya Osaka yanasisitiza vuguvugu la"zao moja kwa kijiji kimoja", kwani ni dhana muafaka kwa mazingira ya Tanzania, na inaaminika kwamba tayari zipo juhudi za namna hiyo kwenye Vijiji na wapo viongozi wazuri wanaojali maendelo ya nyumbani kwao. Ingelikuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa Tanzania kuunga mkono vuguvugu hili na kutoa fursa ya wazalishaji kujifunza kwa wenzao walio ngazi moja. Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kudhani kwamba eti hakuna chochote kwenye vijiji vyao. Kuna mambo mengi mazuri yanayostahili kuigwa lakini pengine wao ndio hawajayatambua. Ni wajibu wa viongozi wa Halmashauri kuanza kuzitambua juhudi za jamii zilizopo, kuzitia moyo, na kubadilishana uzoefu na wengine. Ingekuwa ni njia yenye tija zaidi ya wazalishaji kujifunza kutoka kwa wenzao walio kwenye ngazi moja kuliko kujifunza watu wa ngazi tofauti au kutoka kwenye vitabu. Ni kutokana na mtizamo huu ndipo kitabu hiki kikaandaliwa.

### 3.5 Masuala Mengine

Kuna mengi ambayo hatukugusia hapo juu kutokana na kukosa nafasi. Lakini, yapo ambayo ni ya muhimu kugusia ambayo yanafaa kwa Tanzania kama vile kisamkasa cha Minamata na uzoefu unaotokana na "Ugonjwa wa Minamata"(Minamata Disease) na jinsi walivyoweza kuhuisha jamii kutokana na mkasa huo; Upangaji mipango shirikishi jamii; mipango miji; mipango ya matumizi bora ya ardhi na marekebisho ya ardhi, uzoefu wa Japani kuhusu maendeleo ya kiuchumi na mchango wa Halmashauri katika mkasa huo, n.k.

Kuhusu kisamkasa cha Minamata, mafunzo ya Osaka yanaweka msistizo kwenye umuhimu wake, na inaaminika kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zina mengi ya kujifunza kutokana na kisa mkasa hiki. Masuala ya kisa hiki yatagusiwa kwa undani kwenye kitabu kinachofuata.

## 4.0 MAENDELEO BAADA YA MAFUNZO YA OSAKA YALIYOSABABISHA KUCHAPWA KWA KITABU HIKI

[9] Inaitwa "shule" lakini hakuna majengo. Huwa ni aina fulani ya mafunzo kwanjia ya warsha kwa ajili ya viongozi ili kuwakutanisha pamoja.
[10] "Toyonokuni" jina la kienyeji la eneo hili la Wilaya ya Oita

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 1 hapo juu, mafunzo ya Osaka yalikuwa yameandaliwa mahsusi kwa nchi ya Tanzania kwenye miaka mitano ya mwanzo(2002 – 2007), yaliendelea kwa miaka mingine sita lakini wigo wake ukapanuliwa na kuingiza nchi nyingine tatu (2008 – 2012). Mafanikio makubwa katika miaka hii 11 hapa Tanzania ni kule kuanzishwa kwa Umoja wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi waliosoma Osaka, kwa kifupi TOA. Huu ni mfano wa pekee Duniani kuwa na Umoja wa Wahitimu wa kozi ya aina moja ukijumuisha Wadau Maarufu ambao ni viongozi wa maboresho kama vile Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na wakuu wengine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI). Japokuwa haikutegemewa, lakini ni jambo la kupendeza hata kwa JICA ambao wanaendesha maelfu ya kozi za mafunzo duniani kote.

Kwa nyongeza, TOA wameshaanza kuendesha semina mbalimbali na warsha za mafunzo kama vile Mafunzo baada ya Osaka na Warsha za Mafunzo za Kanda kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Halmaushauri wanachama. Fursa hizi, siyo tu kwamba zina saidia kubadilishana maoni baina ya Halmashauri wanachama, bali yametoa uwanja ambao ni nadra kuupata wa majadiliano na kuhusu uhalisia wa Ugatuaji wa Madaraka, hususan changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza maboresho ya Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa, hakuna asasi ya namna hii hapa Tanzania, inayowahusisha Watendaji wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mkoa. Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT) ipo, lakini wahusika wake wakuu ni Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Wabunge. Vikao vya Jumuiya hii haviwapi fursa Wakurugenzi wa Halmashauri kushiriki kikamilifu na kutoa ushauri wa kitaalamu ingawa wao pia ni wajumbe. Kwa mantiki hii, TOA ina uwezekano mkubwa wa kukua hadi kuwa Umoja wa Watendaji Wakuu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa yaani Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa ambao ni wataalamu na watekelezaji wa ugatuaji wa madaraka na maboresho nchini. Hawa ndio wanaoshughulika kila siku kwenye mstari wa mbele wa maboresho. Maoni na mapendekezo yao ya pamoja yanaweza kuwa ni ya maana sana na ya kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza maboresho.

Kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa, tayari Tanzania imekwishajijengea uzoefu kwa zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji Ugatuaji wa Madaraka kwenda ngazi za msingi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mtaa. Lazima kutakuwepo na idadi kubwa ya mambo ya kufurahisha na uzoefu mzuri kwenye Halmashauri nyingi kote nchini ambao unafaa kushirikisha Halmashauri nyingine. Japani inaamini kwamba aina hii ya kujifunza kwa taasisi zilizo kwenye ngazi zinazofanana inaweza kuwa muafaka zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi yaani kutoka kwenye ngazi tofauti au ya juu sana. Tanzania inaweza kujifunza vizuri kutokana na uzoefu ulioko ndani mfano shughuli za OVOP kama zilivyoelezwa kwenye 3.4. hapo juu. Kitabu hiki cha rejea kiliandaliwa kwa kuzingatia maelezo na msingi huo ulioelezwa hapo juu. Ni matumaini ya TOA na mafunzo ya Osaka kwamba yatachangia kuboresha utendaji ndani ya Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa, kila moja ikimchochea mwenzie, na kuendeleza mambo mema yanayojitokeza, ambayo yatapelekea kwenye ufanisi na mafanikio ya ugatuaji wa madaraka katika nchi hii.

Mwishowe, inastahili kusema kwamba kutokana na matokeo ya kufurahisha yaliyotokana na mafunzo ya Osaka kwa nchi ya Tanzania, ambayo yameelezwa kwenye sura hii, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani (JICA) limeaamua kuendelea kutoa mafunzo ya Osaka kwa miaka mingine mitano, yakilenga Tanzania kwa mara nyingine tena na litatoa msisitizo maalumu katika kuwezesha shughuli za wanaumoja wa TOA na juhudi zake za ujenzi wa kitaasisi. Hii ina maana kwamba, viongozi wengine wengi wa maboresho Tanzania watafaidika kutokana na mafunzo ya Osaka ili waweze kuchangia utekelezaji mzuri zaidi wa maboresho ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi nchini.

# Sura ya Pili: Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato

Ugatuaji wa Masuala ya Fedha Nchini Tanzania huzingatia MSM kuwa na Vyanzo vyao vya mapato vya uhakika, kuwepo kwa mfumo bora wa kutoa na kupokea fedha toka Serikali Kuu, utoaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma zilizogatuliwa, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuhakikisha uwazi na usawa katika kutenga fedha na kuhakikisha usawa katika utoaji wa huduma (rejea sera ya maboresho ya serikali za mitaa ya 1998). Kimsingi, Ugatuaji wa masuala ya fedha kwa Tanzania hujumuisha yafuatayo;

(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitakiwi kupewa majukumu ambayo hayatengewi fedha

(ii) Mfumo wa ruzuku lazima uzingatie utekelezaji wa sera (vipau mbele) za kitaifa kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, na ambazo zitapatiwa fedha kwa ruzuku zenye masharti na kuongozwa na viwango vya chini vya kitaifa

(iii) Mfumo wa ruzuku lazima uzihamasishe Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka vipaumbele vyao kupitia uanzishaji wa ruzuku ambazo hazina masharti na ruzuku za shughuli za maendeleo

(iv) Ruzuku zisizo na masharti zitatolewa kwa utaratibu wa usawa na kwa kufidia Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye uwezo mdogo wa raslimali

(v) Ukokotoaji wa ruzuku lazima ufanyike kwa kutumia fomula (mbinu) yenye vigezo vya uhakika, haki na visivyo na upendeleo

(vi) Ruzuku kutoka Wizara za kisekta lazima zipunguzwe kadri iwezekanavyo

Uboreshaji wa Mapato ni ile hali ya MSM kutumia madaraka waliyopewa na Serikali Kuu kukusanya mapato na kutumia kulingana na vipaumbele vyao. Uboreshaji wa mapato hujumuisha shughuli kama utafutaji wa vyanzo vya mapato, upanuaji wa wigo wa mapato, uhamasishaji wa shughuli za kiuchumi zinazoongeza vyanzo vya mapato na utungaji wa sheria ndogo zinazoongoza ukusanyaji na utumiaji wa mapato.

Katika sura hii, mbinu mbora tatu zimewasilishwa. Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inahusu ukusanyaji bora wa Ushuru wa Mazao ya Misitu. Mbinu hii inaonesha jinsi ambavyo mazao ya misitu yanaweza kupelekea ongezeko katika mapato ya ndani kupitia utafiti wa kina kuhusu njia bora za kukusanya ushuru na kuibadilisha Halmashauri kutoka kudai ushuru wa magogo na kudai ushuru wa mbao. Mbinu hii bora pia inaonesha jinsi mipango ya uelimishaji jamii katika ukusanyaji wa ushuru na matumizi bora ya vituo vya ukaguzi (mabanio) vinavyoweza kuleta ongezeko dhahiri la mapato ya ndani.

Mbinu Bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kuhusu uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani inaelezea jinsi ambavyo MSM zinaweza kuongeza kwa kiasi kikubwa mapato yao ya ndani kutoka katika mazao ya kilimo, hasa mpunga. Mbinu hii inaonesha jinsi ambavyo Halmashauri ilijikuza katika mapato ya ndani kwa kuhamasisha uzalishaji wa mpunga, kupitia sheria ndogo ya ukusanyaji wa mapato, usimamizi sahihi wa vitabu vya risiti, uundaji wa timu ya ukusanyaji wa mapato, utumiaji wa

mikataba ya utendaji na Maafisa Watendaji wa Kata katika ukusanyaji wa mapato na udhibiti thabiti wa vituo vya ukaguzi (Mabanio).

Sura hii inakamilika na Mbinu Bora ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe ambayo inaelezea kwa kina ubunifu katika Mapato ya Ndani kwa ajili ya uboreshaji wa utoaji wa huduma. Mbinu hii Bora inajikita katika kuongeza mapato kwa kutafuta ardhi, kupima viwanja, kuuza viwanja kwa wananchi na kutumia mapato kuendesha zoezi la utambuzi wa thamani za majengo mjini ili kuongeza zaidi makusanyo ya kodi ya majengo na hatimaye kuongeza mapato ya ndani. Mbinu hii Bora pia inaonyesha jinsi mapato yanavyoboresha utoaji wa huduma katika ujenzi wa ofisi mpya, ununuzi wa magari ya ofisi na utoaji bora wa huduma katika ukusanyaji taka, kilimo na elimu.

Kuzingatia kuwa fedha toka Serikali Kuu zinaendelea kupungua na kudhibitiwa zaidi, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinalazimika kuchangamka katika kutafuta vyanzo mbalimbali kama misitu, mazao ya kilimo na Kodi ya Majengo. Mchanganuo wa Mbinu Bora zilizopo katika sura hii unaonesha kuwa;

- Raslimali za asili zinatakiwa kuwa chanzo kikuu cha mapato ya ndani kwa Mamlaka za serikali za mitaa zilizonyingi, lakini chanzo hiki bado kinatumiwa kwa kiasi kidogo. Sababu za chanzo hiki kutumika chini ya kiwango ni kutoainishwa kwa raslimali za asili, utafiti duni, na ushirikishwaji mdogo wa jamii. MSM zinatakiwa kuwa na ubunifu katika kuainisha maliasili ambazo zinaweza kutumika kuongeza uzalishaji na shughuli za kiuchumi na kupelekea kupanuka kwa wigo wa mapato.
- MSM ni taasisi za kisheria zinazojiendesha zenyewe. Katika hili na kwa kuzingatia upungufu wa fedha toka Serikali Kuu, MSM zinatakiwa kujikita katika utafiti wa vyanzo bora vya mapato na kuhamasisha shughuli za kilimo na biashara zenye uwezekano wa kuzalisha mapato zaidi. MSM zinatakiwa kuwa na umakini na ubunifu kuweza kuingia katika shughuli za ardhi na majengo ili kukusanya mapato zaidi na endelevu.
- Mapato yaliyokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali yanahitaji kutumiwa kwa umakini na kuelekezwa kwa walipa kodi husika ili kujenga uhalali wa kulipa kodi. MSM zinatakiwa kutoa huduma bora kwa jamii zinazolipa kodi ili kuongeza uhiari katika kulipa kodi na kuleta uendelevu wa vyanzo vya mapato ya ndani.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI


## UKUSANYAJI BORA WA USHURU KUTOKA MAZAO YA MISITU



*Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilianzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1970. Halmashauri hii ni moja ya Halmshauri Tanohza Mkoa wa Iringa, ipo km 80 kusini mwa manispaa ya Iringa. Halmashauri nyingine ni pamoja na Manispaa ya Iringa, Mji wa Mafinga na Halmashauri za Wilaya za Kilolo na Iringa. Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inapakana na Mkoa wa Njombe kwa upande wa kusini, Mkoa wa Mbeya Upande wa Magharibi, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa upande wa Kaskazini na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo upande wa Kaskazini Mashariki. Makao makuu ya Halmashauri yapo Mafinga Mjini kwenye barabara kuu iendayo Mbeya. Kwa utambulisho wa kimataifa Halmashauri ipo kati ya Latitudo $8^{0}$.0 na $9^{0}$.0 Kusini mwa Ikweta na Longitudo $30^{0}$.0 na $36^{0}$.0 Mashariki mwa Griniwichl. Ardhi yake imefunikwa na misitu 10,411.3 $km^{2}$ na kubakiza 2,427.6 $km^{2}$ tu kwa shughuli za binadamu.




Jamii kubwa ni ya Wahehe ambao huunda takribani 85% ya watu wote. Shughuli kuu ya wakazi ni kilimo ikifuatiwa na ufugaji mdogo wa wanyama. Wabena, Wakinga na makabila mengine wanaunda 15% ya wakazi. Makabila haya yalihamia Mufindi yakitokea Wilaya za Njombe na Makete kujitafutia kipato katika shughuli za uzalishaji Chai na Mbao pamoja na ajira katika taasisi za Serikali. Jedwali Namba 1 linaonesha Tarafa na makabila makuu.

**Jedwali 1: Mgawanyo wa Makabila Makuu Matano Kitarafa**

| S/No. | Ttarafa | Eneo $km^{2}$ | Kata | Idadi ya Makabila | Makabila makuu matano |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Ifwagi | 2,100 | 9 | 3 | Wahehe, Wakinga and Wabena |
| **2** | Kasanga | 1,500 | 8 | 3 | Wahehe, Wakinga and Wabena |
| **3** | Kibengu | 820 | 3 | 2 | Wahehe and Wabena |
| **4** | Malangali | 1,500 | 6 | 3 | Wahehe, Wakinga and Wabena |
| **5** | Sadani | 1,203 | 4 | 2 | Wahehe and Wabena |

| | Jumla | 7,123 | 30 | | |
|---|---|---|---|---|---|

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, idadi ya watu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi iliongezeka kutoka watu 272,071 mwaka 2002 hadi 317,731 mwaka 2012 ikichangia 34% ya idadi ya watu wote wa Mkoa wa Iringa ikiwa na ongezeko la wastani la 1.5% kwa mwaka. Mufindi inakadiriwa kuwa na ongezeko la watu la wastani la chini ikilinganishwa na Wilaya nyingine Mkoani. Ongezeko hili la watu lipo chini ya wastani wa Mkoa ambao ni 1.6% na ongezeko la wastani la kitaifa la 2.4%, kwa mujibu wa makisio ya 2008. Halmashauri hii ndiyo yenye msongamano mkubwa wa watu mkoani ilihali pato lake kwa mwaka ni TZS 1,206,917/=.


Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 5 za Ifwagi, Sadani, Kibengu, Kasanga na Malangali, Kata 30, Vijiji 125, na Vitongoji 808 vilivyogawanyika kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali 2 hapa chini.

**Jedwali 2: Eneo na Mgawanyo wa Kiutawala**

| S/No. | Tarafa | Eneo Km$^2$ | Kata | Vijiji | Vitongoji | % Eneo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ifwagi | 2,100 | 9 | 32 | 150 | 29.5 |
| 2 | Kasanga | 1,500 | 8 | 32 | 158 | 21.1 |
| 3 | Kibengu | 820 | 3 | 16 | 81 | 11.5 |
| 4 | Malangali | 1,500 | 6 | 27 | 133 | 21.1 |
| 5 | Sadani | 1,203 | 4 | 18 | 86 | 16.9 |
| | **Jumla** | **7,123** | **30** | **125** | **608** | **100.0** |

Uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi umejikita zaidi katika kilimo ambacho kinatoa ajira kwa zaidi ya 85% ya wakazi. Mazao yote ya biashara na chakula huzalishwa, mazao ya chakula yakiongoza. Kwa mujibu wa utafiti wa pato la mkoa wa mwaka 2008, kilimo huchangia 90.2% ikifuatiwa na mifugo 0.7%, wakati uwindaji na misitu huchangia 0.2%. Uzalishaji wa wastani katika sekta ya viwanda umetokana zaidi na uwepo wa makampuni makubwa yanayojihusisha na uzalishaji na usindikaji wa Pareto na Chai. Mashirika haya ni pamoja na Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT) na makampuni ya uchakataji na ufungaji wa Chai ambayo ni Kampuni ya Chai ya Uniliver Tanzania, Kampuni ya Chai ya Mufindi na Kampuni ya Chai Bora. Kampuni ya Chai Bora hujihusisha zaidi za Ufungaji wa Chai wakati kampuni nyingine mbili zikijihusisha na Uchakataji. Sekta ya viwanda inaimarika kutokana na uwepo wa viwanda vya kuchakata mazao ya miti ambavyo ni pamoja na Kiwanda cha Karatasi cha Mufindi kilichopo Mgololo, Kiwanda cha Sao Hill na viwanda vingine vidogo vidogo.

**Mchoro 2: Uchangiaji wa Sekta katika Pato la Halmashauri**




## 2.0. TATIZO

Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inafaidika kutokana na uwepo wa fursa nyingi za kiasili kama vile hali ya hewa inayofaa kwa kilimo, mvua za kutosha, ardhi kubwa na jamii ya wachapakazi. Halmashauri ipo mahali pazuri Tanzania kwani inapatikana kati ya barabara kuu iendayo nchi za kusini mwa Afrika na reli iendayo Zambia na Dar es salaam. Hata hivyo katika jitihada za Halmashauri za kukusanya mapato, kutia motisha watumishi, kuboresha mifumo ya ndani na kutoa huduma bora kwa wananchi, Halmashauri ilikuwa na changamoto mbalimbali katika ukusanyaji wa mapato.

Tatizo kubwa la kwanza lilikuwa udanganyifu na ukosefu wa uaminifu ulioshirikisha wakulima binafsi, wasafirishaji wa magogo na mbao, watumishi wa Serikali Kuu na atumishi wa Halmashauri. Katika hali hii wazalishaji wa mbao walishirikiana na wakusanya mapato kuficha idadi kamili ya mbao zilizozalishwa na kusafirishwa na hivyo kupelekea kupungua kwa makusanyo ya mapato mwaka hadi mwaka na kufanya Halmashauri kuwa katika hali ngumu ya kufikia makisio yake ya mapato. Wakati mapato toka kwenye mbao na mazao yake yakipungua, usafirishaji halisi wa mbao kutoka Halmashauri uliendelea kuongezeka kama ilivyojidhihirisha kwa kupotea kabisa kwa misitu iliyokuwepo pembezoni mwa barabara kuu ya Mbeya na katika vijiji.

Changamoto kuu ya pili iliyopelekea Halmashauri kuunda mfumo bora na endelevu wa ukusanyaji mapato ni upunguaji wa usaidizi wa kifedha kutoka Serikali Kuu na washirika wa maendeleo. Tangu mwaka 2008/2009 kuelekea 2010/2011 ruzuku za Serikali Kuu zilianza kupungua kwa kiasi na thamani na kuongeza ugumu katika utoaji wa huduma na motisha kwa watumishi. Hali hii iliongezeka kuwa mbaya zaidi pale ruzuku ya jumla (GPG) ilipofutwa na Halmashauri kulazimika kutenga fedha kwa ajili ya shughuli zilizotumia ruzuku hii. Pia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kupitia Ruzuku ya Mendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) ulipungua sana na kufanya Halmashauri kutemea mapato ya ndani tu kutekeleza majukumu yake ya utoaji huduma na motisha kwa watumishi.

Tatu, mfumo wenyewe wa kukusanya mapato ulileta changamoto kubwa. Mfumo ulikuwa na mapungufu mengi ambayo yalijitokeza katika hali ya uwajibijikaji duni wa wakusanya mapato, uandishi na utunzaji mbovu wa hesabu za Halmashauri, ongezeko kubwa la wakwepa kodi na wizi wa moja kwa moja wa mapato uliofanywa na watumishi waliokuwepo kwenye mfumo. Mfumo huu pia haukuruhusu utoaji taarifa wa papo kwa papo wa yaliyokuwa yakitokea katika vituo mbalimbali vya ukaguzi na pia

vitabu vya risiti vikikosa ulinganifu na uhalisia hali iliyoruhusu wakusanya mapato kuwa na vitabu binafsi vya risiti.

Mwisho, Sheria ndogo ya Halmashauri ilitekelezwa kwa kiwango cha chini sana kutokana na tafsiri tofauti tofauti na zisizokuwa na usawa. Wakusanya mapato walikuwa na tafsiri zao na makampuni makubwa ya mbao na wasafirishaji walikuwa na tafsiri nyingine. Hali hii ilileta tofauti nyingi katika ukusanyaji wa mapato na ongezeko la kesi mahakamani kati ya Halmashuri na walipa kodi. Pia ilitoa mwanya kwa wakusanya mapato kushughulika na wazalishaji, wachakataji na wasafirishaji wa mbao kwa namna tofauti na kupelekea tofauti katika ushuru unaotakiwa kulipwa kwa kipimo kinachofanana.

Mapungufu haya yote ya mfumo wa ukusanyaji mapato yalijidhihirisha katika mapato duni kuweza kutoa huduma za jamii na za kiuchumi, kuongezeka kwa deni la Halmashauri, kuwepo wa watumishi wasiokuwa na motisha, kuwepo kwa madiwani wasio na furaha, kuwepo kwa malalamiko ya wazalishaji na wasafirishaji wa mbao na kuwepo kwa wananchi wasio na hiari ya kulipa kodi nyinginezo. Jedwali 3 hapa chini linaonesha makusanyo duni ya mapato kutokana na mfumo wenye mapungufu mengi.

**Jedwali 3. Makusanyo ya Ushuru wa Mazao ya Misitu Kabla ya Maboresho**

| Mwaka | Bajeti ya Ndani | Makisio ya Ushuru wa Mazao ya Misitu | Makusanyo ya Ushuru wa Mazao ya Misitu |
|---|---|---|---|
| **2008/2009** | 796,862,295/= | 420,000,000/= | 419,850,030/= |
| **2009/2010** | 855,859,040/= | 400,000,000/= | 659,515,975/= |
| **2010/2011** | 1,929,444,740/= | 400,000,000/= | 577,362,964.90 |

## 3.0 LENGO

Kwa kutambua maliasili zilizopo za ardhi, hali ya hewa na watu; Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na Madiwani waliamua kutumia fursa za raslimali watu na teknolojia kuboresha ukusanyaji wa mapato. Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri yatokanayo na ushuru wa mazao ya misitu ili kutoa huduma bora na motisha kwa watumishi. Mahsusi kabisa, hili lingeongeza uhuru wa Halmashauri kujikita katika utekelezaji wa miradi, kutoa motisha kwa watumishi na madiwani na kuiamsha jamii katika kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi kama matokeo ya msukumo wa huduma zilizoboreshwa. Maeneo haya yote ya maboresho ya kijamii na kiuchumi yangeleta ongezeko la mapato ya ndani na uhuru zaidi kutoka Serikali Kuu; mwelekeo dhahiri wa ugatuaji (D by D).

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Halmashauri Ya Wilaya ya Mufindi iliamua kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kufikia malengo. Mkakati muhimu wa kwanza ulikuwa kuendesha utafiti wa kina wa kulinganisha mbinu mbalimbali zilizopendekezwa za kukusanya Ushuru. Utafiti huu pia ulihusisha uamuzi kuhusu kukusanya ushuru kutokana na magogo au mbao. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa ushuru kutokana na mbao unaleta mapato zaidi na ni wa haki zaidi kuliko ushuru utokanao na magogo. Utafiti huu uliendeshwa na Mweka Hazina wa Halmashauri, Mhasibu wa mapato, Mwanasheria, Mkaguzi wa ndani, na Afisa Maliasili.

Pili, timu hii ililazimika kuandaa andiko la mapendekezo ili kulishawishi Baraza kutokomeza mfumo wa ukusanyaji ushuru unaotokana na magogo na kuridhia mapendekezo ya kukusanya ushuru unaotokana na mbao. Andiko lilielezea kwa kina faida za mfumo mpya kwa kuonyesha uhakika, upungufu wa gharama, uimara na uwazi wa mfumo. Mfumo huu mpya uliridhiwa na Timu ya Menejimenti na Baraza la Madiwani na kuutokomeza mfumo wa ushuru utokanao na magogo na kuanzisha ushuru utokanao na kipande cha mbao. Uamuzi huu ulilazimu ubadilishaji wa makubaliano ya kibiashara na mashirika ya

mbao ya Sao Hill na Mufindi Wood na Fiber Board, rasmi kuanzia Julai 1, 2011. Mfumo mpya wa ukusanyaji wa Ushuru haubagui vyanzo vyovyote vya mbao, hivyo ushuru unakusanywa kutoka kwa wazalishaji wote ikiwa ni pamoja na mashirika makubwa, mashamba ya jamii, Vijiji, mashirika ya dini na kadhalika. Kabla ya mfumo huu mpya ushuru ulikusanywa kutoka msitu wa kampuni ya Sao Hill tu. Badiliko hili lilihusisha kubadili tozo ya shilingi 100 kwa mbao na kuanzisha tozo ya 5% kwa thamani ya mbao. Badiliko hili lilikuwa muhimu kwani thamani ya mbao hutegemea soko wakati kipande cha mbao hakina uhalisia wa chanzo, ukubwa na ubora wake. Uamuzi wa kutoza ushuru kwa thamani ya mbao umeleta uhakika na uthabiti katika ukusanyaji wa mapato.

Tatu, ili kuufanya mfumo huu mpya kuwa bora, rahisi na muhimu, ushiriki wa taasisi za Serikali Kuu na vyombo vyake ulikuwa wa lazima. Halmashauri ilishirikisha Mkuu wa Wilaya na jeshi la Polisi hasa katika kushawishi wananchi kukubaliana na mabadiliko haya na katika utekelezaji wa Ukusanyaji wa mapato katika vituo vya ukaguzi. Polisi wanashiriki kila siku kusaidia watumishi waliopo katika vituo vya ukaguzi kuhakikisha utii unakuwepo kwa taratibu zilizowekwa za ukusanyaji wa ushuru wa mbao ambao unahusisha kuhesabu mbao, kukagua risiti, kutoa risiti kwa wasafirishaji ambao hawakulipa kabla na kutoza fani kwa wakiukaji.

Nne, kutokana na badiliko hili kuu katika ukusanyaji wa mapato kwa wazalishaji na wasafirishaji wa mbao na jamii kwa ujumla, mpango wa kujenga uelewa ulikuwa muhimu. Halmashauri iliandaa mpango kabambe wa kujenga uelewa na kuhamasisha jamii kwa ajili ya walipa kodi wote kuhusu mfumo mpya wa ukusanyaji mapato na sifa zake za haki, uwazi na thamani kwa Halmashauri na jamii kwa ujumla. Katika kampeni hii Mkuu wa Wilaya, Madiwani na Watumishi walishiriki.

Tano, Halmashauri ililazimika kuanzisha vituo 5 vya ukaguzi hasa katika maeneo ya Rungemba (mpakani na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa), Nyigo (Mpakani na Halmashauri ya Mji wa Makambako) na Kibengu (mpakani na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo). Katika maeneo mkakati, Halmashauri ilinunua ardhi na kujenga vituo vya ukaguzi vilivyojumuisha vituo vya polisi na watumishi. Katika barabara kuu, Halmashuri ilishawishi wakala wa barabara (TANROADS) kujenga nafasi za maegesho karibu na vituo vya ukaguzi ili kuruhusu magari mengine kuendelea kusafiri wakati malori ya mbao yakikaguliwa. Picha zilizopo hapa chini zinaonyesha askari polisi wa usalama barabarani akisimamisha malori yanayosafirisha mbao ili mtumishi wa Halmashauri aweze kukagua mbao zilizopo, vibali vya kusafirisha mbao, na risiti za ushuru katika kituo cha ukaguzi cha Rungemba.




***Kituo cha Ukaguzi cha Rungemba***




***Wakusanya Ushuru wakilinganisha risiti na rejesta***

Mkakati mwingine ulikuwa kuhuisha sheria ndogo ya Ushuru na kuhakikisha utekelezaji thabiti wa sheria hiyo. Sheria hii ndogo iliboreshwa kwa kuingiza masuala yote ya mabadiliko kutoka tozo ya ushuru kwa kipande cha mbao hadi tozo ya asilimia ya thamani ya mbao, uwepo wa ukaguzi wa mara kwa mara wa mbao zinazoshafirishwa, vituo vya kutoza ushuru wa mbao, mifumo ya kutoa risiti, uingizaji wa taarifa katika rejesta na utoaji taarifa makao makuu. Sheria hii pia ilieleza waziwazi adhabu za vitendo vyote vinavyoweza kuleta ukiukwaji wa viwango na malipo halali ya ushuru.

Mwisho, Halmashauri ilihakikisha kuwa mfumo unafanya kazi kikamilifu na kuweka kipaumbele katika ukusanyaji wa mapato kwa kutenga raslimali fedha na watu za kutosha, kuruhusu watumishi kuwepo katika vituo vya ukaguzi kwa masaa 24 na kutoa motisha ya kutosha kwa wakusanya mapato, yaani shilingi 10,000/= kwa kutwa na shilingi 25,000/= kwa kukesha, zinazolipwa kwa pamoja mwishoni mwa mwezi. Halmashauri pia iliona faida zaidi ya kutumia watumishi wake katika ukusanyaji wa mapato kuliko ubinafsishaji.

**5.0 RASLIMALI**

Ukusanyaji wa Mapato siyo shughuli rahisi. Inahitaji utumiaji wa rasmali za kutosha ili kupata mapato zaidi. Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilitumia raslimali za aina mbalimbali kufanikisha jitihada hii.

**Gharama za Uendeshaji**

- Ujira: Tshs 130,000,000 kwa Mwaka
- Magari na Matengenezo: Ths 40,000,000 kwa mwaka
- Posho za watumishi: Tshs 25,000,000 kwa mwaka
- Jumla ya gharama za uendeshaji 195,000,000 kwa mwaka

**Matokeo ya Matumizi**

- Jumla Ushuru Uliokusanywa kwa Mwaka ni Tshs 1,274,000,000/ (2012/13)

**Mchoro 2: Raslimali zilizotumika**


**6.0 MATOKEO**

Halmashauri imeshuhudia faida kubwa katika jitihada hii ya uboreshaji wa mapato kwa kuzingatia zao moja tu; Mbao. Matokeo makuu yameelezewa kwa kifupi hapa chini.


(i) Ongezeko la mapato kutoka Tshs 659,000,000 mwaka 2009 /2010 hadi Tshs 1,695,170,955 mwaka 2013/2014 kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali 4 na michoro yake hapa chini. Ongezeko la mapato ni tokeo la faida kwani Halmashauri inaweza kuboresha huduma mbalimbali kwa kutumia mapato iliyokusanya yenyewe katika misingi ya uhuru na ugatuaji.

**Jedwali 4: Mtiririko wa Ushuru Kutoka Mazao ya Misitu baada ya Maboresho**

| Mwaka | Bajeti ya Mapato ya Ndani | Makisio ya Ushuru wa mazao ya Misitu | Makusanyo ya Ushuru wa mazao ya Misitu |
|---|---|---|---|
| 2011/2012 | 2,666,768,682/= | 947,106,973/= | 763,671,145.17 |
| 2012/2013 | 2,943,545,748/= | 979,676,500/= | 1,274,052,036/= |
| 2013/2014 | 4,246,937,000/= | 1,394,368,000/= | 1,695,170,955/= |
| 2014/2015 | 4,883,997,550/= | 2,080,413,800/= | 1,407,128,396/= tu hadi Jan 2015 |




Mchoro3: Mtiririko wa Ongezeko la Ushuru




*Mchoro 4: Ongezeko la mapato ya ndani*

(ii) Maboresho katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa kutumia mapato ya ndani. Kwa mfano; ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa 2.6km katika mji wa Mafinga na uchangiaji wa Tshs 256 millioni kuzisaidia jamii katika kujenga zahanati, madarasa na maabara.



*Madarasa yaliyojengwa*




*barabara ya lami Mafinga Mjini*



*Maabara iliyojengwa*

(iii) Mfumo wa kufuatilia Ushuru wa mbao upo. Mfumo huu hutumia ufuatiliaji, vitabu vya risiti vyenye namba za kufuatana na watumishi mahsusi kwa ajili ukaguzi na usimamizi kwa kutembelea vituo. Mfumo huu huhakikisha ushuru unaokusanywa na Maafisa Watendaji wa Kata na wakusanyaji wengine unanakiliwa na kuandikwa vizuri. Katika mfumo huu, makao makuu na vituo vya ukaguzi vinaweza kufanya kwa urahisi zoezi la kulinganisha risiti kwa kutumia risiti za wasafirishaji.




***Rejesta inayoonesha yaliyomo katika kila risiti ya Msafirishaji***

(iv) Jitihada hii imeleta mahusiano bora na walipa kodi (kambuni za kuchakata mbao na wasafirishaji) na hasa wakulima, wanavijiji na jamii kwa ujumla kwa sababu ya kuimarika kwa uwezo wa Halmashauri wa kutoa huduma unaotokana na kuongezeka kwa raslimali fedha. Jitihada hii pia imeboresha ushirikiano kati ya Halmashauri na Polisi katika ukusanyaji wa mapato.

(v) Tokeo jingine muhimu ni kuwa na watumishi wenye motisha na nia thabiti. Kutokana na mafao yatokanayo na ukusanyaji wa mapato ulioimarika Halmashauri inapata urahisi wa kulipa posho mbalimbali za watumishi na madiwani, ambazo huleta motisha na kuwafanya kuwa na ari zaidi kutekeleza shughuli za Halmashauri ikiwa ni pamoja na jitihada za kuongeza mapato.

(vi) Mwisho, utekelezaji wa sheria ndogo ya ushuru na mfumo wake mzima umeleta utayari wa kutosha kwa wadau wote wa ushuru. Wote, wazalishaji na wasafirishaji hupeleka kwa hiari mbao zao kwa watumishi wa Halmashauri, hushiriki katika kuainisha thamani, huomba risiti zao na husimama katika vituo vya ukaguzi kwa ajili ya kulinganisha risiti.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika utekelezaji wa mfumo mpya wa ukusanyaji ushuru Halmashauri imekuwa ikikumbana na vikwazo vingi vinavyotishia uendelevu. Vikwazo hivi ni pamoja na utayari duni wa walipa ushuru, uwepo wa mwingiliano wa kisiasa usiotarajiwa, mazuio ya kimahakama yanayoombwa na wazalishaji na wasafirishaji wa mbao, vitisho vya maisha vya moja kwa moja kwa watumishi wa Halmashauri toka kwa wazalishaji, wasafirishaji na mawakala wao, tofauti za kimaslahi kati ya watumishi wa Halmashauri na madiwani, udanganyifu wa mara kwa mara na ukosefu wa uaminifu kwa baadhi ya wadau. Kujihakikishia uendelevu wa jitihada hii, Halmashauri imejiwekea mikakati ifuatayo;

(i) Ujenzi wa uwezo kwa watumishi wa Halmashauri na madiwani kuhusu utendaji wa mfumo mpya. Mpango huu unatarajiwa kutoa elimu kuhusu mfumo na kujenga uelewa wa pamoja kati ya watumishi na wanasiasa kwa mafanikio ya muda mrefu ya ushuru wa mbao.

(ii) Kufanya uhamasishaji na majadiliano endelevu na wazalishaji na wasafirishaji wa mbao kwa kuhusisha jamii za jirani. Uhamasishaji na majadiliano vinalenga kuleta mabadiliko ya kudumu ya tabia na mitazamo ya wadau na kuwafanya wafurahie nafasi yao kama walipa kodi na Halmashauri kama mtoa huduma. Mpango huu wa uhamasishaji unaweka wazi kuwa

Halmashuri inategemena maliasili zilizopo kupata mapato na maliasili hizohizo kama ardhi huendelezwa na kutumiwa na jamii na kampuni za uzalishaji.

(iii) Ushirikiano endelevu na taasisi za Serikali Kuu kama ofisi ya Mkuu wa Wilaya, jeshi la polisi, na mahakama. Hili ni la lazima ili kuondoa aina zote za uharibifu wa mfumo wa ukusanyaji ushuru kama makubaliano hasi kati ya watumishi wazalishaji yanayonyima Halmashauri mapato stahiki, matumizi ya barabara zizizo rasmi, ukwepaji wa kulipa ushuru pamoja na matumizi ya vitabu vya risiti visivyo rasmi na watumishi wa Halmashauri. Ushirikiano na taasisi za Serikali umeimarisha sana mahusiano kati ya Halmashauri na wadau wa ushuru.

(iv) Motisha kwa watumishi. Halmashauri imeendelea kuboresha utoaji wa aina mbalimbali za motisha kwa watumishi kwa kuzingatia utendaji. Wale wanaokusanya ushuru mwingi na wale wanaofanya kazi usiku kwa masaa mengi hupata motisha zaidi.

(v) Uboreshaji wa ofisi. Halmashauri imeridhia kuwepo kwa maboresho endelevu na ujenzi wa ofisi za kudumu katika vituo vya ukaguzi kwa ajili ya polisi na watumishi. Lengo ni kufanya vituo vya ukaguzi kuwa vyenye hamasa ya kufanya kazi kwa kuwa na mazingira yote stahiki kwa shughuli za kiofisi.

(vi) Mapitio ya mara kwa mara ya mfumo wa ukusanyaji ushuru. Halmashauri hufanya mapitio ya mara kwa mara ya mfumo ili kuzuia majaribio ya udanganyifu na wizi yanayofanywa na wakusanyaji katika vijiji na kata, kufuatilia watumishi katika vituo vya ukaguzi na kudai taarifa za mara kwa mara za wahasibu waliopo makao makuu.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Jitihada hii ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ina upekee wake kutokana namipango ya ndani, nia thabiti na ari dhahiri ya mabadiliko; mpango wa mabadiliko unaoshirikisha wadau wote wa ukusanyaji wa ushuru katika Halmashauri. Mafanikio ya mabadiliko haya yanatokana na siri zifuatazo;

(i) Matumizi ya utafiti wa kisayansi kufanya maamuzi sahihi. Uamuzi wa namna ya kudai ushuru kutoka Magogo au Mbao ulifanyika kisayansi, ambapo tatizo lilibainishwa, mbinu za kukusanya takwimu zilitumika, takwimu zilizokusanywa zilichambuliwa na matokeo kuonyesha kuwa ushuru wa mbao utaisaidia Halmashauri kujiimarisha katika ukusanyaji wa mapato.

(ii) Ushirikiano wa Idara za Halmashauri. Katika suala la ukusanyaji wa ushuru idara zote zinashiriki kikamilifu kuuendeleza mfumo. Kwa mfano, wakati wakusanya mapato na wahasibu wakikusanya fedha taslimu na kutoa risiti, maafisa maliasili hukagua na kuidhinisha ubora na thamani ya mbao zinazozalishwa na kusafirishwa.

(iii) Uongozi thabiti. Uwezo wa timu ya Menejimenti ya Hamlashauri kubaini tatizo, kuratibu wadau mbalimbali na kusaidia utekelezaji wa mfumo mpya wa ukusanyaji ushuru ni matokeo ya Uongozi thabiti.

(iv) Utelekezaji na Utozaji thabiti wa tozo za adhabu (kati ya 200% hadi 500%). Sheria ndogo ya ushuru ina masharti magumu kwa wakwepaji ushuru na wale wanaowasaidia kukwepa kulipa ushuru. Kwa sababu hii, tozo na adhabu za kukwepa au kudanganya kwenye kulipa ushuru ni za juu sana na ni hatari sana kwani adhabu hizi zinafungamana na kutaifishwa kwa mali (mbao na magari) inayoweza kuleta kufilisika.

(v) Utayari wa Watumishi. Wakusanyaji wote wa mapato wana utayari wa kutosha katika jukumu hili chini ya uongozi thabiti wa Mhasibu wa Mapato ambaye muda wote hufuatilia utekelezaji wa mfumo wa ukusanyaji ushuru.

(vi) Utamaduni wa Kupanda Miti. Watu wa Mufindi wana hamasa binafsi katika kupanda miti kama zao la biashara ambayo huleta uendelevu katika ukusanyaji wa ushuru wa mbao. Ni suala dhahiri kabisa kuona vitalu vya miti karibu na kaya ambavyo vitatumiwa katika mashamba ya familia au

kuuzwa kwa wapandaji wengine wa miti. Picha iliyopo hapa chini inaonyesha kitalu cha miti karibu na mlango mkuu wa nyumba.



***Kitalu cha miti karibu na kaya***

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO

**UBORESHAJI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI**




***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ni mojawapo ya Halmashauri tisa za Mkoa wa Morogoro. Halmashauri nyingine ni Manipaa ya Morogoro, Halmashuri ya Mji wa Ifakara na Halmashauri za Wilaya za Morogoro, Mvomero, Kilosa, Gairo, Malinyi na Ulanga. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 5, Kata 23, na Vijiji 98. Halmashauri ina eneo la 14,918 $Km^2$ ambazo ni sawa 1,491,800 Ha ambazo hutumika kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali 1 hapa chini. Kwa mujibu wa sensa ya 2012, Halmashauri ina watu 407,880 ambao 202,789 ni wanawake na 205,091 ni wanaume. Zaidi ya 80% ya wakazi wa Kilombero hujishughulisha na kilimo. Mazao ya chakula hujumuisha mpunga, mahindi, mihogo, ndizi, kunde, viazi vitamu na karanga. Mazao ya biashara ni pamoja na miwa, kokoa na ufuta. Eneo hili lina fursa kubwa sana ya kilimo cha umwagiliaji katika msimu wa kiangazi kwani kuna vijito na mito mingi. Ufugaji, uvuvi, utunzaji wa nyuki na biashara ndogondogo huchangia katika shughuli kuu za kiuchumi.

**Ramani: H/W ya Kilombero Mkoani Morogoro**




H/W ya Kilombero ina nguvukazi ya kutosha, na ni ya pili kwa idadi kubwa ya kaya kimkoa. Ukuaji wa wastani wa idadi ya watu ni 4% kwa mwaka na hii inatarajiwa kuongezeka kwa kasi kadri watu wanavyohamia kwenye Halmashauri hii kufuata fursa za biashara, kilimo na ufugaji ambavyo vinakuwa kwa kasi. Takriban 93% ya watu hujihusisha na uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula na wachache hujihusisha na ufugaji. Kwa miaka mingi, kilimo kilikuwa kwa ajili ya kuishi tu lakini miaka ya hivi karibuni kumekuwa na badiliko kuelekea kilimo cha kibiashara zaidi, hasa kupitia uzalishaji wa matunda na mboga mboga.

H/W ya Kilombero ina ardhi ya uwanda wa chini ikiwa na vijito 38 vinavopitisha maji mwaka mzima sawa na 60% ya maji yote ya Mkoa wa Morogoro. Hii hufanya Kilombero kuwa eneo bora kwa uzalishaji wa mpunga, ikiwa na 63% za kaya zilikilima mpunga. Halmashauri inapata mvua mara mbili zinazofikia 1,200mm na 1,600mm kwa mwaka. Hali hii husaidia sana kuwepo kwa sekta imara ya uzalishaji wa mpunga katika Halmashauri.

Halmashauri imeanza kutumia fursa zilizopo kwa kuwa na shughuli nyingi zilizopangwa ili kusaidia maendeleo ya sekta ya kilimo, pamoja na maboresho ya barabara, uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji na upanuaji wa mawasiliano. Hata hivyo, mipango hii inakwamishwa na upungufu wa fedha pamoja na kuchelewa kwa fedha toka Serikali Kuu ambayo imepelekea kuchelewa kwa jitihada

mbalimbali au kutekelezwa bila kukamilika. Pamoja na hali hii, Halmashauri ina imani ya kutosha na fursa ya ukuaji wa sekta ya kilimo na hivyo inaendelea kuwekeza.
Mpunga ndilo zao kuu linalolimwa katika Halmashauri kwa ajili ya chakula na biashara. H/W ya Kilombero ni mzalishaji mkubwa wa mpunga ikichangia 4% ya uzalishaji wa mpunga kitaifa ikilinganishwa na H/W ya Kahama ambayo huchangia 8%. Mahindi hulimwa kwa ajili ya chakula tu na kama akiba endapo kutakuwa na mavuno duni ya mpunga au bei ndogo ya soko. Mazao mengine yanayolimwa katika Halmashauri hii ni vitunguu, ndizi, ufuta, alizeti na karanga; uzalishaji ukifanyika kwa mifumo ya umwagiliaji ya kisasa na kiasili.

Mazao yanayolimwa katika eneo moja hutegemea zoni ya ekolojia ingawa mpunga hupatikana katika maeneo yote matatu; (i) zoni ya kaskazini mashariki: kuna udongo wa mfinyanzi na mchanga na mafuriko ya mara kwa mara yanayoleta uhakika katika ardhi hii yenye rutuba; mazao makuu katika zoni hii ni mpunga, mahindi, miwa, viazi vitamu, matunda mbalimbali na mbogamboga. (ii) Zoni ya Kati; Mazao makuu yanayolimwa katika eneo hili ni mpunga, mahindi, mihogo, mbogamboga na matunda (machungwa, maembe na mapapai) (iii) Zoni ya Magharibi: ina ardhi nzuri yenye virutubisho vingi inayofaa kwa mazao kama mahindi, mpunga, ndizi, kokoa, alizeti, ufuta, matunda mbalimbali na mbogamboga.

**Jedwali 1: Matumizi ya Ardhi katika H/W ya Kilombero**

| Matumizi | Eneo (Ha) | Eneo (km$^2$) |
|---|---|---|
| **Ardhi inayofaa kwa kilimo** | 445,896 | **4,458.96** |
| **Eneo linalifaa kwa ufugaji** | 120,000 | **1,200** |
| **Eneo lenye majimaji** | 107,626 | **1,076.26** |
| **Misitu ya Asili** | 125,000 | **1,250** |
| **Eneo Tengefu** | 107,915 | **1,079.15** |
| **Misitu iliyopandwa** | 6,698 | **66.98** |
| **Ardhi inayofaa kwa makazi** | 578,665 | **5,786.65** |
| **Jumla** | **1,491,800** | **14,918** |

## 2.0 TATIZO

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ni maarufu kwa uzalishaji wa mpunga kwa sababu ya sifa zake za ardhi ambayo kwa sehemu kubwa kuna mabonde ya mito. Hata hivyo kwa miaka mingi Halmashauri hii ilishuhudia makusanyo ya chini sana ya mapato yake ya vyanzo vya ndani kutokana na mazao mbalimbali ya kilimo na biashara. Kwa mfano mwaka 2009/10, Halmashauri ilifanikiwa kukusanya shs 886 millioni tu wakati uwezo wake wa juu unazidi bilioni kadhaa. H/W ya Kilombero ilifanya vibaya hivi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa sababu zifuatazo;

(i) Makusanyo duni ya mapato ya ndani kutokana na utekelezaji duni wa sheria ndogo ya mapato, ukwepaji kodi na mfumo mbaya wa ukusanyaji ushuru.

(ii) Kukasimu ukusanyaji wa mapato kwa makampuni na watu binafsi wasio waaminifu.

(iii) Makubaliano hasi, ukosefu wa uaminifu na tabia danganyifu kati ya wakusanyaji wa ushuru wa Halmashauri, wakulima na wafanyabiashara kwa nia ya kujinufaisha wenyewe na kuinyima Halmashauri mapato hayo yenye thamani.

(iv) Uwepo wa wanasiasa wapenda madaraka na wasiokuwa na uelewa waliokuwa wakishawishi walipa ushuru na umma kwa ujumla kutokulipa ushuru na kodi mbalimbali kwa hoja kuwa Halmashauri hupokea fedha za kutosha kutoka Serikali Kuu.

(v) Utegemezi mkuu kwa kilimo cha wakulima wadogo wanaotegemea mvua badala ya kilimo cha mitambo cha mashamba makubwa ulifanya mapato ya Halmashauri kutotabirika. Kwa miaka

yenye upungufu wa mvua au ukame Halmashauri ilikuwa ikipata makusanyo ya chini sana ya ushuru.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuiwezesha Halmashauri kutoa huduma bora kwa wananchi. Mahsusi kabisa, Halmashauri ililenga kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa ushuru kwa kupitia upya sheria ndogo ya ushuru. Halmashauri pia ililenga kujaza nafasi zote zilizokuwa wazi za Watendaji wa Kata (kutoka 15 mwaka 2010/11 hadi 23 mwaka 2012/13) ambao ndio muhimu sana katika ukusanyaji wa ushuru. Halmashauri pia iliweka lengo la kuainisha, kuchambua na kukasimu baadhi ya vyanzo vya mapato ili kuwa na ukusanyaji fanisi (kutoka vyanzo 3 mwaka 2010/11 hadi vyanzo 6 mwaka 2012/13) pamoja na kuainisha vyanzo vipya vya ushuru na kufuatilia vema mchakato mzima wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa. Mwisho, lengo kuu katika kuongeza mapato ya ndani ni kufikia mahitaji, uhuru na uamuzi katika kutoa huduma bila utegemezi halisi kwa Serikali Kuu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kama ilivyoelezwa hapo juu, H/W ya Kilombero ina fursa kubwa itokanayo na uzalishaji wa mpunga na uchakataji wa wake. Baada ya kuitambua fursa hii, Halmashauri iliamua kufanya mashauriano na maamuzi ndani ya Timu ya Menejimenti na Maafisa Watendaji wa Kata juu ya nini kifanyike ili kuboresha utendaji katika ukusanyaji wa ushuru na kuongeza mapato. Kutokana na mashauriano haya ilikubalika kuwa Halmashauri inahitaji kufanya utafiti ili kubaini matatizo, vyanzo vipya, uwezo wa kila chanzo na kutoa mapendekezo kuhusu mbinu bora za kuongeza mapato ya ndani. Utafiti ulifanyika na ulielezea masuala yanayozuia ukusanyaji bora wa ushuru. Utafiti pia uliainisha vyanzo vigumu vya mapato ambavyo vinahitaji mikakati ya pekee, mfano ada za vyoo vya umma, masoko na vituo vya mabasi.

Mkakati mwingine wa pili ulikuwa mapitio ya sheria ndogo ya ukusanyaji wa ushuru ili kutoa tafsiri sahihi ya sheria hii na kuruhusu ukusanyaji wa ushuru siyo tu kutoka kwenye mpunga bali mazao ya mpunga kama mchele bora, mchele wa rangi, chipsi za mchele na molasesi. Mapitio ya sheria ndogo pia yalisaidia Halmashauri kujenga hoja na kurekebisha tozo za ushuru kutoka ukadiriaji kwa tani na kuwa asilimia ya ukubwa wa mzigo wa mpunga na mazao yake yanayosafirishwa nje ya Halmashauri.

Halmashauri pia ilijikita katika kubadili na kuboresha vitabu vya risiti ili kuingiza alama sahii za utambuzi kama vile muhuri wa moto wa Halmashauri, namba za mwendelezo, rangi na uchapaji wa kiasi kamili cha tozo kwa ushuru wa mpunga ambacho ndicho chanzo kikuu cha mapato ya ndani. Mbinu hii huhakikisha kuwa wote wanaohusika na utoaji wa risiti hawapati nafasi ya kutoa risiti za kugushi na danganyifu.

Uanzishaji wa timu ya ukusanyaji wa ushuru chini ya uenyekiti wa Mkurugenzi wa Halmashauri ikiwa na wajumbe 10 (watumishi wa Halmashauri na polisi) ni uamuzi mojawapo mkakati kuelekea kuboresha ukusanyaji ushuru wa Halmashauri. Katika mchakato wa kukusanya ushuru wajumbe wa timu hii hupokezana na hutembelea masaa 24 njia zote za kutokea za Kusini na Kaskazini kuhakikisha kuwa wasafirishaji wote wa mazao ya kilimo wanalipa ushuru kwa ufanisi. Wakiwa katika zamu, hulipwa posho ya kutwa nzima na hupatiwa gari.

Mipango yote hii ilihitaji ujazaji wa nafasi zote muhimu katika ukusanyaji wa mapato. Ajira ya Maafisa Watendaji Kata kujaza nafasi zote ilifanyika. Pia Maafisa Watendaji wa Kata wote walipatiwa pikipiki ili kurahisisha na kuwapa motisha katika ufuatiliaji wa ukusanyaji wa ushuru. Jitihada hii pia ililazimu kuanzishwa kwa mfumo wa motisha ambapo 5-10% ya makusanyo hurudishwa kwa Kata husika ili

kuboresha ukusanyaji wa ushuru kwa kuimarisha ofisi, kununua vitendea kazi, kuwapa motisha Maafisa Watedaji wa Kata na kuwalipa maofisa wa ziada wanaohitajika kwenye ukusanyaji ushuru fanisi. Watumishi hawa wa muda hujumuisha watoa taarifa za siri, wakusanya ushuru, walinzi na wabeba mizigo.

Halmashauri iliweka shabaha za makusanyo ya ushuru kwa kila Kata na kutia saini makubaliano ya utendaji kati ya Mkurugenzi na Watendaji wa kata. Shabaha hizi hufanyiwa mapitio kila mwaka wa fedha. Pia wakuu wa idara, maafisa watendaji wa Kata na madiwani walitembelea H/W za Mbarali, Kahama, Manispaa ya Temeke na Majiji ya Mwanza na Mbeya kujifunza uzoefu wa aina mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa Kodi na Ushuru. Matembezi haya yaliandaliwa kwa mfumo wa safari za mafunzo. Mwisho, Halmashauri ilinunua gari moja (Toyota Land cruiser - hard top) maalum kwa ajili shughuli za ukusanyaji wa ushuru ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa masaa 24 na usimamiaji wa mchakato wa ukusanyaji mapato na vituo vya ukaguzi.



***Wakusanya Ushuru, Gari na Polisi***

**5.0 RASLIMALI**

H/W ya Kilombero ilitumia aina mbalimbali za raslimali kuongeza mapato kwa ukusanyaji bora wa ushuru. Raslimali fedha zilitumika katika gharama za utafiti, mikutano ya kufanya maamuzi, gharama za ajira, posho mbalimbali za watumishi, gharama za mafuta, gharama za safari za mafunzo, manunuzi ya vitabu vipya vya risiti, na manunuzi ya pikipiki 23 kwa ajili ya maafisa watendaji wa Kata, kutaja machache.

Raslimali watu pia zilitumika katika kuongeza ukusanyaji wa ushuru. Hizi zilijumuisha utumiaji wa watumishi kati ya 6 – 10 kutoka idara na vitengo vya fedha, kilimo, maji, maendeleo ya jamii, ushirika, maliasili, polisi na watendaji wote wa kata. Hawa wanaendelea kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa ushuru unatekelezwa kulingana na mipango na makisio.

**6.0 MATOKEO**

Halmashauri imeshuhudia matokeo makuu dhahiri kutokana za jitihada za uboreshaji ukusanyaji wa ushuru. Tokeo kuu la kwanza ni ongezeko la utii katika ulipaji ushuru ambapo walipa ushuru kwa ridhaa yao hufanya malipo katika vituo vya kulipia ushuru. Kwa Halmashauri kuongeza utii katika ulipaji wa kodi ni tukio la kupongeza na la kujifunza kwa Halmashauri nyingine.

Pili, Halmashauri imekuwa ikishuhudia ongezeko la mapato ya ndani mwaka hadi mwaka. Taarifa iliyopo hapa chini inaonyesha mafanikio katika ukusanyaji wa ushuru na kuifanya H/W ya Kilombero moja ya miamba ya ukusanyaji wa mapato ndani katika Halmashauri za Wilaya.

**Mapato ya Ndani ya H/W ya Kilombero**

- ***2009/2010 Tshs. 0.886 Bilioni***
- ***2010/2011 Tshs. 1.8 Bilioni***
- ***2011/2012 Tshs. 2.8 Bilioni***
- ***2012/2013 Tshs. 3.4 Bilioni***

Halmashauri ina sheria ndogo thabiti inayoelezea namna zote za kisheria za ukusanyaji wa ushuru, ikijumuisha viwango, faini na tozo zitakazotumika kwa wakiukaji na wajibu wa wadau mbalimbali. Halmashauri huisimamia sheria hii ndogo kwa ukamilifu bila misamaha ya aina yoyote. Wadau wote wa sheria hii ndogo hutarajiwa kufuata kwa ukamilifu misingi na taratibu zote zilizowekwa.

Halmashauri pia imefanikiwa kufikia badiliko chanya katika uwezo wake wa kusaidia utoaji wa huduma. Jedwali 2 hapa chini linaonyesha idadi ya miradi iliyotekelezwa kwa mapato za ndani. Inashangaza na inastahili kusifiwa kwa Halmashauri kuweza kukamilisha vyumba 93 vya maabara katika mwaka 2014/2015.

**Jedwali 2. Usaidizi wa Halmashauri katika utoaji huduma**

| Mwaka | Kiasi kilichangiwa | Aina ya miradi | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Madarasa | Maabara | Nyumba za watumishi | mgahawa | Barabara | Visima | Vyoo | Soko | Ofisi | Minada | Magari |
| **2010/2011** | 150,000,000.00 | 24 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **2011/2012** | 109,348,769.00 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **2012/2013** | 448,089,182.10 | 22 | 0 | 3 | 0 | 5 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| **2013/2014** | 712,586,261.45 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| **2014/2015** | 1,200,000,000.00 | 2 | 93 | 0 | 0 | 0 | 23 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |

Vijiji vyote 98 vya H/W ya Kilombero hupokea 20% ya mapato ya ndani. 20% hukokotolewa kulingana na mchango wa Kijiji kupitia Ukusanyaji wa ushuru na gharama nyingine za Halmashauri. Hili limewezesha kuwepo kwa Serikali za Vijiji imara zinazoweza kupanga na kutekeleza mipango yao ya maendeleo bila utegemezi uliokithiri kwa Halmashauri. Kwa kutumia fedha hizi Vijiji katika H/W ya Kilombero vimeboresha uwezo wao katika utawala, utekelezaji wa miradi, uwezeshi wa jamii na uwezo wa kuajiri na kuwalipa watumishi bila matatizo.

H/W ya Kilombero imeweza pia kuongeza kwa kiasi kikubwa mchango wake kwa jitihada za jamii na miradi mingine ya maendeleo. Maeneo mahsusi ambapo Halmashauri imechangia sana ni pamoja na ujenzi wa mgahawa makao makuu ya Halmashauri na ujenzi wa nyumba 22 za walimu katika shule za sekondari za Luvikila, Mkusi, Idete Crossing, Kisawasawa, Uga, Lungongole, Ipopoo, Msalise, Kiswanya, Sululu, Chiwachiwa, Lyasenga na Tanganyika. Halmashauri pia imejenga maabara katika shule za sekondari, minada ya kisasa, visima virefu na vifupi vya maji na kununua greda. Angalia gharama na picha za miradi iliyotajwa hapa kwenye kiambatisho Na 1.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero imepata matokeo makuu katika ukusanyaji wa ushuru ingawa kuna uelewa mdogo wa jamii kuhusu ulipaji kodi kwa ujumla, kusita kwa mashirika makubwa kutekeleza sheria ndogo mpya ya ushuru, siasa kuingia katika utendaji bila kutarajiwa, mahusiano duni na TRA, utegemezi kwenye kilimo kinachotumia mvua tu na upungufu wa vifaa vya kukusanyia kodi. Hata hivyo Halmashauri imeweka mikakati ya kuhakikisha uendelevu wa jitihada hii ya ukusanyaji wa ushuru. Mikakati hii ni pamoja na;

*Elimu kwa Umma na Ujenzi wa Uelewa.* Halmashauri inaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa kutumia Madiwani, maafisa maendeleo jamii, maafisa watendaji wa Kata na timu ya ukusanyaji wa ushuru. Zoezi hili ni la kudumu kwani jamii ya wakulima hupokea wageni kila mwaka ambao huhitaji kuhamasishwa kuhusu taratibu za ulipaji ushuru. Ni muhimu kutambua kuwa uzalishaji wa mpunga katika H/W ya Kilombero huvutia vijana wengi kutoka maeneo mengi ya Tanzania.

*Kuainisha Vyanzo Vipya vya Mapato.* Halmashauri inaendelea kuainisha vyanzo vipya vya mapato ya ndani kwa kuzingatia shughuli za kiuchumi za jamii na maliasili. Halmashauri bado haijafikia kiwango chake cha juu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Hivyo, kila robo mwaka kuna taarifa zinazowasilishwa katika Baraza la Madiwani zinazopendekeza vyanzo vipya na vyenye mapato zaidi. Lengo la uanishaji wa vyanzo vya mapato usiokoma ni kukusanya mapato zaidi, kutoa huduma bora kwa walipa kodi na kujipatia uhuru kutoka kwenye utegemezi wa Serikali Kuu.

*Kuendeleza na kuboresha Miundombinu.* Utayari wa watu katika kulipa kodi hutegemea imani waliyonayo kwa Serikali. Serikali inapoboresha huduma na miundombinu watu hujenga imani na hiari ya kulipa kodi huongezeka. Kinyume chake pia ni ukweli. Kwa sababu hii Halmashauri itaendelea kujikita katika ujenzi wa minada, masoko, vituo vya mabasi, vyoo vya umma na maduka ambavyo kwa ujumla huwa ni vituo vya kukusanya ushuru, kodi na ada.

*Kupandisha Mji Mdogo wa Ifakara Kuwa Halmashauri kamilifu ya Mji.* H/W ya Kilombero imeshaomba rasmi kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara ambapo Halmashauri itapata sifa ya kukusanya kodi ya majengo. Mji mdogo wa Ifakara una majengo makubwa na yenye thamani kubwa lakini kwa sababu yapo kwenye mamlaka ya Halmashauri za Wilaya majengo haya hayawezi kufanyiwa uthamini na kulazimika kulipa kodi ya majengo. Kuipandisha hadhi Halmashauri kutaongeza mapato zaidi ya ndani kutoka kwenye kodi ya majengo. Wakati kitabu hiki kinachapwa mkakati huu ulikuwa umekamilika kwani Halmashauri ya Mji wa Ifakara tayari imeshaanzishwa.

*Kuongeza Skimu za Umwagiliaji.* Ili Kuongeza mapato zaidi kutoka mazao ya kilimo panahitajika jitihada za kufanya kilimo cha mpunga kuwa cha uhakika na cha kutabirika. Hili linawezekana tu kwa kutumia aina mbalimbali za vyanzo vya maji kwa ajili ya skimu za umwagiliaji. H/W ya Kilombero imeanzisha na kuendeleza skimu za umwagiliaji za Vijiji vya Njagi, Siginali, Mkula and Msolwa.

*Kuhamasisha Kilimo cha Mashamba Makubwa.* H/W ya Kilombero imekuwa ikihamasisha kilimo cha mashamba makubwa kwa kuwakaribisha wawekezaji na makampuni makubwa kuwekeza katika kilimo cha mashamba makubwa ya mpunga kinachotumia mitambo. Halmashauri ina chapisho linalotangaza uwezo wa raslimali zilizopo za uzalishaji wa mpunga na mazao mengine. Kwa sasa kuna makampuni makubwa mawili yanayozalisha mpunga, kuchakata na kufungasha mchele; makampuni haya ni KPL na Ndamila Schemes.



*Mfreji wa umagililiaji Siginali*



*KPL, Umwagiliaji wa kisasa*



*KPL, kiwanda cha mchele*

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**


H/W ya Kilombero imefanya maajabu katika ukusanyaji wa ushuru kwa sababu ya siri mbalimbali. Siri moja kuu ni timu imara inayoshirikisha uongozi wa juu wa Halmashauri, watendaji wa Kata, na Madiwani. Ile hali ya umoja wa timu katika Halmashauri hii ipo kwa kila ofisa kuanzia juu mpaka chini. Kwa mfano katika ukusanyaji wa mapato wakuu wa idara, watendaji wa Kata na watendaji wa Vijiji wana uelewa unaofanana wa makisio ya ukusanyaji kutoka kila Kata au Kijiji na matarajio ya vikwazo kwa kila mwezi. Siri hii imekaziwa na ukweli kuwa Halmashauri hutumia wakusanya mapato wa ndani na siyo kukasimu ukusanyaji kwa makampuni binafsi.

Siri nyingine muhimu ya pili ni Halmashauri kuzingatia motisha kwa watumishi. Kinadharia inafahamika kuwa watumishi huzalisha nguvu na hiari zaidi kwa kazi pale wanapokuwa na motisha. Timu ya menejimenti ya Halmashauri hutumia nadharia hii kupata utendaji bora toka kwa watumishi. Watumishi wanaoshiriki ukusanyaji wa ushuru hupewa motisha kupitia posho mbalimbali, zawadi na mafao mengine. Kwa upande wao, watumishi hutumia utaalamu na nguvu zao katika kukusanya ushuru bila kujihusisha na vitendo vinavyoweza kuinyima Halmashauri mapato.

Tatu, Bonde la Mto Kilombero hutoa fursa ya kudumu kwa Halmashauri kujipatia Mapato. Halmashauri imeunda ushirika imara na wakulima katika kuendeleza miundombinu ili kuboresha uzalishaji na usafirishaji na hivyo kukusanya ushuru zaidi. Wakulima kwa upande wao ni wenye bidi katika kazi na wanaongezeka kila mwaka. Ushikiano huu na kama unavyoboreshwa kupitia uhamasishaji wa jamii kuhusu ulipaji wa ushuru; Halmashauri kwa sasa inafaidika na utayari katika ulipaji wa kodi unaotokana na utoaji huduma ulioboreshwa ambao chanzo chake ni kuongezeka kwa makusanyo.


Mwisho, kutokana na asili na jiografia ya Halmashauri, mazao yote husafirishwa kupitia barabara kuu moja tu ambayo ina matoleo ya Kaskazini na Kusini. Hakuna matoleo mengine ya barabara. Hii husaidia Halmashauri kuyapata magari na malori yote yanayosafirisha mazao kwenda nje ya Halmashauri na kukusanya ushuru; na kuondoa uwezekano wowote wa kukwepa vituo vya ukaguzi vya Halmashauri kwa kupitia barabara na njia zisizo rasmi kama inavyotokea katika Halmashauri nyingine hapa Tanzania.


## Kiambatisho 1:  Michango ya Halmashauri kwa Miradi kutoka mapato ya ndani

| S/N | Mradi | Sekta | Kipindi cha utekelezaji | Mchango (shs) | Picha ya Mradi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Mgahawa makao makuu ya Halmashauri | Utawala | 2011/12-2012/13 | 94,568,719.00 |  |
| 2. | Ujenzi wa nyumba 22 za walimu katika sekondari za Luvikila, Mkusi, Idete Crossing, Kisawasawa, Uga, Lungongole, Ipopoo, Msalise, Kiswanya, Sululu, Chiwachiwa, Lyasenga na Tanganyika | Elimu ya Sekondari | 2010/11-2012/13 | 129,000,000.00 |  |
| 3. | Ujenzi wa maabara | Elimu ya Sekondari | 2014/2015 | 464,000,000.00 |  |
| 4. | Ujenzi wa minada | Mifugo | 2013/2014-2015/2016 | 94,772,890.82 | |
| 5. | Ujenzi wa visima vya maji | Maji | 2014-2015 | 50,000,000.00 |  |
| 6. | Manunuzi ya greda | Ujenzi | 2014-2015 | 730,000,000.00 |  |

# HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE

**UBUNIFU KATIKA MAPATO YA NDANI ILI KUBORESHA UTOAJI HUDUMA**



**PART I: EXECUTIVE VALUATION SUMMARY AND CERTIFICATION**

Taking into account the type, size, location and condition of the property under reference, we are of the opinion that the **Rateable value** of the Properties in Korogwe Town Council as described in this report are as follows:

| S/N | AREAS | TOTAL RATEABLE VALUE | PROPERTY TAX ASSESED |
|---|---|---|---|
| 1 | OLD KOROGWE | 4,711,981,900.00 | 4,731,470.50 |
| 2 | KWAMKOLE | 4,273,156,120.00 | 4,273,156.12 |
| 3 | MTONGA | 15,452,819,990.00 | 15,460,541.83 |
| 4 | KWASEMANGUBE | 9,751,303,800.00 | 9,759,684.80 |
| 5 | MASUGURU | 4,835,318,009.00 | 4,836,143.61 |
| 6 | KILOLE | 5,608,016,650.00 | 5,872,028.05 |
| 7 | MANUNDU | 65,149,742,731.00 | 68,660,146.69 |
| 8 | SPECIAL | 7,190,812,200.00 | 8,083,414.04 |
| | **GRAND TOTAL** | **116,973,151,400.00** | **121,676,585.64** |
| | **SAY** | **117,000,000,000.00** | **122,000,000.00** |

**CERTIFICATION**

This valuation report has been prepared for **KOROGWE TOWN COUNCIL** for the purpose aforesaid. It is hereby certified on behalf of **PROLATY CONSULT LTD**

**PREPARED BY:**

**SYLVESTER ABEL KWIYEGA**
BSC. Land Man. & Valuation (ARU)

**Certified By:**

**EWARD M. ATHANAS**
BSC. Land Man. & Valuation (ARU)
F.I.S.T., F.R.S. (T) F.T.I.V.E.A. **FULLY REGISTERED & LICENCED VALUATION SURVEYOR NO 385**

*Uzoefu wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Mji wa Korogwe ilianzishwa mwaka 1984. Halmashauri hii ni mojawapo ya Halmashauri 11 za mkoa wa Tanga. Halmashauri nyingine ni Muheza, Handeni, Pangani, Lushoto, Korogwe, Mkinga, Kilindi, Bumbuli, Mji wa Handeni na Jiji la Tanga. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, idadi ya watu ni 68,303. Shughuli za kiuchumi katika mji wa Korogwe ni kilimo (mpunga, mahindi, maharagwe na katani), viwanda vidogovidogo na ufugaji. Halmashauri ya Mji wa Korogwe ina Kata 8 ambazo ni Manundu, Mgombezi, Kwamndolwa, Magunga, Kwamsisi, Kilole, Old Korogwe and Mtonga Msambiazi, Mitaa 17 na Vijiji 7.

Mji wa Korogwe ni wa pili kwa ukubwa wa miji baada ya Jiji la Tanga. Halmashauri ina eneo la $212Km^2$ ambalo ndilo eneo dogo kabisa kati ya Halmashauri 11 mkoani. Halmashauri hii imeunganishwa vizuri na maeneo mengine ya Mkoa wa Tanga, mikoa ya kaskazini ya Kilimanjaro na Arusha, na Dar es salaam kwa upande wa Kusini. Jiji la Tanga lipo takribani 93 Km, Arusha 344 Km na Dar es Salaam 305 Km. Jiografia ya mji wa Korogwe hurahisisha uhamaji kutoka vijijini kuja mjini wa makundi mbalimbali ya watu hasa vijana watafutao ajira na masoko kwa bidhaa za kilimo na nyinginezo. Hali hii imeleta ongezeko la shughuli za kiuchumi zisizo rasmi katika Mji wa Korogwe.

**2.0 TATIZO**

Halmashauri ya Mji wa Korogwe ilianzishwa baada ya kugawanyika kwa Halamashauri ya Wilaya ya Korogwe. Halmashauri hii ilianzishwa kutokana na ongezeko la watu, kuimarika kwa miundombino, kuongezeka kwa sekta ya viwanda na maboresho katika huduma za kiuchumi na kijamii. Tangu kuanzishwa kwake, Halmashauri hii imekuwa ikikumbana na changamoto nyingi katika utoaji wa huduma kwa wananchi kutokana na makusanyo ya chini sana ya mapato kutoka katika vyanzo vya ndani. Changamoto hizi zilijumuisha upungufu wa nafasi za ofisi na vyombo vya usafiri, upungufu wa viwanja ambavyo vimepimwa kwa matumizi ya makazi, taasisi na viwanda, uhaba wa vifaa vya kukusanyia taka, upungufu wa madarasa, maabara, nyumba za walimu na upungufu wa raslimali za kuendesha shuguli za kawaida za Halmashauri. Haya yote yalileta pengo kubwa katika utoaji wa huduma kwani yote yanahitaji fedha za kutosha. Uwezo wa Halmashauri kukusanya mapato kutoka vyanzo vyake ili kujaza mapengo katika utoaji wa huduma uliendelea kuwa chini. Hili lilileta misuguano ya mara kwa mara kati ya Halmashauri na wananchi wa Korogwe Mjini. Utoaji duni wa huduma wa Serikali za Mitaa mara nyingi hufanya watu kutoridhirika na huendana na uzito katika kulipa kodi na ushiriki wa jamii katika jitihada za maendeleo. Kwa ujumla hali hii hutengeneza duara linalojidhihirisha katika ukusanyaji wa chini wa mapato, uwezo mdogo wa kutoa huduma na kasi hafifu ya kuleta maendeleo kwa wananchi.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu lilikuwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia vyanzo ambavyo havijazoeleka; kwa kupima na kuuza viwanja. Lengo tarajiwa la jitihada hii likiwa kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Malengo mahsusi ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe kujikita katika uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato yalikuwa;

(i) Kupima ardhi na kuuza viwanja kwa ajili makazi, starehe, biashara na viwanda kwa wakazi wa Korogwe. Uuzaji huu ungeongeza idadi ya majengo ambayo yamethaminiwa na kuleta chanzo cha uhakika cha mapato kupitia kodi ya majengo.

(ii) Kuainisha majengo yote mjini, kuendesha zoezi la uthamini, kuamua kiasi cha kodi kwa kila jengo na kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa kukusanya kodi ya majengo.

(iii) Kuwashirikisha wananchi katika utoaji wa huduma hasa katika ukusanyaji taka ngumu kwenye maeneo ambayo huzalisha taka ngumu kwa tani nyingi kwa siku kama maeneo ya sokoni na stendi kuu.

(iv) Kuimarisha uwezo wa Halmashauri kuchangia katika uboreshaji wa huduma kwa kujenga ofisi za kisasa, maabara, minada, madarasa na nyumba za watumishi.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Upimaji wa ardhi ni sanaa na sayansi ya kuanzisha na kuainisha kona, mistari, mipaka na picha za ardhi, zilizochapwa kwenye makaratasi, ushahidi wa kihistoria na viwango vilivyopo vya utekelezaji. Upimaji wa ardhi pia hujumuisha huduma shirikishi kama mchanganuo na matumizi ya takwimu za upimaji, upangaji na uchoraji wa vitalu, uandishi wa maelezo ya kisheria, uchoraji wa ramani, michoro ya ujenzi na vipimo sahihi vya pembe, urefu, eneo na ujazo. Ili kuongeza mapato ya ndani, mwaka 2013, Halmashauri kupitia idara ya ardhi iliamua kupima, kutenga na kuuza viwanja kwa ajili makazi, vituo vya biashara, taasisi na viwanda. Ili kufikia malengo mikakati ifuatayo ilitekelezwa;

(i) Kutafuta na kuainisha eneo la ardhi ili kupima viwanja. Halmashauri iliunda kikosi kazi ambacho kilikabidhiwa jukumu la kutafuta na kuanisha eneo la ardhi ili kupima viwanja. Kikosi kazi hiki kilipata eneo ambalo lilikuwa halitumiki kikamilifu na lililokuwa linamilikiwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Halmashauri iliingia kwenye makubaliano na Wizara ambapo Wizara iliombwa kuhamisha mnada wa wanayama na kupewa eneo lingine kwa ajili ya shughuli za mnada wa wanyama. Shughuli za mnada zilihamishiwa eneo la Mgombezi ambapo miundombinu mipya na ya kisasa ya mnada ilijengwa.

(ii) Kuandaa andiko la Mradi. Idara ya Ardhi iliandaa andiko la mradi na kuweka pendekezo la kutafuta mkopo wa jumla ya shs 333, 000,000/=. Fedha hizi zingetumika kwenye upimaji wa ardhi. Halmashauri haikuwa na kiasi hiki cha fedha ilibidi mbinu nyingine ya utekelezaji iamuliwe na timu ya menejimenti ya Halmashauri na Baraza la Madiwani. Pendekezo lilipelekwa kwenye baraza kupata kibali cha utekelezaji wa mradi kwa mfumo wa mkopo. Ilikubaliwa pia kuwa mshirika au kampuni ya kibiashara itafutwe ambayo itaweza kupima ardhi kwa kutumia fedha na wataalam wake na alipwe kipindi cha uuzaji halisi wa viwanja vilivyopimwa. Halmashauri iliridhia utaratibu huu na kuruhusu idara ya Ardhi kuanza ushawishi na washirika mbalimbali.

(iii) Majadiliano yalifanyika na kukubalika kuwa Chuo cha Ardhi Morogoro kipime ardhi iliyotengwa, kiainishe viwanja na kijenge barabara za mitaa kwa makubaliano kuwa gharama zote zitalipwa baada ya kuuza viwanja vilivyopimwa. Zoezi la upimaji viwanja lilichukua miezi 3 na kuzalisha jumla ya viwanja 1,532 vilivyopimwa.

(iv) Ukadiriaji wa gharama na Uuuzaji wa viwanja. Zoezi la kuuza viwanja lilianza kwa kukadiria gharama za viwanja kwa kuzingatia ukubwa, matumizi ya kiwanja na mahali kilipo au kinapotazama. Bei ilianzia shs 1,500/= hadi shs 2,500/= kwa meta za mraba. Hivyo pato tarajiwa kutokana na uuzaji wa viwanja vyote lilikuwa shs 3.3 billioni. Wakati kitabu hiki kinaandikwa viwanja 662 vilikuwa vimeshauzwa na Halmashauri ilikuwa imekusanya shs 1.3 bilioni. Uuzaji wa viwanja vilivyobaki ulikuwa unaendelea.

(v) Utoaji wa hati za Umiliki. Wanachi walionunua viwanja vilivypimwa walipewa hati za umiliki na kuruhusiwa kuendeleza viwanja. Uendelezaji wa viwanja hufanywa baada ya eneo kupangwa, michoro kuandaliwa na mifano ya jengo kupitishwa na Halmashauri na kutolewa kwa kibali cha ujenzi. Hili linalenga kuhakikisha kwamba majengo yanayojengwa katika eneo hili jipya lenye viwanja vilivyopimwa yanaunda mji uliopangwa vizuri kulingana na barabara, miundombinu ya umeme na maji na uhakika wa usafi wa mji siku za mbele.

(vi) Kupanga na kuandaa bajeti ya kutumia fedha zitokanazo na uuzaji wa viwanja vilivyopimwa. Halmashauri iliandaa mpango na kuidhinisha matumizi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya idara ya Ardhi, kufanya uthamini wa majengo yote ndani ya Halmashauri na kuwa na ripoti ya uthamini, manunuzi ya magari 2, manunuzi ya trekta za kusafirishia taka, ujenzi wa

madarasa na maabara, ujenzi wa miundombinu ya mnada wa wanyama, kulipa madeni ya Halmashauri na kulipa ada za shule za wanafunzi walio katika mazingira magumu.

**Jedwali 1: Baadhi ya Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Uuzaji viwanja**

| SN | Maelezo | Kiasi Tshs. |
|---|---|---|
| 1 | Kurejesha madeni na kulipa ada ya kupima viwanja (Chuo Cha Ardhi Morogoro) | 330,000,000 |
| 2 | Ujenzi wa miundombinu yam nada wa wanyama | 79,842,000 |
| 3 | Ujenzi wa jengo la ofisi ya idara ya ardhi | 153,782,096 |
| 4 | Ujenzi wa madarasa 9 shule za msingi | 99,000,000 |
| 5 | Michango kwa miradi ya maendeleo kama Maabara katika shule za sekondari | 192,582,958 |
| 6 | Manunuzi ya magari Mawili kwa ajili ya idara ya ardhi na Mkurugenzi | 205,000,000 |
| 7 | Zoezi la uthamini wa majengo 5,500 | 192,000,000 |
| 8 | Kulipa madeni kwa watumishi na watoa huduma | 50,000,000 |

## 5.0 RASLIMALI

Shughuli hii ya kuongeza mapato kupitia kupima na kuuza viwanja ni ya aina ya kipekee ambayo Halmashauri mpya za miji zilizoanzishwa zinaweza kuchukua kama somo na kutekeleza katika mazingira yao. Raslimali kuu katika shughuli hii ni raslimali watu kwa kuzingatia sifa na stadi zao hasa ubunifu na ugunduzi wa wajumbe wa timu ya menejimenti ya Halmashauri. Hii ilihusisha kudhihirisha fikra kwa matokeo halisi kwa kutumia vizuri fursa zilizopo. Mahsusi kabisa katika shughuli hii ni hili la idara ya Ardhi kubuni mradi, kuutetea mbele ya timu ya menejimenti ya Halmashauri na Baraza la Madiwani, kutafuta kampuni ya kutekeleza mradi kwa mkopo na kusimamia mchakato wa upimaji wa viwanja pamoja na uuzaji wake. Halmashauri pia ilitumia fedha kadhaa kwa kulipa posho na gharama za mafuta. Chuo cha Ardhi Morogoro kilichopima viwanja kilipokea shs 300 milioni baada ya Halmashauri kuanza kuuza viwanja.

## 6.0 MATOKEO

Halmashauri ya Mji wa Korogwe imepata mafanikio mengi kutokana na mbinu hii jumuishi ya kuongeza mapato. Tokeo kuu muhimu ni uwepo wa viwanja vilivyopimwa 1,532 vikiwa na barabara za mitaa na maeneo ya wazi ya umma. Uuzaji na utumiaji wa viwanja kwa ajili ujenzi vitazuia mji wa Korogwe kuingia katika ongezeko la makazi duni ambayo huambatana na changamoto katika utoaji wa huduma za kiafya, usambazaji wa maji na umeme. Kimkakati kabisa Halmashauri ya Mji wa Korogwe imeazimia kuzuia ongezeko la makazi yasiyopangwa kupitia jitihada hii.

Wakati wa uhakiki wa mbinu hii Halmashauri ilikuwa imeuza viwanja 662 na kupata shs 1.3 bilioni. Hili lilikuwa tokeo kuu. Halmashauri ilitumia fedha zilizopatikana kukilipa chuo cha Ardhi Morogoro jumla ya shs 300 milioni gharama za upimaji wa ardhi. Fedha zilizobaki zilitumika kujenga ofisi za idara ya Ardhi, kuboresha huduma za taka ngumu, kununua magari na kuchangia ujenzi wa maabara na madarasa. Jengo la idara ya ardhi limechukua idara nyingine pia kama TASAF na Elimu. Picha zilizopo hapa chini zinaonyesha jengo na magari ambayo yalinunuliwa kwa fedha zilizopatikana kwa kuuza viwanja vilivyopimwa.



Jengo la Idara ya Ardhi





Gari la Mkurugenzi




Gari la idara ya Ardhi

Halmashauri pia ilitumia fedha zilizopatina kwenye uuzaji wa viwanja kuendesha zoezi la uthamini wa majengo mjini. Kitabu cha taarifa za uthamini kipo na kimesaidia sana ukusanyaji wa kodi. Halmashauri imeanza kukusanya kodi ya majengo kulingana na tozo zilizochanganuliwa kuanzia 0.01% mpaka 0.02% na makisio ya kodi ya majengo kwa mwaka ni shs 124,000,000/=. Chanzo hiki cha mapato ni cha uhakika sana kwa sababu majengo huendelea kupanda thamani na hayahamishiki. Makisio yanaonyesha kuwa mapato yatakayopatikana baada ya kukamilika kwa uthamini ni mara tatu ya kiasi ambacho Halmashauri ilikuwa inakusanya kabla ya uthamini. Ukusanyaji wa kodi ya majengo ulitumia tozo ya aina moja.




***Kitabu cha Taarifa ya Uthamini***

Halmashauri imetumia fedha zilizopatikana kweye uuzaji wa viwanja kuboresha huduma za elimu. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Serikali Kuu iliagiza Halmashauri zote kujenga na kukamilisha majengo kwa ajili ya maabara katika shule zote za sekondari ambazo zipo katika Kata zote. Halmashauri ya Mji wa Korogwe haikupata ugumu katika ujenzi wa maabara kama ilivyokuwa katika Halmashauri nyingine. Fedha zilikuwepo tayari kutokana na jitihada hii. Halmashauri pia ilijenga na kukarabati madarasa na vyoo katika shule za msingi na sekondari.



***Madarasa ya zamani na mapya S/M Kwangumi***



***Madarasa ya zamani na mapya S/M Kitopeni***

Kama ilivyotajwa hapo juu ardhi iliyotumiwa na Halmashauri kuanzisha viwanja vilivyopimwa ilimilikiwa na wizara ya kilimo na ilikuwa ikitumika kwa shughuli za minada. Halmashauri ilitumia fedha zilizopatikana kwa uuzaji wa viwanja kuhamisha mnada wa wanyama kama fidia ya eneo lililopimwa. Halmashauri imejenga miundombino ya mnada mipya na ya kisasa katika eneo la Mgombezi.



***Miundombino Mipya na ya Kisasa ya Mnada***

Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato uliitia motisha Halmashauri ya kuainisha wanafunzi wote watokao katika mazingira magumu katika kaya ambazo zina matatizo ya kulipa ada za shule ili kuwalipia na kununua mahitaji muhimu ya shule kama vitabu na sare. Orodha hii pia ilijumuisha wanafunzi wenye ulemavu waliokuwa katika familia maskini. Halmashauri ilianzinsha mpango wa usaidizi wa wanafunzi hawa kwa kutumia fedha zilizotokana na uuzaji wa viwanja vilivyopimwa.

Kuimarika kwa mapato ya Halmashauri kutokana na uuzaji wa viwanja na matokeo ya zoezi la uthamini wa majengo viliongeza uwezo wa Halmashauri ya mji kulipa madeni mbalimbali. Halmashauri ilikuwa na madeni mengi kwa watumishi, hasa walimu ambao walikuwa hawajalipwa posho za likizo na uhamisho na wakadarasi ambao walikuwa wametoa huduma mbalimbali kwa Halmashauri. Kwa kutumia fedha zilizotokana na jitihada hii; wakati mbinu hii inaandikwa Halmashauri ilikuwa imelipa zaidi ya nusu ya madeni.

Halmashauri ya Mji iliboresha na kupanga upya mfumo wa ukusanyaji taka ngumu. Kumaliza kabisa tatizo la ukusanyaji wa taka ngumu, Halmashauri iliamua kutumia asasi za kijamii (CBOs) zilizopo mjini. Mkutano wa pamoja kuhusu ukusanyaji na uteketezaji wa taka uliitishwa kati ya Halmashuri na Maafisa watendaji wa Kata, Maafisa watendaji wa Mitaa na wenyeviti wa Mitaa. Ilikubalika kuwa viongozi wa Mitaa wawajibike katika ukusanyaji wa taka. Asasi za kijamii (CBOs) zilihamasishwa kuhusu ukusanyaji wa taka ngumu na mbinu za ushirikishwaji katika ukusanyaji na uteketezaji. Watumiaji wa mfumo waligawanywa katika makundi mbalimbali (makazi, taasisi, maeneo ya biashara) na ada za kukusanya taka ziliainishwa kulingana na sheria ndogo ya ukusanyaji taka ya Halmashauri. Halmashauri, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilinunua trekta la tani 3 na tela kwa ajili ya kusafirisha na kutupa taka ngumu. Asasi za kijamii (CBOs) zilipatiwa jukumu la kukusanya ada za ukusanyaji, usimamizi na usafirishaji wa taka kwenda kwenye dampo, kulipa mafuta na vibarua wa trekta na kuwashughulikia wavunja sheria ndogo. Usimamizi wa ukusanyaji wa taka ngumu umegatuliwa kwenda kwa jamii kwa kutumia asasi za kijamii (CBOs) na kufanya Halmashauri ya Mji wa Korogwe kuwa ya Kipekee. Fedha za maboresho haya ya mfumo wa ukusanyaji taka ngumu zilitokana na uuzaji wa viwanja vilivyopimwa.




***Trekta la ukusanyaji taka na Dampo***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Jitihada nyingi katika ukusanyaji wa mapato huleta matokeo yasiyodumu kutokana na upangaji duni kwa ajili ya uendelevu. Hata hivyo, Halmashauri ya Mji wa Korogwe imeweka mikakati mbalimbali kuhakikisha kuwa jitihada hii inaleta mabadiliko na maboresho ya kudumu katika ukusanyaji wa mapato. Mikakati hii imeelezewa hapa chini.

(i) Ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi yenye ofisi za kisasa za kukatia tiketi, maduka, na gereji na kuzikodisha. Mradi huu unakaribia kutekelezwa na lengo ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ya uhakika na ya kudumu.

(ii) Ujenzi wa kituo cha Kisasa cha Biashara ambacho kitakuwa na maduka makubwa, maduka ya kawaida, maduka ya kipekee, migahawa, maeneo ya kukusanyia taka, vyoo vya umma na bustani.

(iii) Ukusanyaji wa mapato kutoka eneo la mnada wa wanyama na eneo la masubirio lililopo Mgombezi. Ardhi inayozunguka eneo hili pia itaendelezwa ili kuwepo na maduka na vibanda ambavyo vitakodishwa kwa wafanya biashara wadogo na kuongeza chanzo kingine cha mapato.

(iv) Kufanya Uthamini endelevu wa majengo mapya ili kuimarisha ukusanyaji wa kodi. Halmashauri imejizatiti kufanya uthamini wa majengo mara kwa mara ili kuyatambua majengo mapya na kuendana na kasi ya ukuaji wa mji wa Korogwe. Ukuaji wa mji unaenda kwa kasi sana kwani Korogwe mjini ndio kituo cha jamii za kilimo za Halmashauri za Wilaya za Korogwe, Lushoto, Handeni, Muheza na Mkinga.

(v) Kulipa fidia kwa wamiliki wa ardhi na kupima viwanja zaidi kwa kutumia mapato ya ndani. Wakati mbinu hii inaandikwa zoezi la kupima viwanja zaidi ya 100 kwa malengo ya biashara lilikuwa limeanza. Halmashauri imedhamiria kuondoa ongezeko na kuzaliana kwa makazi yasiyopangwa katika mji wa Korogwe kwa kuwa mbele katika upangaji wa matumizi ya ardhi, upimaji na uuzaji wa viwanja vilivyopimwa.

(vi) Kuvutia Wawekezaji na waendeleza ardhi. Halmashauri imefanya matangazo mengi kupitia vyombo vya habari vya umma na vya jamii kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo pamoja na uwepo wa viwanja vilivyopimwa. Halmashauri imeanza kupata majibu chanya kutoka wawekezaji mbalimbali binafsi na wa umma. Kwa mfano shirika la nyumba la taifa (NHC) limemiliki viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi.

(vii) Kuendelea kuainisha vyanzo vipya vya mapato ili kupanua wigo wa kodi. Halmashauri imejiandaa kufanya utafiti wa kina katika fursa mbalimbali zilizopo ili kuongeza mapato kutoka katika sekta za kilimo, biashara, maduka ya jumla na Viwanda.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mafanikio yaliyofanywa na Halmashauri ya Mji wa Korogwe yana sababu zake katika siri zifuatazo ambazo zilisaidia utekelezaji wa upimaji wa viwanja. Siri hizi ni pamoja na;

- Ubadilishaji thabiti wa fikra na kuleta uhalisia. Ugunduzi na ubunifu nchini Tanzania kwa ujumla mara nyingi hausifiwi sana. Uwazi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe kuheshimu na kutumia fikra mpya, ugunduzi na ubunifu ni siri kubwa katika kuwezesha kupima ardhi na kufanya uthamini wa majengo; lengo likiwa kuongeza uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kujipatia uhuru zaidi kutoka kwenye utegemezi wa fedha za Serikali Kuu.
- Mfumo wa Uongozi unaongozwa na Matokeo wa Mkurugenzi wa Halmashauri. Menejimenti na Uongozi huwa na nafasi muhimu katika kufikia malengo ya taasisi. Matumizi ya fikra mpya katika mbinu hii yaliwezekana kutokana na sifa za Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye ni mahiri katika kushirikisha watumishi kwenye ufanyaji wa maamuzi, kuongoza kwa mifano na kuwasimamia watumishi kutoa matokeo dhahiri. Sifa hizi ziliwezesha mafanikio ya mbinu hii.
- Matumizi bora ya Utaalam. Watumishi katika idara ya Ardhi na Timu ya Menejimenti kwa ujumla walijipanga kitaalamu zaidi ili kufanikisha mradi. Uandaaji wa andiko la kitaalam la mradi, utafutaji wa kampuni ya kutekeleza mradi kwa mkopo na usimamizi wa kuhakikisha matokeo ya mradi; zote ni hatua za kitaalam ambazo zinahitaji utaalamu.
- Mahusiano bora kati ya taasisi za Serikali. Mafanikio ya mradi huu pia yalitokana na utendaji bora wa pamoja wa taasisi mbalimbali za serikali zinazojumuisha Halmashauri, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi na Chuo cha Ardhi Mororogoro.

# Sura ya Tatu: Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma

Utoaji huduma ni jukumu muhimu katika mahusiano ya taasisi za serikali na wananchi. Huduma ni mfumo au mpangilio unaokidhi mahitaji ya jamii. Helmsing (1995) anaeleza kuwa utoaji wa huduma ni uamuzi wa lazima unaofanywa na maafisa wa kuchaguliwa au kuajiriwa kutumikia au kutoa bidhaa na huduma kwa wapokeaji. Utoaji wa huduma ni wa namna ya mtazamo na mwelekeo, ukihusisha sifa na desturi za kimataifa.

Utoaji huduma ni mchakato endelevu na unaojirudia wa kupanga na kutoa huduma zinazozingatia mpokea huduma. Huhusu ushiriki wa mpokea huduma katika kuainisha wapokea huduma na kutambua mahitaji yao. Utoaji wa huduma pia unahitaji mchakato wa kubuni na kupanga huduma kati watumiaji, watoaji, wasambazaji na washirika katika kuanzisha, kubuni na kupanga huduma na kuhakikisha mahitaji ya watumiaji wa huduma yanafikiwa. Hatimaye utoaji wa huduma unahusu uzalishaji, usambazaji na uwasilishaji wa huduma ambazo zinakidhi lengo na zinafaa kwa mahitaji ya watumiaji. Katika utoaji wa huduma muda wote panahitajika mfumo wa ufuatiliaji na uboreshaji wa kukusanya maoni ya watumiaji na vipimo vya utendaji ili kuwezesha ufuatiliaji na uboreshaji wa bidhaa na huduma wa mara kwa mara.

Utoaji wa huduma ni shughuli ya msingi ya Serikali. Serikali huwepo, pamoja na sababu nyingine, kwa sababu ndio chombo pekee kinachoweza kutoa kwa usahihi maelekezo kuhusu huduma muhimu kama usalama wa raia, ulinzi, miundombinu, usimamizi na ukarabati wa barabara na kadhalika. Ulazima na Umuhimu wa masuala haya huleta uhalali katika shughuli za Serikali. Imewekwa katika katiba na mikataba ya kimataifa kwamba serikali inawajibika na huduma za msingi katika maeneo mengi ya kijamii ambayo ni pamoja na elimu, hifadhi ya jamii, mahitaji ya msingi, ulinzi wa kisheria na makazi. Serikali lazima iwapatie wananchi uhakika wa kuendeleza utoaji huduma; kupatikana huduma kwa wote bila kujali tofauti za kijamii na kiutamaduni na kwa bei zinazofaa. Hili lina matokeo kwa taasisi za Serikali. Uwazi, ufanisi, upatikanaji na mambo mengine, huleta ubora katika bidhaa zitolewazo na Serikali kama huduma kwa wananchi wake.

Kwa wananchi wengi, Serikali yao ya Mtaa ndio Serikali yenye mashiko zaidi, pia ndiyo ngazi ya Serikali ambayo huwasiliana nayo zaidi katika maisha yao ya kila siku. Mfumo wa Tanzania wa Serikali za Mitaa unaonyesha kuwa MSM hutoa huduma ambazo zina asili ya kijamii, yaani, afya, maji, elimu, ustawi, usimamizi wa taka, na zile zenye asili ya kiuchumi, yaani, ardhi na makazi, muindombinu, kilimo, mazingira na maendeleo ya jamii.

Nadharia ya utoaji huduma shirikishi iliyotumika katika kitabu hiki, ina maana ya utoji huduma ambao huhusisha wadau wote. Kiini cha ushiriki ni jamii ambayo hufaidika na huduma zitolewazo na jamii yenyewe, MSM, Serikali Kuu, mashirika yasiyo ya kiserikali na hata mashirika ya kimataifa. Utoaji huduma shirikishi huweka jamii faidika kama msingi wakati wa kupanga, utoaji wa huduma na upimaji wa ubora wa huduma. Utoaji huduma shirikishi huleta uendelevu wa huduma inayotolewa.

Katika sura hii, mbinu bora saba kuhusu utoaji huduma shirikishi zimewasilishwa. Mbinu bora ya H/W ya Handeni yenye kicha cha habari “Mpango wa Niache Nisome” inaeleza mchakato wa kupambana na utoro katika shule za sekondari na inaonyesha mikakati ambayo inaweza kutumiwa na MSM kupambana na utoro wa wasichana katika shule za Sekondari. Mikakati hiyo ni pamoja na kuiga mkakati wa “Niache Nisome”, kutafiti na kuainisha visababishi asilia vya ndoa na mimba za mwanafunzi wa kike, kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike na kushirikisha jamii nzima katika kuwalinda wasichana waliopo shuleni. Mpango huu pia unashirikisha mikakati ya kuboresha mazingira ya kujifunzia ya wasichana waliopo shuleni.

Mbinu Bora ya H/W ya Lushoto inaelezea matumizi ya teknolojia inayotumia nguvukazi katika jamii kujenga barabara zinazopitika misimu yote katika maeneo ya milima na magumu kufikika. Inaonyesha jinsi idara ya uendelezaji wa miundombinu ilivyoridhia teknolojia inayotumia nguvukazi katika jamii, ilivyoainisha mafundi katika vijiji, ilivyowapa mafunzo mafundi na ilivyojenga barabara za vijijini zenye ubora na miundombinu mingine kwa kutumia mafundi wenyeji. Mbinu hii bora pia inaonyesha jinsi MSM zinavyoweza kutumia akaunti maalum (*force account*) kutekeleza ujenzi wa miradi katika maeneo ambayo hayawavutii wakandarasi.

H/W ya Mufindi ina mbinu bora katika sura hii inayoeleza kuhusu ujenzi wa barabara ya Isipii – Mpanga Tazara kwa kutumia teknolojia niayotumia nguvukazi. Inaonyesha sifa muhimu za jitihada za jamii zinazosaidiwa na Halmashauri. Mbinu bora hii inaonyesha jinsi jamii inavyojipanga yenyewe, kufanya maamuzi kuhusu ujenzi wa barabara na kuisaidia Halmashauri kuokoa gharama ili kutoa huduma nyingine. Mbinu hii bora inaonyesha jinsi teknolojia inayotumia nguvukazi na jitihada za jamii zilivyowezesha kuokoa gharama kwa 85%.

Mbinu Bora ya H/W ya Moshi kuhusu jitihada za jamii katika uboreshaji wa barabara za vijijini ni jitihada ya wananchi wa kata ya Kimochi. Jamii ilikuwa ikipata matatizo katika kuzifikia huduma za kijamii na kiuchumi kuokana na barabara mbaya za vijijini. Jamii ilikabiliana na kumaliza tatizo hili kwa kufanya ushawishi ili mkutano wa kijiji ufanyike, kuunda kamati ya uendeshaji, kuchangisha fedha, kuhamasisha jamii, kukodi mitambo ya ujenzi wa barabara na kusimamia shughuli za ujenzi. Halmashauri ilitoa msaada wa kitaalamu tu.

Mbinu bora ya H/W ya Siha inaeleza kuhusu ushirikishwaji wa jamii katika usafi wa mazingira ili kuondoa milipuko ya mara kwa mara ya magonjwa yatokanayo na vinyesi. Halmashauri ilianzisha kampeni ya usafi wa mazingira, ilitumia mbinu chokozi, iliendesha mafunzo kwa wawezeshaji mbalimbali na ilitumia mbinu mbadala ya kuhesabu vinyesi kubadili desturi ya Wamasai ambayo inapinga kwa nguvu zote matumizi ya Choo. Hatimaye jamii ya Wamasai imebadili mitizamo na kukubali kutumia vyoo.

Mbinu Bora ya Mkoa wa Kilimanjaro kuhusu usimamizi wa matumizi endelevu ya ardhi inaonyesha jinsi ambavyo H/W za Mwanga na Siha zilitekeleza kikamilifu jitihada hii kupitia uelimishaji jamii shirikishi, uundaji wa vikundi vya wakulima, uandaaji wa makinga maji (matuta), ufundishaji wa wadau, uanzishaji wa vitalu vya miti, upandaji miti kwa wingi na uanzishaji wa mnyororo wa kitaasisi katika uzalishaji, ushirika na huduma.

Mbinu Bora ya mwisho katika sura hii inatoka H/W ya Ngorongoro na inahusu Utalii wa Kiutamaduni na Uhifadhi Shirikishi wa Misitu. Mbinu hii inaonyesha jinsi Halmashauri imefanikiwa kupitia uelimishaji jamii, usimamizi shirikishi wa misitu, uanzishaji wa kamati za maliasili za vijiji, uainishaji wa mipaka ya

misitu, uundaji wa makundi ya skauti za misitu, uanzishaji wa miradi midogo ya utunzaji wa misitu na uainishaji wa maeneo na wafaidika wa utalii.

Mambo dhahiri ya kujifunza yanayotokana na mbinu bora zilizopo katika sura hii yanaonyesha;

- Utoaji wa huduma si wa Serkali Kuu na Serikali za Mitaa pekee, bali jamii kwa ujumla zinahitaji kupewa fursa ya kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma zao. Jamii kupitia jitihada zao binafsi zinaweza kufanya mengi katika kutimiza mahitaji yao na ya huduma zinazohitaji. Kukiwa na mtazamo chanya wa umoja wa jamii, watu wanakuwa tayari kwa maendeleo yao.
- Ubunifu na kujitoa kwa watumishi wa MSM na upendo kwa watu wanaowahudumia, huleta tofauti kubwa katika utoaji wa huduma na huongeza ufanisi, uhakika na uendelevu katika huduma zinazoanzishwa na kutolewa.
- Teknolojia inayofaa na inayotumia nguvukazi inaweza sana kusaidia MSM na jamii kupunguza gharama katika miradi ya ujenzi kama barabara, madarasa, zahanati na ofisi.
- Hapa Tanzania hatujatumia sana rasilimali zilizopo. Kuna raslimali nyingi ambazo hazitumiki zikisubiri watu wenye ubunifu kuzitumia. Ardhi iliyowazi inaweza kubadilishwa kuwa misitu na maeneo ya utalii. Utamaduni tajiri uliopo unaweza kuunganishwa na maliasili kutunza mazingira, kuimarisha utalii na kuongeza fursa za ajira.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

**MPANGO WA NIACHE NISOME – UONDOAJI WA UTORO WA MTOTO WA KIKE KATIKA SHULE ZA SEKONDARI**




***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ni mojawapo ya Halmashauri 11 za Mkoa wa Tanga inayopatikana 187 Km Magharibi mwa makao makuu ya Mkoa. Halmashauri hii inapatikana kati ya Latitudo 4.9$^{o}$ – 6.0$^{o}$ Kusini na Longitudo 36.8$^{o}$ – 38.5$^{o}$ Mashariki. Inapakana na Halmashauri za Wilaya za Pangani na Muheza kwa upande wa Mashariki, Korogwe na Simanjiro upande wa Kaskazini, Bagamoyo upande wa Kusini na Kilindi upande wa Magharibi. Halmashauri ina eneo la 7,080 Km$^{2}$. Halmashauri haina ukanda wa pwani bali ina vilima vilivyotawanyika. Mto Msangazi ndio mto mkuu unaotoa maji katika Halmashauri iliyopo kati ya 600m – 1,200m juu ya usawa wa bahari. H/W ya Handeni hupata aina mbalimbali za hali ya hewa ikiwa na joto la wastani la 29$^{o}$C. Kawaida, Halmashauri hii ina misimu miwili ya mvua (mvua fupi na ndefu) zenye wastani wa 500m – 1000mm kwa mwaka.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 355,702, kati yao 179,816 ni wanawake na 175,886 ni wanaume, na ongezeko la watu la wastani la 3.3%. Katika maeneo mengi Halmashauri ina watu wachache. Msongamano mkubwa wa watu hupatikana karibu na barabara kuu za Mkata - Handeni, Manga –Kabuku - Segera - Mandera, Handeni – Korogwe, Handeni – Mziha na katika vijiji vinavyozunguka mji wa handeni. Kiutawala Halmashauri ina Tarafa 7, Kata 23, Vijiji 112 na Vitongoji 983.




*Ramani ya Kiutawala H/W ya Handeni*

Jamii za H/W ya Handeni ni za wakulima, wafugaji, wafanyabiashara na watumishi, kilimo kikiwa ndio chanzo kikuu cha kipato na kinaajiri takribani 90% ya watu wote, ikifuatiwa na ufugaji. Mazao makuu ni mahindi, maharage, machungwa, mihogo, alizeti, pamba, embe, ndizi, mbogamboga na mtama.

**2.0 TATIZO**

Tangu mwaka 2005 Serikali ilielekeza kila Kata nchini Tanzania kujenga na kuanzisha shule za sekondari. Hili liliongeza idadi ya shule za sekondari za jamii na uandikishaji wa kidato cha kwanza nchi nzima. H/W ya Handeni pia ilianzisha shule katika Kata zote 23. Pamoja na kuwa hili ni badiliko chanya, jamii katika Vijiji hazikuwa tayari, hivyo kuwepo kwa tabia ambazo ziliathiri maisha ya shule ya mwanafunzi wa kike katika shule za sekondari. Kwa mfano, wasichana wengi ambao waliolewa mara tu baada ya kumaliza elimu ya msingi, baada ya ongezeko la uandikishaji ilibidi waende shule. Kwa kung'ang'ania desturi, pamoja na umaskini, idadi kubwa ya wasichana na wavulana waliacha shule na kujihusisha na biashara ndogondogo hasa kwa wavulana na ndoa za lazima kwa wasichana. Zaidi ya ndoa za lazima, mimba pia ziliongezeka mashuleni. Sababu nyingine zilikuwa umaskini wa kaya, ukosefu wa mabweni ya wasichana, wasichana kuishi mbali na familia zao ili kuwa karibu na shule za sekondari na desturi za jamii ambazo zinapingana na elimu, hasa elimu ya mtoto wa kike.

Kati ya mwaka 2009 na 2011, H/W ya Handeni ilishuhudia ongezeko la idadi ya utoro wa wanafunzi uliojidhihirisha katika tofauti ya walioandikishwa kujiunga na elimu ya sekondari na wale wanaomaliza kidato cha nne. Hali hii iliwaathiri zaidi wanafunzi wa kike kwa sababu ya mimba za utotoni, utoro na ndoa za utotoni. Hili lilikolezwa na utamaduni wa jamii ya Handeni ambao hausaidii mtoto wa kike kusoma. Matokeo yake, kati ya mwaka 2010 hadi 2012, wanafunzi 61 waliacha shule kwa sababu ya mimba. Maeneo yaliyoathirika sana ni Kata ya Mazingara (Shule ya sekondari Mazingara, mimba 11), Kata ya Misima (shule ya sekondari Misima, mimba 7) na Kata ya Ndolwa (shule ya sekondari ya Ndolwa, mimba 9). Jedwali 1 linaonyesha mimba kwa kila shule na jedwali 2 linalinganisha kuandikishwa kwa wanafunzi na kumaliza elimu ya sekondari.

**Jedwali 1: Mimba katika baadhi ya shule za Sekondari**

| Year | 2009 | 2010 | 2011 |
|---|---|---|---|
| Mazingara | 12 | 9 | 11 |
| Misima | 8 | 13 | 7 |
| Ndolwa | 6 | 5 | 9 |
| Jumla | 26 | 27 | 27 |

**Jedwali 2: Kuandikiswa wanafunzi na Kumaliza (2007/10 and 2008/11)**

| | ME | KE | Jumla | | ME | KE | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuandikishwa 2007 | 1467 | 1325 | 2792 | Kuandikishwa 2008 | 1409 | 1389 | 2798 |
| Kumaliza 2010 | 792 | 937 | 1729 | Kumaliza 2011 | 1066 | 891 | 1957 |
| % Kumaliza | 52% | 70% | 61% | % Kumaliza | 75% | 64% | 69% |

H/W ya Handeni pia ilikuwa na changamoto nyingine nyingi ambazo ziliathiri elimu ya mtoto wa kike katika shule za sekondari. Changamoto hizi zimeelezwa kwa kifupi hapa chini;

(i) Mazingira duni ya kujifunzia na kufundishia yaliyoambatana na upungufu wa madarasa, maabara, upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, upungufu wa walimu, ukosefu wa mabweni, ukosefu wa jitihada za kutoa chakula shuleni na ukosefu wa kujifunza toka kwa wengine.

(ii) Kaya nyingi za H/W ya Handeni zinaathiriwa na umaskini uliokithiri hivyo kufanya mahari kuwa sehemu ya kipato cha muda. Hali hii hushawishi familia nyingi kukubaliana na ndoa za utotoni hata kwa wasichana waliopo shuleni. Kwa sababu za umaskini, wasichana hulazimika kupokea zawadi toka kwa wanaume waovu hali inayoleta unyanyasaji wa kijinsia.

(iii) Uhaba wa maji katika maeneo ya shule hulazimu wasichana kuzunguka maeneo mbalimbali kutafuta maji na kujiweka katika mazingira ya kufanyiwa unyanyasaji wa kijinsia.

(iv) Uwepo wa Vijiwe vya Vijana wasio na ajira vyenye walevi, watumia madawa, waendesha pikipiki na wafanya biashara ndogondogo unaosababisha wanafunzi wa kike kuingia katika vishawishi mbalimbali.

**2.0 LENGO LA MPANGO WA NIACHE NISOME**

Baada ya kugundua ongezeko la utoro kwa wasichana katika shule za sekondari, mwezi Oktoba mwaka 2012, Mkuu wa Wilaya wa kipindi hicho alianzisha mpango wa NIACHE NISOME ili kuhakikisha wanafunzi wa kike wanavutiwa, wanapata motisha wa kuendelea na kumaliza masomo yao ya sekondari. Mahsusi kabisa mpango huu ulikuwa na malengo yafuatayo;

- Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia
- Kuondoa mimba na utoro mashuleni
- Kuzielimisha jamii za Handeni kuhusu umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike
- Kuzipa uwezo kamati za shule kushughulika kimakakati na suala la utoro
- Kuondoa na kupiga marufuku vijiwe vya vijana wasio na ajira karibu na shule
- Kuboresha huduma mashuleni hasa maji, kufunga umeme wa jua na kutoa chakula cha mchana.

**3.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

H/W ya Handeni iliurithi mpango wa “Niache Nisome” kutoka kwa Mkuu wa Wilaya na kuweka hatua za makusudi za kufikia malengo yaliyotajwa hapo juu. Baada ya mashauriano na maamuzi ya timu ya menejimenti ya Halmashauri na Baraza la Madiwani, Halmashauri ilianza kutekeleza mpango huu kwa kutumia mbinu zilizoelezewa hapa chini.

H/W ya Handeni iliendesha utafiti ili kujua idadi na sababu za ndoa za wasichana waliopo shuleni na mimba zinazopelekea utoro. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wasichana wa shule waliolelewa katika familia maskini hawakuwa na uelewa wala stadi za kujilinda na mahusiano ya mapema ya kimapenzi na magonjwa ya zinaa. Pia ilionekana dhahiri kuwa wasichana kutoka familia maskini hawakuthamini elimu hivyo kuwa tayari kwa ndoa zilizopangwa na wazazi wao. Utafiti pia ulionyesha makundi ya marafiki mashuleni na maeneo ya jirani yalichangia uwepo wa mahusiano ya kimapenzi ya mapema.

Pili, Halmashauri iliendesha mikutano ya kuelimisha jamii katika Vijiji kuhusu umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike na kufanya mikutano na kamati za shule kwa lengo la kuzifanya kaya na jamii kuuendeleza mpango. Mikutano hii ilijumuisha maelezo kuhusu madhara ya ndoa za utotoni, madhara ya muda mrefu ya tamaduni potofu, thamani ya mtoto wa kike mwenye elimu sahihi na uondoaji wa duara la umaskini kupitia elimu ya mtoto wa kike katika kaya na jamii.

Tatu, Halmashauri iliainisha makundi ya marafiki na kuyapatia elimu ya pamoja kuhusu athari za mapenzi ya utotoni na tabia zisizofaa. Makundi haya yalisaidiwa kuunda timu na kuchagua viongozi wa timu; mkakati uliolenga kuwa na mbinu ya wao kujidhibiti na tabia zisizofaa. Vikundi hivi pia vilishauriwa kujiingiza katika shughuli zinazoleta kipato ambazo zitawafanya kuwa na kazi muda wote wa mchana na

hivyo kuachana na tabia ya kufuatilia wanafunzi wa kike. Katika hili, Halmashauri ilifanya ufuatiliaji kila robo mwaka kubaini mabadiliko kuelekea tabia njema kati ya wanafunzi na makundi ya vijana.

Nne, Halmashauri iliwajengea uwezo wanafunzi wa kike kwa kuwaelimisha kwa kina kuhusu afya ya uzazi, umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike na stadi za kujilinda na vishawishi vinavyoleta mahusiano ya kimapenzi. Pamoja na hilo Halmashauri ilikazia mpango huu wa kujenga uelewa kwa kutengeneza na kugawa fulana (T-shirts) zilizoandikwa jina la mpango “NIACHE NISOME” kwa wanafunzi wa kike. Walimu na wazazi walielekezwa kuwahamasisha wanafunzi wa kike kuvaa fulana hizo wakiwa katika matembezi kwenye maeneo ya umma. Hili lililenga kusambaza ujumbe kuwa jamii inatakiwa kuwasaidia watoto wa kike kuendelea na masomo.

Tano, Halmashauri iliunda kikosi kazi kilichojumuisha madiwani, watumishi, polisi na wanajamii kufanya ufuatiliaji wa wasichana ambao walikuwa hawahudhurii shule, kujua sababu za kutohudhuria shule na kuwaleta shuleni. Kama imetokea mwanafunzi ameolewa, kikosi kazi hiki kilivunja ndoa kwa kumleta mwanafunzi shuleni. Hili lilifanyika kulingana na sheria na kanuni za elimu. Kwa kushirikiana na asasi isiyo ya kiserikali ya CAMFED TANZANIA, Halmashauri ilibaini wanafunzi wa kike 790 ambao walikuwa wakuu wa kaya kutokana na vifo, ulevi, ukatili wa nyumbani, talaka na umaskini uliokithiri wa wazazi au walezi. Wanafunzi hawa wa kike walipatiwa ushauri na usaidizi ili waendelee na masomo yao bila usumbufu.

Baada ya utekelezaji wa mikakati mikuu iliyoelezwa hapo juu, Halmashauri ilihamishia jitihada zake katika mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kufanya maboresho.

(i) Ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari na kuboresha makazi kwa kufunga umeme wa jua, kuchimba visima vya maji na kuajiri walezi
(ii) Utoaji wa chakula cha pamoja cha mchana shuleni. Halmashauri ilihakikisha wanafunzi katika shule 147 za msingi na 29 za sekondari wanapata chakula kila siku kwa mwaka mzima. Utaratibu huu hutekelezwa kwa mfumo wa kuchangia gharama ambapo wazazi huchangia fedha taslimu au vyakula.
(iii) Ujenzi na ukarabati wa nyumba za walimu, madarasa na vyoo vya watumishi na wanafunzi.



***Ujenzi wa madarasa na mfumo wa kuvuna maji ya mvua katika shule za sekondari***

(iv) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kununua vitabu vya kiada na ziada kwa ajili ya wanafunzi na walimu, kununua madawati na kuanzisha miundombimu ya jamii kama viwanja vya michezo.
(v) Kuajiri walimu zaidi na kuwapatia motisha ili wakubali kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni na magumu ya vijijini.

(vi) Kuanzisha mfuko wa elimu. Halmashauri ilitafuta wadau mbalimbali ili kuchangia mfuko wa elimu ambao unasaidia wanafunzi wenye mazingira magumu. Halmashauri imerasimisha mfuko huu na unaendeshwa kwa mafanikio kupitia sheria ndogo. Mpaka mwiisho wa mwaka 2014 Mfuko ulikuwa na jumla ya shs. 93,000,000/=.

(vii) Kuingia makubaliano (MoU). Halmashauri iliingia kwenye makubaliano na Serikali za Vijiji katika kila Kijiji ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanabaki shuleni. Ikitokea utoro, hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa viongozi wa Vijiji na wazazi/walezi.

(viii) Kuimarisha elimu ya kujitegemea ambapo wanafunzi wanashiriki katika shughuli za kilimo na uzalishaji mashuleni. Kwa mfano, shule nyingi huzalisha mahindi yanayotumika kwa chakula shuleni. Shule zinapata mbegu na huduma za ugani kutoka Halmashauri.



***Wanafunzi wa kike katika elimu ya kujitegemea***

## 5. RASLIMALI

Kutekeleza mpango wa NIACHE NISOME Halmashauri haikuandaa bajeti maalumu bali shughuli zilitekelezwa kwenye bajeti za kawaida za mwaka. Jedwali lililopo hapa chini linaonyesha fedha zilizotumika kutekeleza baadhi ya shughuli za mpango wa NIACHE NISOME kati ya mwaka 2012 na 2014.

**Jedwali 3: Baadhi ya gharama za utekelezaji wa mpango wa Niache Nisome**

| Na | Aina | Washiriki | siku | kiasi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Posho | 19 | 8 | 45,000 | 6,840,000 |
| 2 | Chakula na Vinywaji | 240 | 8 | 5,000 | 9,600,000 |
| 3 | Vifaa vya ofisi na shajara | 1 | 1 | 5,000,000 | 5,000,000 |
| 4 | Dizeli | 1 | 1 | 6,000,000 | 6,000,000 |
| | **Jumla kuu** | | | | **70,640,000** |

## 6.0 MATOKEO

H/W ya Handeni ina jamii ambayo inatunza mila na tamaduni zake imara hivyo kuleta ugumu katika kuleta mabadiliko na kuanzisha masuala ya kisasa. Katika mpango huu Halmashauri ilifanikiwa kupata matokeo chanya kutokana na kutumia mbinu shirikishi ambapo siyo tu Serikali Kuu na taasisi za MSM zilishiriki bali vijana, wazee, kaya, walimu, kamati za shule, wanafunzi wa kiume na kundi lengwa lenyewe, wanafunzi wa kike. Serikali za Vijiji pia, kupitia makubaliano (MoUs) zilichangia sana katika kubadili fikra, mitazamo, na tabia za wanavijiji kuhusu mwanafunzi wa kike. Baadhi ya matokeo dhahiri ya mpango wa NIACHE NISOME yameelzwa hapa chini.

H/W ya Handeni ilipata mafanikio makubwa katika kuboresha mahudhurio shuleni kwani mahudhurio ya wanafunzi yalipanda kutoka 72% mwaka 2011 hadi 86% mwaka 2013. Pia mimba zilipungua kutoka 29 mwaka 2011 mpaka mimba 3 mwaka 2013. Mpango wa NIACHE NISOME ulilenga kufikia mimba sifuri na utoro wa wanafunzi wa kike sifuri ifikapo mwaka 2015.

Mpango huu ulitangazwa katika vyombo vya habari kama inavyonekana hapa chini.

THE CITIZE

**Handeni.** A deliberate campaign aimed to fight pregnancy among schoolgirls in Handeni District, Tanga Region has apparently started to pay off following a dramatic fall in reported cases; it was revealed here last week.

Between January and May this year only six cases were reported compared to 22 pregnancies during the same period last year, according to the officer commanding district (OCD) Zuberi Chembera.

He attributed the drop of reported pregnancy cases among schoolgirls to a campaign dubbed 'Niache Nisome' which was initiated by the district commissioner Muhingo Rweyemamu.

He added that the campaign has been successful because residents of the district have started to utilise the services of Gender Desk set up by the Police Force in order to address the problem of early pregnancy.

The OCD urged people to continue reporting such pregnancies because by so doing they would sensitize people on how assist the innocent school girls to avoid being made pregnant.

The desk was set up by the police in every district and region in collaboration with the Education Department and respective defence and security committees and is also aimed to educate the parents on the hazards of early pregnancies.

"At least there is some hope now with the drop of the reported pregnancies," the area police chief told this newspaper in an interview, adding; "people should not fear to come to us to report such cases".

It is estimated more than 8,000 primary and secondary school girls in Tanzania are forced to abandon studies due to pregnancy each year, it was disclosed here last week.

To make matters worse, many of the kids born by the school dropouts end up as street children because their parents cannot afford paying for their up keep and education.

***Gazeti la Citizen; Jumatatu Julai 21, 2014***

Halmashauri kupitia mpango wake wa elimu kwa umma, makubaliano na Serikali za Vijiji (MoUs) na ushirikiano na asasi mbalimbali zisizo za kiserikali imefanikiwa kubadili mitazamo ya jamii ya Handeni kuelekea kuamini na kusaidia elimu ya mtoto wa kike. Kaya nyingi zimekubali kutenga fedha kwa ajili ya elimu ya mtoto wa kike badala ya kumfanya mtoto wa kike kuwa chanzo cha fedha taslimu kupitia mahari.
Badiliko la mtazamo wa jamii kwa ujumla na upigaji marufuku wa vijiwe vya vijana wasiokuwa na ajira vimesaidia sana kupungua kwa udhalilishaji wa wanafunzi wa kike wakiwa katika safari za kutoka nyumbani kwenda shule na kurudi. Vijana waliokuwa kwenye vijiwe pia wamebadili tabia zao na kutafuta shughuli za uzalishaji ili kuongeza kipato. Hili lina matokeo katika ubora wa kuishi wa kaya kwani ushiriki wa vijana kwenye shughuli za uchumi huleta uhakika katika kaya wa mahitaji kama chakula, maji na ada za shule.

Serikali za Vijiji, kamati za shule, wazazi na walimu wamefanya kazi kubwa kwa pamoja kufikia utekelezaji wa sheria na kanuni za elimu. Hili linahusu jamii nzima kuhakikisha kuwa wasichana wanahudhuria shule, wanaheshimiwa wakiwa katika maeneo ya umma na hawafanyiwi vitendo vya utesaji na udhalilishaji katika mazingira yoyote yale.

Halmashauri imefanikiwa sana katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hili linadhihirika katika kuongezeka kwa madarasa, madawati, vitabu, mabweni, vyoo, nyumba za walimu, umeme wa jua, mfumo wa kuvuna maji ya mvua, visima vya maji n.k. Mpaka Desemba 2014 Halmashauri ilikuwa imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kuwa na huduma zilizoorodheshwa kwenye jedwali 4 hapa chini.

**Jedwali 4: Huduma zilizopo Mashuleni**

| Miundombinu | Idadi | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Shule za Msingi | Shule za Sekondari | |
| Nyumba za watumishi | 210 | 61 | 271 |
| Madarasa | 844 | 311 | 1,155 |
| Matundu ya vyoo | 1,042 | 390 | 1,432 |
| Mabweni | - | 6 | 6 |
| Mifumo ya kuvuna maji ya mvua | | 14 | 14 |
| Madawati | 13,695 | 12,586 | 26,281 |

Halmashaauri pia imeshuhudia ongezeko la ufaulu wa kidato cha nne katika mitihani ya taifa ambapo ufaulu umeongezeka toka 30% mwaka 2012 hadi 39.1% mwaka 2013 na ufaulu wa kidato cha pili umeongezeka kutoka 31% mwaka 2012 hadi 48% mwaka 2013. Shule zote za Msingi na Sekondari katika H/W ya Handeni zimeanzisha mpango wa elimu ya kujitegemea ili kuhakikisha watoto wote wanapata stadi za kujituma na kujitegemea. Shule pia zinafaidika na wanafunzi kushiriki katika shughuli za elimu ya kujitegemea kwani wanazalisha mazao ambayo yanatumika kutoa chakula cha mchana. Mwisho, utoaji wa chakula wakati wa mchana kwa shule zote za msingi na sekondari kumeimarisha malengo ya NIACHE NISOME kwa kuhakikisha kuwa wasichana wana furaha shuleni kwani huduma zote za msingi zinapatikana kwa urahisi kuliko katika kaya za wazazi/walezi wao.

### 7.0. MIKAKATI YA UENDELEVU

H/W ya Handeni ikishirikiana na taasisi zote za Serikali Kuu na vyombo vya dola; hasa polisi, imedhamiria kuona kuwa matokeo chanya ya mpango wa NIACHE NISOME yanakuwa ni ya kudumu na mabadiliko yaliyotokea katika mtazamo na tabia ya jamii hayapotei. Hili litaweza kufikiwa kwa mikakati iliyotajwa hapa chini.

(i) Utafutaji endelevu wa wadau mbalimbali wa kuchangia maendeleo ya sekta ya elimu hasa mfuko wa elimu
(ii) Utoaji endelevu wa elimu kwa wazazi kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wao na kuendelea kutoa adhabu kwa wazazi ambao watoto wao wanaacha shule.
(iii) Ujenzi endelevu wa uelewa kwa jamii ya Handeni kuhusu umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike na kuzuia kuolewa kwa wanafunzi.
(iv) Kuwezesha michezo mashuleni kwa kuanzisha mashindano kati ya madarasa na kati ya shule na kutoa zawadi kwa wanafunzi na shule zinazoshinda.
(v) Kupata msaada endelevu kutoka jeshi la polisi ili kuhakikisha Amani na Usalama katika H/W ya Handeni ambayo huleta uhakika wa mazingira salama ya shule kwa wanafunzi kwa ujumla na kwa namna ya pekee wanafunzi wa kike.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mabadiliko mara zote huleta hofu na taasisi nyingi na watu wameshindwa kuanzisha na kuleta mabadiliko yenye matokeo chanya. H/W ya Handeni imefanikiwa siyo tu kubadili mahudhurio na ufaulu kwa wanafunzi wa shule za sekondari bali tamaduni, fikra na tabia imara za jamii ya Wazigua. Inashangaza; ni kwa namna gani mabadiliko haya yaliwezekana na nini hasa kilichotumika kufanikisha mabadiliko haya? Halmashauri hii inatoa somo kwa MSM nyingine kupitia siri za mafanikio. Siri hizi ni;

(i) Ushiriki wa wazazi na wadau wengine katika kuchangia maendeleo ya elimu katika Halmashauri.
(ii) Matumizi bora ya idara nyingine za Serikali kama polisi na mahakama.
(iii) Utashi wa Kisiasa. Wanasiasa ambao wana upendo na jamii na wanaweza kuona mahitaji na mapungufu wananchi waliyonayo, kuchukua hatua stahiki za kutatua matatizo na kufurahia mafanikio ya jamii iliyobadilika. Wanasiasa hawa ni wapenda mafanikio na mabadiliko na wana utamaduni wa kuacha nyayo katika kila jamii wafanyayo kazi za masuala ya maendeleo.
(iv) Ukaguzi wa mara kwa mara wa shule unaofanywa na timu za wilaya na ya kanda. Timu hizi hupokea taarifa kuhusu masuala mengi ya elimu ikiwa ni pamoja na utoro na mimba na kuchukua hatua stahiki kabla masuala hayajaharibika.
(v) Uongozi wenye dira wa Mkuu wa Wilaya ambaye kimkakati kabisa alielekeza nguvu katika kupambana na changamoto zinazozunguka elimu ya mtoto wa kike.

## Kiambatisho 1: Mikakati ya Uendelevu

| S/No. | Mkakati | Mradi/shughuli | Jumla | | | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 | |
| 5.1a | Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi | Kununua vitabu vya kiada na ziada | 251,726 | 271,876 | 281,876 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kununua madawati | 20,504 | 21,171 | 22,152 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kujenga madarasa | 882 | 898 | 963 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kujenga nyumba za watumishi (walimu) | 220 | 221 | 254 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kujenga vyoo | 1028 | 1072 | 1518 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| 5.1b | Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari | Kununua vitabu vya kiada na ziada | 7,395 | 10,000 | 3,000 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kununua madawati | 4,426 | 4,000 | 4,200 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kujenga madarasa | 9 | 8 | 6 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kujenga nyumba za watumishi (walimu) | 5 | 4 | 2 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | Kujenga vyoo | 8 | 8 | 20 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| 5.2 | Kutoa chakula mashuleni | **i.b.** Halmashauri kusimamia utoaji wa chakula katika shule za msingi 147 ifikapo mei 2014 | msingi - 18 | Primary – 36 | Primary – 147 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| | | **ii.b.** Sekondari 29 ifikapo mei 2014. | Sekondari. 5 | Sec. 23 | Sec. 29 | Serikali kuu, wazazi, wadau mbalimbali kamaWorld Vision Tz |
| 5.3 | Kuanzisha mfuko wa elimu | Kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia mfuko ili kutekeleza shughuli mbalimbali za elimu | Tsh.7,000,000 | Tsh. 20,000,000 | Tsh. 93,000,000 | Watumishi, madiwani, wadau mbalimbali |
| 5.4 | Kutekeleza mpango wa "Niache Nisome" | Kuwaelimisha wazazi na wadau wengine kuhusu umuhimu wa elimu katika jamii | 0 | Sekondari. 29 | Sekondari. 29 | Ofisi ya mkuu wa wilaya, mkurugenzi wa Halmashauri, wazazi |
| 5.5 | Kufanya makubaliono (MoU) | Kufanya makubaliano kati ya Halmashauri na serikali za vijiji ili kuhakikisha wanafunzi wanahudhuria shuleni na wazazi wanaokiuka wanaadhibiwa | 0 | Vijiji – 112 | Vijiji – 112 | Mkurugenzi Mtendaji |
| 5.6 | Kuelimisha wazazi | Halmashauri imelifanya suala shule ajenda ya kudumu kwenye mikutano yote rasmi ya maendeleo kuanzia kitongoji hadi kata | Sekondari 29 zitafikiwa | Sekondari 29 zitafikiwa | Sekondari 29 zitafikiwa | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji |
| 5.7 | Elimu ya kujitegemea | Halmashauri inahamasisha kila shule kulima walau hekta moja ya mazao ya chakula kama mahindi, mtama, mhogo ili kutumiwa na wanafunzi kama chakula | Sekindari 5 | Sekondari 23 | Sekondari 23 | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji |

# HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO

**MATUMIZI YA TEKNOLOJIA ITUMIAYO NGUVUKAZI KATIKA JAMII**




***Uzoefu wa Halmashauri Wilaya ya Lushoto***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ipo upande wa Kaskazini mwa Mkoa wa Tanga kati ya Latitudo $40^0$ 25' – $40^0$ 55' Kusini na Longitudo $30^0$ 10' – $38^0$ 35' Mashariki. Hupakana na Jamhuri ya Kenya na H/W ya kwa upande wa Kaskazini Mashariki, H/W ya Korogwe upande wa Kusini, H/W ya Mkinga na H/W ya Muheza upande wa Mashariki. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, idadi ya watu katika H/W ya Lushoto ilikuwa 332,436, (153,847 wanaume na 178,589 wanawake) na ukuaji wa idadi ya watu wa 1.1%. Takribani 85% ya wakazi wote hujihusisha na kilimo (kilimo cha mashamba madogo) na ufugaji na waliobaki 15% hujihusisha na biashara ndogondogo.

Halmashauri ina eneo la 3,500 $Km^2$ linalochukua takribani 12.8% ya Mkoa wa Tanga. Milima ya Magharibi ya Usambara huchukua sehemu kubwa ya ardhi ambayo ipo kati ya 300m – 2100m juu ya usawa wa bahari. Ukanda wa juu hufunika takribani 75% (2625 $Km^2$) ya eneo lote la Halmashauri, na una mwinuko wa kati ya 1000m – 2100m juu ya usawa wa bahari. Ukanda wa chini huchukua 25% (875 $Km^2$) ya eneo la Halmashauri ni una mwinuko wa kati ya 300m – 600m juu ya usawa wa bahari. Milima na miinuko yake huchukua 90% ya ardhi yote ya H/W ya Lushoto. Miinuko hii huwa ya wastani hadi ya wima na kuna mabonde mengi membamba pamoja na miamba.

**<u>Ramani ya H/W ya Lushoto</u>**




## 2.0 TATIZO

Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ipo kwenye ardhi ya milima ambayo huleta changamoto ya kudumu kwenye usafishaji ardhi ili kujenga barabara kutokana na ugumu wa kutumia vifaa na mashine za ujenzi wa barabara. Milima iliyo wima na yenye kupanda na kushuka hufanya baadhi ya Vijiji na jamii kufikiwa kwa shida suala linaloleta ugumu kwa Halmashauri kutoa huduma kwa jamii hasa zilizopo katika maeneo ya milima. Milima hii pia haivutii wakandarasi wenye sifa kuchukua kazi za ujenzi katika eneo hili. Hata wale wanaoshinda zabuni za ujenzi hulazimika kutumia nguvukazi zilizopo Vijijini. Baadhi ya wakandarasi waovu hawawalipi kwa haki wanavijiji na hivyo kuwepo kwa misuguano kati ya jamii na Halmashauri

ambayo ndio inatoa mikataba kwa wazabuni. Mara nyingi, bei zinazopendekezwa na wakandarasi huzidi bei halali za ujenzi kwa 40 – 50%. Pia kulikuwa na matukio ya kutokuelewana kati watendaji na wanasiasa katika mchakato wa kutoa zabuni kwa wakandarasi wa nje. Hakika, kuna maeneo ambayo hayawezi kusafishwa kwa kutumia mashine. Pia ukosefu wa umiliki wa jamii wa miradi iliyotekelezwa na wakandarasi wa nje ulileta uharibifu, ukosefu wa marekebisho ya kawaida na hivyo kukosa uendelevu. Haya yote yalilazimu utumiaji wa teknolojia inayotumia nguvukazi kwa kutumia akaunti maalum (*force account*) katika ujenzi wa barabara za maeneo magumu kufika.

**3.0 LENGO**

H/W ya Lushoto imekuwa ikilenga kufungua barabara katika Vijiji na jamii zote ingawa kuna ardhi kinzani ya milima. Ukanda wa juu una jamii ambazo zinajishughulisha na kilimo cha mazao ya aina mbalimbali kama kahawa, chai na matunda ya hali ya hewa ya baridi. Pia aina mbalimbali za mboga hulimwa kwenye ukanda wa juu. Hivi vyote vinahitaji miundombinu ya uhakika ya barabara ili kuruhusu usafirishaji wa mazao ya mashambani. Hivyo lengo kuu la Halmashauri katika jitihada hii lilikuwa kuhakikisha jamii inapata huduma za msingi za kijamii na kiuchumi kupitia miundombinu iliyoboreshwa. Jitihada hii ililenga;

(i) Kufungua maeneo magumu kufikika na kujenga barabara ndogo zinazopitika misimu yote ili kuzipa fursa jamii kujiimarisha katika kilimo, makazi na usafirishaji.

(ii) Kuziingiza jamii katika miradi ya maendeleo kwa kutumia teknolojia inayotumia nguvukazi. Ushiriki wa jamii katika ujenzi wa barabara huimarisha jamii katika misingi ya ushiriki, ufanyaji wa maamuzi, umiliki na huipatia jamii fursa ya kuongeza kipato kwani teknolojia inayotumia nguvukazi siyo ya kujitolea bali nguvukazi inayotumika hulipiwa.

(iii) Kuchora na kujenga miundombinu ya gharama nafuu kwa kutumia ufuatiliaji wa karibu na shirikishi wa wanajamii na usimamizi wa ziada kutoka kwa wataalamu wa Halmashauri.

(iv) Kuimarisha umililki wa jamii wa miradi yao ya maendeleo. Kutokana na ushiriki thabiti, jamii hujisikia kufungamana na miradi yao na hivyo kulazimika kufanya matengenezo ya mara kwa mara.

(v) Kuhamasisha kujifunza kwa uzoefu kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo moja kwa moja kati ya wanajamii na watumishi wa Halmashauri.

(vi) Kutumia nguvukazi isiyotumika katika shughuli zalishi za maendeleo. Shughuli za kilimo kimsingi ni za msimu na kuna misimu ambapo watu hushinda bila kazi wakisubiri mazao ya shambani kukomaa. Katika kipindi hiki kuna nguvukazi isiyotumika ambayo inaweza kutumiwa katika jitihada nyingine za maendeleo ikiwa ni pamoja na kujenga barabara na kuziboresha.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Teknolojia inayotumia nguvukazi katika jamii ni mbinu ya kiinjinia ambayo hutumia nguvukazi na vifaa vyepesi kama njia kuu ya kuzalisha. Ingawa matumizi ya teknolojia hii katika ukarabati na matengenezo ya barabara yanadhihirika katika matokeo yake ya ukuaji wa kiuchumi ndani ya H/W ya Lushoto, kuegemea kwake kwenye matumizi ya vifaa na akaunti maalum (*force account*) kama njia ya malipo kunagusa sekta zote za umma na binafsi. Akaunti Maalum (*Force Account*) hujumuisha shughuli katika mradi wa ujenzi ambazo hufanywa bila kuwepo kwa makubaliano ya gharama, na hutekelezwa kwa maelewano kuwa mkandarasi atamdai mmiliki kulingana na gharama za vifaa na mitambo, pamoja na asilimia fulani ya ongezeko la gharama na faida. Kwa maneno mengine shughuli zinazofanyika kwa akaunti maalum humaanisha kandarasi za ujenzi ambazo hulipwa kwa misingi ya muda na vifaa vilivyotumika. Pamoja na umuhimu wake kwenye maeneo magumu kufikika, akaunti hii maalumu siyo maarufu katika kanuni za mfumo wa manunuzi ya umma.

Idara ya Uendelezaji wa Miundombinu ilibaini kuwa ujenzi wa barabara katika Vijiji vilivyopo katika miinuko wima ya milima ya Usambara hauwezi kutekelezeka kwa kutumia mfumo rasmi wa manunuzi ya kampuni za ujenzi ambazo hutumia mitambo mizito kutoboa barabara na kujenga kwa kiwango cha changarawe au lami. Hivyo ilikuwa muhimu kuandaa andiko kamilifu kuhusu wazo la kutumia teknolojia itumiayo nguvukazi katika jamii. Andiko hili liliwasilishwa katika vikao vya timu ya menejimenti ya Halmashauri na Baraza la Madiwani ili kupitishwa na kupata makubaliano ya pamoja kwani lilikuwa na vigezo vya akaunti maalumu ambayo si rafiki na kanuni na maelekezo ya mfumo wa manunuzi ya umma.

Baada ya andiko kuidhinishwa, Halmashauri iliendelea kwa kuzihamasisha jamii kuunda vikundi vya Vijiji vya mafundi wa fani mbalimbali. Uelimishaji jamii wa awali ulifanywa na Madiwani kupitia mikutano ya hadhara, ukiwahamasisha mafundi kushiriki mikutano ya utambuzi iliyoendeshwa na wahandisi na mafundi wa Halmashauri.

Kupitia kwa mhandisi wa ujenzi wa Halmashauri utambuzi wa mafundi ulifanyika katika kila kata na kufuatiwa na uundaji wa vikundi vya mafundi vya kata, utungaji wa katiba za vikundi na usimikaji wa uongozi wa vikundi. Mafundi walipangwa kwenye mfumo wa vikundi ili kuleta uendelevu katika shughuli zao na usimamizi bora wa fedha kwani ushiriki katika ujenzi wa barabara ni moja ya shughuli au miradi ya kuongeza kipato. Halmashauri pia ilivipatia mafunzo vikundi vya mafundi vya Kata kuhusu stadi za ujenzi wa miundombinu ya msingi (kukumbusha vipimo vya ujenzi) na stadi za usimamizi (usimamizi wa fedha, ufunguaji wa akaunti, uandishi na utunzaji wa vitabu vya fedha, uandishi wa taarifa za utekelezaji, stadi za manunuzi, n.k.)



***Mhandisi wa Halmashauri akitoa mafunzo***

Baada ya mafunzo kabambe Halmashauri iliviwezesha vikundi kusajiliwa kwa kutoa maelelzo kuhusu mchakato wa usajili. Shughuli hii ilifanywa na idara ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na mwanasheria wa Halmashauri. Usajili wa vikundi vya mafundi vya Kata ni muhimu kwani ni baada ya kusajiliwa na kupewa vyeti ndipo vinaweza kuingia mikataba kati ya na Serikali za vijiji au kati yao na Halmashauri. Mikataba hii ya ujenzi inahusisha miundombinu ya aina mbalimbali kama madarasa, maabara, zahanati, kalavati na nyumba za watumishi.

Kuwezesha ujenzi wa barabara, uchambuzi wa miradi ya ujenzi (ngazi ya Halmashauri) kubaini inayoweza kutekelezwa na wakandarasi wenye sifa na inayoweza kutekelezwa na vikundi vya mafundi vya kata ulikuwa muhimu. Miradi ambayo inatekelezwa na vikundi vya kata ni ile inayohusu maeneo yenye miinuko wima ambayo inajumuisha marekebisho madogo, marekebisho ya mara kwa mara na ujenzi wa barabara mpya katika maeneo yasiyofikika. Maeneo haya kimsingi hayawavutii wakandarasi wanaotumia mitambo mizito.

Kutangaza zabuni, kutunuku na kuingia mikataba na wakandarasi wenye sifa. (a) Kwa miradi ya ujenzi wa barabara, Halmashauri iliainisha waziwazi miradi ya kutekelezwa na vikundi vya mafundi vya Kata na pamoja na kiasi cha fedha kwenye mikataba. Suala la pekee kwenye utaratibu huu ni kuwa, mkandarasi mwenye sifa analazimika kurudisha cheki ya malipo kwa Halmashauri ili Halmashauri iweze kuingiza fedha za ujenzi wa barabara kwenye akaunti za vikundi. Kwa mbinu hii vikundi vya mafundi vinapata motisha kwani kuna uhakika wa malipo. Utaratibu huu humlazimu mkandarasi kutoa ushauri wa kitaalamu kwa vikundi katika maeneo husika ili kukamilisha mradi na kulinda hadhi ya mkandarasi. (b) Kwa ujenzi wa majengo ya umma (kama madarasa, maabara, zahanati, nyumba za watumishi, mabweni, vituo vya habari n.k.) fedha zinapelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za vikundi vya mafundi wa kata ili kutekeleza miradi iliyopewa vipaumbele. Kamati ya Maendeleo ya Kata hufanya mchakato wote wa manunuzi. Kwenye uchaguzi wa wazabuni Kamati ya Maendeleo ya Kata hutoa upendeleo kwa vikundi vya mafundi vya kata, kutunuku shughuli za ujenzi na kutoa malipo. Taratibu hizi (a&b) hulandana na taratibu za manunuzi ya umma, maelekezo ya matumizi ya fedha za umma, uwajibikaji na ukaguzi.

Kupanga kimkakati mafundi wasaidizi 12 katika Kata ili kuwezesha vikundi vya mafundi vya Kata kutekeleza miradi (kufanya mikutano kwenye maeneo ya ujenzi, kuandaa ratiba za kazi, manunuzi ya vifaa, ujenzi kwa kuzingatia vipimo na viwango, uandishi wa taarifa n.k.). Mafundi 4 waliopo kwenye Kata za maeneo yasiyofikika kwa urahisi wamepatiwa pikipiki ili kurahisisha safari zao.

**<u>Baraba zilizojengwa kwa Teknolojia itumiayo nguvukazi</u>**

***Ujenzi wa barabara (tangu 2010 to 2015) :***

- ***Halmashauri – Maguzoni (1.4km) – Lami***
- ***Mnazi – Mbaramo (2.1km) - Zege***
- ***Mbaramo – Wangwi (6km) – changarawe***
- ***Zimbiri – Mbaramo (6km) –***
- ***Baghai – Tewe (12km) – changarawe***
- ***Lunguza – Tewe (5.1km) – changarawe***
- ***Daraja la Kigumbe kata ya Kwai***

**<u>Majengo yaliyojengwa kwa Teknolojia itumiayo nguvukazi</u>**

***Ujenzi wa majengo ya umma (2013 hadi 2015):***

- ***Jengo la utawala shule ya sekondari ya Ndurumo***
- ***Bweni la wasichana shule ya sekondari ya Magamba***
- ***Ofisi ya kata ya Mbaramo***
- ***Kituo cha habari za Utalii***



*Kituo cha habari za utalii kilichojengwa kwa teknolojia itumiayo nguvukazi*

## 5.0 RESOURCES

Katika mpango wake wa kufungua na kuboresha barabara ili kuwa na huduma bora za ushafirishaji mwaka mzima, H/W ya Lushoto ilitumia aina mbalimbali za raslimali. Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, raslimali watu ni pamoja na watumishi wa Halmashauri, wahandisi, mafundi, mafundi wa Vijijini na wanajamii katika Vijiji na Kata. Halmashauri pia ilitumia raslimali fedha kama ilivyo kwa ufupi kwenye jedwali 1 hapa chini.

**Jedwali 1: Fedha zilizotumika kujenga barabara**

| SHUGHULI | CHANZO CHA FEDHA | GHARAMA HALISI |
|---|---|---|
| Uhamasishaji wa jamii | - | - |
| Utambuzi wa vikundi | OC | Mafuta (840Litres@2100=1,764,000.00 |
| Mafunzo kwa vikundi | Mfuko wa barabara | Mafuta (840Litres @2100=1,764,000.00 |
| Ujenzi wa barabara:<br>Halmashauri – Maguzoni (1.4km) – Lami | Mfuko wa barara | 119,492,400.00 (Vifaa na nguvu kazi) |
| Mnazi – Mbaramo (2.1km) - Zege | Mfuko wa barara | 84,687,500 Vifaa na nguvu kazi |
| Mbaramo – Wangwi (6km) – Changarawe | Mfuko wa barara | 3,700,000 Nguvukazi |
| Zimbiri – Mbaramo (6km) – Changarawe | Mfuko wa barara | 3,920,000 Nguvukazi |
| Baghai – Tewe (12km) – Changarawe | Mfuko wa barara | 21,680,800.00 Nguvukazi |
| Lunguza – Tewe (5.1km) – Changarawe | Mfuko wa barara | 10,180,000.00 Nguvukazi |
| Daraja la Kigumbe kata ya Kwai | Mfuko wa barara | 8,700,000.00 vifaa na nguvu kazi |
| Ujenzi wa majengo ya umma:<br>Jengo la utawala shule ya sekondai Ndurumo | Ruzuku ya maendeleo | 18,000,000.00 vifaa na nguvu kazi |
| Bweni la wasichana shule ya sekondari Magamba | Ruzuku | 70,000,000.00 vifaa na nguvu kazi |
| Ofisi ya kata ya Mbaramo | Ruzuku | 7,000,000.00 Vifaa na nguvu kazi |
| Manunuzi ya pikipiki 4 | Ruzuku | 14,500,000.00 |
| Usimamizi wa kawaida | Mfuko wa barabara | 6,600,000.00 |

## 6.0 MATOKEO

H/W ya Lushoto imefikia malengo yote ambayo ilipanga kufikia kwa utaratibu huu wa teknolojia itumiayo nguvukazi. Tokeo la jumla katika mbinu hii ni maboresho katika utoaji wa huduma kwa Vijiji vilivyopo katika milima yenye mwinuko mkali na vilivyojitenga lakini vikiwa na uchumi imara kupitia kilimo cha mazao ya aina mbalimbali, mbogamboga na matunda. Baadhi ya matokeo mahsusi ya mbinu ya Matumizi ya teknlojia itumiayo nguvukazi katika jamii yameelezewa hapa chini.

Halmashauri imesajili vikundi vya mafundi vya Kata 28 vyenye wajumbe, katiba na akaunti za benki. Wanavikundi wote wamepata mafunzo ya stadi za awali za ujenzi wa miundombinu (ukumbushaji wa vipimo vya ujenzi) na stadi za usimamizi (usimamizi wa fedha, ufunguaji wa akaunti za benki, uandishi na utunzaji wa vitabu, uandishi wa taarifa za utekelezaji, stadi za manunuzi n.k.)

Halmashauri sasa inatamba kwa kuwa na "barabara zinazopitika misimu yote" na majengo ya umma katika Kata za maeneo magumu kufikika kama Mnazi – Mbaramo, Mbaramo – Wangwi, Zimbiri – Mbaramo, Baghai – Tewe, Lunguza – Tewe na daraja la Kigumbe kata ya Kwai. Miaka michache iliyopita maeneo haya yalikuwa hayafikiki kwa gari.



***Barabara za Lami, Changarawe na Zege zilizojengwa kwa teknolojia itumiayo nguvukazi***

Halmashauri imepeleka mafundi wasaidizi katika kata zote zilizopo maeneo magumu kufikika. Hawa wana ari katika kusaidia vikundi vya mafundi vya Kata na Vijiji katika maboresho ya barabara ya mara kwa mara kwani barabara zilizopo milimani huhitaji matengenezo ya mara kwa mara kutokana na mmonyoko na uporomokaji wa udongo. Wanavijiji wana ari ya kupeana taarifa wao kwa wao na vikundi kuhusu maeneo yanayohitaji matengenezo ya haraka. Mafundi wasaidizi pia husaidia jamii kwenye ujenzi wa majengo ya umma kama madarasa, maabara na nyumba za watumishi.

Mbinu hii ya Matumizi ya teknolojia itumiayo nguvukazi imesaidia kupunguza gharama na kuleta thamani ya fedha katika shughuli za ujenzi wa barabara. Matumizi ya vikundi vya mafundi na wanavijiji huokoa gharama zaidi ya 50% ya gharama zote za kutumia mitambo mizito kujenga barabara. Uokoaji wa gharama pia hutokana ukweli kuwa kuna maeneo ya milima na miinuko ambayo hayawezi kufikiwa kamwe na mitambo ya ujenzi wa barabara. Hivyo mbinu hii ya teknolojia itumiayo nguvukazi ni bora na sahihi kwa maeneo haya. Jedwali 2 linaonyesha gharama ziliokolewa kwa kutumia mbinu hii.

**Jedwali 2: Gharama Halisi na Gharama Zilizopendekezwa**

| SHUGHULI | GHARAMA HALISI KWA KUTUMIA VIKUNDI | KILOMETA ZILIZOJENGWA | GHARAMA ZA MKANDARASI | GHARAMA ZA MKANDARASI KWA KM | FEDHA ZILIZO OKOLEWA (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara: Halmashauri – Maguzoni (1.4km) – Lami | 119,492,400 | 1.4 | 398,308,000 | 420m | 70 |
| Mnazi – Mbaramo (2.1km) - Zege | 84,687,500 | 2.1 | 330,750,000 | 538m | 74 |
| Mbaramo – Wangwi (6km) – Changarawe | 3,700,000 | 6 | 9,000,000 | 1.8 | 50.9 |
| Zimbiri – Mbaramo (6km) – Changarawe | 3,920,000 | 6 | 9,000,000 | 2.6 | 50.6 |
| Baghai – Tewe (12km) – Changarawe | 21,680,800 | 12 | 72,000,000 | 3.6 | 69.9 |

| SHUGHULI | GHARAMA HALISI KWA KUTUMIA VIKUNDI | KILOMETA ZILIZOJENGWA | GHARAMA ZA MKANDARASI | GHARAMA ZA MKANDARASI KWA KM | FEDHA ZILIZO OKOLEWA (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Lunguza – Tewe (5.1km) – Changarawe | 10,180,000 | 5.1 | 30,600,000 | 1.7 | 66.7 |
| Daraja la Kigumbe kata ya Kwai | 8,700,000 | Daraja la 3.5m upana 5m urefu | 24,870,000 | Daraja la 2.2m upana 2.5m urefu | 65 |
| Ujenzi wa majengo ya umma: Jengo la utawala sekondari ya Ndurumo | 36,000,000 | Ujenzi wa jengo la utawala lenye $216m^2$ | 64,800,000 | Ujenzi wa jingo la utawala lenye $120m^2$ | 44.4 |
| Ujenzi wa bweni la wasichana shule ya sekindari Magamba | 94,000,000 | Ujenzi wa bweni la wasichana lenye $1885m^2$ | 282,275,000.00 | Ujenzi wa bweni la wasichana lenye $627m^2$ | 66.7 |
| Ujenzi wa ofisi ya kata Mbaramo | 7,000,000.00 | Ujenzi wa ofisi yeneye $56m^2$ | 16,800,000.00 | Ujenzi wa ofisi yenye $23.3m^2$ | 58.3 |

Halmashauri pia iliokoa gharama za kutosha na kupata thamani ya fedha katika ujenzi wa majengo ya umma. Jedwali 3 linaonyesha mifano ya gharama zilizookolewa.

**Jedwali 3: Gharama zilizookolewa kwenye ujenzi wa majengo ya umma**

| Shughuli | Gharama halisi kwa kutumia vikundi (Tshs) | Gharama za Mkandarasi (Tshs) | Zilizookolewa (%) |
|---|---|---|---|
| Ujenzi wa majengo ya umma: Jengo la utawala sekondari ya Ndurumo | 36,000,000 | 64,800,000 | 44.4 |
| Ujenzi wa bweni la wasichana shule ya sekondari Magamba | 94,000,000 | 282,275,000 | 66.7 |
| Ujenzi wa ofisi ya Kata Mbaramo | 7,000,000 | 16,800,000 | 58.3 |

Kupitia matumizi ya teknolojia itumiayo nguvukazi H/W ya Lushoto imefanikiwa katika yafuatayo;

(i) Halmashauri inaweza kutoa huduma za umma (elimu, afya na usafiri) kutokana na kuwepo kwa miundombinu iliyoboreshwa hasa katika maeneo magumu kufikika.

(ii) Jamii zilizopo katika Kata zilizopo kwenye maeneo magumu kufikika zinaweza kuyafikia masoko ya mazao yao ya kilimo (tangawizi, iliki na mazao mengine) kwa urahisi.

(iii) Usafiri wa umma umeimarika na wananchi wanaweza kufika kwa urahisi katika makao makuu ya Halmashauri na vituo vya biashara.

(iv) Kuna umiliki wa kutosha wa miradi iliyojengwa katika jamii. Hii ni kwa sababu vikundi vya mafundi vya Kata vilishiriki katika utekelezaji wa miradi na usimamizi wa fedha na kujenga mtazamo chanya wa kuthamini miradi yao. Hii imeleta uhakika katika utunzaji na ukarabati endelevu wa miundombinu iliyojengwa.

(v) Vipato vya jamii zilizopo katika maeneo haya magumu kufikika vimeongezeka na kupelekea matumizi ya pikipiki kama njia mbadala na rahisi ya usafiri wa umma na mazao ya kilimo.

(vi) Baada ya utekelezaji wa miradi, vikundi vya mafundi hutenga 5% za akiba zao ili kutoa msaada wa ustawi wa jamii kwa wazee (2.5%) na walemavu (2.5%). Hili limefanya jamii kwa ujumla kupongeza na kuviunga mkono zaidi vikundi vya mafundi.

(vii) H/W ya Lushoto imekuwa na kundi kubwa la mafundi wenye uzoefu ambao hutumiwa mara kwa mara na wakandarasi wenye sifa katika Halmashauri nyingine. Mafundi hawa wamesaidia pia kupunguza gharama za usimamizi na ufuatiliaji kwani Halmashauri huwatumia kwa mazoezi haya bila kutuma wahandisi toka makao makuu.

(viii) Mbinu hii ya Matumizi ya Teknolojia inayotumia nguvukazi imejenga uhusiano mzuri kati ya jamii zinazoishi kwenye kata zenye ugumu kufikika na Halmashauri, kati ya madiwani na watumishi na kati wakandarasi na jamii.



***Injinia wa Halmashauri akiwa na mtumia barabara mwenye furaha***

(ix) Mbinu hii ya Matumizi ya Teknolojia inayotumia nguvukazi imeonyesha ubora katika matumizi ya akaunti maalum ili kuokoa gharama na kukamilisha miradi yenye ubora ndani ya muda uliopangwa na kuleta maendeleo ya jamii kwa haraka.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

H/W ya Lushoto imejiwekea mikakati mbalimbali ya kuifanya mbinu hii kuwa endelevu na kuhakikisha kuwa jamii zilizopo kwenye maeneo magumu kufikika zinaendelea kupata huduma endelevu za umma. Mkakati mojawapo kabambe ni uimarishaji wa vikundi vya mafundi ili vifikie kusajiliwa kama wakandarasi jamii. Hii itasaidia Halmashauri kuingia mikataba ya ujenzi na wakandarasi jamii siku za mbele, badala ya utaratibu wa sasa wa kuviunganisha vikundi vya mafundi na wakandarasi binafsi waliosajiliwa.

H/W ya Lushoto imeweka mkakati wa kuhakikisha barabara nyingi zinaanzishwa na kuboreshwa katika Kata na Vijiji vyote vinavyochukuliwa kuwa “vigumu kufikika”. Sambamba na hili Halmashauri imedhamiria kuimarisha ushirikiano imara na vikundi vya mafundi vya Kata na jamii ili matengenezo ya barabara ya mara kwa mara kwenye maeneo magumu kufikika yafanyike kwa muda na ufanisi.

Mikakati mingine inajumuisha (i) mafunzo na ubadilishanaji wa uzoefu wa mara kwa mara wa vikundi vya mafundi pamoja na kuwapeleka viongozi wa vikundi kwenye mafunzo zaidi katika chuo cha Teknolojia rahisi na sahihi (ATTI) kilichopo Mbeya (ii) kuimarisha shughuli za vikundi vya mafundi kwa kuvisaidia kumiliki vifaa vya ujenzi kwa mfumo wa teknojia inayotumia nguvukazi na (iii) ufuatiliaji endelevu na usimamizi saidizi unaofanywa na idara ya Ujenzi.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

H/W ya Lushoto hupata changamoto zilezile ambazo Halmashauri nyingine za Tanzania hupata. Kupata matokeo chanya katika matumizi ya teknoljia inayotumia nguvukazi kuna sababu nyingi zilizojificha ambazo ziliwezesha mafaniko haya. Hizi zinajumuisha;

(i) Utayari wa mafundi kujipanga katika vikundi vya Kata na kukubali jukumu la ujenzi.
(ii) Utayari wa Wanasiasa (madiwani, mkuu wa wilaya, mbunge) kusaidia mpango huu.

(iii) Uongozi wenye dira wa mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri na umoja kati ya wajumbe wa timu ya menejimenti ya Halmashauri katika utekelezaji wa mbinu hii.
(iv) Matumizi bora na makini ya mfumo wa akaunti maalumu (*force account*).
(v) Ubunifu wa Mhandisi wa Halmashauri katika kuanzisha na kutekeleza mbinu hii huku akijitoa na kufanya kazi na jamii bila kuchoka.
(vi) Usimikaji wa mafundi wasaidizi 12 katika kila Kata iliyopo katika maeneo magumu kufikika ambao wanaishi na jamii na kufuatilia shughuli za kila siku.
(vii) Ufuatiliaji wa karibu wa wakandarasi unaofanywa na Halmashauri kila siku za utekelezaji ili kuhakikisha ubora wa miradi.



***Jengo jipya la Halmashauri lilisimamiwa kwa karibu na Mhandisi wa Halmashauri***

(viii) Kupanga matumizi ya fedha kimkakati na kwa vipaumbele kwa ajili ya Kata zilizopo katika maeneo magumu kufikika na kwa miradi inayozingatia mahitaji sahii ya jamii.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI


**UJENZI WA BARABARA YA ISIPII- MPANGA TAZARA KWA TEKNOLOJIA ITUMIAYO NGUVUKAZI**



***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi***

## 1.0 INTRODUCTION

Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilianzishwa mapema miaka ya 1970. Halmashauri hii ni mojawapo ya Halmashauri 5 za mkoa wa Iringa na ipo 80Km Kusini mwa Manispaa ya Iringa. Halmashauri nyingine ni Manisapaa ya Iringa, Mji wa Mafinga na Halmashauri za Wilaya za Iringa na Kilolo. H/W ya Mufindi inapakana na Mkoa wa Njombe upande wa Kusini, Mkoa wa Mbeya upande wa Magharibi, H/W ya Iringa Kakazini na H/W ya Kilolo upande wa Kaskazini Mashariki. Makao Makuu ya Halmashauri yapo Mafinga Mjini kwenye barabara kuu iendayo Mbeya. Kwa utambulisho wa kimataifa Halmashauri inapatikana katika Latitudo 8$^{o}$.0’ na 9$^{o}$.0’ Kusini mwa Ikweta na Longitudo 30$^{o}$.0’ na 36$^{o}$.0’ Mashariki mwa Griniwichi. Ardhi ya Halmashauri imefunikwa na misitu (10,411.3 Km$^{2}$) na 2,427.6Km$^{2}$ pekee ndio zimebaki kwa shughuli za binadamu.




Kabila kuu ni Wahehe ambao huunda 85% ya wakazi wote. Shughuli kuu ya wakazi hawa ni kilimo ikifuatiwa na ufugaji mdogo. Wabena, Wakinga na wengine ndio huunda 15% ilitobaki. Makabila haya yalihamia Mufindi wakitoka Halmashauri za jirani za Njombe na Makete katika kutafuta kazi kwenye viwanda vya Chai na Mbao ikiwa ni pamoja na ajira katika taasisi za serikali. Jedwali 1 hapa chini linaonyesha Tarafa na makabila makuu.

**Jedwali 1: Mgawanyo wa Makabila Makuu Matano kwa Tarafa**

| S/No. | TARAFA | ENEO km$^{2}$ | KATA | IDADI YA MAKABILA | ORODHA YA MAKABILA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ifwagi | 2,100 | 9 | 3 | Wahehe, Wakinga and Wabena |
| 2 | Kasanga | 1,500 | 8 | 3 | Wahehe, Wakinga and Wabena |
| 3 | Kibengu | 820 | 3 | 2 | Wahehe and Wabena |
| 4 | Malangali | 1,500 | 6 | 3 | Wahehe, Wakinga and Wabena |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **5** | Sadani | 1,203 | 4 | 2 | Wahehe and Wabena |
| | **Jumla** | **7,123** | **30** | | |

Ikilinganishwa na Sensa yawatu na makazi 2001, idadi ya watu ya H/W ya Mufindi iliongezeka kutoka 272,071 mwaka 2002 hadi 317,731 mwaka 2012 ambao ni 34% ya wakazi wote wa Mkoa wa Iringa na ongezeko la wastani la mwaka la 1.5%. H/W ya Mufindi inakadiriwa kuwa na ongezeko la chini la watu ikilinganishwa na Halmashauri nyingine Mkoani. Ongezeko hili lipo chini ya ongezeko la Mkoa la 1.6% na Ongezeko la wastani la kitaifa la 2.4%. kwa mujibu wa makisio ya idadi ya watu ya mwaka 2008, H/W ya Mufindi ndio yenye msongamano mkubwa wa watu Mkoani na pato lake kwa mwaka likiwa TZS 1,206,917.


Halmashauri imegawanyika katika Tarafa tano za Ifwagi, Sadani, Kibengu, Kasanga and Malangali, Kata 30, Vijiji 125 na Vitongoji 808 vilivyogawanyika kama ilivyonyeshwa kwenye Jedwali 2.

**Jedwali 2: Eneo na Mgawanyiko wa Kiutawala**

| S/No. | Tarafa | Eneo $Km^2$ | Kata | Vijiji | Vitongoji | % Eneo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Ifwagi | 2,100 | 9 | 32 | 150 | 29.5 |
| **2** | Kasanga | 1,500 | 8 | 32 | 158 | 21.1 |
| **3** | Kibengu | 820 | 3 | 16 | 81 | 11.5 |
| **4** | Malangali | 1,500 | 6 | 27 | 133 | 21.1 |
| **5** | Sadani | 1,203 | 4 | 18 | 86 | 16.9 |
| | **Jumla** | **7,123** | **30** | **125** | **608** | **100.0** |

Uchumi wa H/W ya Mufindi umetawaliwa na kilimo ambacho huajiri zaidi ya 85% ya wakazi. Mazao yote ya biashara na chakula huzalishwa, ya chakula yakizalishwa zaidi. Kwa mujibu wa utafiti wa pato la Mkoa wa mwaka 2008, kilimo huchangia takribani 91% ya pato lote la Halmashauri ambapo uzalishaji wa mazao huchangia 90.2% ikifuatiwa na ufugaji (0.7%), pia uwindaji na misitu huchangia 0.2%. Maendeleo mazuri kiasi ya sekta ya viwanda yametokana na uwepo wa makampuni makubwa yanayojihusisha na uzalishaji na uchakataji wa pareto na chai. Makampuni haya ni Kampuni ya Pareto ya Tanzania (PCT) na Kampuni ya Kuchakata na Kufungasha Chai (Uniliver Tea Tanzania Ltd, Mufindi Tea Company and Chai Bora). Kampuni ya Chai Bora, kimsingi ni ya kufungasha chai wakati makampuni mengine mawili ni ya uchakataji. Sekta ya viwanda pia inaimarishwa na uwepo wa viwanda vinavyo chakata magogo ikiwa ni pamoja na Kiwanda cha Mufindi cha Karatasi (MPM) pale Mgololo, Kiwanda cha Sao Hill na viwanda vingine vingi vidogo.

**Mchoro 1. Mchango wa Sekta Kwenye Pato**



**2.0 TATIZO**

Kijiji cha Mpanga – TAZARA kimejitenga na kipo 155Km kutoka Mafinga Mjini (Makao Makuu ya H/W ya Mufindi). Vijiji vya jirani vipo 25km kwa pande zote. Barabara pekee ya kwenda makao makuu ya Halmashauri ipo Kijiji cha Isipii 25km kutoka Mpanga – TAZARA. Kwa miaka takribani 27 na kutokana na ukosefu wa fedha (zilizokadiriwa 800 milioni) za ujenzi wa barabara, Kijiji kilitegemea reli ya TAZARA tu kama namna pekee ya usafiri na mawasiliano. Ili mtu aweze kufika makau makuu ya Halmashauri, njia pekee ilikuwa kupanda treni mpaka Makambako ambapo ni 80km na kuunganisha kwa basi kutoka Makambako mpaka Mafinga umbali mwingine wa 101km. Zaidi ya hiyo ratiba ya treni ilikuwa mara mbili tu kwa wiki tena usiku wa manane. Kurudi Kijijini ilibidi kushinda Makambako na kusubiri treni suala ambalo lilikuwa linahusisha gharama kubwa za kuishi. Baadaye ratiba ya Treni ilipunguzwa na kuwa ya mara moja kwa wiki. Mara kwa mara huduma za TAZARA zilisitishwa kutokana na kuharibika treni au reli na migomo ya wafanyakazi iliyochukua siku, wiki au miezi kadhaa. Kutokana na matatizo haya yote wanakijiji waliteseka kwa haya yafuatayo;

- Utawala duni; kuwafikia maafisa watendaji wa Kata, watendaji wa Vijiji na maafisa ugani kutoka makao makuu lilikuwa suala gumu. Pia ilikuwa ni vigumu sana kuwafanya watumishi kuishi na kuboresha utoaji wa huduma. Kwa kuzingatia tatizo hili Halmashauri ililazimika kukifanya kijiji kimoja cha Mpanga – TAZARA kuwa Kata, suala ambalo ni la gharama kubwa.
- Utoaji duni wa huduma uliodhihirika katika ugawaji wa vifaa vya elimu na huduma za gari la wagonjwa kwani shule na zahanati hazikuweza kufikiwa na magari ya Halmashauri au magari mengine.
- Usafirishaji duni, usiotabirika na ghali wa mazao ya kilimo. Eneo la Isipii – Mpanga TAZARA linafaa sana kwa uzalishaji wa mananasi, viazi vikuu, ndizi, mhogo na matunda, lakini mazao haya hayakuweza kuyafikia masoko na kuongeza vipato vya kaya kutokana na ukosefu wa barabara.
- Matumizi duni ya raslimali za ardhi na maji; kijiji cha Mpanga – TAZARA kina ardhi ya milima yenye fursa za kilimo na misitu lakini zimekuwa zikitumiwa kwa kiwango duni kutokana na ugumu wa kufikika.
- Viwango duni kabisa vya maisha. Kutokana na matatizo haya yote wanavijiji wa eneo la Isipii – Mpanga TAZARA walishuhudia kuporomoka kwa vipato, makazi duni na kushuka kwa huduma vyote kwa pamoja vikileta umaskini uliokithiri na viwango duni vya kuishi.

**3.0 LENGO**

Wanaviji wa Isipiii – Mpanga TAZARA waliweka azimio imara la kufanikisha kufungua barabara. Lengo kuu la jamii lilikuwa kupata huduma bora za kijamii na kiuchumi katika Kata na Kijiji cha Mpanga – TAZARA kwa kujenga barabara ya 25Km kutoka kijiji cha Isipii hadi Mpanga – TAZARA. Matokeo tarajiwa yalijumuisha;

- Usafirishaji bora wa bidhaa
- Upatikanaji wa uhakika wa huduma za afya (usafirishai wa madawa n.k.)
- Kuongeza utayari wa watumishi kuishi kijijini
- Kuwavutia kwa wingi wawekezaji kwenye kilimo na hasa misitu
- Kuongeza thamani ya ardhi – kupandisha uhitaji wa ardhi
- Kuongeza safari za ukaguzi za maafisa elimu ili kuboresha elimu ya msingi
- Kuboresha usafirishaji wa mazao ya kilimo kwenda kwenye masoko (kuwepo kwa pikipiki binafsi kwa wanakijiji)
- Mawasiliano bora kati ya kijiji na masoko

- Kuongezeka kwa mahusiano na maeneo ya jirani
- Kuongeza viwango vya kuishi

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Ujenzi wa barabara ulihusisha awamu mbili. Awamu ya kwanza ilifanyika kipindi cha mwaka 2008 – 2009. Shughuli za awamu ya kwanza zilihusisha uhamasishaji mkuu wa jamii na ukusanyaji wa raslimali; ikimaanisha wanakijiji kujipanga na kuweka kipaumbele katika ujenzi wa barabara ya Mpanga TAZARA – Isipii. Hili lilihusisha mikutano katika ngazi ya kijiji ili kuanza kuchimba barabara, kushauriana na vijiji vingine faidika (Isipii, Ibwanzi, Ihanu, Lulanda and Ikanga) na kupeleka maamuzi ya Kijiji kwenye Halmashauri ya Wilaya. Kijiji cha Lulanda kilianza kidogokidogo kuchimba 10Km za barabara kuelekea kijiji cha Mpanga – TAZARA, ambacho nacho kilijiunga kuchimba barabara kuelekea kijiji cha Isipii.

Baada ya kushuhudia jitihada za Vijiji, Halmashauri ya Wilaya iliamua kutoa usaidizi wa utaalam na fedha. Hili lilitokea baada ya uhamasishaji na ushawishi kwa madiwani ili watenge raslimali kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Upimaji shirikishi wa barabara uliohusisha upimaji na uchoraji wa barabara ya kutoka Isipii mpaka kijiji cha Mpanga – TAZARA ulifanyika mwaka 2008/09. Wataalmu wawili wa barabara wakishirikiana na wanavijiji wa Isipii, Ibwanzi, Ihanu, Lulanda, Ikanga and Mpanga – TAZARA walishiriki kwa hiari kwenye kazi za kupima na kusafisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa barabara.



***Miti mikubwa iliyoondolewa***

Ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia inayotumia nguvukazi ulianza mwaka 2008/09 na kukamilika 2009/10 ulihusisha watu 40 kwa siku kutoka vijiji faidika. Wanavijiji kutoka Isipii, Ibwanzi, Ihanu, Lulanda, Ikanga and Mpanga – TAZARA walishiriki katika ujenzi huu kwa kukata miti, kuchimba ardhi, kukusanya mawe, kujenga mifereji na kulaza mbao ili kujenga madaraja. Shughuli zote hizi zilisimamiwa na wataalamu wa Halmashauri ambao walifanya kazi na wanavijiji usiku na mchana.



***Shughuli za ujenzi zikiendelea***

Kujenga uwezo wa Viongozi wa Magenge. Wanavijiji na wataalam wa Halmashauri waliunda vikundi vya vijana katika kila kijiji kilichopo kwenye barabara ya Isiipii – Mpanga – TAZARA na kuunda magenge ya mafundi wenyeji. Kila genge lilipatiwa kiongozi. Viongozi wa magenge walipatiwa mafunzo kwa lengo la kujenga uwezo wa mafundi wenyeji. Mafunzo yalielezea masuala ya uhamasishaji jamii, ukaguzi wa barabara, ukarabati wa barabara na utumiaji wa raslimali na vifaa vya asili katika matengenezo ya

barabara.  Viongozi wa magenge wana jukumu la kuhakikisha barabara inapitika mwaka mzima kwa kushirikisha wanagenge na jamii kwa ujumla katika vijiji vyote.

Awamu ya pili ya ujenzi wa barabara ya Isipii – Mpanga – TAZARA ilifanyika katika mwaka ya fedha wa 2012/2013. Baada ya kupata mafanikio katika awamu ya kwanza jamii na Halmashauri zilijikita katika kuboresha barabara ili ifikie kiwango cha Wilaya kwa kutumia tecknolojia inayotumia mitambo. Jamii ilijipanga kuhakikisha kuwa matengenezo ya barabara yanafanyika kwa muda hasa wakati wa msimu wa mvua. Shughuli za Magenge na Viongozi wao ziliongezwa na kuhusisha ukaguzi wa mara kwa mara wa maeneo ambayo yanahitaji marekebisho ya haraka hasa wakati wa msimu wa mvua.



***Barabara iliyoshindiliwa vizuri katika eneo la milima***

**5.0 RASLIMALI**

Jamii na Halmashauri zilitoa aina mbalimbali za raslimali katika awamu zote mbili. Bajeti iliyotengwa kutoka fedha za ndani za Halmashauri kwa ajili ya awamu ya kwanza zilikuwa shs 18 milioni na baadaye Halmashauri ilitenga shs 105 milioni kwa ajili ya awamu ya pili. Halmashauri pia ilitumia magari 2 kwa usafiri wa wataalamu wa Halmashauri na vifaa na ilihakikisha mafuta yanakuwepo kipindi chote cha ujenzi wa barabara.

Halmashauri pia ilitoa wataalamu kwa ajili ya upimaji, ujenzi, usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya teknolojia itumiayo nguvukazi. Tatu, jamii kwa ujumla ilishiriki kwa hiari katika ujenzi wa barabara. Ushiriki wa jamii kutoka vijiji sita vya Isipii, Ibwanzi, Ihanu, Lulanda, Mpanga - TAZARA na Ikanga ulifanyika kila siku kwa idadi ya watu wasiopungua 40 wakifanya kazi katika mradi. Kuboresha ushiriki wa jamii Halmashauri ilihakikisha vifaa vyote vinavyotumika katika teknolojia itumiyo nguvukazi kama mashine za kushindilia udongo za mikono, magreda, majembe, mundu na mapanga vinakuwepo. Ushiriki wa jamii ulipunguza gharama za ujenzi kutoka makadirio ya shs 800 milioni mpaka shs 123 milioni tu (yaani 15% tu ya gharama za kandarasi)

**6.0 MATOKEO**

Jamii na Halmashauri zilifikia malengo ya kujenga barabara kwa teknolojia inayotumia nguvukazi. Barabara hiyo ya 25Km na yenye thamani kubwa kwa jamii ipo na inawezesha magari madogo, pikipiki, baiskeli na watu kupita; ingawa haipitiki kwa mwaka mzima hasa msimu wa mvua nyingi. Barabara hii imeboresha mawasiliano ya wananchi wa vijiji sita na makao makuu ya Halmashauri. Walimu, watumishi wa afya, na maafisa ugani sasa hufurahia kwenda makao makuu ya Halmashauri kupata huduma mbalimbali kwa kutumia barabara hii ambayo imepunguza sana muda uliokuwa unatumika kwa njia ya reli na Makambako.



***Barabara iliyochongwa vizuri ikipita katikati ya misitu ya savana***

Kumekuwa na maboresho katika huduma za afya na elimu kwa magari ya wagonjwa na mitihani yanaweza kufika kijijini Mpanga – TAZARA. Shule za Msingi sasa zinaweza kutembelewa ili kufanyiwa ukaguzi na ufuatiliaji wakati vituo vya huduma za afya vijijini vinaweza kupatiwa madawa na vifaatiba kutoka Halmashauri. Maboresho katika huduma za afya yamejidhihirisha kwani kwa sasa pikipiki zinatumia barabara hii kupeleka wagonjwa hospitali zilizopo katika maeneo mengine ya Halmashauri. Hili ni tokeo la kuwepo kwa barabara.

Uwepo wa viongozi 12 wa magenge waliopata mafunzo ya teknolojia itumiayo nguvukazi ni tokeo kuu. Viongozi hawa hupanga vikundi ili kugundua mapema uharibifu wa barabara na kufanya matengenezo. Ikitokea uharibifu mkubwa wa barabara viongozi hawa hutoa taarifa za haraka kwa jamii ili jamii ishiriki kwenye shughuli za ukarabati. Mara chache, viongozi wa magenge huomba msaada wa Halmashauri wa vifaa na utaalamu wa teknolojia itumiayo nguvukazi.

Barabara imeleta mabadiliko makubwa katika kiutawala. Wakati maafisa watendaji wa Kata, watendaji wa vijiji na madiwani wanaweza kwenda kwa urahisi makao makuu ya Halmashauri, watumishi kutoka makao makuu ya Halmashauri wanaweza kufuatilia na kusimamia utoaji wa huduma bila vikwazo. Utayari wa watumishi kuishi kijijini umeimarika kwani shule ya msingi ina walimu 7 na zahanati ina watumishi kadhaa.

Barabara ya Isipii – Mpanga - TAZARA imeleta fursa kubwa ya uwekezaji katika vijiji sita. Wawekezaji wenyeji wamevutiwa sana hasa wale wanajishughulisha na upandaji wa miti kufuata barabara iliyojengwa. Vijiji vya Isipii na Mpanga – TAZARA vimejaliwa milima ambayo hupata mvua za kutosha kwa mwaka na kufanya upandaji na uvunaji wa miti kuwa biashara yenye faida sana. Fursa hii haikutumika katika vijiji hivi kutokana na ukosefu wa barabara.



***Miti liyopandwa milimani karibu na barabara ya Isipii – Mpanga Tazara***

Viwango vya maisha ya watu waishio karibu na barabara ya vijiji vya Isipii – Mpanga –TAZARA vinapanda. Wakati baadhi ya wanajamii wanamiliki pikipiki, ujenzi wa nyumba za kisaa umeongezeka kwani vifaa vya ujenzi vinaweza kusafirishwa kwa urahisi kuja vijijini. Maduka na biashara zinaongezeka

na uuzaji wa mazao ya kilimo na usafirishaji wake vimekuwa vya uhakika. Haya yote huleta uhakika katika pato la kaya na hivyo kuimarika kwa viwango vya maisha na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Pamoja na mafaniko yaliyopatikana, kuna changamoto kama maporomoko ya ardhi ya mara kwa mara, milima na upungufu wa fedha ambavyo kwa pamoja vinahitaji mikakati ya uendelevu. Mkakati mmoja muhimu ni ushirikiano bora kati ya jamii na Halmashauri. Ushirikiano huu huhakikisha kuwa barabara inapitika mwaka mzima kwani marekebisho ya kawaida kufanywa kwa urahisi na wanakijiji na Halmashauri.

Mkakati wa pili ni uanzishaji wa magenge na viongozi wa magenge. Viongozi 12 wa magenge wamesajiliwa kama wakandarasi wa daraja la tatu katika teknolojia itumiayo nguvukazi ili kutoa huduma za ujenzi na ukarabati wa barabara katika vijiji vya jirani na kulingana na teknolojia iliyopo. Viongozi wa magenge pia huhakikisha jamii zina motisha wa kutunza barabara katika kila kijiji. Magenge haya yanapata motisha kwani Halmashauri inapofanya matengenezo makubwa ya barabara, magenge haya hupewa kandarasi na hulipwa kwa huduma zao.

Mkakati wa mwisho unahusu uhamasishaji usiokoma wa wadau mbalimbali ili kupanga na kutenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara ikiwa ni pamoja uboreshaji wa maeneo korofi na ukarabati wa msimu. Halmashauri pia hutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati na maboresho ya barabara hii.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya ujenzi wa barabara ya Vijiji vya Isipii na Mpanga – TAZARA yana siri nyingi za mafanikio. Siri hizi zinajumuisha utayari wa jamii kushiriki kikamilifu katika mchakato wote kuanzia upimaji, uchoraji na uteelezaji, ushiriki kamilifu wa Madiwani katika kuhamasisha jamii na utambuzi na matumizi ya teknolojia itumiayo nguvukazi katika ujenzi wa barabara. Siri nyingine ni uwepo na utayari wa Halmashauri kutoa utaalamu (watumishi kutoka ofisi ya mhandisi wa wilaya), umoja imara wa watumishi mbalimbali wa Halmashauri na utekelezaji bora wa kutimiza hitaji la jamii (barabara). Katika yote utimizaji wa hitaji la jamii kwa kutumia teknolojia itumiayo nguvukazi katika kujenga barabara ndio kiini cha siri hizi zote.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

**JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUBORESHA BARABARA ZA KIJIJI**



*Uzoefu wa Kata ya Kimochi*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilianzishwa Januari, 1994 kwa sheria namba Serikali za mitaa namba 8 na 9 ya1982. Halmashauri inapatikana kati ya longitudo $37^0$ hadi $38^0$ Mashariki na Longitudo $2^0 3^0$ hadi $50^0$ Kusini. Halmashauri inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Rombo upande wa Kaskazini, Nchi ya Kenya upande wa Mashariki, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga upande wa kusini, Halmashauri za wilaya za Hai na Simanjiro upande wa Magharibi.

Ukanda wa kati uko kati ya 901m - 1500m juu ya usawa wa bahari na ni mzuri kwa shughuli za kilimo kama kahawa, mahindi, maharagwe na matunda. Pia kuna ufugaji wa ng'ombe. Ukanda wa juu upo kandokando ya Mlima Kilimanjaro na una mgandamizo mkubwa wa watu kwa eneo (400-800 kwa $km^2$) na upo kati ya 1501m-5892m juu ya usawa wa bahari. Wakazi wa ukanda huu hujishighulisha na kilimo, upandaji wa miti na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Mazao makuu yanayozalishwa ni kahawa, ndizi, matunda na mbogamboga. Pia kuna uzalishaji mkubwa wa kutokana na kuwepo kwa miti ya aina mbalimbali.




Kwa mujibu wa  sensa ya 2012,Halmashauri ina idadi ya watu 466,737 kati yao 225,767 ni wanaume na 240,970 ni wanawake na wastani wa watu katika kaya ni 4.2. Halmashauri ina tarafa 4, Kata 31, Vijiji 145 na Vitongoji 689. Kata ya Kimochi ina watu 13,562. Kati yao wanaume ni 6476 na wanawake 7086.

Halmashauri Wilaya ya Moshi ina barabara zenye jumla ya urefu wa 697.34 km na kati ya hizo, barabara zenye urefu wa 176.3 km ziko chini ya usimamizi wa Halmashauri na 520.94km barabara za vijijini. Barabara zenye urefu wa takribani 176.3km ni za changarawe na zinapitika kwa mwaka mzima. Barabara zenye urefu wa 520.94km ni barabara ya udongo zisizopitika kipindi ya mvua. 80% ya barabara za Halmashauri ziko milimani na udongo ni wa volcano.

**2.0 TATIZO**

Licha ya ukweli kuwa barabara za vijijini ni muhimu kwa uchumi, kwa miaka mingi Kata ya Kimochi ilikuwa na barabara zisizopitika msimu wa mvua. Hii ilifanya wananchi kushindwa kupata huduma za kiuchumi na kijamii (hospitali, kanisani, sokoni n.k). Kwa mtazamo mwingine barabara mbovu zingesababisha ajali na kuongeza muda wa kusafiri hasa kwenda na kutoka Moshi mjini ambako kuna shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii. Hii ilichangiwa na ukweli kwamba mfuko wa barabara hausaidii kurekebisha barabara za vijiji.

**Jedwali 1: Orodha ya barabara ambazo hazikupitika**

| Na | Jina la barabara | Urefu (km) | Pesa iliyotolewa | Matatizo | Vikwazo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Old Moshi-Mdawi-Kisaseni | 7.9 | Hakuna | Kuna mashimo makubwa na imekatika katika sana kiasi cha kuathiri watumiaji-wagonjwa na watalii | Hakuna fedha ya kutosha serikalini. Maji mengi hutiririka juu ya barabara wakati wa mvua |
| 2 | Manyumbu-Kisaseni-Kitimbirihu | 3.8 | Hakuna | Haipitiki na inateleza | Maji mengi hutiririka juu ya barabara msimu wa mvua |
| 3 | Mangawo-Kisaseni-Kitimbirihu | 3.0 | Hakuna | Haipitiki na inateleza | Maji mengi hutiririka juu ya barabara msimu wa mvua |
| 4 | Matiko-kishimbo kwa Goodluck-Mharaeni | 1.6 | Hakuna | Haipitiki na inateleza | Maji mengi hutiririka juu ya barabara msimu wa mvua |
| 5 | Ufundi kwa mrodi Kombere | 4.5 | Hakuna | Haipitiki na inateleza | Maji mengi hutiririka juu ya barabara msimu wa mvua |
| 6 | Nduweni-Mangoro | 0.25 | Hakuna | Haipitiki na inateleza | Maji mengi hutiririka juu ya barabara |
| 7 | Mailunyi-Kilyambala | 0.25 | Hakuna | Haipitiki na inateleza | Maji mengi hutiririka juu ya barabara msimu wa mvua |



*Sehemu za barabara Nduweni-Mangoro na Mailunyi Kilyambala kabla ya Ukarabati*

**4.0 MALENGO**

Lengo kuu la jamii ya kata ya kimochi lilikuwa kuhakikisha jamii inapata barabara za kijiji za uhakika kwa ajili ya usafishaji fanisi, kufikia kwa urahisi huduma za kijamii na kiuchumi kwa mwaka mzima na hatimaye kuboresha maisha ya kupitia jitihada za jamii. Malengo mahsusi yalikuwa;

(i) Kuboresha na kuhifadhi barabara zao ili zipitike mwaka mzima
(ii) Kuimarisha usafirishaji wa mazao ya kilimo hadi sokoni, hasa Moshi mjini
(iii) Kuhakikisha kufika kwa urahisi kwenye huduma za afya, elimu, ibada na masoko

## 5.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Wananchi wa kata ya Kimochi waliamua kutumia nguvu zao wenyewe kutengeneza barabara za kijiji. Kwasasa juhudi kama hizi ni muhimu sana kutokana na ufinyu wa bajeti na miradi kutokamilika katika Tanzania. Pia Mchakato wa fursa na vikwazo kwa maendeleo Ulioboreshwa (O&OD) huhitaji jitihada za wananchi kujiletea maendeleo ya wenyewe badala ya kusubiri Serikali kufanya kila kitu. Aidha mfumo ulioboreshwa wa ruzuku (LGDG) unawataka wananchi kutumia jitihada zao wenyewe kuleta maendeleo. Sehemu hii itaendelea kueleza kwa kina umuhimu wa jitihada za Jamii ili MSM katika Tanzania ziweze kuiga ili kuchochea maendeleo ya jamii.

Jitihada za jamii humaanisha juhudi za jamii au binafsi, kaya au vikundi vya jamii katika kuboresha huduma za kijamii, bila kusubiri misaada toka serikalini au mashirika yasiyo ya kiserikali. Mtu binafsi, kaya au kundi hugharimikia mradi fulani kwa kutoa fedha au nguvu. Huku umiliki unaweza kuwa wazi au usiwe wazi kisheria, haifikiriwi kuwa serikali au shirika lisilo la kiserikali humiliki mradi wote au sehemu yake.

Jitihada za kujikwamua kwa kutumia juhudi binafsi huandaliwa kuanzia ngazi ya chini kabisa kwa kushirikisha watu bila kutegemea fedha za serikali, ili kukidhi mahitaji muhimu (mfano chakula n.k) kwa kukusanya rasilimali zao wenyewe. Mikakati binafsi ya kujikwamua ni mipango inayowezesha jamii kukidhi mahitaji yao muhimu. Mipango hii huilazimisha jamii kutumia rasilimali zilizopo tu bila kutegemea msaada kutoka kwingine. Mpango huu ulazimisha jamii kuangalia uwezo wao wenyewe wa kufanya jambo fulani ili waweze kunufaika. Ili jamii iweze kujiletea maendeleo yenyewe lazima kuhimiza na kutumia watu vizuri ili wakubali kuchagua mradi ambao watatekeleza bila kushindwa.

Mkakati kama huu huhitaji zaidi kuwa na watu wenye fikra, uadilifu na maono sawa kuliko kuwa na mtaji na mazingira mazuri ya uwekezaji. Ni lazima mambo yote muhimu yawepo kwa wakati mmoja, serikali pia huandaa mazingira bora kwa wenye mikakati kama hii. Mifumo mingi ya kijamii ni lazima iwe rafiki pia. Miradi ambayo huanzishwa na wananchi wenyewe inaweza kuwa ya idadi yoyote ilimradi ni rafiki kwa mazingira ya maeneo yao. Kigezo muhimu ni kuwepo taasisi na/au utashi wa kujenga, kuunga mkono na kusimamia miradi ili ifanikiwe na idumu. Serikali lazima iweke mazingira mazuri na kuzuia mila na tamaduni zinazokinzana na maendeleo.


Juhudi za kujiletea maendeleo hulenga kutumia rasilimali (watu, pesa na vitu) katika jamii ili kuinua hali ya maisha yao. Jitihada kama hizi vijijini hulenga kuinua maisha ya jamii nzima, bila kujali kama kuna vikwazo au la. Hatimaye jitihada za kujiletea maendeleo vijijini huwa ni chachu ya mabadiliko vijijini kwa kuboresha maisha ya wote. Kuna misingi miwili ya kujitegemea; kuishi kama mtu binafsi, na ushirika/jumuiya, na msingi wa mahitaji ya jamii. Misingi hii ni muhimu kusaidia jumuiya kujiletea maendeleo, na uthibiti wa jitihada hizo. Msingi wa kuishi kama mtu binafsi au katika kundi husisitiza uhitaji wa ulinzi na kuishi katika jumuiya. Hii hulazimisha watu kuishi katika kundi kwa kuhofia usalama wao. Kwa msingi huu, juhudi binafsi huwa ni njia ya kuwaleta watu katika jumuiya ili kuuangana kwa pamoja ili kila mtu na jamii ipate faida. Msingi wa uhitaji kwa upande mwingine huona kuwa kila jamii

ina mahitaji fulani, ambayo wameridhia hivyo hutafuta majibu yake. Juhudi binafsi za kujiletea maendeleo huhusishwa na: (i) Kuhoji hali waliyonayo na jinsi ya kuiboresha, (ii) Kujitambua kuwa wanao uwezo wa kukidhi mahitaji yao wenyewe, (iii) Sababu nyingine kama maisha ya mjini, elimu na mwingiliano wa wageni-wenyeji huondoa dhana potofu, (iv) Kujitenga na kudharau (kama ilivyozoeleka katika jamii za vijijini), (v) Kuelewa kuwa rasilimali ni chache lakini hupata thamani kwa kushirikiana.

Kama ilivyoelezwa hapo juu, mahitaji ya jamii husababisha kubuni mbinu za kujikwamua wenyewe. Wananchi wa Kata ya Kimochi walikasirishwa sana kwa kushindwa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania kushindwa kufika katika mazishi ya kiongozi wa kanisa mwaka 2013. Ikiwa imebakia mwaka mmoja kufanyika sherehe za kutimiza miaka 100 tangu kuanzisha ukristo (hasa katika kijiji cha Mdawi) hii ikiwa ni sehemu ya kwanza kupokea ukristo Tanganyika (ukitoka Bagamoyo), viongozi wachache wa kanisa waliweka mikakati iliyoshirikisha jamii kuboresha barabara kabla ya sherehe kuanza.

Ili haya yafanikiwe wananchi wa Kijiji cha Mdavi walipanga na kuweka mikakati ifuatayo;

(i) Kushawishi viongozi wa Kijiji kuitisha mkutano mkuu wa kijiji. Ilikuwa muhimu kushawishi viongozi kwani waliogopa wananchi kuwahoji juu ya utendaji kazi wao.
(ii) Kuunda kamati ya kusimamia iliyokuwa na watu watatu (mwenyekiti, katibu na mhasibu). Kamati iliwajibika kutengeneza andiko la kukarabati barabara zote kijijini, vifaa na gharama zake.




***Kamati Teule na kumbukumbu za Mradi***

(iii) Zoezi la kuchangisha pesa: Kamati ilikadiria TZS 21 milioni na kila kaya itoe TZS 25,000 kwa ajili ya vifaa na kukodisha mashine. Pia kamati ilihamasisha michango kutoka kwa wakazi wa Kijiji cha Mdawi waishio sehemu mbalimbali nchini. Hatimaye kamati ilipata jumla ya TZS 12,454,050; 2,894,000 zikiwa ni michango ya kijiji, na TZS 9,560,050 ni michango ya watu binafsi na waishio miji mbalimbali nchini.
(iv) Kuhamasisha jamii: Kamati ya usimamizi ilipanga jinsi wananchi kushiriki ujenzi wa barabara katika vitongoji. Wananchi walifyeka miti na nyasi, walitoa mawe makubwa ili mitambo (grader) iweze kufanya kazi. Jamii walitekeleza shughuli hizi kupitia msaragambo (kufanya kazi kwa pamoja ambalo kila mzee wa kaya huwakilishwa).





*Mitaro ya maji* *Mawe yaliyokuwa barabarani*

(v) Kukodisha mashine za ujenzi: Kamati ilikodisha tingatinga na mashine ya kugandamiza changarawe na lori la kusomba kifusi/changarawe

(vi) Kazi ya ujenzi ilianza kwa wananchi kusafisha maeneo yote ya barabara za kitongoji; waliondoa mawe makubwa na kuchimba mitaro. Walitumia mitambo (grader) kuchonga barabara. Halmashauri ilitoa msaada wa kiufundi kwa kutumia ofisi ya Mhandisi kutengeneza michoro, ramani, gharama za mradi na kutengenza kalavati.





***Ujenzi wa barabara Ukiendelea***

## 6.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Kijiji cha Mdawi chini ya mwavuli wa Kata ya Kimochi walitumia aina mbalimbali za rasilimali ili kutimiza malengo yao ya kuboresha barabara za vijiji na usafirishaji. Nguvu kazi ilijumuisha wanannchi wote wa Kijiji cha Mdawi na vitongoji vyote, viongozi wa kanisa, watumishi toka Halmashauri ambao ni Mhandisi wa Wilaya, mafundi wawili na mafundi wasaidizi wawili. Kijiji kilitumia rasilimali fedha kama jedwali 2 linavyoonesha.

**Jedwali 2: Pesa Iliyochangishwa**

| No | Chanzo cha pesa | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Wakazi wa Mdawi (25,000 kila kaya) | 2,894,000 |
| 2 | Watu binafsi- Mdawi | 2,519,250 |
| 3 | Waishio nje | 3,040,800 |
| 4 | Mkopo toka kanisani (SACCOS) | 4,000,000 |
| | JUMLA | 12,454,050 |

## 7.0 MATOKEO

Kijiji cha Mdawi ni mfano mzuri wa kuigwa kwa jinsi juhudi za wananchi zinavyoweza kumaliza matatizo yao na kukidhi mahitaji yao. Wakati wa kuandika mbinu hii bora, kijiji cha Mdawi kilikuwa na barabara za changarawe zenye urefu wa 19.6km na zinazopitika mwaka mzima. Haya ni mafanikio makubwa sana

kwa watu walioishi Kimochi kwani barabara zilikuwa kikwazo katika maisha yao; hazikupitika kwa kuwa zilikuwa na matope, utelezi na mawe.



***Barabara iliyoboreshwa kwa kiwango cha changarawe***

Usafirishaji wa mazao ya kilimo kwenda kwenye masoko hasa Moshi Mjini Ymeimarika. Jamii ya Kijiji cha Mdawi na Kata ya Kimochi kwa Ujumla ni ya wachapakazi wakijihusisha na uzalishaji wa kahawa, ndizi, mahindi maharage, na aina mbali mbali za mbogamboga na matunda. Baadhi ya mazao haya yanahitaji usafiri wa uhakika kufikia masoko kwani huharibika. Barabara zilizoboreshwa zimeondoa tatizo hili na kufikika kwa masoko makubwa kama Moshi mjini na Jiji la Arusha kumeimarika na kuinua kipato cha wananchi na kuboresha maisha yao.

Wananchi wa Kijiji cha Mdawi wana furaha sana kuliko huko nyuma kwa kuwa wanafikia kwa urahisi huduma za kijamii (elimu, afya, kanisa). Shule za msingi za zahanati katika kijiji cha Mdawi zilikuwa na matatizo katika kupata vifaa vya kutolea huduma. Baada ya ukarabati wa barabara za vijiji magari kutoka makao makuu ya Halmashauri yanaweza kuleta vifaa kwa urahisi katika shule na zahanati. Magari ya kubebea wagonjwa pia yanafika kwa urahisi kwenye zahanati wakati viongozi wa kidini wanafika kwa urahisi kwenye makanisa na kaya kwa ajili ya kutoa huduma za kiroho.



***Shule za Msing Mdawi na Kisaseni zinazohudumiwa na barabara***

Kupitia jitihada za jamii hali ya umiliki wa miradi imeimarika na inajidhirisha kupita ushiriki kamilifu katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara za vijiji kupitia Msaragambo. Jamii imeimarisha mshikamano wake na inaweza kujipanga katika kutekeleza mipango mingine ya maendeleo. Stadi za kujiendesha wenyewe zilizopatikana zinawezesha jamii kutambua mahitaji yao, kupanga suluhisho, kutafuta rasmali na kutatua matatizo. Kwa ujumla jamii ya Kijiji cha Mdawi ina furaha na imehamasika

kuendelea kushiriki katika mipango ya maendeleo jambo linaloleta amani na tulivu, ambavyo ni muhimu katika maendeleo ya jamii.

**8.0: MIKAKATI YA UENDELEVU**

Kijiji cha Mdawi kimeweka mikakati mbalimbali ya kuendeleza kuboresha za vijiji katika kata ya kimochi. Mikakati hii imejikita katika misingi ya jitihada za jamii ambapo changamoto za jamii hushugulikiwa na kutatuliwa na jamii yenyewe. Mikakati hii ni pamoja na

(i) Kuwepo kwa kamati imara ya usimamizi inayohimiza wananchi kufanya ukarabati wa mara kwa mara. Ili kuondoa mkanganyiko wa usimamizi wa shughughuli zote za ujenzi na ukarabati wa barabara za vijiji wananchi wameipa madaraka haya kamati ya usimamizi badala ya Serikali wa kijiji. Jamii inaamini kuwa serikali ya kijiji imejikita katika kutii miongozo na taratibu za serikali badala ya kujikita katika utoaji huduma.

(ii) Kijiji cha Mdawi kimetenga siku mbili kila wiki kupitia kwa ajili ya ukarabati wa barabara. “Msaragambo”. Wananchi hutoa ushirikiano mzuri sana katika siku hizo mbili. Kazi hizi hufanywa na watu wazima, vijana, wanumme kwa wake kutoka kila kaya.



***Wanakijiji cha Mdawi wakikabaratii barabara***

(iii) Upandaji wa miti na nyasi kandokando ya barabara kuzuia mmonyoko. Wanakijiji ca Mdawi wana ufahamu juu ya umuhimu katika kuboresha hali ya hewa, kuzuia mmomonyoko na kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji. Barabara zote zina miti inayozuia kumegiuka kwa kngo za barabara.

(iv) Kuendeleza majadiliano kati ya Halmashauri na kamati ili kuboresha barabara za kata ya Kimochi kiwango cha lami.

(v) Uendelevu wa barabara na jitihada za jamiii vitadumu kwa kuwa mhandisi wa Halmashauri anatoa ushirikiano mkubwa kwa jamii. Wataalamu kutoka ofisi ya mhandisi wa wilaya wanakuwepo kila wiki ya ukarabati wa barabara kutoa usaidizi wa kitaalam.

**9.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Jitihada za jamii zilichangia maendeleo wakati wa ukoloni na miaka ya mwanzoni uhusu ya Tanzania huru, hasa katika mkoa wa Kilimanjaro. Kati ya miaka 1980 hadi 2000, Jitihada za jamii za kujiletea maendeleo zimeathiriwa na mtazamo wa wananchi kuwa serikali inaweza kukidhi mahitaji yao yote. Siku za karibuni hata wanasiasa wamekuwa wakikwepa kusaidia/kuchangia jitihada za jamii kwa kuhofia kupoteza umaarufu wao na kisha kupoteza kura wakati wa uchaguzi. Hata hivyo wananchi waliojipanga

vizuri kama wanakijiji wa Mdawi wanaendelea kufaidikia kutokana na siri za mafanikio kama inavyoelezwa hapa chini:

(i) Taasisi za kidini zilizochochea sana wananchi kujiletea maendeleo. Wanakijiji cha Mdawi ni waaminifu, wana utayari, waliojipanga na wawajibikaji. Sifa hizi zinatokana na historia na miongozo ya kidini.



***Kanisa la Mdawi na Kituo cha Maombezi cha Kitimbirihu***

(ii) Kijiji kina watu wabunifu, waaminifu, wenye kujituma kuleta maendeleo yao kama sehemu ya utamaduni wao.
(iii) Kuna uongozi ulio hamasika na wenye uaminifu. Uaminifu na uwazi juu ya matumizi ya fedha imekuwa ni chachu kwa wapenda maendeleo kushiriki zaidi.



***Bw. Justo Elias Mboho – Mhasibu***



***Bw.Damson Ringo - Katibu***

(iv) Halmashauri kutoa utaalamu wa kiufundi wakati wa ujenzi wa barabara.
(v) Wananchi wamepata ujuzi wa kufanya shughuli kwa pamoja katika kuibua, kupanga na kutafuta vyanzo vya rasilimali za mradi.
(vi) Kuwepo kwa watu wa Mdawi waishio sehemu nyingine lakini wenye kupenda kuchangia maendeleo ya kijiji chao.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA


**USHIRIKI WA JAMII KATIKA USAFI WA MAZINGIRA**




***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya wilaya ya Siha ni kati ya Halmashauri saba za mkoa wa Kilimanjaro na ilianzishwa Julai, 2007. Halmashauri inapatikana kati ya Longitudo ya $37^0 3'$ hadi $37^0 15'$ Mashariki na Latitudo ya $2^0 5'$ hadi $3^0$ Kusini. Halmashauri ya Siha ina ukubwa wa eneo la $1158km^2$. Halmashauri inapakana na Halmashauri za Wilaya za Hai upande wa Kusini, Longido na Rombo upande wa Kaskazini Magharibi, Meru na Hai upande wa Kusini mashariki na nchi ya Kenya kwa upande wa Kaskazini. Wakazi wengi ni "Wachagga". Makabila mengine ni Meru na Wamasai ambao ni wafugaji. Kwa mujibu wa sensa ya 2012, Halmashauri ina wakazi 116,313, kati yao wanaume ni 56,500 na wanawake 59,813 na kuna wastani wa watu 4.3 katika kaya. Halmashauri ina Tarafa 5, Siha kati, Siha Mashariki, Siha Kaskazini, Siha Kusini na Siha Magharibi, Kata 15, Vijiji 60, na Vitongoji 170




Shughuli za kijamii na kiuchumi hufanyika katika maeneo matatu. Nyanda za juu kati ya 1200m-1400m juu ya usawa wa bahari na hupata mvua kati ya 800mm-1200mm kwa mwaka. Sehemu kubwa ni misitu na ni vyanzo vya maji. Shughuli kubwa ni kilimo na ufugaji wa ndani. Mazao yanayolimwa ni kahawa, mahindi, ndizi, nyanya, mbogamboga, matunda, ngano, shahiri, na alizeti. Uwanda wa kati upo kati ya 900m-1000m juu ya usawa wa bahari na hupata mvua wastani wa 600mm-900mm kwa mwaka. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na punda kwa kutumia njia za asili. Uwanda wa chini upo kati ya 700m na 960m juu ya usawa wa bahari na hupata wastani wa mvua kati ya 400mm-600mm kwa mwaka. Mazao yanayolimwa ni mahindi, maharage, ndizi na viazi vitamu, mtama, mbaazi, mihogo na mbogamboga.




Kwa karne nyingi zilizopita takribani robo tatu ya wakazi wa Halmashauri ya Siha ni wabantu. Wenyeji ni wachaga kutoka Wasiha na Wamachame, wengine ni Wamaasai na Wameru. Wamaasai ndiyo wafugaji wanaohama na wako katika Halmashauri nzima. Wasiha na Wamachame ambao ni wakulima wanaishi kusini mwa Mlima Kilimanjaro na magharibi mwa wilaya ya Meru. Makabila mengine ni Wasafwa, Wahaya, Wanyiramba, Wasukuma, Wapare, Wasambaa n.k wengi wao hujishugulisha na kilimo mseto.

## 2.0 TATIZO

Maana ya usafi wa mazingira ni juhudi za makusudi za kuboresha na kulinda afya na hali za watu kwa ujumla. Usafi wa mazingira ni mfumo unaowezesha kuhifadhi uchafu unaozalishwa na binadamu na wanyama kama utumiaji sahihi wa choo na kuzuia haja kubwa kuzagaa hovyo. Misingi ya usafi wa mazingira inahitaji kuweka miundo mbinu ya kuhifadhi uchafu wa mwanadamu (mfano haja kubwa na ndogo), kuweka misingi ya kudumu ya afya kama ukusanyaji wa taka, kutunza uchafu wa viwandani kama hewa, taka ngumu na maji taka. Kutunza usafi wa mazingira ni njia ya kuimarisha afya zetu kwa kuwa humkinga mwanadamu na hatari za mazingira machafu na huhifadhi vizuri uchafu wote.

Uchafu anaozalisha mwanadamu kama haja kubwa ni chanzo cha maambukizi ya magonjwa kama kipindupindu, homa ya matumbo, polio, homa ya ini, minyoo kamba, nimonia na minyoo tumbo. Pia husababishwa na maji yasiyo salama, na huathiri ukuaji wa viungo, na ubongo hasa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano. Kinachodhuru afya ya mwanadamu ni siyo tu ni uchafu anaozalisha mwanadamu ukichanganyika na maji, bali pia vyuma vizito, sumu za viumbe na kemikali huatarisha afya ya mwanadamu na mazingira- hasa uchafu wa viwandani ukichanganywa na mifumo ya maji taka.

Usafi wa mazingira hujumuisha upatikanaji wa maji safi na salama, hewa nzuri, ukusanyaji na kutupa uchafu wanaozalisha binadamu na wanyama, kuzuia wadudu na kemikali kuingia katika chakula, kuwa na nyumba bora na mazingira masafi na salama.

Halmashauri ya Wilaya ya Siha ilikuwa inapata mlipuko wa magonjwa kama kuhara, kipindupindu, minyoo na amoeba katika Vijiji kumi (Ngarenairobi, Matadi, Miti mirefu, Mawasiliano, Lekrumuni, Kandashi, Olkolili, Ormelili na Wiri) ambavyo viko katika uwanda wa chini ambamo wafugaji wa kimaasai huishi. Mila na tamaduni za kimasai zina kinzana na usafi wa mazingira kwa kutotumia choo za kisasa. Ipo imani iliyojengeka miongoni mwa wamaasai vijana na wanawake kuwa wazee huwa hawajisaidii haja kubwa. Wakazi wote katika vijiji hivi walijisaidia vichakani na maeneo yaliyowazi. Tatizo lilikuwa linakuwa kubwa wakati wa uhaba wa maji maana si kawaida yao kunawa mikono baada ya kujisaidia. Hii ilisababisha mlipuko wa magonjwa yatokanayo na kinyesi cha binadamu kama jedwali 1 linavyoonesha hapa chini.

**Jedwali 1: Mlipuko wa Magonjwa 2008-2012**

| Mwaka | Amoeba | Kuhara | Kipindupindu | Homa ya matumbo | Minyoo |
|---|---|---|---|---|---|
| **2008** | 1751 | 150 | 0 | 11 | 830 |
| **2009** | 1604 | 120 | 0 | 9 | 301 |
| **2010** | 1894 | 103 | 0 | 0 | 156 |
| **2011** | 1669 | 80 | 0 | 13 | 132 |
| **2012** | 1430 | 65 | 0 | 12 | 123 |

## 3.0 MALENGO

Halmashauri ya Wilaya ya Siha ilifanya mkakati wa kubadili jamii ya Wamaasai ili kuzuia uharibifu wa mazingira na kuzuia na kuondoa magonjwa yatokanayo na uchafu. Lengo kuu lilikuwa ni kuweka mbinu za kuondoa kabisa mlipuko wa ugonjwa utakanao na vinyesi katika sehemu zote.

Malengo mahususi yalikuwa ni:

(i) Kubadili mtazamo, tamaduni, na tabia za Wamaasai juu ya utumiaji vyoo kuwa haviathiri utu wao katika familia na jamii.
(ii) Kuiwezesha jamii ya Wamaasai kupitia programu za kuwahamasisha kuelewa umuhimu wa usafi, athari za kuharibu mazingira, faida za kukaa katika mazingira safi na gharama za kutibu magonjwa yatokanayo na kutotumia vyoo.
(iii) Kuhamasisha utumiaji wa vyoo majumbani, kunawa mikono baada ya kutumia choo, na kufanya usafi katika mazingira yao.
(iv) Kuonesha aina mbalimbali za vyoo vinavyo shauriwa kutumiwa.
(v) Kuweka mazingira ya nyumba na kijiji chao katika hali ya usafi.

## 4.0 MIKAKATI UTEKELEZAJI


Kwa mara ya kwanza kampeni ya usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha ilianza mwaka 2012/2013, Wizara ya Afya ikishirikiana na Benki ya Dunia ili kutekeleza mpango wa usafi wa taifa. Pamoja na mpango wa usafi utokanao na juhudi za wananchi, Halmashauri ilitumia njia ya kuihusisha jamii yenyewe ili waone umuhimu wa kubadili tamaduni zao. Njia hii ya uboreshaji wa afya kwa juhudi za wananchi wenyewe huanzishwa kwa vipindi vya mafunzo, kuzungukia mazingira (yenye vinyesi na kuchunguza jinsi ambavyo uchafu huu hatimaye huingia katika vyanzo vya chakula na maji). Mikutano na shughuli zinazohusisha watoto na wanafunzi. Nia ilikuwa ni kuhakikisha jamii yote inashirikishwa juu ya athari za kutotumia vyoo na kuiwezesha jamii kuchukua hatua kumaliza tatizo. Baada ya hatua hii, jamii ilichukua jukumu la kujenga vyoo vya shimo kwa nguvu zao wenyewe. Halmashauri haikutoa kifaa chochote zaidi ya kuwapa ushauri tu. Baadaye, wakaguzi walienda kuthibitisha kama jamii nzima inatumia vyoo. Ilipo thibitisha kuwa wote wanatumia vyoo, jamii zinazowazunguka zilialikwa na sherehe zilifanyika huku wakihamasisha jamii zilizoalikwa zitumie vyoo. Mashindano na kufanya kazi hii kwa pamoja inasisitizwa ndani ya vijiji, maana majirani wanahamasishana kuondoa tatizo la kutotumia vyoo. Juhudi za kufanya jamii iwe na mazingira masafi yenyewe ni njia ya gharama nafuu, na hakuna msaada wowote zaidi ya kuiwezesha jamii kwa kuwashirikisha kwa kutumia mwezeshaji ukiondoa mafunzo ya wawezeshaji yenyewe.

Halmashauri ya wilaya ya Siha ilitumia njia ya mafunzo ya kubadili mila na desturi. Shughli halisi ilikuwa ni kutembelea (maeneo yenye vinyesi na kuchunguza jinsi ambavyo uchafu huo huingia katika maji au wanyama), kujadili kuonesha kwa vitendo, na kutengeneza mpango kazi wa kumaliza tatizo la kujisaidia

hovyo. Hii ilikuwa ni kuiwezesha jamii kutambua kuwa kutotumia choo ni hatari kwa afya ili wachukue hatua sahihi.

Wafanyakazi wa Halmashauri walitumia mbinu chochezi na shirikishi kubadili mtazamo wa jamii kutumia vyoo. Mbinu hii hushirikisha jamii kutambua kuwa kujisaidia hovyo kwenye mazingira ni hatari sana hivyo huamua wenyewe kukomesha tabia hii baada ya kufanya tathimini kwa pamoja juu ya hali ya usafi katika mazingira yao. Kwa kutumia njia hii jamii inaweza kufikia malengo yao na kuwa endelevu kutokomeza tabia ya kujisaidia hovyo katika mazingira.

**Mbinu za kutia hamasa**




Juhudi za jamii kujiletea usafi huhusisha mikakati ifuatayo:

(i) Mafunzo kwa maafisa 2 kama wasimamizi wa kampeni za usafi katika Halmashauri. Mafunzo kuwepo kwa afisa afya na afisa maendeleo ya jamii.
(ii) Kufanya mikutano juu ya usafi ili kushawishi wadau kuunga mkono kama menejimenti ya Halmashauri (CMT), Timu ya menejimenti ya afya ya Halmashauri (CHMT), madiwani na watu wenye ushawishi
(iii) Kufanya mafunzo kwa siku mbili kwa wajumbe wa CMT, watendaji wa Vitongoji na Vijiji na afisa maendelo ya jamii (CDO) ili kutengeneza daftari la takwimu
(iv) Kuzungukia vijiji vyote 10 kwa siku 10 ili kuhakiki na kupima mabadiliko
(v) Kufanya tathmini katika vijiji vyote 10 juu ya hali ya kujisaidia hovyo, gharama za tiba, njia za uchafu kuingia kinywani na fomu za kutangaza hali halisi.

*Hatua za kuchukua:*

- *Wanajamii kufanya mkutano wa wazi. Hakikisha viongozi wa kamati ya afya na wazee hawakosi. Afisa ugani atakuwa mwezeshaji wa mkutano, wenyekiti wa kijiji achague mahali na muda wa mkutano*
- *Afisa ugani ataonesha kwa vitendo watu wote walio udhuria. Watatumia choo ya shimo mfano, watatumia jani kujisafishia baada ya kujisaidia. Wataonesha ilivyo rahisi jani kukatika na kuruhusu vidole kushika kinyesi (tumia mkaa au udongo wa mfinyazi kama kinyesi). Mwezeshaji haoishi mikono baada ya jinsi choo kilivyobakia mikononi mwa mwezeshaji*
- *Kisha mwezeshaji atauliza maswali; mfano, kitu gani kimebakia mikononi mwangu? Mnatumia majani? Kaya ngapi hutumia maji na sabuni?*
- *Mwezeshaji atapeana mkono na viongozi waliopo, mara nyingi, wazee na kisha kuwaomba wazee pia wawasalimie majirani zao kwa kupeana mikono. Kwa kutumia mkaa au udongo wa mfinyazi kwenye mikono ya mwezeshaji kama "alama ya kinyesi" itaonekana inavyosambaa wanapopeana mikono.*
- *Zungusha nafaka kama karanga kwa wale waliopeana mikono na kinyesi cha mwezeshaji. Waambie waanze kula karanga. Hii itafumbua uelewaji wa kila mtu kuwa kupeana mikono inaweza kuwa njia ya kula kinyesi chake, na huonesha umuhimu wa kunawa mikono kwa sabuni.*
- *Mwezeshaji awaulize watu kukadiria idadi ya mikono waliyopeana kwa siku hiyo, wiki iliyopita, mwezi uliopita, n.k kisha aulize, "unaweza kuwa umekula kinyesi cha watu wangapi?". Hii ni sawa na tathimini iliyofanyika kwa kuhesabu watu waliojisaidia hovyo hapo kijijini. Hesabu inaweza kuwa ni kinyesi cha watu 280 kwa wiki, na hii itawafanya wananchi wote washtuke na waelewe umuhimu wa kunawa mikono baada ya kujisaidia.*



***Mwezeshaji akionesha namna ya kutathimini idadi ya vinyesi***

(vi) Kutoa mafunzo kwa jamii na shule katika vijiji kumi (Ngarenairobi, Matadi, Miti mirefu, Mawasiliano, Lekrumuni, Kandashi, Olkolili, Ormelili na Wiri) juu ya umuhimu wa choo na matumizi sahihi.



***Kuonesha namna ya kutumia choo***

(vii) Kufanya mashindano ya kitaifa ya usafi vijijini. Kijiji cha Wiri kiliibuka mshindi wa kunyakua zawadi yaTZS 600,000 kutoka iliyokuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii. Halmashauri ya Wilaya ya Siha ilishika nafasi ya pili na kuzawadiwa pikipiki mbili, moja kwa ajili ya wilaya na nyingine ya Kijiji cha Wiri.

(viii) Kunzisha vikundi viwili kwa ajili ya kuhamasisha na hivi vikundi viliendeleza kuhimiza watu kufanya usafi, kutembelea kaya na kufanya mikutano vijijini. Wahamasishaji waliwakumbusha watu katika kaya na makundi yote juu ya kutunza usafi katika mazingira yao. Pia waliandika ripoti na kuituma kwa idara ya afya ya Halmashauri.

(ix) Fulana 70 zenye neno *"Jenga choo bora uepukane na maradhi" na "Nawa mikono kwa sabuni"*. Fulana zilivaliwa na wafanyakazi wa afya, viongozi wa vijiji, madiwani na wadau wa usafi wa mazingira.

(x) Kufanya mafunzo ya wiki mbili kwa mafundi ili waweze kutengeneza vyoo vya shimo vyenye kupitisha hewa na kuwezesha watumiaji kunawa mikono kwa gharama nafuu.

(xi) Kubaini kaya ambazo hazina vyoo na zinazojisaidia hovyo. Ilibainika kaya 9544 kati ya 5307 (18%) hazikuwa na vyoo.

(xii) Kuzungukia wananchi katika vitongoji ili kuona hali ya usafi, kubaini maeneo yaliyo na vinyesi na kukusanya uchafu huo ili kuzuia kuku na nzi kusambaza na kula kinyesi, kuonesha jinsi ya kinyesi kinavyoweza kusambaa na kurudi majumbani.

(xiii) Kuwapatia bwana na bibi afya mafunzo ya siku tatu (3); jinsi ya wanajamii kutunza usafi wa mazingira yao wenyewe kwa kutumia wawezeshaji 4 kutoka wilayani.

(xiv) Kuweka vyoo za mfano katika vituo viwili. UNICEF ilisaidia kuweka vyoo 12 katika vijiji vya Ngarenairobi na Orkolili.



***Choo ya Mfano***

(xv) Ukarabati wa vyoo vya shule za msingi za Kilari na Mawasiliano kupitia kampeni ya usafiri kitaifa

## 5.0 RASILIMALI

Halmashauri ya Wilaya ya Siha ilitumia rasilimali mbalimbali kuwezesha jamii za kimaasai kuboresha usafi wa mazingira yao. Fedha zilizotumika zinaoneshwa na jedwali na 2 hapa chini. Raslimali watu pia walihusika sana kama maafisa afya wa Vijiji.

**Jedwali 2: Fedha Zilizotumika**

| No | Shughli | Gharama (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Mikutano ya uhamasishaji | 2,726,997 |
| 2 | Tathmini ya kwanza katika vijiji 10 | 2,208,970 |
| 3 | Kuanzisha zoezi katika vijiji 10 | 8,920,226 |
| 4 | Mashindano ya kitarafa ya usafi na mazingira | 2,990,000 |
| 5 | Kuanzisha vilabu na kuchapisha fulana | 4,956,300 |
| 6 | Kutoa mafunzo kwa mafundi 20 | 4,649,229 |
| 7 | Kuzungukia vijiji na kufanya tathmini ya usafi | 3,066,278 |
| 8 | Semina elekeze kwa bwana na bibi afya vijijini | 1,080,00 |
| | **Jumla** | **31,198,500/=** |

## 6.0 MATOKEO

Jitihada za kujiletea usafi katika mazingira zilileta mabadiliko makubwa katika jamii. Jamii ya kimaasai imebadilika ghafla na kuacha kujisaidia hovyo na kuanza kutumia vyoo. Ni kwasababu imani potofu kuwa wazee hawajisaidii imeepotea pia. Watu wote kwenye kaya wamejenga na wanatumia vyoo kwa kujiamini. Mabadiliko yanaonesha kuwa kaya 504 kati ya 5307(9%) wamejenga choo bora ndani ya miezi mitano ya kufanya kampeni.



***Choo cha shimo nyuma ya nyumba***

Tokeo la pili ni kuwa kila kijiji kina sheria ndogo ya kujenga vyoo. Sheria hizi ndogo zinataka kila kaya kujenga na kutumia vyoo ili kuweka nyumba zao na mazingira katika hali ya usafi wanaokiuka utaratibu huu hulipa kati ya TZS 20,000 - 50,000.

Tokeo la tatu ni kupungua kwa magonjwa yatokanayo na kinyesi cha binadamu. Magonjwa sugu kama homa ya matumbo, kuhara na amoeba yamepungua sana baada ya kujenga na kutumia vyoo. Hii imepunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano. Ujenzi wa vyoo pia umewafanya wafugaji wajenge nyumba za kudumu badala ya kuzunguka katika maeneo mengi wakitafuta malisho ya ng'ombe.

Vijiji vimepata vyoo vya mfano ambavyo vijiji jirani hutumia kujifunzia. Jitihada hizi za kujiletea usafi wa mazingira pia zimewapa mafunzo mafundi 20 ili waweze kusaidia kutengeneza vyoo kwa ngazi ya kaya.

**7.0 MIKAKATI ENDELEVU**

Halmashauri imeweka mikakati mbalimbali ili matokeo yawe ya kudumu, jamii ibadili mtazamo na tabia na ujenzi na matumizi ya vyoo yawe endelevu kwa kufanya yafuatayo:

(i) Halmashauri inaendelea kuelewesha wazee juu ya umuhimu wa usafi wa mazingira kwa kuzipa Serikali za Vijiji naJjamii kusimamia swala hili.
(ii) Kuendelea kusimamia ujenzi na matumizi ya vyoo, kufanya ukaguzi, kutoa zawadi kwa washindi, na kuhamasisha vikundi vya usafi na mazingira kuendelea na kazi zao.
(iii) Kuendelea kuwashawishi Wamaasai kupitia mikutano inayoitishwa na wazee kuacha kujisaidia hovyo.
(iv) Kuendelea kuwawezesha wanawake kushiriki kutoa maamuzi ili kuondoa dhana potofu juu ya uwezo wa wanawake kushiriki kuleta maendeleo.
(v) Kushirikiana na watu binafsi ili watoe vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kuboresha nyumba na vyoo kupitia mikutano ya jamii na vijiji.
(vi) Kutumia njia za kujenga choo kwa kutumia mawe.

**8.0 SIRI YA MAFINIKIO**

Kupitia mikakati ya jamii kujiletea usafi wa mazingira yenyewe, Halmashauri ya Wilaya ya Siha imebadili mtazamo na tabia sugu na ngumu zilizojikita katika mila na desturi za wamaasai. Jitihada hizi za jamii kujiletea usafi wa mazingira zenyewe zimefanyika katika nchi nyingi za kiafrika bila mafanikio. Halmashauri za Tanzania na nchi nyingine zinaweza kujifunza katika siri zifuatazo:

(i) Utayari na wepesi wa kuzikubali na kuzitumia mbinu zilizopendekezwa na Wizara ya Afya Na Ustawi Wa Jamii (iliyokuwa) na UNICEF kuleta mageuzi ya kujiletea usafi wa mazingira.
(ii) Ubunifu wa wafanyakazi hasa wale wa idara ya afya kwa kutumia njia ya kuwahusisha na kuwashirikisha wananchi kuamua wanachotaka kufanya badala ya kuwalazimisha.
(iii) Kutumia vikundi vya wasanii kuwatumbuiza huku wakihamasisha kubadili mtazamo na tabia.
(iv) Mashindano ya usafi wa mazingira kati ya vijiji na kutoa zawadi. Hii iliamsha hamasa kwa wanajamii na vijiji kuongeza kasi ya kujenga vyoo.
(v) Jamii ya Wamaasai iliunga mkono wazo la usafi wa mazingira. Wazo linapokubaliwa na wazee basi vijana na akina mama hulitekeleza bila kikwazo. Ndiyo maana hakuna tena kujisaidia hovyo na ujenzi wa vyoo umefanikiwa.

# MKOA WA KILIMANJARO

**USIMAMIZI WA MATUMIZI ENDELEVU YA ARDHI**



***Ndiva - Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga***



***Utunzaji wa Mazingira Bonde la Mto Lawate - Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha***

**1.0 UTANGULIZI**

Mkoa wa Kilimanjaro ni kati ya mikoa 31 ya Tanzania. Mlima Kilimanjaro upo katika mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa huu unapakana na nchi ya Kenya upande wa Kaskazini Mashariki, Mkoa wa Tanga upande wa Kusini, Mkoa wa Manyara upande wa Kusini Mashariki na Mkoa wa Arusha upande wa Magharibi. Mkoa wa Kilimanjaro ulianzishwa mwanzoni mwa miaka 1960. Mkoa una ukubwa wa 13,209 $km^2$ au 1.4% ya eneo la Tanzania. Kiutawala, mkoa umegawanyika katika Halmashauri sita mbazo ni Manispaa ya Moshi, Halmashauri za Wilaya za Moshi, Rombo, Mwanga, Same, Hai na Siha. Mkoa una Tarafa, Kata 153 na Vijiji 472.




Chapisho linelezea mbinu bora mbili kutoka Halmashauri za Wilaya ya Mwanga na Siha. Halmashauri ya Wilaya ya Siha ilianzishwa July 2007. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo $37^0$3'-$37^0$15' Kusini; Longitudo $2^0$5'-$3^0$ Mashariki ya Griniwich. Halmashauri ina eneo la 1158km2. Halmashauri inapakana na Halmashauri za Wilaya za Hai upande wa Kusini, Longido na Rombo upande wa Kusini Magharibi, Meru na Hai upande wa Kusini Mashariki, upande wa Kaskazini ni nchi ya Kenya . Wachagga ndio wakaazi wengi katika Halmashauri hii. Wengine ni Wameru na Wamasai ambao ni wafugaji.

Halmashauri ya Mwanga ni kati ya Halmashauri 7 za mkoa wa Kilimanjaro. Halmashauri hii inapakana na Halmashauri zaa Wilaya za Same upande wa Kusini, Moshi upande wa Kaskazini, Simanjiro upande wa Magharibi, na Jamhuri ya Kenya upande wa Kaskazini Mashariki. Halmashauri ina ukubwa wa eneo la 2,641$Km^2$, Tarafa 5, Kata 20 na Vijiji 70. Kuna nyanda mbili za uoto; uwanda juu (Ungweno na sehemu za Tarafa za Lembeni na Usangi- 808$km^2$). Uwanda huu upo kati ya 1200m-2000m juu ya usawa wa bahari na Uwanda wa chini zina eneo la 1833 $km^2$ na ziko kati ya 700m – 800m juu ya usawa wa bahari. Kwa mujibu wa sensa ya 2012 ya watu na makazi, Halmashauri hii ina watu 121,442 kati yao 63, 199 ni wanawake, na 68 245 ni wanaumme. Ongezeko la watu ni 1.2% na wastani wa watu ni 4.5 kwa kaya.

**2.0 TATIZO**

Kati ya miaka ya 1960 na 1970 bei ya zao la kahawa ilishuka ghafla katika soko la dunia kutokana na ugonjwa wa kahawa (berry disease). Wakulimia hawakuwa na budi kutafuta njia mbadala bila kujali kama ilikuwa endelevu. Hivyo utamaduni wa Wachagga wa kutumia kilimo chenye mfano wa bustani kinachohifadhi rutuba ya ardhi kikatoweka kutokana na kuanzishwa kwa njia mbadala za kujipatia kipato. Shughuli hizi mpya zilisababisha kung'oa mibuni kupisha kilimo cha maua, ukataji mbao, biashara ndogondogo na uvamizi wa hifadhi ya msitu kwa ajili ya mbao na kuni.

Kwa mila na desturi za wakazi wa Siha mifumo ya ardhi na umiliki wake ulimpa fursa mwanaume kumiliki ardhi na kahawa na mwanamke kumiliki ndizi na maziwa. Baada ya kuyoweka kwa kilimo cha kahawa matumaini ya wanaume kiuchumi yalififia, wanawake wakawa watunza familia. Wanaume wakaacha majukumu yao ya kumiliki na kutunza ardhi. Kushuka kwa uzalishaji wa zao la kahawa kulisababisha wakulima wengi wahamie kwenye kilimo cha mazao mbadala kama mbogamboga, mahindi na maharage, na uvunaji wa miti. Ukataji wa miti bila kupanda mingine ulileta mmomonyoko wa ardhi kwa kuwa kwa kupindi kirefu ardhi iliachwa wazi na kuharibiwa na maji ya mvua.

Pia Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ilikumbana na wimbi la wahamiaji wengi lililo sababisha ongezeko la watu katika nyanda za juu zaidi ya uwezo wake. Kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji kama kilimo, ufugaji, ukataji wa miti na mbao, uchomaji wa misitu, utumiaji mbovu wa maji na ardhi uliharibu mazingira. Mimea ilipungua na maji ya umwagiliaji yalipungua katika mashamba ya mpunga, mahindi, na mbogamboga. Ulimaji mbovu sehemu za juu za mito, kama Ziwa Jipe uliondoa rutuba na kusababisha magugu kwenye maji yaliyoharibu mazalia ya samaki na shughuli za uvuvi kama picha inavyoonesha hapa chini.



***Ziwa Jipe Lililojaa Udongo na Magugu***



***Mmomonyoko wa Udongo***



***Mazao yaliyonyauka kwa sababu ya mmomonyoko wa udongo*.**

Wakazi wa Halmashauri ya wilaya ya Mwanga walikuwa wakishuhudia kuporomoka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na hivyo kupungua kwa kipato cha kaya na pato la Halmashauri kwa ujumla. Hali

ilisababisha matatizo mengine ya kijamii kama ongezeko la utoro na kuacha shule, wazazi kushindwa kulipa ada, ongezeko la magonjwa na vifo na umaskini kwa ujumla.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu lilikuwa ni kuhifadhi ardhi kwa matumizi endelevu kwa kuwa ndiyo msingi wa maendeleo ya kiuchumi, uhakika wa chakula, na chanzo cha ongezeko la pato la kaya ili kuboresha hali ya maisha na mazingira ya mkoa wa Kilimanjaro.Malengo mahususi yalikuwa ni:-

i. Kuhakikisha kuna uhifadhi wa ardhi na miti, kupanda nyasi shuleni na kuanzisha bustani za kimila za Wachagga na Wapare.
ii. Kuhamasisha utunzaji wa bonde la mto Lawate na kusimamia maji ya umwagiliaji.
iii. Kuhifadhi udongo na maji kwa kutumia sheria ndogo za uhifadhi wa ardhi
iv. Kuhimiza shughuli za kupanda miti na kuhifadhi misitu
v. Kuongeza mazao ya chakula na biashara
vi. Kuanzisha ufugaji nyuki kama chanzo mbadala cha kuongeza kipato na shughuli rafiki wa mazingira.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Serikali kupitia sekretarieti ya mkoa wa Kilimanjaro ilianzisha mradi wa kuhifadhi ardhi kwa ufadhili wa UNDP. Mradi huu katika wilaya ya Siha ulijikita zaidi katika bonde la mto Lawate. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga mradi ulikua Kijiji cha Kwamboa. Mbinu zillizotumika ni:-

Kuongeza uelewa kwa kushirikisha jamii: Katika Halmashauri Wilaya ya Siha watu walishirikiana kuchagua eneo la mradi. Bonde la mto Lawate lilichaguliwa kwa kuwa ndilo lililokuwa limeharibiwa sana. Mradi ulianza kwa kujenga uelewa wa Baraza la Madiwani na Wakuu wa idara. Katika ngazi ya jamii ujenzi wa uelewa ulihusisha Afisa Tarafa 1, Maafisa watendaji wa Kata 2, Walimu wakuu 3 wa shule za sekondari, walimu wakuu wa shule 12 za msingi na viongozi 2 wa dini katika bonde la mto la mto Lawate.

Kuundwa kwa vikundi vya wakulima: kupitia mradi wa hifadhi endelevu ya ardhi Halmashauri ilihamasisha wakulima kuunda vikundi, kutafuta pesa na kutunisha akaunti za benki, kutengeneza matuta, kupanda miti na kutumia majiko yanayotumia nishati kidogo. Hii ilihihusha pia uandaaji wa katiba za vikundi, uchaguzi wa viongozi wa vikundi na usajili wa vikundi kupitia idara ya maedeleo ya jamii

Uandaaji wa Makinga Maji (matuta): kwa kushirikiana na maafisa ugani, wajumbe wa kamati ya Kijiji na wakulima wakubwa waliweka matuta kwenye bonde la mto yenye urefu wa 40,000m katika eneo 1000ha kati ya 2,150ha katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha. Shughuli kama hii ilifanyika pia katika Halmashauri Wilaya ya Mwanga kama picha inavyoonesha hapa chini.




*Mkulima akiandaa mifereji na matuta* *Matuta imara eneo la Kwamboa*

Mafundisho kwa wadau muhimu: Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ilitoa mafunzo kwa wakulima wa Mwanga juu ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia chanzo cha maji cha Ndiva kilicho kilichoboreshwa. Mafunzo pia yalihusu uandaaji wa ratiba ya umwagiliaji na sheria na kanuni za utumiaji wa maji ya umwagiliaji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha, maafisa ugani 9, wakulima walioteuliwa 50, na wajumbe wa kamati ya mazingira ya kijiji 45 walipatiwa mafunzo kuhusu njia za kuzuia mmomonyoko wa udongo, kutengeneza matuta kwa vipimo, uhifadhi wa kingo za mito, uvunaji wa maji ya mvua , na mbinu bora ya kulima.



***Wajumbe wakamati ya mazingira ya kijiji wakipatiwa mafunzo***

Uanzishwaji wa vitalu vya miche ya Miti: Halmashauri ilianzisha vitaru vya miche ya miti sehemu za makazi na shuleni ili miche ipatikane katika eneo la mradi wa hifadhi endelevu ya ardhi. Mfano, Halmashuri ya Wilaya ya Mwanga ilipanda miti 15,212. Katika Halmashauri ya wilaya a Siha, wakulima18, shuel za msingi 2 (Lokiri na Kirisha) walifundishwa namna ya kuanzisha na kutunza vitalu vya miti. Wakulima 2 walianzisha vitaru vya miche majumbani mwao na walipatiwa zana za bustani kama koleo, majembe, reki, ndoo za kumwagilia, chekecheo and toroli, mbegu za miti za kuanzia, mifuko ya plastiki na mbolea. Angalia picha na jedwali 1 hapa chini.





***Kitalu cha miche shule ya msingi chomvu, kata ya chomvu***



*Uandaaji wa vitalu vya miche sekondari ya Siha*

**Jedwali 1: Halmashauri ya Mwanga:  Vitalu Vya Miche 2013**

| Kitalu | Kilipo | Miti iliyopandwa | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|
| **Chomvu** | Chomvu | Gravellier | 3,400 |
| | | Cypress | 1,300 |
| | | Cedrella | 2,000 |
| **Kikundi cha wanawake Mwero** | Mbore | Gravellier | 2,000 |
| | | Mikoromaji | 200 |
| | | Mipapai | 1,000 |
| **Kikundi cha Michezo Usangi** | Lomwe | Gravellier | 1,500 |
| **Nzinyangwa eliezeri** | Vuchama | Gravellier , | 1,000 |
| | Naambwe | Mikoromaji | 1,500 |
| **Shighatini shule ya msingi** | Shighatini | Gravellier | 1,500 |
| | | Mkoromaji | 1,500 |
| **Jitihada ya Hifadhi Kijiji** | Mwanga | Gravellier | 1,000 |
| | | Mikoromaji | 800 |
| **Jumla** | | | **15,212** |

Upandaji wa miti:  wananchi walipanda miti kwa wingi kama zoezi la kuifadhi misitu. Kuanzia mwaka 2003/04  hadi 2012/13, jumla ya miti 2,857,415 ilipandwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga. Katika Halmashauri ya  Wilaya ya Siha miche 10,000 ilioteshwa kwenye vitalu kwa mwaka wa kwanza. Shule ya msingi Lokiri iliotesha miche 3,000 kwenye kitalu chake na kupanda miche 6000. Wanafunzi miche 2,000 (kila mwanafunzi miche 5), na shule jirani walipanda miche ya miti 100, na serikali za vijiji zilipanda miche 300 kandokando ya barabara.




*Ugawaji wa miche kwa wakulima*



*Upandaji miti (viongozi, walimu na wanafunzi)*

Uanzishaji wa shughuli za kuongeza kipato: Shughuli za kuwapatia wananchi kipato zilianzishwa katika vijiji vya Kigonigoni, Kambi ya Simba, Simbomu and Vuchama Ngofi Wilayani Mwanga. Uchunguzi uliofanyika katika Halmashauri ya Siha ulibaini kuwepo na shughuli ndogondogo zakujipatia kipato. Wajasiriamali 72 walitambuliwa, pia kulikuwa na makundi manne ya ufugaji nyuki ambayo ni Kyasama, Kyihowo, Ukyinsha na Kishisha. Vikundi hivi vilipatiwa mafunzo ya uhifadhi wa udogo, ufugaji nyuki na kupatiwa mizinga ya kisasa 89. Wakulima wapatao 30 waliofanya ubunifu wa kutunza mazingira walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali juu ya kufunga bidhaa na kuweka maandishi kwenye vifungashio.

Kuboresha Ndiva (bwawa): Kutokana na maombi ya Vuchama Ngofi kuhusu kuboresha ndiva, Halmashauri ilifanya ukarabati kwa kushirikiana na TIP (Traditional Irrigation and Environmental Development Organisation Project). Ujenzi ualianza 2009 hadi 2011. Bwawa/Ndiva lina ujazo wa $200m^3$ kwa ajili ya kumwagilia 30Ha na kuwahudumia wakulima 30 wanaozalisha kahawa, ndizi, mahindi, maharagwe, na mbogamboga. Ukarabati pia ulihusisha kurekebisha mifereji na kuongeza kiasi cha maji yanayopita.

Kuanzisha kilimo cha mazao ya thamani kubwa: Halmashauri ilianzisha mazao mapya, mazao yanayoleta kipato haraka kama mbogamboga, iliki, pilipili n.k. Angalia picha hapa chini.



***Mazao ya thamani kubwa***

Ujenzi wa barabara: Halmashauri ilishirikina na wananchi kujenga barabara za vijiji ili kusafirisha mazao toka shambani hadi sokoni.



***Barabara mpya ya Kijiji***

Kuanzishwa kwa mashamba darasa: Halmashauri ilianzisha mashamba darasa ili wakulima wajifunze wao kwa wao. Katika vituo hivi, vikundi vya wakulima vilianzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutandaza mabomba, kuweka pipa la maji na mabomba ya kusambaza maji kama picha inavyoonesha hapa chini.



***Ndiva, tanki la maji na mabomba ya kumwagilia wilayani Mwanga***

Kuazisha Klabu za wanafunzi za kutunza mazingira: Klabu za kutunza mazingira zilianzishwa shuleni. Picha iliyopo hapa chini inaonesha Klabu ya kutunza mazingira katika shule ya sekondari ya Siha.



***Wanachama wa klabu ya kutunza mazingira shule ya sekondari Siha***

Jitihada za Ujanishaji Mashuleni. Ujanishaji mashuleni unahusisha elimu ya uhifadhi endelevu wa mazingira. Vijana wengi huzingatia masuala ya mazingira na wanavutiwa kufanya mabadiliko chanya katika mazingira yanayo wazunguka. Shule zinajiuhusisha na Ujanishaji huhimiza wanafunzi kuchukua jukumu la kuhifadhi mazingira na kufanya maamuzi shuleni. Masuala ya ujanishaji huingizwa kwenye mitaala ya shule; na huhusisha mfumo wa zawadi ili kuimarisha ushiriki changamfu. Msingi mkuu wa Ujanishaji unalenga kuhusisha masomo wanayojifunza na mwonekano wa mazingira ya shule zao. Mara nyingi shule hizi hufanikiwa na kufanya vizuri kitaaluma. Ujanishaji Mashuleni ni njia bora ya kuleta maendeleo endelevu kama sehemu ya maisha ya shule.

**Jitihada za Ujanishaji Mashuleni**

- Walimu wawili walienda Sweden na Afrika ya Kusini kujifunza namna ya kendesha mairadi ujanishaji mashuleni
- Kuandaa kitabu cha mradi:' Kitabu Cha Walimu na Wanafunzi Cha Shule za Sekondari Wilayani Siha".
- Kufanya utambulisho wa mradi kwa wadau kama wakuu wa idara, madiwani, walimu, wanafunzi na jamii inayowazuguka.
- Kutoa maelezo kwa wanafunzi na walimu jinsi ya kutumia kitabu.
- Kuanzisha vitalu vya mmiche ya miti.
- Kuanzisha makundi ya mazingira na vilabu mashuleni.
- Kupanda miti na maua kwenye mazingira ya shule.
- Kuanzisha mashindano ya ujanishaji shuleni na kutoa zawadi kwa washindi.

Muhusiano kati ya taasisi: Halmashauri inashirikiana vikundi vya wakulima na taasisi za kuweka na kukopa ( SACCOS na Mwanga community Bank) ili kutoa mikopo kwa wakulima.

**5.0 RASILIMALI**

Mradi wa kutunza mazingira uligharimu jumla ya TZS 159 milioni kama jedwali 3 linavyoonesha hapa chini.

**Jedwali 3: Fedha zilizotumika**

| Wilaya ya Mwanga | | | Wilaya ya Siha | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **Kiasi (TZS)** | **Chanzo** | **Shughuli** | **Kiasi (TZS)** | **Chanzo** |
| Vifaa vya ujenzi wa mfereji 3-6 km na mabomba | 32,000,000 | UNDP | Kujengewa uwezo | 21,950,400 | UNDP |
| Kuchimba mitaro, kusomba mawe, mchanga na kokoto | 9,600,000 | Nguvu za jamii | Misaada ya vifaa | 61,523,794 | UNDP |
| Usimamiaji | 3,200,000 | Halmashauri | Usimamizi na kufuatilia | 13,675,852 | UNDP |
| - | - | - | Shule za kuifadhi mazingira | 2,000,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Siha |
| - | - | - | Ziara ya mafunzo ya walimu 2 Africa ya Kusini na Sweden | 15,000,000 | Marafiki wa Sweden |
| **JUMLA** | **44,800,000** | - | - | **114,150,046** | **158,950,04** |

Rasilimali watu: mradi huu ulihusisha mhandisi wa umwagiliaji wa Wilaya, watalaamu wa umwagiliaji, wanafunzi, viongozi wa jamii na watendaji wa vijiji na wananchi ambao ndio wanufaika walijitolea kushiriki hatua zote za mradi.

**6.0 MATOKEO**

Mradi huu wa Uhifadhi Endelevu wa Mazingira katika Halmashauri za Mwanga na Siha umeleta matokeo yanayoonekana na yasiyoonekana wazi kama yanavyoelezwa hapa chini:

Uwepo wa maji ya umwagiliaji: Baada ya kuboresha Ndiva/bwawa na kuweka mabomba, ufanisi uliongezeka.Maji yaliyokuwa yameadimika kwa sababu ya uharibifu wa mazingira yanapatikana kwa wingi sasa. Mfano, chanzo cha maji cha Shighatini kilikauka na ikawa sehemu ya watoto kuchezea lakini jitihada endelevu za kuifadhi mazingira zimefanikisha kurudisha chanzo hiki kwa ajili ya maji ya kutumia majumbani na umwagiliaji kama picha inavyoonesha hapa chini.



*Alama inaonesha eneo la chanzo cha maji Shighatini*




*Bango-Linazuia shughuli eneo la maji ya mto*

Utumiaji wa mbinu mpya:  Jedwali 4 linaonesha wakulima wakitumia njia za kisasa kutengeneza matuta kuzuia mmomonyoko kwenye mteremko, utumiaji wa mbolea, na kufunika udongo/ardhi ili kuhifadhi maji ardhini. Mashamba mengi yamewekewa makinga maji (matuta) kwa kuzingatia vipimo.

**Jedwali 4: Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga – Matuta kwa matumizi endelevu ya ardhi.**

| Kijiji | Makinga Maji (matuta) | | | | Zao Linalolimwa | Aina ya zao (kg) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umbali Uliokusudiwa (m) | Umbali uliofikiwa (m) | Eneo/(ha) l matuta | Jumla eneo(ha) liliohifadhiwa | | Kabla | Baada |
| **Vuchama Ngofi** | 120,000 | 33,800 | 33.8 | 43.8 | Kahawa/ndizi, Mahindi/maharage & kilimo cha maua | Mahindi 90 kgs /.75 ha. Maharage 40kgs/0.75 ha. Mbogamboga | Mahindi 450 Kgs/.75 Ha. maharage 200Kgs/0.75 Ha. Mbogamboga TZS. 483,100/= kwa 0.5 Ha. |
| **Shighatini** | 110,000 | 32,000 | 32 | 38 | Ndizi,mahindi/maharage | | |
| **Ndanda** | 100,000 | 20,000 | 20 | 30 | Ndizi,mahindi/maharage | | |
| **Mbore** | 130,000 | 35,000 | 35 | 50 | Ndizi,mahindi/maharage Kilimo cha maua | Mahindi 90 kgs /ha. Maharagwe 40kgs/ ha. Mbogamboga | Mahindi 400 Kgs/.Ha. maharage 200Kgs/Ha. Mbogamboga TZS 480,000/ 0.5ha. |
| **Chomvu** | 125,000 | 40,000 | 40 | 52 | Ndizi/ kahawa ,mahindi/maharage | Kahawa 50 kgs / ha Ndizi 50 Mikungu wa Hekta. | Kahawa 250 - 300 Kgs /Ha Ndizi 200 Mikungu kwa ha |
| **Ndorwe** | 128,000 | 34,000 | 34 | 44 | Ndizi/ kahawa, mahindi/maharage | Kahawa 50 kgs / ha Ndizi 45 mikungu kwa ha. | Kahawa 250 - 300 kgs /ha Ndizi 150 mkungu kwa ha. |
| **Kighare** | 90,000 | 12,000 | 12 | 20 | Ndizi,mahindi/maharage | | |
| **Kirongaya** | 120,000 | 18,000 | 18 | 27 | Ndizi,mahindi/maharage/ Kilimo cha maua | | |
| **Kimbale** | 25,000 | 7,000 | 7 | 10 | Ndizi, mahindi, maharage Kilimo cha maua | Nyanya | Nyanya TZS 580,000/ 0.2ha. |

Uhamasishaji wa kilimo mseto: Wakulima wamerudia kwa kasi kilimo chao kinachozingatia matumizi mazuri wa ardhi ili kupata mazao mengi na ya aina tofauti huku wakihifadhi mazingira yao. Uoto wa asili nao umerejea kwenye maeneo yaliyokuwa yameharibiwa, na bustani za kiasili zimerudi kama picha inavyoonesha hapa chini.




Kupungua kwa Tope katika ziwa Jipe: Uoto wa asili unaozunguka ziwa Jipe umeimarika baada ya kupungua uchafu na maji yanayoingia ziwani yameongezeka na kusababisha kuongezeka kwa mazalia ya samaki kama picha chini inavyoonesha.



***Mazingira ya Ziwa Jipe baada ya jitiada za kuifadhi mazingira***

Uzalishaji wa mazao yenye thamani: Wakulima wameanza kuzalisha mazao kama ndizi iliyoboreshwa kutokana na migomba aina ya Jamaica, vitunguu swaumu, pilipili, iliki na ufugaji wa ng'ome wa maziwa.



***Vitunguu swaumu, Ndizi yenye ubora (aina ya Jamaica)***

Shughuli mpya za kuongeza kipato: wakulima wamekubali kufanya shughuli mpya ili kuongeza kipato kama ufugaji wa nyuki na kuchakata asali kazi mabayo inafanywa zaidi na wanawake baada ya kupatiwa zana za kisasa na kutundika mizinga upenuni mwa nyumba badala ya kutumia miti mirefu kama picha zinavyoonesha hapa chini.



***Wanawake wa Siha wakijihusisha na ufugaji wa nyuki***

Mazao yameongezeka: Uzalishaji kwa eneo ameongezeka sana kama jedwali 5 linanvyoonesha. Hii ni kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji kimewezesha uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa mwaka mzima.

**Jedwali 5: Uzalishaji kabla na baada ya kuboresha mazingira**

| Zao | Ukubwa/ eneo | Kiasi -2012 | Kiasi 2015 |
|---|---|---|---|
| Kahawa | Tani/ ha | 0.25 | 0.5 |
| Ndizi | Tani/ ha | 10 | 30 |
| Mahindi | Tani/ha | 1 | 4 |
| Asali | Lita mzinga | 1( nyuki wasio uma) | 2 |
| | | 3(nyuki wanaouma) | 6 |

Fursa za masoko: Kuboreshwa kwa barabara ili kufungua masoko kwa mazao ya kilimo na misitu. Katika Halmashauri zote mbili, wananchi walishiriki kufungua njia katika maeneo korofi na Halmashauri zote mbili zikachonga barabara na kuweka karavati na madaraja.

Kuongezeka kwa kipato: kutokana na yote yaliyoelezwa hapo juu, pato la kaya limeongezeka (angalia jedwali 6) mfano , Kikundi cha Vuchama Ngofi chenye wanachama 60, wastani kipato chao kimeongezeka kutoka TZS 300,000 had TZS 3,600,000 kwa mwaka. Bwana Juma Mbwambo ambaye ni mkulima mbunifu na mwenye eneo la 0.25 ekari, alipata TZS 580,000 kila alipovuna.

**Judwali 6: Mapato ya kikundi cha Vuchama Ngofi kuto ekari 0.5**

| No. | Zao la kilimo | Mauzo (TZS) |
|---|---|---|
| **1.** | Biringanya | 218,500/= |
| **2.** | Vitunguu | 73,600/= |
| **3.** | Kabichi | 68,700/= |
| **4.** | Karoti | 24,900/= |
| **5.** | Pilipili hoho | 53,600/= |
| **6.** | Saladi | 43,800/= |
| **Jumla** | | 483,100/= |

Kuimarika kwa hali ya maisha: kiwango cha hali ya maisha ya wanajamii kwa ujumla kimekuwa kizuri kama dalili zinavyoonesha kuwa wanaisha kwenye nyumba bora, zenye umeme na lishe na lishe bora.

Kuongezeka kwa mshikamano: Jamii nzima ina mshikamano. Uwezo wa kifedha wa wanawake umeondoa hali ya kuwategemea wanaume na imeimarisha familia zao. Wakulima wamejengewa uwezo, wanaaminika na wanapatiwa mikopo kutoka taasisi za edha.

Jitihada za Ujanishaji: Katika ya Wilaya ya Siha shule zimejitahidi kupanda miti na bustani za maua. (angalia picha chini). Wananchi wamepanda miti kandokando mwa barabara za vijiji



***Mazingira ya kijani – shule za wilaya ya Siha***

Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wana mtazamo chanya juu ya kupanda na kutunza miti katika mazingira; mashiriki ya dini nayo huchangia katika upandajai miti. Mfano kanisa la Kilutheri

huwataka wanafunzi kufuata misingi ya kikristo kwa kupanda miti 5 ndani ya eneo la kanisa na migine 5 nyumbani kwao ili kuongeza miti iliyopandwa na kujenga tabia ya upandaji miti.

**7.0 MIKAKATI YA ENDELEVU**

Mazingira ya kijani: Ili kutimiza lengo hili, lazima zoezi la kupanda miti, kutengeneza matuta na kilimo mseto viimarishwe. Ni lazima jamii itumie vijana kupanda miti na kuhifadhi mzingira kwa kuwahimiza wanafunzi kuanzisha Klabu za mazingira shuleni.

Kuimarisha vikundi vya wakulima: Kuwawezesha wakulima kutambua kuwa ni muhimu kuweka nguvu yao pamoja na kutumia taasisi za kifedha vizurina kuendelea kukumbushia umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Inasisitizwa wakulima kutumia mboji na kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia matone, kuongeza kipato kwa kufuga nyuki, kuanzisha na vitalu vya miti katika shule za msingi na sekondari.

Uhifadhi mazingira kuwa agenda ya kila mtu: Uhuifadhi wa mazingira ni shughuli ambayo ipo katika mipango na bajeti za Halmashauri.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Uongozi wa ngazi za Msingi: Maono ya uongozi wa ngazi za msing ndio mafanikio ya mkoa wa Kilimanjaro. Kazi ya sekretariati ya mkoa, wakurugenzi wa Halmashauri, na timu za wataalamu kwa kushirikiana na wanasiasa waliwezesha jamii nzima ielekeze nguvu katika miradi endelevu ya matumizi bora uya ardhi. Kulikuwa na uelewano mkubwa kati ya wanasiasa na wafanyakazi wa serikali za mitaa; hii iliwatia moyo wafanyakazi.

Kuheshimu juhudi za wananchi: Halmashauri inaheshimu jitihada na vipaumbele vya wananchi. Uharibifu wa mazingira unagusa mahitaji na vipaumbele vya wananchi hii ilisaidia kukusanya nguvu ya wananchi katika shughuli zote za uhifadhi na Usimamizi wa Matumizi endelevu ya Ardhi.

Ushirikiano imara kati ya wadau mbalimbali: Kuwepo kwa ushirikiano thabiti na UNDP, ELCT-Dayosisi ya kaskazini, utawala wa shule za msingi na sekondari, viongozi wa vijiji, vikundi na Klabu za mazingira. Kwa kushirikiana na SARI, Tengeru, Mlingano na SUA, Halmashauri zimetumia matokeo ya tafiti katika uhifadhi wa mazingira endelevu.

Uwepo wa wananchi wachapa kazi. Jamii za mkoa wa Kilimanjaro zina wananchi wachapa kazi na wenye nia ya kuongeza kipato bila kuathiri mazingira. Hii imechangiwa pia na kuwa na eneo dogo la ardhi ambalo wanapenda lizalishe kwa muda mrefu.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

**UHAMASISHAJI WA UTALII WA UTAMADUNI NA UHIFADHI SHIRIKISHI WA MISITU**







***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ni miongoni mwa Halmashauri 7 za mkoa wa Arusha. Halmashauri ina eneo la 14,036 $km^2$ na kati ya hizo 59% ni mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. Eneo linalobakia (41%) liko chini ya usimamizi wa hifadhi ya wanyama pori ya Loliondo na Ziwa Natron na lina hifadhi ya misitu. Eneo kubwa ni mteremko kuelekea kwenye bonde la ufa. Halmashauri ipo kati ya 1,320m na 1,535m juu ya usawa wa bahari na sehemu iliyoinuka zaidi ni 1675m juu ya usawa wa bahari. Kuna vilima vilivyotawanyika upande wa magharibi na Kusini. Halmashauri inapakana na nchi ya Kenya kwa upande wa Kaskazini, Halmashauri za Longido na Monduli kwa upande wa Mashariki, Karatu kwa upande wa Kusini, Itilima, Meatu na Serengeti kwa upande wa Mashariki.

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ina Tarafa 3 ambazo ni Sale, Loliondo na Ngorongoro, Kata 5, Vijiji 72 na Vitongoji 243. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2012 Halmashauri ina watu (74,278), kati yao wanawake ni 91,668 na wanaume 82,610. Kuna ongezeko la watu 2.9% na mgandamizo wa watu ukiwa12.4. Shughuli kuu za uzalishaji ni ufugaji (80%,) kilimo (13%) na utalii kama picha zinavyoonesha hapa chini.



***Ufugaji wa Ng'ombe, Kilimo na Utalii ni Kati ya Shughuli za Kiuchumi Wilayani Loliondo***

**2.0 TATIZO**

Jamii zinazoishi kando kando ya misitu ya Loliondo zina uhusiano mkubwa wa kimila na matumizi ya misitu hii kwa shughuli za utmaduni na imani. Japokuwa Wamaasai wa Loliondo wana ufahamu wa uhifadhi wa misitu na mali asili, kuna hatari kubwa sana ya kupotea kwa misitu ya asili kutokana na kizazi cha sasa kutozingatia njia za asili za uhifadhi wa misitu. Hii inadhirishwa na uhabifu mkubwa wa maliasili kupitia uvunaji haramu wa mbao, kilimo cha mazao mapya kwa kufyeka misitu na biashara ya kuni.

Vitendo hivi haramu vinamaliza misitu na kuharibu vyanzo vya maji. Misitu yote inayotegemewa na jamii (Loliondo 1, Seriani na Enguserosambu) ina eneo 112.05 $km^2$. Mwaka 2005 kiasi cha 200ha za msitu ziliharibiwa. Hivi karibuni (2012-2014) jumla ya magunia ya mkaa 112 na takribani tani 7 za mbao zilikamatwa na kutaifishwa. Halmashauri ilichukua hatua za kukomesha shughuli zote haramu. Kufikia mwaka 2014 kesi 13 za ukataji magogo zilikuwa zimefunguliwa mahakamani. Picha hapa chini zinaonesha vitendo haramu vya uharibifu wa misitu.




***Vitendo haramu katika hifadhi ya misitu***

Mwaka 2005 mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ilipiga marufuku shughuli za kilimo katika eneo la hifadhi Tarafa ya Ngorongoro. Hii ilisababisha umaskini mkubwa kwa kaya zilizotegemea kilimo kama njia ya kujipatia pato na kuwalazimu kutafuta njia mbadala ya kuishi. Kwa bahati nzuri Tarafa ya Ngorongoro ni maarufu kwa kuwa na wanyama pori wengi wa aina mbalimbali wanaovutia wapiga picha na mashirika ya wawindaji. Kama chanzo mbadala cha mapato utalii kuhusu mila na tamaduni za kimaasai ulianzishwa na vijana wa kimasai waishio vijijini waliokuwa wakicheza kandokando ya barabara waliwavutia watalii na kuwauzia vitu mbalimbali. Lakini wanawake na vijana hawakunufaika kwa kuwa hawakujipanga vizuri kwa ajili ya shughuli hiyo. Hivyo jamii ilitafuta ushauri kutoka Halmashauri na uongozi wa mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ili waanzishe utalii wa mila na utamaduni za kimaasai unaojulikana kama utalii wa kwenye maboma( cultural Boma) ambapo jamii ya kimasai ingeonesha vitu walivyotengeneza na kunufaika na utalii.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la kuanzisha shughuli hizi ilikuwa ni kuboresha hali ya maisha kwa kujishughulisha na kazi za kuihifadhi mazingira. Lengo mahsusi ni:

i. Kuhakikisha kuna uongozi na usimamizi wa kudumu wa hifadhi ya misitu ya Lioliondo 1, Seriani, na Enguserosambu.
ii. Kulinda vyonzo vya maji na mifumo yake.
iii. Kuiwezesha jamii kumiliki mali asili.
iv. Kuboresha maisha ya familia kwa kuwawezesha kujipanga na kufanya utalii endeleveu kwa kutumia mila na utamaduni.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Usimamizi Shirikishi wa Misitu: Usimamizi Shirikishi wa Misitu Ulifanyika kwa kusambaza wasimamizi wa hifadhi ya misitu ya Loliondo 1, Seriani, Enguserosambu kwenye vijiji vinavyozunguka misitu hii kwa kuwa hawa ndiyo wanufaikaji na faida wanzopata ni motisha ya kuhifadhi misitu.

Kujenga uelewa: Halmashauri ilifanya kampeni juu ya usimamizi endelevu wa misitu na vyanzo vya maji na mifumo yake. Pich hapa chini inaonesha wazee na wanasiasa wakijengewa uwezo wa uelewa juu ya kutunza misitu.



***Mkuu wa Wilaya na Wazee wa Kimila (Oloiboni) wakati wa kuhamasisha utunzaji mazingira***

Uanzishaji wa kamati za vijiji za mali asili: Vijiji vyote vinavyozunguka misitu hii vilianzisha kamati za mali asili za vijiji kwa ajili ya kusimamia matumizi ya mali asili. Baadaye Halmashauri iliendesha mafunzo kwa wajumbe 425 kwa malengo ya kuhifadhi misitu.

Kuweka mipaka ya misitu: Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mabalimbali waliweka mipaka ya misitu ya Loliondo 1, Seriani na Enguserosambu ili kuzuia/kupunguza watu kuingia katika maeneo ya hifadhi.

Kuunda kikosi cha skauti wa misitu: Kikosi cha skauti wa msitu kina jukumu la kuhakikisha misitu ni salama. Mafunzo ya skauti 15 yalitolewa juu ya kutunza mali asili katika chuo cha Likuyu Sehamaganga. Mafunzo yaligharamiwa na Frankfurt Zoological society na TAWIRI. Picha hapa chini inaonesha maskauti waliopata mafunzo.



***Maskauti waliopata mafunzo***

Ziara za mafunzo; Halmashauri iliondaa ziara ya kujifunza kwa wajumbe 50 wa kamati za kuhifadhi mazingira za vijiji kwenda Halmashauri za Longido na Babati. Wajumbe hawa walijifunza jinsi ya kutunza maliasili na jinsi jamii nzima inavyoweza kunufaika.

Kuanzisha miradi midogo ya kuhifadhi misitu: Jamii inayozunguka misitu ilianzisha miradi rafiki wa mazingira kama kufuga nyuki na kutengeneza majiko yanayotumia nishati ndogo. Kaya zipatazo 22 zilipata mizinga 34 katika kijiji cha Oloirien na Enguserosambu ili kupambana na uharibifu wa misitu. Wananchi 40 walipewa majiko banifu katia vijiji vya Magaiduru na Enguserosambu.




***Ufugaji nyuki ulioboreshwa***

Kuanzisha bodi ya wadhamini: Bodi ya wadhamini ilianzishwa kwa ajili ya msitu wa Enguserosambu. Bodi ina wajumbe 10 kutoka vijiji vitano; Enguserosambu, NAAN, Ng'awa, Tinaga, na Orkiu. Bodi husimamia shughuli zote za kuifadhi misitu kwa niaba ya wananchi. Wananchi walitengeneza sheria ndogo ili kulinda na kuhifadhi misitu inayowazunguka.

Utalii endelevu wa Mila na Tamaduni. Ili kuhakikisha utalii wa mila na utamaduni unashamiri mikakati iliwekwa. Majadiliano na ushauri vilifanyika kati ya mamlaka ya hifadhi ya ngorongoro na baraza la wafugaji shughuli za utalii wa mila na tamaduni endelevu, ikifuatiwa na mafunzo kwa jamii kuhusu masuala ya utalii. Jumla ya wananchi 627 kutoka vijiji 14 vya Ololosokwan, Engaresero, Sukenya, Pinyinyi, Arash, Losoito, Soitsambu, Piyaya, Oloipiri, Irkeepusi, Oloirobi, Misigiyo, Olbalbal, Endulen, walipatiwa mafunzo.

Kutambua maeneo ya utalii na faida zake: Maeneo ya utalii wa mila na utamaduni yalitambuliwa na faida zake zilibainishwa kwa vigezo vya kuwa wazi kwa utalii. Kisha maeneo yalitengwa kwa shughuli za utalii na maboma 16 ya kazi hii yalijengwa. Utalii wa vitu vya mila na utamaduni uliimarishwa baada ya kuanzishwa kwa umoja na usimamizi wa utalii ndani ya mamboma. Wajumbe wa umoja wa maboma hutoka kila kitongoji ambapo boma limejengwa kwa zamu. Kila baada ya miaka miwili kitongoji kilichagua vijana na wanawake wanne kwa kuangalia uwezekano wa kukaa kwenye maboma ya utamaduni. Wajumbe wa boma huchagua mwenyekiti, katibu, mweka hazina na afisa habari. Vijana hucheza ngoma za kitamaduni na wanawake huuza bidhaa. Mapato ya boma yanatokana na kiingilio cha TZS 20,000 kwa kila gari la watalii. Wajumbe wa boma hulipwa TZS 20,000 wakati viongozi hulipwa TZS 45,000 kwa mwezi.



***Boma la utamaduni***

**5.0 RASILIMALI**

Rasilimali fedha: shughuli za kuanzisha uhifadhi wa misitu ziligharimu TZS 65 milioni ambazo zilichangiwa na wadau mbalimbali kama inavyooneshwa hapa chini.

**Jedwali 1: Fedha zilizotumika kuanzisha hifadhi ya misitu**

| Chanzo | Kiasi (TZS) |
|---|---|
| Halmashauri ya Ngorongoro | 28, 000,000 |
| Wizara ya mali asili na utalii | 10, 000,000 |
| Frankfurt Zoological Society | 18, 200,000 |
| GIZ | 8, 800,000 |
| **Jumla** | **65,000,000** |

Rasilimali watu: Wananchi walishiriki katika shughuli mbalimbali pia maafisa misitu, skauti wa misitu, maafisa utalii, watendaji wa vijiji na kata na wajumbe wa Halmashauri ya vijiji walishiriki kikamilifu.

**6.0 MATOKEO**

Shughuli za kuhifadhi misitu zimewezesha matokeo yafuatayo. Wananchi wanamiliki shughuli za kutunza misitu. Kuna kamati na bodi za vijiji za kusimamia rasilimali za misitu. Vikundi vya kutunza mazingira vimeimarishwa kupitia shughuli za kuongeza kipato kama kufuga nyuki (angalia picha hapa chini).



***Ufugaji wa nyuki katika msitu wa Seriani***

Uvunaji endelevu wa mazao ya misitu; Misitu mikubwa hutoa mazao mbali mbali ya asili ambayo huvunwa kwa udhibiti. Misitu hii pia imeboresha hali ya hewa ya maeneo ya vijiji vinavyozunguka. Msitu wa Enguserosambu ni chanzo cha maji (chemchem) na mito inayotiririka hadi ziwa Natron (angalia picha chini). Skauti wa misitu 15 wamepatiwa mafunzo ya kutumia vyombo ya kisasa kama kamera na GPS kufanya doria eneo la hifadhi ya misitu kwa kushirikiana na Halmashauri, Frankfurt, zoological society na TAWIRI.



***Hifadhi ya msitu wa Enguserosambu***

Kutokana na utalii wa utamaduni na mila za kimaasaimaboma 16 yalijenga kwa shughuli za utalii na kuanzishwa mipango ya maendeleo ya shughulizi hizi kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya.







***Vitu vinavyouzwa*** ***Wanawake karibu na Boma la Irkeepusi*** ***Watalii katika boma la utalii***

Kuongezeka kwa vivutio vya utalii kupitia maboma 16 yaliyoanzishwa 2016. Pia watalii wameongezeka katika maboma kutoka 1537 mwaka 2012 hadi 3700 mwaka 2014. Kupitia utalii wa maboma jamii imeuza sanaa zao na ngoma wanazocheza. Mtalii akifurahi humtunza mchezaji kwa pesa.

Shughuli hizi zimeongoza kipato ambacho kimeboresha maisha ya wananchi. Baadhi ya maboma ya utamaduni yamekusanya mali kama ng'ombe, mbuzi na kondoo kwa ajili ya maziwa, lakini inpobidi huuza baadhi ya mifugo ili kununua maji na mahitaji mengine. Asilimia 2 ya mapato yote kwa mwaka hutumika kusaidia watoto/wanafunzi wa sekondari wanaotoka familia maskini. Utalii wa maboma umewafanya vijana wa kimaasai kukaa vijijini badala ya kutorokea mijini na kufanya bishara ndogondogo.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili jitihada hii iwe endelevu, kazi ya kuelemisha, kuhamasisha na kujenga uwezo wa kutunza misitu inaendelea katika vijiji vyote vinavyozunguka misitu. Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kwa kushirikiana na wadau wengine wanasaidia kuwawezesha wananchi kupata mikopo yenye riba nafuu. Kuna mikakati ya kuboresha zaidi uhusiano uliopo kati ya wanavijiji na Halmashauri katika kutunza misitu kupitia mikutano inayofanyika mara mbili kwa mwaka ili kujadili kwa pamoja maswala ya kuhifadhi misitu na maendeleo kama picha inavyoonesha hapa chini.





***Mikutano wa wadau***

Halmashauri inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za kuhifadhi misitu. Pia kuna shughuli endelevu za kuwawezesha wananchi kufuga nyuki, na kuna bajeti ya kununulia mizinga. Halmashauri imeanzisha vitalu vya miche ya miti katika vijiji vinavyozunguka hifadhi. Halmashauri inaendelea wakati wote kuelimisha na kuwajengea uwezo wananchi juu ya shughuli za utalii wa utamaduni kupitia ofisi ya Utalii.

Kuna juhudi za kujenga maboma ya utalii zaidi kwa ushirikiano na mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na Baraza la wafugaji. Jitihada hizi zinafanyika sambamba kujenga uwezo wa uendeshaji makini wa maboma ya utalii kupitia ushawishi wa watu maarufu. Fedha zaidi zinapatikana kutoka serikalini na watu binafsi, matangazo ya utalii wa utamaduni unafanyika kupitia mabango ya matangazo, majarida na vipeperushi

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Imani iliyojengeka juu ya misitu, jamii ya kimaasai hufanya shughuli za mila na utamaduni na sherehe misituni. Hivyo jamii yote ya kimasai huheshimu misitu na bidhaa yake. Ni mara chache jamii hii huchoma na kukata miti.

Wanadamu, mifugo na wanyamapori huishi sehemu moja: Wanadamu, mifugo na wanyamapori huishi pamoja bonde la Ngorongoro na maeneo mengi ya hifadhi. Kuwepo kwa sheria za kulinda na kuzuia vijiji vinavyozunguka misitu kumesaidia kupunguza uvamizi na kufanya vitendo haramu katika misitu. Uongozi imara ni pamoja na wazee wa kimila, wafanyakazi na jamii katika kuifadhi misitu.

Maeneo maalumu ya kihistoria, kuwepo kwa maeneo ya pekee ulimwengu ya kihistoria kama bonde la Ngorongoro, wanyama wengi wa aina mbalimbali na utofauti wa tamaduni na mila za kabila la wamaasai vimechangia sana. Kuna mchanga unaohama, bonde la Oldupai, bonde la Ngorongoro, sehemu ya kuwindia wanyama ya Loliondo, mlima wa Oldongo Lengai unatoa, sehemu ya njia ya kuhama kwa wanyama wa mbuga Serengeti n.k. Vivutio hivi huendelea kuwaleta watalii kwenye utalii wa maboma ya asili na huitia hamasa jamii kuendelea kuhifadhi mazingira.

Ushauri kwa wadau mbalimbali, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imewahusisha wadau katika kuhifadhi mali asili mfano kushirikiana na Frankfurt Zoological society, TAWIRI na GIZ katika kuboresha usimamizi endelevu wa misitu. Pia mikutano ya mara kwa mara hufanyika kuhusu uhifadhi wa mazingira.

# Sura ya Nne: Maendeleo ya Jamii Kiuchumi

Sura ya nne ina mbinu bora tano zinahusu jitihada za wananchi kujiletea maendele ya kiuchumu zinazohusiana na dhana mpya ya "zao moja kijiji kimoja". Dhana hii husisitiza maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe kwa kuibua miradi yenye upekee na vijiji vingine. "Kijiji kimoja Zao Moja" (OVOP) ni harakati zilizoanza miaka ya 1970 katika eneo la Oita nchini Japani malengo yakiwa kuinua uchumi vijijini. Lengo mahususi la dhana hii lilikuwa ni kuhamasisha kila kijiji cha Oita kuchagua mradi wa uzalishaji ambao unautofauti wa aina fulani katika mkoa na kuzalisha kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Dhana ya "Kijiji Kimoja Zao Moja" inalenga kuinua maendeleo ya jamii na uchumi katika mkoa kupitia kujitolea kuinua uwezo wa wananchi wa ngazi ya chini kabisa. Kabla ya kuanzisha harakati hizi katika eneo la Oita, waanzilishi walipata ushirikiano mkubwa wa jamii kupitia mashindano ya mpira na walikuwa na ushirikiano na miji rafiki ya nchi za nje. Mbinu hizi ziliwaweka watu pamoja, ziliwajengea uwezo wa kimaendeleo, na walishirikishana ujuzi waliopata. Mikakati mingine iliyofuata ilikuwa ni kuanzisha sera za jamii kuongeza zaidi thamani ya bidhaa, kuboresha mifumo, kuanzisha zao jipya au la pekee, ufundi wa kuchakata mazao ya kilimo, utalii, na mtazamo juu ya hali ya jamii.

Dhana ya "Kijiji Kimoja Zao Moja" inaonekana kuwa ni njia ya kuimarisha ujasiriamali wa watu wa vijijini kwa kutumia rasilimali, elimu na uzoefu, kufanya kazi zinazoongeza thamani kwa kuvipa utofauti bidhaa zao na kujenga uwezo wa rasilimali watu katika shughuli za uchumi kijijini. Kutumia ujuzi na rasilimali zilizopo bila kuathiri mazingira ni jambo linalotiliwa mkazo sana katika shughuli za dhana huu. Hii pia ina uhusiano na dhana ya maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe. Katika harakati za Kijiji Kimoja Zao Moja, kuna msemo maarufu usemao "Fikiri kimataifa lakini tenda kulingana na Mazingira" (*Think globally but act locally*")

Sura hii ina mbinu bora tano. Mbinu bora ya Halmashauri ya Iringa inaelezea juu ya juhudi za kuwa na uhakika wa chakula katika ngazi ya kaya katika Tarafa ya Pawaga. Wananchi wa Pwaga kwa muda walikuwa na tatizo la uhaba wa chakula. Ili kuondoa tatizo hili, Halmashauri ilianzisha mikakati maalumu ya kuhamasisha watu kupitia mchakato wa fursa na vikwazo kwa maendeleo, kuibua miradi ya umwagiliaji, kutengeneza andiko la mradi, kuunda miradi ya kisasa ya umwagiliaji, kujenga maghala, na kuunda SACCOS na AMCOS. Mikakati hii iliwezesha Tarafa ya Pawaga kuwa na chakula cha kutosha na kupata ziada katika kaya.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Korogwe inahusu kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji wa mpunga majira ya Mwaka na kuboresha hali ya maisha kupitia kutumia kilimo cha kisasa cha mpunga, ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, Kuanzisha chama cha ushirika imara, kuibua maeneo mapya ya umwagiliaji, kuomba vibali vya umwagiliaji, kuwapa ujuzi wakulima, kununua zana za kilimo na pembejeo, kuimarisha mawasiliano na kushirikishana mbinu mbalimbali.

Mbinu bora za mkoa wa Tanga zinatoka katika manispaa ya Tanga, Halmashauri za wilaya ya Mkinga na Pangani na zinahusu ufugaji wa ng'ombe wa maziwa unaofanywa na wafugaji wadogowadogo. Mbinu bora hizi zinaonesha kuwa wakulima wameachana na uvuvi na kuanza ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Ili kufanikisha lengo hili, kiwanda wa maziwa cha Tanga kilianzishwa (Tanga fresh milk processing factory), wananchi walihamasishwa, kuanzisha utaratibu wa kukopeshana mitamba, kuunda vyama cha ushirika cha ngazi ya vijiji na Mkoa, kuanzisha vituo vya kukusanyia maziwa, na kuongeza masoko ya maziwa.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya meru inaeleza uratibu fanisi wa wadau wa mnyororo wa thamani wa maziwa ambao unatumia utatu wa wadau katika kuzalisha, kuchakata na kuuza mazao ya maziwa ikiwa ni pamoja na ongezeko dhahiri la thamani. Jitihada hii ilifanikiwa kwa kuanzisha chama cha ushirika wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa wa Meru (MEDAFCO), kununua ardhi kwa ajili ya kujenga vituo vya kukusanya maziwa, kuongeza huduma za ugani, kuboresha barabara za vijijini na kuhamasisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi.

Mbinu bora katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai ijulikanayo kama mnyororo wa thamani ya maziwa katika jamii inaonesha kuwa kikundi cha wanawake wa Nronga (Nronga women group) wanashirikiana na Halmashauri kuongeza thamani ya maziwa. Jitihada hizo zimedumu kwa muda mrefu kwa kuwa mbinu zimekuwa zikibadilika ili mradi uendelee kuboreshwa. Mbinu ambazo wanawake wamekuwa wakizitumia tangu miaka ya 1950 ni kufuga ng'ombe wazuri wa maziwa, kununua mashine za kuchakata maziwa, kuunda kikundi cha kuuza maziwa, kuongeza thamani ya maziwa yanayokusanywa, kutoa mafunzo kwa akina mama na kuunda SACCOS.

Mbinu hizi bora katika sura hii ya nne zina mafunzo makuu yafuatayo:

"Kijiji Kimoja Zao Moja" sio mbinu zinazoanzia ngazi ya juu, hivyo ili Halmashauri ifanikiwe kuleta maendeleo ya kiuchumi ngazi ya chini ni lazima itumie wataalamu na viongozi kwa ajili ya maandalizi na ijikite katika kuhamasisha jamii ziweze kutambue fursa zilizopo, kuandae na kujenga uwezo wa vikundi vya uzalishaji, kutunga sheria ndogondogo na kuunda mahusiano kati ya wazilishaji na taasisi za kifedha. Hii inaonesha kuwa Halmashauri lazima isimamie mchakato huu hadi wazalishaji wawe tayari kuendesha shughuli zao zote.

Ni changamoto kwa Halmashauri zote kupata masoko ya mazao ya wananchi. Penye soko la uhakika wazalishaji hupeleka bidhaa. Ni wajibu wa afisa ugani kuwapa taarifa muhimu wakulima na kuhakikisha wana pembejeo na soko la mazao yao.

Uwezeshaji thabit ni muhimu katika mchakato wa Kijiji Kimoja Zao Moja. Wawezeshaji huwakutanisha wazalishaji na taasisi za utafiti na teknolojia, taasisi za huduma za kifedha, walaji/wateja kwa ajili ya kujua matakwa yao na kupeana uzoefu. Ubora na umahiri wa wawezeshaji ndiyo ndio kiini cha mafanikio. Ni muhimu Halmashauri kuandaa na kutumia wawezeshaji wenye elimu na ujuzi wa kutosha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wananchi ili wainue maendeleo yao kiuchumi. Hivyo ubora wa wawezeshaji na idadi yao ni kigezo kikubwa katika kufanikisha dhana hii.

Maono ya uongozi ni ufunguo wa mafanikio ya Kijiji Kimoja Zao Moja. Ni dhairi kuwa Mkurugenzi au mtu mwingine anapoanzisha dhana hii katika Halmashauri lazima apewe muda wa kutosha ili asimamie shughuli hizo hadi matokeo yaonekane. Hakuna uhakika kama wanaorithishwa shughuli hizi huwa na maono kama waliozianzisha. Pasipokuwa na mwendelezo wa shughuli kama hizi wakulima hukatishwa tamaa kwa kutofikia malengo yao.

Ni lengo la wadau kuongeza thamani za mazao kwa kutumia vifungashio vizuri na kutumia nembo na alama zinazokubalika kimataifa. Wazalishaji hawana budi kuacha kuuza mazao yasiyochakatwa ili wadau

wasaidie vikundi vyao katika shughuli za mchakato wa mnyororo wa thamani. Kuongeza thamani na mnyororo wa ongezeko la thamani ndilo jibu la uzalishaji mdogo na uhaba wa chakula.

Mnyororo wa ongezeko la thamani unaweza kuongeza thamani kila hatua kama kila kitu kimepangwa vizuri. Kijiji Kimoja Zao Moja inabidi ikidhi soko la mlaji wa eneo husika, kitaifa na kimataifa. Zaidi ya yote siyo lazima shughuli hizi ziwe za mazao ya kilimo tu. Zipo rasilimali nyingi, maporomoko, mapango, chemichemi za maji moto, mawe ya kipekee, miti, vyakula, na nyumba ambavyo vinaweza kutumika kwa ajili ya kutekeleza dhana hii. Hii inaonesha kuwa zipo rasilimali nyingi za Tanzania ambazo hazijatambulika kuinua maisha bora ya mtanzania.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

**KAMPENI YA UHAKIKA WA CHAKULA KATIKA KAYA - TARAFA YA PAWAGA**



***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya wilaya ya Iringa ipo kati ya latitudo $7^0$- $8^0$30" kusini na longitudo $34^0$- $37^0$ Mashariki. Inapakana na Halmashauri za Mpwapwa upande wa Kaskazini, Kilolo upande wa Mashariki, Mufindi upande wa Kusini, Chunya kwa upande wa Magharibi na Manyoni upande wa Kaskazini Magharibi. Halmashauri ina eneo la 20516km$^2$, kati ya hizo 9857.5km$^2$ eneo la makazi na sehemu iliyobakia ni mbuga za taifa, misitu, milima ya mawe na maji. Jumla ya 480,158ha zinafaa kwa kilimo lakini ni 34% tu zinazotumika kwa shughuli za kilimo.

Kwa mujibu wa sensa ya 2012, Halmashauri ina watu 254,033 kati yao 123,243 ni wanaume na 130,289 ni wanawake. Mgandamizo wa watu ni 25 kwa kila km$^2$. Kuiutawala Halmashauri in Tarafa 6 ambazo ni Kalenga, Kiponzelo, Idodi, Pawaga, Mlolo na Ismaini; Kata 28, Vijiji 133, vitongoji 718 na kaya 68,578. Takribani 80% ya shughuli za uchumi zinakana na shughuli za kilimo. Kilimo huchangia karibu 21% ya pato la mkoa ambalo ni TZS 1, 447,270 kwa takwimu za 2008 (RAS – Iringa).

## 2.0 TATIZO

Tarafa ya Pawaga inapatikana Kaskazini mwa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na inapakana na mkoa wa Dodoma.Tarafa ya Pawaga ipo nyuma ya bonde la ufa, ina ukame na mvua zisizoaminika hivyo kusababisha wakulima kupata mavuno machache. Ukame ulichangia kuleta njaa na kwasababu ya uhaba wa chakula kila mwaka wananchi walitegemea misaada ya chakula. Zao la mtama ndilo tu hustahimili lakini bei zake katika soko ni ya chini sana kuwezesha kaya kupata chakula mwaka mzima (ieleweke kwamba mchele ni chakula kikuu kwa jamii ya pawaga). Hali hii ilifanya Halmashauri kutathmini hali ya chakula ngazi ya kaya kabla ya kuomba chakula kutoka ofisi ya waziri mkuu. Msaada wa chakula kilichogawiwa kwa watu kiliambatana na sharti la kuilpiaTZS 50 kwa kila 1kg waliyopokea. Kujirudiarudia kwa baa la njaa na kutolewa kwa chakula cha msaada ilijulikana kama "mbochelo" yaani msaada wa chakula cha bure. Uhaba wa chakula kwa watu wa Pawaga lilionekana ni maumivu yasiyoisha kwa watu na Halmashauri. Tatizo hili lingewezi kuisha kwa kuimarisha hali ya chakula katika ngazi ya kaya kwa kuanzisha kilimoja cha umwagiliaji.

**Maoni ya Mhe. Diwani juu ya kijiji cha Magozi Diwani wa kata mpya ya Ilolo (mwenye guo ya njano)**

*"Magozi ilifikiriwa kuwa na uhaba wa chakula na kijiji maskini sana kwa vigezo vyote katika ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa"*



........nimekuwa diwani wa kata ya Ilolo Mpya tangu 1994. Nakumbuka kijiji cha Magozi ndicho kilikuwa kipya katika kata mpya ya Ilolo na tarafa ya Pawaga. Kijiji kilianzishwa 1980 baada ya kuwaondoa watu katika mbuga iliyopo tarafa ya Ruaha ili kuongeza eneo la hifadhi. Kijiji kipo nyuma ya bonde la ufa hivyo hukumbwa na ukame na baa la njaa. Mazao yanayohimili ukame ni mtama na uwele, lakini bei yake ilikuwa ya chini muno na wakazi wa Magozi hawakuzoea kula vyakula vingine tofauti na wali. Takribani kwa miaka 27 mfululizo wananchi wa kijiji cha Magozi walikumbwa na baa la njaa na waliishi kwa kutegemea msaada wa chakula kutoka serikalini, vikundi vya wasamalia wema kama WFP, Concern na Kanisa la Angilkana kama njia ya kujikwamua na tatizo. Wananchi walifanya kazi za vibarua katika vijiji vya Tarafa ya Pawaga ambavyo vilishaanzisha kilimo cha umwajiliaji kutoka mto Ruaha kwa kuzalisha mpunga kama vibarua. Wananchi wa Magozi walidhalilishwa kwa kuitwa "matrekta ya Magozi". Hii ni kutokanan na kutumika kwa ujira mdogo kwa jirani zao ambao walifaidika na miradi ya umwagiliaji ya Mlenge, Mkombelo na Lugangga. Muda wa kukaa na kupanga maendeleo ya kijiji chao haukuwepo kwakuwa muda mwingi uliishia kutafuta chakula. Maisha ya wananchi wa Magozi yalikuwa magumu sana. Wananchi waliishi katika nyumba za hali ya chini sana zijulikanazo kama "tembe" zilizojengwa kwa udongo, hakukuwa na duka wala huduma za afya karibu, hakukuwa na sehemu za burudani na mashine za kusanga nafaka, vyoo vilikua vibovu, hali ya lishe na usafi wa mazingira ulikuwa duni pia. Kabla ya 2008, kijiji cha Magozi kilifikiriwa kuwa ni kijiji maskini mkoani Iringa na Tanzania kwa ujumla......

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu lilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa chakula, kuongeza uhakika wa chakula na kipato kwa wananchi wa tarafa ya Pawaga. Malengo mahususi yalikuwa ni:

- (i) Kuongeza uzalishaji wa chakula kwa ekari kwa kutumia mbinu bora za kilimo
- (ii) Kuwawezesha wananchi kujenga miradi ya umwagiliaji
- (iii) Kuwezesha wananchi kukarabati mfumo mmoja wa umwagiliaji maji wa zamani
- (iv) Kusaidia wananchi kuinua pato la kaya katika kata
- (v) Kuhamasisha wananchi kulima mpunga kama zao mbadala
- (vi) Kuhamasisha wananchi kutumia maji kwa makini

***Mhe.Diwani akitathmini kijiji cha Magozi***

***"…t**umedhamiria kuondo tatizo la uhaba wa chakula na udhalilishaji…."*

*….. Baada ya kupata shida kwa miaka mingi, wananchi wa Magozi walipata hamasa kutoka kwa jirani zao waliokua wameanzisha miundo mbinu ya umwagiliaji kwa ushirikiano na wafanyakazi wa Halamshauri na Mradi wa Participation Agricultural Development and Empowerement Project (PADEP). Tathmini ilifanyika kubaini hali halisi na kuweka vipaumbele kwa kutumia mchakato wa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Ilibainika kuwa uhaba wa chakula ndilo lililokuwa tatizo kubwa kuliko yote na fursa iliyokuwepo ni kutumia mto Ruaha kwa kilimo cha mpunga kama zao mbadala la biashara na chakula. Azimio lilikua ni kuondoa uhaba wa chakula kwa kuanzisha mradi wa umwagiliaji na kutumia njia za kisasa za kuchakata mpunga kupitia mnyororo wa ongzeko la bthamani katika kijiji cha Magozi.*

*Upembuzi yakinifu shirikishi ulifanyika na gharama za mwanzo zilikuwa ni Tzs 243 milioni, utekelezaji wa mradi ulifanyika kwa ushirikiano na wadau mbalimbali kama WFP, UNICEF, Anglican Church (Tzs 70 milioni), Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (Tzs 40 milioni) na wananchi Tzs 28 milioni kwa kutoa nguvu zao na kukusanya vitu. Mamlaka ya bonde la mto Rufiji ilitoa kibali cha kutumia maji ya mto Ruaha kwa ajili ya kilimo. Tulidhamiria kuondoa uhaba wa chakula na dharau………*

4

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Ili kuhakikisha kuna chakula cha kutosha katika wilaya ya Iringa mikakati ifuatayo ilitekelezwa.

Kuhamasisha wananchi, wananchi walihamasishwa kupitia mchakato wa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Katika mchakato huu wananchi waliibua matatizo/changamoto, kutoa maamuzi, utekelezaji, kusimamia na kufanya tathmini ya mradi ili kuondokana na kutegemea misaada ya chakula cha kutoka nje. Picha ifuatayo inaonesha wanakijiji wa Magozi wakishiriki katika mchakato wa kutambua fursa na vikwazo vya maendeleo.



***Kikao cha mchakato fursa na vikwazo kwa maendeleo***

Kutambua miradi ya umwagiliaji ya zamani: Wananchi walishiriki kutambua miradi iliyokuwa inatumika huko nyuma ili kuweka misingi ya kuboresha mifereji ya umwagiliaji maji na kuandaa maandiko ya miradi. Wananchi kwa kushirikiana na wawezeshaji kutoka Halmashauri waliandika andiko kwa ajili ya kupata fedha za miradi ya umwagiliaji minne ya Mlenge, Luganga, Magozi na Mkombozi.

Ujenzi na ukarabati wa miradi ya zamani: Ujenzi na ukarabati wa miradi ya umwagiliaji ulifanywa na wananchi kwa kushirikiana na mhandisi wa umwagiliaji. Ili kufanya miradi ya umwagiliaji iwe endelevu na imilikiwe na wananchi, umoja wa watumiaji maji (Water User association- WUA) uliundwa na

mafunzo yakusimamia maji kwa mashamba yote yalifanyika. Picha ifuatayo inaonesha seheme ya mifereji inapochukulia mradi wa Mlenge.



***Mfereji wa kupitishia maji ya umwagiliaji wa Mlenge***

Kuanzishwa mfumo wa ghala; Maghala matatu yalijengwa katika Vijiji vya Kimande, Igodikafu na Itunundu. Ghala hizi zililenga kusaidia kukusanya mpunga hadi kupatikana kwa bei nzuri kwa wakulima. Kwa mfumo huu, ghala zilikuwa kama benki zilizowawezesha wakulima kupata bei nzuri baada ya msimu wa mavuno.

Kupata zana za kilimo: Wawezeshaji kutoka Halmashauri waliunganisha vikundi vya wakulima, kuvipatia mafunzo na kuviunganisha na wauzaji wa vifaa vya kilimo ambapo vifaa vilivyonunuliwa ni power tiller 126, matrekta 9, mashine 3 kwa ajili ya mnyororo wa ongezeko la thamani.

Kuundwa kwa SACCOs na AMCOs: Wananchi walianzisha vyama vya kuweka na kukopa na kuuza mazao. Wawezeshaji waliwafundisha wakulima kuhusu kufunga bidhaa, kuweka nembo na alama na kutangaza bei za bidhaa kwenye soko.



***Wakulima walifundishwa kwenye mradi wa Mlenge***

Kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha: Wawezeshaji walipanua wigo na kuwaunganisha wakulima na taasisi za kifedha ili waweze kupata mtaji wa miradi yao ya umwagiliaji. Walijenga vituo vitatu vya kuuzia mazao katika vijiji vya Luganga, Ilolo mpya na Itunundo. Vituo hivi pia ni sehemu ya kupatia taarifa za masoko ya mazao ya kilimo.

Kutatua migogoro: Wananchi walitengeneza mbinu za kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwa kutumia kamati ya usuluhishi inayoundwa na wakulima na wafugaji ili kumaliza tofauti zao kwa makubaliano.

Kuanzishwa mpango wa matumizi ya ardhi: Ili kutumia ardhi ipasavyo wananchi walianzisha mpango wa matmumizi bora ya ardhi na kupunguza migogoro kupitia mhandisi wa umwagiliaji wa Wilaya.

Ufahamu wa mazingira: wawezeshaji wa Halmashauri walifanya kampeni kuhusu kuhifadhi mazingira na njia bora za kutumia maji.

Kuanzishwa kwa skauti wa kijiji: wananchi kwa kushirikiana na hifadhi ya Ruaha walianzisha skauti wa vijiji katika vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi kwa ajili ya kudhibiti wanyama wanaovamia mashamba.

Kuimarisha ushirikiano na wadau: wananchi waliimarisha ushirikiano na wadau kama mamlaka ya Bonde la mto Rufiji, Wilaya za Mufindi, Iringa na Kilolo. ili kukabili changamoto za kuhifadhi eneo la mto Ruaha walitekeleza sheria ya kuhifadhi mazingira ya 2004 inayozuia kutengeneza matofali na kukata miti katika kingo za mito.

**Maoni ya Mh Diwani juu ya utekelezwaji wa mradi katika kijiji cha Magozi**

*..“ Hatuhitaji msaada wa chakula zaidi bali tuwezeshwe kupata chakula chetu wenyewe kwa kutumia rasilimali adimu, Mto Ruaha”..*

*....... Mradi ulitekelezwa kwa ushirikiano wa wadau kama TASAF (TZS 105 milioni), WFA, UNICEF, Anglican church (TZS 70 milioni), Halmashauri (TZS 40 milioni) na wananchi wa vijiji vitatu vya Ilolo, Mkombilenge na Magozi kwa pamoja vikijulikana kama MKILIMA walitoa TZS28 milioni kwa kuchangia nguvu zao na kuleta vifaa. Ujenzi ulianza 2016 kwa kujenga sehemu ya kuchukulia na kuruhusu maji kwa ajili ya vijiji vitatu, mifereji mikubwa ilikuwa ya Magozi-9km Ilolo-12km na Mkombilenge-18km. Katika msimu wa 2007/08, kilimo cha umwagiliaji cha mpunga kilianza kwa kusaidiwa na mfuko wa maendeleo wa Wilaya wa umwagiliaji (District Irrigation Development Fund -DIDF). KATI YA 1300Ha, 750Ha ziko chini ya kilimo cha umwagiliaji katika kijiji cha Magozi pekee, hivyo bado kuna uwezekano wa kupanua kilimo.Kama mradi, tumejipanga kama umoja wa watumia maji tukiwa na katiba yetu na uongozi wetu.....*

## 5.0 RASILIMALI

Rasilimali fedha: vyanzo vya pesa ni kutoka DADPS, DIDF na Halmashauri kama jedwali linavyoonesha hapa chini.

**Jedwali 1: Rasilimali fedha kutoka 2009-2013/14**

| Mwaka | Kiasi kilichopokelewa (TZS) |
|---|---|
| 2009/10 | 2,533,655,000 |
| 2011/11 | 1,850,000,000 |
| 2011/2012 | 2,120,000,000 |
| 2012/2013 | 0 |
| 2013/2014 | 1,831,000,000 |
| 2014/2015 | 128,329,610 |
| Jumla | 8,462,984,610 |

Rasilimali watu. Jumla ya maafisa kilimo saba wanakaa kata za Ilolo mpya, Itunundu na Mlenge katika Tarafa ya Pawaga ili kutoa msaada wa karibu wakisaidiana na afisa umwagiliaji wa Wilaya.

Uwepo wa chanzo cha maji. Bonde la mto Ruaha hupitia Pawaga ni eneo zuri kwa kilimo cha umwagiliaji. Miradi mine ya umwagiliaji ilitengenezwa katika tarafa ya Pawaga yenye ukubwa wa 18,300ha na inayofaa kwa umwagiliaji ni 7,350ha.



**Mifereji ya umwagiliaji**

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa mikakati iliyotajwa hapo juu ulizaa matunda yafuatayo:

Uboreshaji wa mazao ya kilimo: Wakulima wanatumia mbegu bora (kama Zambia, AFA Mwanza na Fire dume), matumizi ya trekta badala ya jembe la mkono, kutumia viua magugu badala ya kupalilia na kuvuna kwa kutumia mashine.



***Vitalu vya Miche Bora ya Mpunga***



***Mashine la Kulimia***



***Mashine ya Kuvunia Mpunga***

Kuongezeka kwa mazao kwa eneo na uzalishaji kwa ujumla: Uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani 0.6 mwaka 2004 hadi tani 1.6 kwa ekari mwaka 2013. Hii iliongeze uzalishaji toka tani 12,192 mwaka 2004 hadi tani 58,370 mwaka 2013



***Mashamba ya mpunga skimu ya umwagiliaji-Magozi***

Matokeo mengine ni pamoja na (i) kuwepo chakula cha kutosha katika ngazi ya kaya kiasi cha kutosha milo mitatu kwa siku. (ii) kuwepo kwa ongezeko la kipato katika ngazi ya kaya na hii imewawezesha wakulima kukidhi gharama za shule, matibabu na huduma nyingine. (iii) maisha ya wanakijiji yameboreka kwa kiasi kikubwa. Hili linadhihirishwa na ujenzi wa nyumba za kisasa, ufungaji wa umeme wa nguvu ya jua kwa ajili ya mwanga na matumizi ya simu, manunuzi ya meza za kucheza *pool,* utumiaji wa simu za kisasa, uanzishwaji wa maduka, kutuma pesa kupitia mitandao kama M-pesa, Tigo-pesa na Airtel money. Shughuli nyingine ni za saluni za kike na kiume na vyombo vya usafiri kama pikipiki (bodaboda). Picha hapa chini inaonesha maisha yalivyoboreshwa.

Kabla Baada



Kabla Baada





*Pikipiki*



*saluni ya kiume*



*duka la dawa*



*solar*



*pool table*

Mafanikio mengine makubwa ni kupata soko la mchele wa Pawaga. Kwa kutumia vifungashio na nembo kama "PAWAGA RICE" wakulima wamepata soko la uhakika. Kuna ongezeko la ajira, kilimo cha umwagiliaji kimewawezesha wananchi kujiajiri. Pia kilimo hiki kimewafanya vijana kukaa vijijini. Jitihada hizi zimekuwa chanzo cha kuongezeka kwa mapato katika Halmashauri kutokana na kodi ya mazao kutoka TZS 8 milioni mwaka 2011 hadi TZS 36 milioni mwaka 2014.

**Maoni ya Mh. Diwani juu ya maendeleo ya Magozi**

.......” *Wa mwisho awa wa kwanza”* .....

Kwa sasa wananchi walioko katika mradi wa umwagiliaji wa Tarafa ya Pawaga ni wa kwanza katika kuzalisha. Baada ya kulima kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji na kuboresha mbinu za kilimo, wastani wa eneo la kilimo kwa kaya limeongezeka kutoka ekari 0.25 hadi ekari 5. Kwa sasa wanaolima kwa kutumia jembe la mkono ni 10% tu. Matumizi ya dawa za kuua magugu badala ya kupalilia na kutumia mashine za kuvuna mpunga badala ya mikono yameongezeka.

Uzalishaji umeongezeka kutokana na kukubali kutumia mbegu bora kama Zambia, Afaa-Mwanza Fayadume na SARO-5 hadi kufikia wastani wa magunia (18-20) kwa ekari sawa na (3.888-4.32 tani/ha). Japo SARO-5 inaweza kutoa hadi tani 4.6 kwa ha, zile mbegu tatu za mwanzo ndizo zinapendelewa zaidi kwa sababu zinatoa mchele wenye Ladha nzuri, una harufu nzuri na unasoko la kudumu. Kwa mafanikio ya muda wa kati, msaada wa chakula katika Kijiji cha Magozi sasa ni historia kwa wakazi wa Magozi. Maisha ya wakazi wa Magozi yameimarika kutokana na biashara ya mpunga/mchele na vijana wamebakia vijijini. Kuna uhamiaji wa watu kutoka vijiji vingine kuja kutafuta kazi za mashambani na nyingine kama vibarua, kukoboa mpunga, ufundi seremala na uashi ambavyo vyote vimetengeneza ajira. Uwezo wa kaya kuchangia manedeleo ya mradi umeongezeka hadi kufikia Tzs 360,000 kwa kila kaya kwa mwaka. Wananchi wamejenga ofisi ya Kijiji. Watu binafsi hasa vijana wamejenga nyumba za kisasa. Ingawa haijaunganishwa kwenye gridi ya umeme wa Taifa, wanatumia umeme wa nguvu za jua kwa ajili ya runinga. Kusema uweli tulichelewa kimaendeleo ukilinganisha na majirani zetu, lakini mabadiliko yanavutia. Kama jamii, tunajifunza na tunatarajia kufanya makubwa zaidi. Baadhi ya wajasiriamali wetu wamewekeza mapato ya mchele kwa kujenga nyumba mijini. Huduma za usafiri wa pikipiki zimekuwa kitu cha kawaida. Vijana wengi wanapikipiki na taratibu tunaanza kupata usafiri wa Toyota Noah. Tunataka kuanza kilimo cha misimu miwili kwa mwaka ili kutumia miundo mbinu ya umwagiliaji vizuri na kuongeza mazao mara dufu. Tunatarajia kuboresha mazao yetu, kwa kutumia mashine ya kuchakata na kuweka mchele katika viwango. Vijana wanazidi kutafuta bei nzuri ya mazao yetu, na shirika la maendeleo la Japan (JICA) na PHRD wanasaidia harakati hizi. Mradi wa Magozi ni miongoni mwa miradi 14 inayonufaika na TASDP (Tanzania

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Kuna harakati za kuimarisha umoja wa wanachama wa umwagiliaji na wamekubaliana kuchangia 5% ya mapato yao ili kusimamia miradi. Wakulima wanaendelea kupata elimu juu ya mazao ya kilimo, usimamizi na utunzaji wa fedha. Halmashauri itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu katika shughuli zote za mchakato wa mnyororo wa kuongeza thamani. Jamii itaendelea kushirikiana na RUBADA ili kupata kiasi cha maji zaidi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kuvuna mara mbili kwa mwaka. Vikundi vya vijana vitaendeleza harakati za kutafuta masoko ya mchele.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Siri za mafanikio ni pamoja na (i) kushiriki kwa wananchi katika mchakato mzima wa kuibua, kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi. (ii) kutumia watu wengi wenye ujuzi tofauti na wadau tofauti kama njia ya kutekeleza mradi (hii ilihusisha maafisa umwagiliaji, UNICEF, WFP, Anglican Church, Uyole Research Institute). (iii) Mradi kukubalika mbele ya wanasiasa (madiwani). (iv) Uongozi imara wa Vijiji/Kata ulileta mshikamano mkubwa kwa wananchi ili waweke nguvu zao pamoja. (v) Kuwepo kwa ardhi nyingi yenye rutuba katika Tarafa ya Pawaga. (vi) Ushirikiano mzuri kati ya sekta binafsi na sekta ya umma (PPP)

katika kutafuta rasilimali. (vii) Kujitoa kwa hali ya juu kwa wafanyakazi wa Halmashauri, mfano mhandisi wa umwagiliaji alisimamia shughuli za mradi kila siku.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE


**UMWAGILIAJI KWA UZALISHAJI MPUNGA WA UHAKIKA**



***Uzoefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe inapatikana Latitudo ya $4^0 15''$ na $5^0 15''$ Kusini, Longitudo $38^0$ na $38^0 45''$ Mashariki. Halmashauri ina eneo la $3{,}544km^2$. Kwa mujibu wa sensa ya 2012 Halmashauri ina watu 247, 363, na kati yao 121,152 ni wanaume na 126,211 ni wanawake. Kiutawala Halmashauri ina Tarafa 4, Kata 20 na Vijiji 122 na Vitongoji 610.




***Ramani ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe: Utawala***


Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo cha mazao na ufugaji, matumizi ya mali asili, biashara na viwanda vidogovidogo. Kilimo ni uti wa mgongo katika Halmashauri na takribani 90% ya watu wote hutegemea kilimo na ufugaji. Takribani 133,397ha zinafaa kwa kilimo. Wapo wakulima wadogowadogo na wakubwa wenye mashamba makubwa.

Kuna tofauti za miinuko na hali ya hewa inayowezesha kupatikana mazao katika nyanda tatu. Kuna uwanda wa milima, uwanda wa chini wa maji, na uwanda wa ukame wa wastani. Umwagiliaji upo kandokando ya mito. Sehemu kubwa ya ardhi inaudongo tofauti, mchanga na mfinyazi na uoto wa asili ni wa kitropiki zaidi.

Nyanda za milima ni 25% ya eneo lote na hupatikana kati ya 900m-1500m juu ya usawa wa bahari. Nyanda za chini huchukua 35% ya eneo lote na lipo kati ya 600m-800m juu ya usawa wa bahari na una hewa yenye unyevunyevu wenye joto na hupata mvua za wastani wa 800mm-1000mm kwa mwaka. Kuna mito kadhaa kama Pangani, Soni na Lwengera ambayo hutoa maji ya umwagiliaji. Mazao ya chakula yanayolimwa ni mahindi, mpunga, maharage, mihogo na nyanya. Mazao ya biashara ni korosho, pamba, katani na matunda kama maembe, machungwa na machenza. Pia kuna mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku kwa ajili ya maziwa na nyama. Nyanda za chini kuna maeneo ya Korogwe (kata ya Ng'ombezi), tarafa za Magoma na Mombo (kata ya Makuyuni). Mbinu bora hii inahusu tarafa ya Mombo.

Eneo la kilimo cha umwagiliaji linajumuisha maeneo ya ukanda wa chini wenye majimaji na ukame kiasi ambamo mito mikubwa hupita. Halmashauri ina eneo zuri la umwagiliaji lenye ukubwa wa 18,000ha lakini ni 6000Ha sawa na 33.3% ya eneo ambalo kwa sasa lina kilimo cha umwagiliaji. Mpunga ndilo zao kubwa linalozalishwa kwenye mabonde haya na kilimo hutegemea maji ya mito. Pia kilimo cha

umwagiliaji hufanyika sehemu za milimani ambako kuna eneo mfano wa kisahani kwa ajili ya kilimo cha nyanya, vitunguu na kabichi.




***Maeneo ya kilimo Katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe***

Eneo lenye ukame kiasi huchukua takribani 40% ya eneo lote na linapatikana kati ya 400mm-700m juu ya usawa wa bahari na hupata mvua chini ya 600 mm kwa wastani kwa mwaka.

**2.0 TATIZO**

Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe imeshuhudia ongezeko kubwa la watu. Hii imesababishwa na uwepo wa watu wengi sehemu za milimani ambao huharibu mazingira. Kupungua kwa wastani wa mvua kwa mwaka na matumizi mabaya ya maji kulipunguza maji kwa ajili ya umwagiliaji maeneo ya chini na yenye ukame ambayo ni maarufu kwa  kilimo cha mpunga na mbogamboga. Tangu 1967 hadi 1978 wakulima wa Mombo walijihusisha na umwagiliaji japo kwa kutumia njia za kizamani ambazo hazikutoa mazao mengi (tani 2 kwa Ha), matumizi ya mbegu duni, kutokea mafuriko na ukame, kurokushirikiana katika shuguli za kilimo,kuvuna mara moa kwa mwaka, migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na kutokuwepo kwa kwa ongezeko la thamani ya mazao. Yote haya yalisababisha mavuno kuwa machache, umaskini ulitawala na hali ya maisha ilibakia kuwa duni miongoni mwa wakazi wa Tarafa ya Mombo.



***Umwagiliaji kabla ya maboresho***

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la kuanzisha jitihada hiii ni kuwa na matumizi bora ya ardhi na maji, kuongeza uzalishaji, kwa eneo, kuongeza kipato, na kupunguza umaskini wa wakazi wa Halmashuri ya Wilaya ya Korogwe. Malengo mahsusi yalikuwa ni;

(i) Kupima maeneo ya umwagiliaji na kuyagawa kwa wakulima
(ii) Kujenga miundombinu mipya na kukarabati miundombinu ya zamani ya umwagiliaji
(iii) Kuweka mfumo endelevu wa utumiaji maji kwa mujibu wa kibali
(iv) Kuboresha mfumo wa kilimo ili uweze kuongeza uzalishaji, kuongeza kipato cha wakulima, na kuwezesha kuwepo kwa uhakika wa chakula kila kaya
(v) Kutafuta soko la uhikika la mchele wa Mombo ndani na nje ya Tanzania
(vi) Kuwandaa wakulima kuzalisha kwa vikundi na katimaye kuunda chama cha ushirika.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Mradi wa umwagiliaji wa Mombo ulianza 1967 ukiwa na wakulima 40. Mradi umefanya maboresho na mabadiliko ya kisasa ya uzalishaji wa mpunga. Ili kuweza kufikia malengo yaliyotajwa hapo juu mikakati mbalimbali ilitekelezwa kama inavyoelezwa hapo chini:-

Ukarabati wa mwanzo wa mradi: mwaka 1979 mradi ulifanyiwa ukarabati kwa kujengwa mfumo wa wazi wa kuchukua maji kwenye mashamba. Bwawa pia lilijengwa ili kukidhi kiwango cha maji kwenye mashamba. Ukarabati uligharimiwa na shirika la maendeleo la Ujerumani (Germany Development organization (GTZ). Mkakati wa pili ulikuwa ni kupima ekari 300 na kugawa upya ardhi ya umwagiliaji; Wakulima walikubali kwa hiari na ekari 360 zilipimwa na kugawanywa kwa kila mwanachama 0.5 Ekari. Hii inaonesha kuwa baadhi ya wanachama walipoteza ardhi yao. Kati ya ekari 360 zilizopimwa, ni ekari 220 zilizotengwa kwenye safu 16. Mkakati wa tatu, Halmashauri aliwasaidia wakulima kuomba kibali cha kutumia maji kutoka mamlaka ya mto Pangani. Uongozi wa ushirika wa mradi wa umwagiliaji wa Mombo uliomba kibali na kupewa cheti cha umiliki no 2508.

Kuunda na kusajili chama cha ushirika: Mwaka 1979 Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ilisaidia Mradi wa Umwagiliaji wa Mombo kuunda na kusajili chama cha ushirika (Namba ya usajili 2207). Chama cha ushirika cha Mombo kilikuwa na wanachama 350 (wanaumme 135 na wanawake 115). Kuundwa kwa Chama cha ushirika wa wakulima wa Mombo ilikuwa ni kuhakikisha wakulima wanafanya uchaguzi wa kidemokrasia, wanafanya vikao kwa mujibu wa katiba, wanafuata taratibu na wanajihusiha na shughuli za uzalishaji kwa kuwatumia wafanyakazi wenye ujuzi toka Halmashauri.

Ukarabati wa pili wa mradi: Mwaka 2000 Halmashauri ilipata fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya ukarabati. Ukarabati wa awamu ya pili ulihusu ujenzi wa tuta la kuzuia mafuriko, kuzuia bwawa kujaa udongo, kujenga/ kukarabati mifereji ya kusambaza maji na kuboresha barabaraza ili kufikia mashamba.
Picha hapa chini zinaonesha uboreshaji wa mifereji ya zamani ya umwagiliaji, milango ya kutawanya/ kugawia maji na bwawa.









***Mifereje iliyoboreshwa*** ***Mlango Wa Maji*** ***Bwawa***

Mafunzo kwa wakulima: Maafisa ugani na wataalam wa umwagiliaji walitoa mafunzo kwa wakulima wa mpunga juu ya kuunda ushirika na vikundi vya uzalishaji, matumizi bora ya maji na ardhi, kutumia kilimo cha mbolea ya mboji, kuchagua na kutumia mbegu bora, kuandaa vitalu, na njia za kupanda na kupandikiza. Maafisa ugani wa Wilaya waliwashawihsi wakulima kutumia mbegu bora kwa kuwapa wakulima mbegu zilizoboreshwa zenye kutoa mazao mengi, zinazo komaa haraka, na zinazo stahimili magonjwa mengi kama picha zinavyoonesha hapa chini.





***Shamba la mpunga na shamba darasa***

Kwa ushirikiano na afisa masoko wa Halmashauri, afisa kilimo na wanasiasa, wakulima wa mpunga walitafuta masoko ya mchele wa mradi wa umwagiliaji Mombo. Utafiti ulionesha kuwa kuna soko la kutosha ndani na nje ya mkoa wa Tanga. Masoko ya uhakika zaidi yalikuwa Dar es salaam, Moshi na Arusha. Ili kuimarisha mkakati wa Masoko, mtandao wa mawasiliano na kupeana habari kati ya wakulima wa mpunga, wanaushirika na wadau wengine (PPP) ulianzishwa. Mtandao ulisaidia kupata habari za masoko, technologia, taasisi za kifedha na utendaji mzuri wa wakulima wa mpunga.

## 5.0 RASILIMALI

Halmashauri ya Wilaya Korogwe ilitumia TZS 1.4 bilioni kati ya 1979 hadi 2014 kwa shughuli mbalimbali kama jedwali 1 linavyoonesha.

**Jedwali 1: Rasilimali za Mradi wa Umwagiliaji Mombo**

| Shughuli | Fedha (TZS) | Chanzo |
|---|---|---|
| Ukarabati wa mradi 1979 | 14,000,000 | GTZ |

| | | |
|---|---|---|
| Kupima ekari 360 na kuzigawa upya 1979 | 10,000,000 | Halmashauri |
| Kupima ekari 360 na kuzigawa upya 1979 | 336,000,000 | Benki ya Dunia |
| Ukarabati –awamu yapili 2000 | 15,000,000 | Halmahsauri |
| Mafunzo kwa wakulima | 10,000,000 | DADPs |
| Kusambaza mbegu bora | 22,000,000 | DADPS |
| Ujenzi na uboresha endelevu wa miundo mbinu | 100,000,000 | PHDR |
| Kununua zana za kilimo (mashini za kufyeka, kuvuna na kukopoa ) ujenzi wa nyumba ya mashine za ghala | 1,407,000,000 | PHDR |
| **Jumla** | **1,407,000,000** | |

**5.0 MATOKEO**

Halmashauri ya Wilay ya Korogwe imefanikiwa kaitika mambo mbalimbali ya uzalishaji na uchakataji wa mpunga. Halmashauri imesimamia mradi huu kwa zaidi ya miaka 40. Wakulima wa mpunga katika mradi huu wameongezeka kutoka wakulima 40 hadi 429 (196 wanaume, 233 awanaweke). Wakulima wamejipanga vizuri na wana chama cha kuweka na kukopa (SACCOS). Pia, wakulima wa mpunga wamejenga ofisi za SACCOS.



***Ofisi za SACCOS***

Mradi unamilikiwa na wakulima kwa kuwa wao hufanya shughuli zote za utunzaji, usafi na kugawa maji kwenye mashamba. Kwa hiari yao wakulima husafisha mifereji ya umwagiliaji kupitia ***msaragambo***. Vikundi ya wakulima hutumia ratiba kushiriki kazi za ***msaragambo*** na kugawa maji kwenye mashamba.




***Ratiba ya Kazi na Kazi za Msaragambo***

Wakulima wameshuhudia ongezeko la uzalishaji kwa hekta kutoka 2t/ha hadi 8t/ha na kutoka kuvuna mara moja hadi kuvua mara tatu kwa mwaka kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji. Ongezeko la mavuno limewawezesha wakulima kuchangia upanuzi wa mfereji mkubwa (287 meta).



***Mfereji mkubwa ulioboreshwa***

Maisha ya wakulima yameboreshwa: Mabadiliko makubwa ya kipato katika kaya na hali ya maisha ya wakulima wa mpunga yamewawezesha wakulima kujenga nyumba za kisasa, kwa kutumia matofali ya kuchoma na kuezekwa kwa bati. Miaka kumi iliyopita wakulima wa Mombo waliishi kwenye nyumba duni zilizoozekwa kwa nyasi.



***Nyumba za zamani***





***Nyumba za kisasa***

Ufyatuaji na uchomaji wa tofali ni fursa nyingine ya kuongeza kipato kwa vijana kwa kuwa soko lipo. Tofali zinapata soko la wakulima wa mpunga wenye fedha kwa kuwa hupenda kujenga nyumba za tofali za kuchoma. Pia, wakulima wanamiliki vyombo vya usafiri kama pikipiki, vyombo vya mawasiliano kama simu za mkononi, radio na runinga. Wakulima wa mpunga hutumia pikipiki kusafirisha pembejeo, mazao ya shambani, wagonjwa, na nyasi kwa ufugaji wa ndani.



***Mkulima akibeba nyasi kwa kutumia pikipiki***

Wakulima wa mpunga na jamii inayowazunguka wana uhakika wa chakula katika kaya kutokana na kuvuna mara tatu kwa mwaka. Wanawake wamewezeshwa kuwa na maeneo ya kulima mpunga, kushiriki kwa kuchangia mawazo katika chama cha ushirika, wameongeza kipato kwa kuwa kwa

ujumla wao wana eneo kubwa la kuzalisha mpunga zaidi ya wanaumme kama picha inayooonesha hapa chini.



***Wanawake waliowezeshwa wakishiriki kufanya maamuzi   na nyumba wanazomiliki***

Kuna ongezeko la wanafunzi wa sekodnari na kupungua kwa utoro kutokana na uwezo wa wazazi kulipa ada na gharama nyingine. Mkulima mmoja alikuwa na maoni haya.

> ***"….Kilimo cha umwagiliaji kimetupa fahari, kulikuwa na shida katika kijiji hiki, watoto wetu wasingeweza kwenda shuleni kwa kuwa hatukuwana na ada.Wavulana walienda mijini kutafuta kazi, tuliishi nyumba duni, lakini kwa sasa, angalia nyumba yangu nzuri, watoto wangu hawako hapa, wapo shuleni, mmoja yuko shule ya bweni Arusha. Nina uwezo wa kukopa ada kwa sababu nina magunia ya mpunga ndani, napata pesa kila siku…."***

Kuongezeka kwa mavuno ya mpunga kumeongeza wanachama wanaojiunga na mfuko wa afya ya jamii (community health fund- (CHF) kwa kuwa kuna pato la uhakika katika haya. Hii imefanya wakulima wawe na uhakika wa kupata huduma za afya na kuboresha hali ya maisha kwa ujumla.
Kilimo cha umwagiliaji Mombo kimegeuka na kuwa kituo cha mafunzo ya miradi mingine katika Halmashauri mfano, Chekelei walikuja hapa kujifunza. Wakulima pia walipokea wageni kutoka Halmashauri za Wilaya za Makete, Njombe, Arusha, Babati, Hai, Same, Mtwara na Lindi. Wageni wengine waliokuja kujifunza walitokea nchi za Uganda, Kenya na Sudan Kusini.



***Wageni Kutoka Uganda waliofika kwa  Ziara ya Mafunzo***

Kutokana na uongozi imara wa chama cha wakulima, wakulima wamewajengea imani wafadhili. wafadhili wameunga mkono mradi wa umwagiliaji wa Mombo kwa kununua mashine za kuvuna, kukoboa na ujenzi wa ghala kwa TZS 1 bilioni kama picha hapa chini zinaonesha.




*Mashine za Kuvunia Mpunga*



*Jengo la Kukobolea na kusaga nafaka*

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Halmashauri ya wilaya ya Korogwe inaweka nguvu zake zote kuboresha uzalishaji wa mpunga kama zao mbadala la biashara na kufanya mradi uwe endelevu kwa kutumia mikakati ifuatayo. Halmashauri inahakikisha kuwepo kwa uhusiano mzuri na Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ambayo ipo sehemu ya juu ya mto ili uwepo utumiaji endelevu wa maji ya mto Soni ambao ndio unaozalisha maji ya umwagiliaji katika mradi wa Mombo. Zipo harakati za kujenga bwawa kubwa kwenye mto soni kwa ajili ya wakulima wa Mombo na jirani zao (kama Kwemkumbo). Hadi sasa utafiti unaendelea, sehemu ya kujenga bwawa imepatikana na vipimo vya miinuko ya ardhi tayari vimefanyika. Zipo pia harakati za kuanzisha miradi mingine ya umwagiliaji ili kuongeza kipato cha wakulima miradi hivyo ni Kwemazandu, Makorora, Chekelei, Mafuleta, Madumu, Chepete, Mkomazi, Mswaha, Mandera, Magoma, Kerenge, Mapangoni, Madala, Kizara na Kwemkumbo. Utoaji wa udongo katika bwawa lililopo unaendelea. Halmashauri kupitia fedha za DADPs imeendelea kuwasaidia wakulima kwa kuwapa TZS 22,000,000.

Wakulima wanashauriwa kuendelea kutoa michango yao kwa lengo la kununua zana za kisasa za kilimo na kutunza miundo mbinu. Halmashauri inaendelea kutoa mafunzo kwa wakulima na jamii nzima ili kutunza maji na vyanzo vyake. Wakulima wanaendelea kupata ushauri ili washirikiane na wanaochakata mazao ya kilimo na wakala wa masoko ili kutengeneza mnyororo wa thamani kutokana na uzalishaji na uuzaji. Halmashauri inawaunganisha wakulima na taasisi za masoko na uchakataji. Pia, Halmashauri inawawezesha wakulima kutengeneza mtandao ndani na nje ya Halmashauri ili waweze kupanua uwigo wa mawazo juu ya namna ya kutafuata masoko na kutumia telenologia za kisasa ili kuongeza uzalishaji. Halmashauri imeendelea kuimarisha mifumo ya fedha ya Vijiji kama SACCOS ili kuwawezesha wakulima kupata mikopo yenye riba nafuu, kuuza mazao yao, na kuongeza uzalishaji.

## 8.0 SIRI ZA MAFANIKIO

Halmashauri ya Wilaya Korogwe ilifanikiwa kwa sababu zifuatazo. Siri ya mafanikio ya mradi wa umwagiliaji Mombo ilitokana na utayari wa wakulima kukubali kugawa upya ardhi, umwagiliaji na kutumia mbegu mpya za mpunga. Wakulima walishiriki kikamilifu hatua zote za kuzalisha mpunga. Uwepo wa chama cha wakulima imara kikitumia misingi ya utawala kama uwazi, kuamua kwa pamoja, kushirikisha wanawake, uthibiti na usimamizi wa fedha vyote hivi vimeongeza imani kwa wanachama na wafadhili .

Utumiaji wa mikakati ya serikali kuu na misaada kutoka DADPs, ASDP, na kituo cha utafiti vimesaidia sana wakulima kuanzisha kilimo cha umwagiliaji. Misaada hii ilitumiwa vizuri na Halmashauri kuanzisha mashamba darasa ya wakulima, kusambaza mbegu na kushawishi sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu za mpunga.

Uongozi imara wa Halmashauri kwa ushirikiano na Mkurugenzi Mtendaji walishiriki na kusimamia shughuli zote za maendeleo ya mradi. Mhandisi wa umwagiliaji aliahidi kuwasaidia wakulima kila wakati.

Zaidi ya yote, kauli mbiu ya wakulima wa mpunga ni "UMWAGILIAJI- KILIMO CHA UHAKIKA' KILIMO CHA UHAKIKA – UMWAGILIAJI" Kauli mbiu hii ilimaanisha kuwa umwagiliaji ndiyo njia ya uhakika ya kuleta kilimo cha uhakika; wakulima lazima wamwagilie mashamba yao. Kauli mbiu hii inatia hamasa na imetumika vizuri kuimarisha wakulima kuona kuwa kilimo cha umwagiliaji ndiyo mbinu bora ya kupata uhakika wa chakula na kuondoa umaskini.

# MKOA WA TANGA

## JITIHADA ZA WAKULIMA WADOGO KUZALISHA MAZIWA



*Uzoefu wa Jiji la Tanga Mjini Halmashauri za Wilaya za Mkinga na Pangani*

**1.0 UTANGULIZI**

Mkoa wa Tanga upo kaskazini Mashariki mwa Tanzania na upo pwani ya bahari ya Hindi. Mkoa unapakana na nchi ya Kenya na mkoa wa Kilimanajaro kwa upande wa Kaskazini, mkoa wa Manyara upande wa Magharibi, mkoa ya Morogoro na Pwani upande wa Kusini. Kwa upande wa Mashariki, mkoa unapakana na bahari ya Hindi. Kwa mujibu ya sensa ya 2012, mkoa una watu 2,045,2015 (URT, 2012), Mkoa una Halmashauri 11.

Uzalishaji maziwa wa wakulima wadogo mkoani Tanga unatokana na sera ya ufugaji ng'ombe wa maziwa ya 1983. Maendeleo ya uzalishaji wa maziwa mkoani Tanga yalianza katika ya miaka ya 1970 ambapo mkazo ulikuwa kwenye mashamba makubwa yaliyomilikiwa na Tanzania Sisal Authority (TSA) yaani Mamlaka ya Mkonge Tanzania na mashamba ya serikali ya ng'ombe wa maziwa. Kwa msaada wa serikali ya Uholanzi, programu ya kuongeza uzalishaji kutoka kwa wafugaji wadogo (Tanga smallholder dairy extension programu -SDEP) ilianza 1985 kwa kuwatumia wakulima saba. Idadi ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa iliongezeka hadi 900 mwaka 1992. Mikakati na mbinu za SDEP zililenga wakulima wa mijini na vijijini. Katika harakati hizi, Halmashauri tatu ndizo zimekuwa mfano wa kuigwa katika mchakato wa mnyororo wa kuongeza thamani. Halmashauri hizi ni za jiji la Tanga na Wilaya za Mkinga na Pangani. Mbinu bora hizi ni mifano mizuri juu ya wafungaji wa ng'ombe wa maziwa walivyoshirikiana na sekta binafsi kutengeneza mnyororo wa soko la maziwa na bidhaa za maziwa ya ng'ombe. Pia ni mifano inayoonesha kuwa uwezeshwaji wa kudumu hubadili fikra za watu ili hatimaye wakubali kutumia njia mbadala za kuboresha maisha yao.

Halmashauri ya Jiji la Tanga ipo kati ya Longitudo 38°53' na 39°10' Mashariki na Latitudo 5° na 5°10' kusini. Hupakana na Halmashauri za Wilaya za Muheza kwa upande wa Kusini na Magharibi, Mkinga upande wa Kaskazini, na bahari ya Hindi upande wa Mashariki. Mji una ukubwa wa 600km$^2$ za nchi kavu na Bahari ya Hindi 62km$^2$. Mji upo kati ya 0m-17m juu ya usawa wa bahari. Hali ya hewa ni joto kuanzia 24°-33°c. Kwa mujibu wa sensa ya 2012, mji una watu 273,332 (130,920 ni wanaumme na 142,412 ni wanawake) na ongezo la watu ni 1.2% kwa mwaka. Nguvu kazi ni 52% ya watu wote. Takribani 19.1% ya watu huishi katika viunga vya jiji na hujishughulisha na uvuvi, kilimo na ufugaji. Kata ya Pingoni ni maarufu kwa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa katika jiji wa Tanga. Kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, wafugaji wa ng'ombe wa maziwa wa Pingoni wamebadili kilimo cha mashamba ya katani kuwa mashamba ya ng'ombe wa maziwa.

Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ilianzishwa 1/7/2006 baada ya kumegwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Halmashauri ina Tarafa mbili, Kata 21,Vijiji 85, na Vitongoji 335. Inapakana na nchi ya Kenya kwa upande wa Kaskazini na Mashariki, Halmashauri za Jiji la Tanga, Korogwe Mji na Lushoto kwa upande wa Magharibi. Halmashauri ina ukubwa wa 2,948km$^2$ kwa ajili ya kilimo, malisho ya wanyama, na hifadhi ya wanayama ya Umba. Sensa ya mwaka 2012 inaonesha kuwa kuna watu 118,065 (57,76 ni wanaume na 60,305 wanawake) na ongezeko la watu ni wastani wa 1.27 kwa mwaka. Halmashauri ipo 1,600m juu ya usawa wa bahari na inapata kiasi cha mvua kati ya 500mm na 1,200mm kwa mwaka. Halmashauri ina ukanda wa pwani ambao unafaa kwa kilimo (katani, matunda, korosho, mihogo minazi, na kilimo cha maua). Kata ya Maramba ni maarufu kwa kuzalisha maziwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga. Wakulima wameanzisha uzalishaji wa maziwa baada ya kufanya kazi za vibarua kwenye mashamba makubwa ya mkonge.

Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ipo 47km kutoka Tanga mjini. Inapakana na bahari ya Hindi upande wa Mashariki, Halmashauri za Handeni upande wa Magharibi, Muheza upande wa Kaskazini na Bagamoyo upande wa Kusini. Halmashauri ina eneo la 1,830.8km$^2$. Halmashauri ina Kata 13, vijiji 33, na vitongoji 94. Sensa ya mwaka 2012 inaonesha kuwa Halmashauri ina watu 54,025 (26,870 ni

wanaumme na 27,155 ni wanawake) na kuna kaya 13,177. Historia inaonesha kuwa jamii ya watu wa Pangani ni wavuvi, wakulima wa minazi na hufanya biashara ndogondogo. Sehemu ndogo wakaazi hufuga kuku, mbuzi na ng'ombe wa kienyeji.

**2.0 TATIZO**

Baada ya kusitishwa kwa SDEP mwaka 1994 mradi wa kuzalisha maziwa wa wafugaji wadogo (Tanga small Holder Dairy Development Project (TSDDP) ulianzishwa mkoani Tanga kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani tu. Mradi ulihusisha wakulima wachache wenye mtaji wa kutosha kukidhi gharama za kufunga ng'ombe wa maziwa. Mradi ulikamilika mwaka 2004 na mafanikio yake hayakuwa mkubwa. Wakazi wa mkoa wa Tanga kwa kiasi kikubwa sana waliuza nguvu-kazi yao kwenye mashamba ya mkonge, uvuvi, na mashamba ya watu binafsi. Kutoweka kwa uzalishaji wa mkonge miaka ya 1980 kuliwaacha wakazi wengi bila ajira na walitumbukia katika dimbwi la umaskini.

Mikakati ya kufufua uchumi ya mwaka 1980 kama "structural adjustment program (SAPs) lisababisha kufa kwa viwanda vingi na mji wa Tanga ukawa na hali mbaya ya ukosefu wa ajira. Mwaka 2002 uzalishaji wa nazi ulishuka sana kutokana na ugonjwa, ukame, na mabadiliko ya hali ya hewa. Mabadiliko ya hali ya hewa pia yaliathiri uvuvi wa samaki. Soko la korosho nalo lilishuka sana. Haya yote yaliathiri uchumi wa kaya na uwezo wao kuhimili nguvu ya soko. Licha ya mkoa kuwa na ardhi ya kutosha kwa kilimo na malisho mazuri ya mifugo, wananchi hawakujua namna ya kufuga ng'ombe wa maziwa na walikuwa na mtazamo hasi juu kufuga ndani ng'ombe wa maziwa. Wakulima hawakuwa na umoja, soko halikuwa zuri kwa kuwa watu hawakuwa na uwezo wa kununua maziwa. Haya yote yalichangia kudhoofisha kipato na hali ya maisha. Matatizo yote haya yaliitaji mikakati ya haraka.

**3. MALENGO**

Uanzishwaji wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa katika mkoa Tanga ulilenga kuinua hali ya maisha kwa kuongeza pato la kaya. Malengo mahususi yalikuwa ni;

(i) Kubadili mtazamo wa watu juu ya uvuvi na kilimo cha mashamba madogo kuelekea ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.
(ii) Kutengeneza fursa za ajira kwa kuwekeza katika ufugaji wa ng'obme wa maziwa.
(iii) Kuongeza uzalishaji na ubora wa maziwa kutoka 2.5 lita/ng'ombe/siku hadi 8 lita/ng'ombe/siku.
(iv) Kuongeza mbolea ya samadi ili kusaidia shambani na kupata nishati ya biogas.
(v) Kuanzisha ufugaji wa ng'ombe bora wa maziwa.
(vi) Kuhamasisha kuongeza thamani katika bidhaa ya maziwa na kuanzisha mnyororo wa thamani.
(vii) Kuongeza pato la kaya na kiwango cha lishe.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kuanzishwa kwa kiwanda cha kuchakata na kuuza maziwa cha TANGA FRESH 1994. Kiwanda hiki kipo Tanga mjini na kilianza kazi 1996 ili kuongeza uzalishaji wa maziwa wa wafugaji wadogo na kuongeza kiwango kinachokidhi mahitaji ya maziwa na bidhaa zitokanayo na maziwa mjini Tanga na viunga vyake. Ongezeko la ufugaji wa ng'ombe wa maziwa mkoani, lilisababisha ziada ya maziwa ambayo ilibidi itafutiwe soko la kudumu. Tanga Fresh ni kiwanda kikubwa cha kuchakata maziwa Tanzania, kinamilikiwa na Tanzania Dairy Cooperative Union (TDCU) kwa kushirikiana na sekta binafsi. Zaidi ya

wakulima wadogo 6,000 wana uhakika wa kupeleka maziwa katika kiwanda hiki. Kiwanda kimetengeneza mfumo wa kuhifadhi maziwa kuanzia Tanga yanapozalishwa hadi soko la Dar es Salaam.

Kuhamasisha Jamii: Mwaka 1994 maafisa ugani wa Halmashauri kwa kushirikiana na serikali ya Uholanzi waliendesha mafunzo ya ufahamu na hamasa ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, faida zake, na kama chanzo mbadala lakini endelevu cha kipato kwa wavuvi wa samaki na wakulima wa minazi.



***Mkutano wa Uhamasishaji***

Mafiasa ushirika na maafisa ugani wa Halmashauri waliwawezesha wakulima kuunda vikundi na hatimaye kuunda chama cha msingi cha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa (a) "umoja wa vijana wafugaji Pingoni" (UVIWAPI) –SACCOS, (b) katika Halmashauri ya Mkinga wakulima walianzisha vikundi 15 ya kufuga ng'ombe wa maziwa kila kimoja kikiwa na watu 20.






***Bibi Chamwaga-Mkiti wa UVIWAPI SACCOS*** ***Ofisi ya MADAFCO***

Hii ilifuatiwa na kuanzishwa kwa mtandao wa (Mtandao wa vikundi vya wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa Maramba- MTAVIWAMA) Mwaka 1990 MTAVIWAMA ilianzisha ushirika wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa Maramba Division Dairy Farmers Coopearative Society (MADAFCO) kwa wakulima 455 na kilisajiliwa mwaka 1994. Wakati wa kuchapisha mbinu bora hii hii, wanachama wa MADAFCO walikuwa 3,000. Kupitia mafunzo ya wakulima kuhusu mtandao wa vikundi wakulima wa Halmashauri ya wilaya ya Pangani walianzisha mtandao wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa "*mtandao wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa*" (MWAPA) na "ushirika wa wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa" (WAWAPA) . WAWAPA kama chama cha ushirika ni kituo cha kukusanyia na kuuzia maziwa ya wakulima na ni kitovu

cha kuunganisha wadau wote wa maziwa. Pia WAWAPA hutoa huduma za ugani na mikopo ya masharti nafuu.

Kuundwa kwa Ushirika wa Mkoa wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa: kutokana na uwezeshaji maafisa na Halmashauri vyama vya msingi vilijiunga na kuunda ushirika wa mkoa (Tanga Dairy cooperative union (TDCU). Kazi kubwa ya TDCU ni kukusanya mazao ya maziwa na kuyatafutia soko. TDCU ina miliki hisa 42% za kiwanda cha maziwa "TANGA FRESH kilichopo Tanga mjini. TDCU inaundwa na MADAFCO (Mkinga) WAWAPA (Pangani) na UVIWAPI (Tanga). Aina hii ya ushirikiano wa serikali na sekta ya binafsi ni muhimu sana kulinda maslahi ya ubora na usalama wa walaji (Swinnen et al, 2007). Na kwa upande mwingine unamhakikishia mzalishaji wa maziwa soko la kudumu la maziwa na mnyororo wa thamani endelevu.

Kupata Ardhi: Halmashauri ya Jiji wa Tanga kwa kushikiana na Serikali ya Uholanzi ilinunua ardhi iliyokuwa shamba la mkonge (1,026ha) eneo la Pingoni na kuwagawia vijana wakulima 375 kila mmoja ekari 4. Lakini kila mkulima alilipa TZS 20,000 ili kupata ardhi. Kupitia utaratibu wa kuaminiana wa kupeana mitamba, kila mkulima alipata mtamba kama mtaji. Mpango wa kuhamilisha ng'ombe ulianzishwa na wakulima wanne walipata mafunzo Arusha National Artificial Insermination Centre (NAIC). Uhamilishaji wa ng'ombe ni njia mbadala ya kupata aina nzuri ya ng'ombe wazazi wa maziwa. Wakulima waliopata mafunzo kutoa huduma hii kwa wakulima wengine.




***Baada ya kupat mafunzo: Mr. Chiwangi*** ***Mkulima aliyepata mafunzo akitoa huduma***

Kujenga vituo vya kukusanya maziwa: MADAFCO ilijenga vituo hivi Maramba kwa kutumia fedha zake na TDCU ilitoa pipa la kuhifadhi maziwa 6,000lita katika Halmashauri ya Wilaya Mkinga. Vituo vinne vya kukusanyia maziwa vilijengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani; mapipa ya kupoozea yalitolewa na kiwanda cha maziwa cha Tanga Fresh. Kiwanda kilitoa mapipa ya kuhifadhi maziwa ya ukubwa wa 6,500 lita Pingoni. Kila ushirika hukusanya maziwa kama isipokuwa kama soko lipo basi vyama vya msingi huuza maziwa kwa walaji moja kwa moja. Kutokana na muundowa chama, TDCU huchukua maziwa yote ambayo ni ya ziada na kuyatafutia soko.





***Pikipiki ya kubebea maziwa*** ***kitua cha mziwa na pipa la kuhifadhia maziwa***

Halmashauri ya jiji la Tanga kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeboresha baadhi ya miundombinu ya uzalishaji wa maziwa na ubora wa maziwa. Mfano, kwa kushirikiana na shirika la Umoja wa Mataifa kitengo cha makazi ya watu duniani (UN-habitat) wafugaji wa ng'ombe wa maziwa 15 walipata TZS 2,300,000 kila mmoja ili kuboresha nyumba zao maeneo ya Pingoni. Pia ujenzi wa mitambo ya gesi kwenye makazi ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa kushirikiana na TPBP. Halmashauri kwa kutumia mfuko wa DADPS pia ilijenga mabwawa ya kunyweshea ng'ombe maeneo ya Pingoni.



***Bwawa la maji eneo la Pingoni***

Kuhamasisha ufugaji wa ng'ombe kupitia mkopo wa kupewa mtamba " kopa ng'ombe lipa ng'ombe" kwa kutumia mfuko wa DADPS ilinunua mitamba na kuisambaza kwa wakulima kupitia mpango maalum. Kila mkulima alipaswa kujenga zizi bora. Kati ya wakulima 10 katika kijiji, wakulima 2-5 walipewa mitamba ambao waliwatunza hadi walipopata mitamba mingine. Mtamba wa kwanza walimpa mwanachama mwingine katika kundi ili kufanya mtandao wote upate mitamba.



***Mitamba iliyotayari kupandishwa mjini Tanga na Pangani***

Halmashauri iliendesha mafunzo kwa wakulima ili kuboresha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ujasiriamali na uendeshaji wa ushirika. Mfano, Halmashauri ya Jiji la Tanga ilitoa mafunzo kwa wafugaji 514.

**5.0 RASILIMALI**

Wananchi hawakuwa na utamaduni wa kufuga ng'ombe hivyo ilichukua muda na gharama nyingi. Rasilimali zote zilifikia kiasi cha TZS 3,36,876,736. Mfano kupitia Halmashauri, Tarafa ya Maramba iligawa mitamba 681 na madume 23 kwa Vikundi ya wakulima. Halmashauri ya jiji la Tanga mjini iligawa mitamba 50 kwa wafugaji wa Pingoni na Halmashauri ya Pangani iligawa mitamba 549 kwa vikundi vya wakulima kama majedwali 1, 2 & 1 yanavyoonesha hapa chini.

### Jedwali 1: Fedha zilizotumika Kata ya Pingoni Jiji la Tanga

| Shughuli | Michango ya Wadau wa Maendeleo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wafadhili | Serikali kuu | Jiji | Wananchi | Jumla |
| Ununuzi wa ardhi na mitamba,uboreshwaji mioundo mbinu na ukarabati sitiri za maziwa | 327,900,000 | 36,000,000 | | 56,300,000 | 442,000,000 |
| ujenzi wa nyumba bora | 34,500,000 | | | 34,500,000 | 69,000,000 |
| ujenzi wa mifumo ya biogas | 45,000,000 | | | 22,800,000 | 67,000,000 |
| Ujenzi wa bwawa | 40,371,000 | | | 8,074,200 | |
| Kununu mitamba 50 | 26,000,000 | 54,306,000 | | | 80,306,000 |
| Kukarabati mdaraja mawili | 5,000,000 | 4,200,000 | 8,700,000 | 12,500,000 | |
| **Jumla** | **478,771,000** | **94,506,000** | **8,700,000** | **134,174,200** | **658,306,000** |

### Jedwali 2: Fedha Zilizotumika katika Tarafa ya Maramba Halmashauri ya Mkinga

| Mchango wa Mdau | Mwaka | Bei kwa kila bidhaa | Jumla |
|---|---|---|---|
| DADPs ilitoa mitamba 75 na madume 5 | 2008-2013 | Mitamba 900,000/= Madume 600,000 | 678,000,000/= |
| Mradi wa TASAF ulitoa mitamba 45 na madume 8 | 2010 -2012 | Mitamba 750,000/=Madume 500,000/= | 37,750,000/= |
| Mfuko wa ABBORT ulitoa mitamba 342 na madume 10 | 2011 -2015 | Mitamba 1,000,000/=Madume 700,000/= | 349,000,000/= |
| Tanga Fresh kupitia "Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa" walitoa mitamba 219 | 2002 -2013 | Mitamba 850,000/= | 186,150,000/= |
| Mcnago wa jamii ulikuwa ni kujenga mazizi ya ng'ombe 581 | 2008- 2015 | 500,000/= | 290,500,000/= |
| Mradi wa LAND "O" LAKES and DADPS walitoa seti 5 za vifaa vya kupandikiza mbegu ili kuboresha uzaliji wa maziwa kwa ng'ombe mmoja | 2013-2014 | 2,500,000/= | 12,500,000/= |
| LAND "O" LAKES kama wadau walitoa seti 70 za vyombo vya kukamulia na vikifaa vya kupimia maziwa | 2013 | 105,000/= | 7,350,000/= |
| LAND "O" LAKES walitoa pikipiki kwa shughuli za kupandikiza mbegu | 2014 | 8,750,000/= | 8,750,000/= |
| **Jumla** | | | **1,570,000,000/=** |

### Jedwali 3: Fedha Zilizotumika Halmashauri ya Pangani

| Shughuli /bidhaa | Fedha (TZS) | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|
| Ujenzi wa vituo 4 vya kukusanyia maziwa | 112,085,736/= | ASDP |
| Ununuzi wa ng'ombe wa maziwa 90 | 45,000,000/= | TADAT |
| Ununuzi wa ng'ombe wa maziwa 199 | 199,000,000/= | ASDP |
| Ujenzi wa kituo cha kata cha huduma za kupandikiza mbegu | 175,000,000/= | ASDP |
| Usimamiaji/uangalizi | 5,000,000/= | Halmashauri |
| Ununuzi wa ng'ombe wa maziwa 549 | 160,400,000/= | Farmers |
| Ununuzi mapipa 4 kwa ajili ya kuhifadhia maziwa | 137,360,000/= | Tanga fresh |
| ununuzi wa mashine za kufua umeme ( generators) 4 | 46,000,000/= | Tanga fresh |
| Uchangiaji wa ujenzi wa kituo 1 cha kukusanyia maziwa | 5,000,000/= | RC church |
| Ununuzi wa ng'ombe wa maziwa 20 | 16,000,000/= | Mfuko wa Jimbo (CDCF) |
| Ununuzi wa ng'ombe wa maziwa 240 kwa ajili ya mradi wa ***kopa ng'ombe lipa ng'ombe*** | 216,000,000/= | WAWAPA |
| Ununuzi wa madumu 75 ya kukamulia na ndoo 75 | 4,725,000/= | Land O Lakes |
| Ununuzi wa mapipa 4 ya Nitrogen kwa huduma za kupandikiza mbegu | 15,000,000/= | Land O Lakes |

| | | |
|---|---|---|
| **Jumla** | **1,136,570,736/=** | |

Maafisa wa ugani walitoa ushauri wa kitaalamu wa kilimo na ushirika wakati wote. Mfano, jumla ya maafisa ugani 15 waliajiriwaili kusaidia wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika Kata za Tarafa ya Maramba. Maafisa ugani waliwajibika kutoa mafunzo ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, uzalishaji wa maziwa, usafi wa mazingira, ukusanyaji na usafirishaji wa maziwa hadi sehemu ya kukusanyia. Maafisa maendeleo ya jamii (community development Officers –CDOs) walihusika kuhamasisha jamii kubadili mtazamo juu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Wataalam kutoka TANGA FRESH walitoa mafunzo kwa wakulima juu ya mambo ya kuzingatia katika vituo vya kukusanyia maziwa ili kuzingatia ubora wa maziwa; kuanzia hatua ya kukamua, kukusanya, kusafirisha hadi kiwandani ili kupata bidhaa bora kwa mlaji. Baada ya muda mrefu wa kuelimisha wafugaji waikubali wao wenyewe kuanzisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.



***Afisa ugani akitibu ng'ombe***

**6.0 MATOKEO**

Jitihada za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa katika Halmashauri ya jiji la Tanga zina matokeo mengi chanya. Wakazi wa Maramba, Pingoni, na Pangani wameanzisha ufugaji wa ng'ombe kama chanzo mbadala kuongeza kipato. Wanachi hawa hawategemei sana kilimo cha mazao na uvuvi kama chanzo cha mapato, ujasiriamali wa pwani umehamia katika  mnyororo wa thamani wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa kuaongeza njia za kujiongezea kipato ,kuboresha uzalishaji na kutafuta masoko ya ndani ya bidhaa za maziwa.



*Ufugaji wa ndani maendeo ya pwani*

Uboreshaji wa ufugaji wa ndani: Wafugaji wameunda vikundi vya uzalishaji na SACCOS zinazotoa mikopo midogo kwa ajili ya kununulia madawa ya mifugo, ada za shule, kupata nishati ya biogas, ufungaji wa vifaa vya nguvu za jua (solar panels) na masuala ya afya n.k. Mfano, Pangani kuna ushirika wa wafugaji imara (WAWAPA). Wanachama wameongezeka kotoka 64 mwaka 2005 hadi 400 mwaka 2013. Ushirika huu umedumu kutokana na uongozi imara. WAWAPA hutoa huduma za ugani kwa wafugaji mfano ulishaji bora na matumizi sahii ya madawa. Pia wazalishaji wameongezeka. Mfano, vikundi vya wafugaji yameongezeka Pangani kutoka 10 hadi 57 kwa miaka 10 hadi 2014.

Fursa za ajira: Idadi kubwa ya wakulima wanajihusisha na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa muda wote katika Kata ya Pingoni. Kuna fursa nyingine zaidi zilizotengenezwa katika Halmashauri za Mkinga na Pangani.

Kukubali ufugaji wa ng'ombe wa maziwa:  Wakulima wamekubali kufuga ng'ombe  wa kisasa wa maziwa, kujenga mazizi na majosho bora, kulisha nyasi kavu, kutoa chanjo na kutumia njia za uhamilishaji wa ng'ombe,  na wakulima wanne waliopata mafunzo wanaendelea kutoa  huduma katika Kata ya Pingoni, Tarafa ya Maramba na Halmashauri ya  pangani.

Ng'ombe  wa maziwa wameongezeka kutoka 375 mwaka 2000 hadi 814 mwaka  2014 na  kufanya uzalishaji wa maziwa uongezeke. Ongezeko la maziwa liko wazi katika Tarafa ya Maramba kutoka 3lita/ ng'ombe/siku mwaka 2007/ 08 hadi wastani wa 10 lita/ng'ombe/siku mwaka 2014/15. Katika Halmashauri ya Pangani uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka wastani wa 2.5 lita/ ng'ombe /siku hadi 8 lita/ ng'ombe/siku. Kwenye vituo vya Kata vya kukusanyia maziwa kuna ongezeko kutoka 700lita kwa siku mwaka 2001 hadi 2000lita kwa siku mwake 2014.



*Uboreshaji wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa*

Kuongeza vituo vya kukusanyia maziwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kutoka kituo kimoja 2005 hadi 5 mwaka 2013.




***Vituo vipya na vya zamani vya kukusanya maziwa Pangani***

Kuongezeka kwa bei ya maziwa: Wakulima wamepata bei nzuri mfano, lita moja huuzwa TZS 680 kwenye kituo cha kukusanya maziwa. Wakulima hulipwa mara mbili kwa mwezi (Tarehe 15 na 30). Kwa bei ya rejareja bei ni TZS 100/ 1lita na kipato kimeongezeka hadi wastani wa TZS 312,000 kwa mwezi. Hii imekuwa ni ajira ya uhakika ya wakulima na shughuli za uzalishaji. TDCU husaidia kutafuta bei nzuri: Hii imeongeza pato la kaya mfano katika Kata ya Pingoni pato la kaya limeongezeka kutoka TZS 30,000/ kwa mwezi mwaka 2001 hadi TZS 350,000 kwa mwezi mwaka 2014. Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga pato limepanda kutoka TZS 240,000 mwaka 2011/2012 hadi TZS 753,794 mwaka2013/14.

Gawio la hisa za kiwanda cha maziwa Tanga Fresh limeongeza pato la kaya: Mfano MADAFCO ilipokea gawio la mwaka kati ya TZS 9 milioni 2010 hadi TZS 14 miloni 2014 na kuzigawa kwa wanachama sawa na maziwa waliyouza kiwandani. Hii imewajengea uwezo wafugaji kuchangia miradi ya jamii. Wanachama pia wana uwezo wa kumudu huduma za afya, elimu na maji. Kiwango cha hali ya maisha kimeboreshwa pia kwa kuwa wananchi wamejenga nyumba bora, wana uwezo wa kulipia huduma za elimu, afya na usafiri. Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ilikuwa nyuma sana lakini kwa sasa kiwango cha maisha ya wafugaji kimekuwa kimeimarika kwa kujenga nyumba bora, kununua pikipiki, kuweka umeme wa nguvu wa jua majumbani, kulipa ada za shule n.k



***Nyumba ziliboreshwa***



***Pikipiki***



***Nishati mbadala (Biogas)***



***Umeme wa nguv za jua***

Kuongezeka kwa unywaji wa maziwa: Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa umeongeza uhakika wa chakula na lishe. Kupitia ufugaji wa ng'ombe wa maziwa unywaji wa maziwa kwa mtu mmoja katika kaya umeongezeka na kuboresha kiwango cha lishe. Mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, utapia mlo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano umepungua kutoka 1.8% mwaka 2009 hadi 0.1% mwaka 2013. Hii ni kwa sababu kiasi fulani ni lazima kibakie nyumbani bila kuuzwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Vilevile, kipato kinachopatikana kutokana na mauzo ya maziwa hutumika kununulia vyakula vya kuongezea protini kama samaki na nyama.




***Duka la bidhaa za maziwa***

Kuanzisha uzalishaji wa nishati ya biogas kumewapatia uwezo wanawake kutumia nishati ya biogas majumbani umeongezeka maeneo ya Maramba, Pingoni na Pangani. Wanawake wamewezeshwa na wanathamini sana nishati ya biogas. Katika Halmashauri ya Wilaya Pangani kuna wafugaji saba walioweka mitambo ya kufua gesi kwa msaada wa CARMATEC na SIMGAS.



***Mitambo ya Biogas***



***Jiko linalotumia biogas***

Kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri: Kwa mfano, Halmashauri ya Jiji la Tanga inapata TZS 3.4milioni kwa kila mwezii kutoka kiwanda cha maziwa (Tanga Fresh). Hii imesaidia Halmashauri kuboresha huduma kwa kukarabati miundo mbinu, kununua madawa, ujenzi wa soko, madarasa na zahanati. Pia asilimia 10% ya mapato hutumika kama mikopo kwa wanawake na vijana.

Kiwanda cha maziwa (Tanga Fresh) ni soko la uhakika. Kila siku kiwanda hukusanya kiwango cha maziwa kinachozalishwa na kutafutiwa soko na kiwanda cha maziwa (Tanga fresh). Utaratibu huu umeondoa hofu kwa wafugaji wanaozalisha maziwa kwani mazao yao yana soko la kudumu.

Umiliki wa ng’ombe wa maziwa ni dhamana ya mkopo: Ufugaji wa ng’ombe wa maziwa ni dhamana tosha kwa mfugaji kupata mkopo kutoka taasisi za fedha. Mikopo husaidia kuboresha maisha kwa kupata lishe bora, malazi bora na vyombo vya usafiri kama pikipiki.



***Faida za mikopo kwa wafugaji***

Jitihada za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa zimesambaa hadi Kata nyingine. Mfano mafanikio ya Kata ya Maramba yamekuwa kivutio na chachu kwa wananchi wa Mapatano, Dakeni na Duga. Halmashauri zao zimeanzisha miradi kama hii katika Kata zao. Kata ya Palungu imepokea mitamba 15, Kata ya Mayomboni mitamba 10 na Kata ya Duga mitamba 25. Pia Ushirika umeanzisha kituo cha kukusanya maziwa. Matokeo haya yamesababisha vijana kubaki kijijini. Vijana wengi zaidi wamezidi kujishughulisha na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa badala ya kutokomea mijini. Miongoni mwao wameanza kununua ng'ombe kupitia mikopo badala ya kusuburia utaratibu wa kupewa mitamba.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Jitihada hizi zina changamoto kubwa ambazo ni; uhitaji wa mitamba kuwa juu zaidi ya upatikanaji wake, upungufu wa maeneo ya kuchunga ng'ombe, upungufu wa madume bora, magonjwa ya wanyama, uhaba wa huduma za mahabara ya wanyama, uelewa duni juu ya uhamilishaji wa ng'ombe kwa wafugaji wapya, na bei za maziwa kuwa chini. Pamoja na changamoto hizi, Halmashauri kwa kushirikiana na TDCU na wafugaji zimeweke mikakati ifuatayo:

Kuboresha vyama vya wafugaji. Ili kudumisha juhudi hizifisi ya mkoa ya maendeleo ya mifugo ilifanya kazi kubwa ya kuunda vyama vya msingi cha wakulima na TDCU. Hata hivyo jitihada za kuimarisha usamimizi wa vyama vya wafugaji zinaendelea ili viimarike.

Halmashauri, TDCU na vyama vya msingi vya wakulima vinaendelea kuimarisha huduma za kilimo na ufugaji kwa kuajiri maafisa ugani. Kibali tayari kimeombwa Ofisi ya Rais - Utumishi ili kuajiri maafisa mifugo. Pia kuna mafunzo endelevu kwa bwana mifugo wasaidizi (paravets - mhudumu wa afya za wanyama kwa kila kundi) kwa huduma za kwanza kwa mifugo, uhamilishaji ng'ombe, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na ujuzi wa kuongeza thamani ya maziwa. Maafisa ugani wamepewa pikipiki kuwawezesha kuwafikia wafugaji kwa urahisi, hususan kwa huduma za uhamilishaji wa ng'ombe. Kazi za ugani ni za muda wote hivyo huhitaji kujitoa zaidi. Hivyo kutumia mbinu za kuongeza motisha ni muhimu sana. Mfano kutoa vifaa vya kujikinga na ajali, kupandisha vyeo inapostahili na kuwepo kwa usafiri wa uhakika.

Kujenga vituo vya kilimo: Haya ni maeneo muhimu kwa kuwapatia wakulima mbinu za kisasa. Pia vituo hutumika kudhibiti ubora wa maziwa kwa kufuata misingi ya usafi, kupima ubora wa maziwa, kuwafundisha wafugaji ubora wa maziwa, kuchakata maziwa, na kutengeneza vyakula vya wanyama kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Matangazo na mtandao kwa niaba ya wafugaji: TDCU itaendelea kushawishi kiwanda cha maziwa cha Tanga Fresh kuongeza bei ya maziwa ili kukidhi gharama za uzalishaji na kupata faida. TDCU itaendelea kujadiliana na Halmashauri, Mamlaka ya Mkonge na kituo cha jeshi ili kuwapatia wafugaji eneo zaidi la

kufugia ng'ombe wa maziwa. Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa wataendeleza ushirikiano uliopo unaohusisha maafisa ugani, wafugaji, wafadhili na kiwanda cha Tanga Fresh.

Kutunza na kukarabati miundo mbinu (barabara za vijijini na mabwawa) ili kurahisisha usafirishaji wa maziwa kwenda kiwandani na kupata maji. Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa watajenga tangi la maji la chini na sehemu ya kupulizia wanyama ili kuzuia wadudu na magonjwa.



***Daraja linalotunzwa na wafugaji Jijini Tanga***

Mpango wa kukopeshwa mitamba, vyama vya msingi vya wakulima, na mtandao wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa utaendelea kuimarisha mpango wa kukopeshana mitamba (pata mtamba lipa mtamba) au "kopa mtamba lipa maziwa".

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Ubunifu ulisaidia kubadili mtazamo wa wavuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, vibarua wa mashamba ya mkonge, na walioachishwa kazi katika Halmashauri ya jiji la Tanga , na wakulima wa minazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kuwa wajasiriamali. Hili zoezi lilichukua mchakato mrefu uliohitaji uvumulivu na uangalizi wa karibu sana kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1990 na matokeo halisi yalionekana mwaka 2015. Siri za mafanikio ni kama inavyoelezwa hapa chini.

Kuendeleza ufahamu na utayari wa mfugaji: Mafanikio yalitegemea nguvu ya maafisa ugani kuwabadili wafugaji kushiriki shughuli za ujasiriamali. Baadhi iliwachukua muda mrefu kubadilika na walibadili mtazamo wao kwa kuangalia mafanikio ya wafugaji wa mwanzo. Taratibu wakulima walipata utayari na ujasiri wa kufanya shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Uwezeshwaji kwa vitendo: Maafisa mifugo, maafisa maendeleo ya jamii na maafisa ushirika kwa pamoja walifanya uwezeshwaji makini wa wakulima juu ya ufahamu, mipango na utekelezaji wa shughuli zote za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Mfano, afisa ugani wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani alifuga ng'ombe wawili wa maziwa nyumbani kwake kama shamba darasa kwa jamii nzima. Jamii iliona kila kitu na faida zake. Pia hii ilibadili mtazamo wa wananchi na kuona kuwa nao wanaweza kupata faida za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Watu wazima hujifunza vizuri kwa kuona vitendo halisi.

Uwezo mkubwa wa vyama vya wafugaji: Uendeshaji wa vyama vya wafugaji na kuzingatia misingi ya ushirika kama demokrasia na uwazi katika kufanya maamuzi katika vyama vya MADAFCO, WAWAPA, MVIWAPA na TDCU ili kukidhi mahitaji ya wanachama. Vyama vya misingi vya wakulima vinatoa vyakula vya wanyama, madawa, vinakusanya na kuhifadhi maziwa kupitia SACCOS, na vyama vya wakulima

vimewezesha wanachama kupata mikopo. Haya yote huwavutia wakulima kuingia katika ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.


Kutumia wadau tofauti: Mafanikio yanajumuisha ushirikiano wa wadau kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya juu kabisa (wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, maafisa ugani, vyama vya msingi, TDCU, UN-Habitat, na Tanga Fresh Ltd). Mfano Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa ushirikiano na Serikali ya Uholanzi, ofisi ya mkuu wa mkoa, TDCU, kiwanda cha maziwa (Tanga fresh ltd) na Umoja wa Mataifa - Makazi waliwezesha vikundi vya vijana kwa kuwapa maeneo ya kufugia, kukopeshwa mitamba kupitia mpango maalumu na kuboresha miundo mbinu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Soko la uhakika: Kiwanda cha maziwa (Tanga Fresh Ltd) ni soko la uhakika la maziwa ya wafugaji na malipo yanafanyika kwa awamu kila mwezi. Umiliki wa kiwanda cha maziwa kwa 42% na TDCU unawezesha kuhakiki faida.

Mtandao wa kitaasisi: Mafanikio yametokana na mahusiano mazuri na mtandao kati ya wafugaji, TDCU, Tanga fresh Ltd, NAIC, wadau wa maendeleo na Halmashauri. Kupitia njia hii wadau mbalimbali kama Serikali ya Uholanzi walianzisha mpango wa "Kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Kupitia mtandao wafugaji wamepata utalaamu wa kuboresha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

**MPANGILIO BORA WA WADAU KATIKA MNYORORO WA THAMANI YA MAZIWA**




***Modeli ya Utatu ya Kata ya Songoro - Halmashauri ya Wilaya ya Meru***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Meru ni miongoni mwa Halmashauri saba za mkoa wa Arusha na inaundwa na Tarafa 3, Kata 16, Vijiji 71, Mitaa 4 na Mamlaka ya Mji mdogo wa Usa-River. Halmashauri ina eneo la 1,268$km^2$. Kwa mujibu wa sensa ya 2012, Halmashauri ina watu 268,144. Kijiografia Halmashauri ina maeneo matatu ambayo ni nyanda za juu na kati zinazofaa kwa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwani zina hali ya hewa na uoto mzuri. Pia kuna ukanda wa chini.

Kabla ya 1980 kilimo cha kahawa kilishamiri sana. Baada ya kuporomoka kwa soko la kahawa kilimo cha maua kilianza kuwa chanzo kikubwa cha mapato, lakini wakulima wadogo walianzisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kama chanzo mbadala cha mapato. Kwa kawaida wakazi wa Meru hufanya kilimo mseto kwa kutumia mbolea inayozalishwa hapo nyumbani kwa ajili ya mazao ya shabani na kilimo cha maua na mabaki ya mimea na nyasi hutumika kama chakula cha wanyama. Wakazi wa Meru ni mahiri kwa mfumo wa ufugaji wa ndani. Halmashauri ya Wilaya ya Meru ni mashuhuri kwa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini. Kuna ng'ombe wa maziwa 83,000 na huzalisha lita 2.7 milioni kwa mwaka. Pia kuna hali nzuri ya hewa, kituo cha taifa cha uhamilishaji ng'ombe cha National Artificial Insemination Centre (NAIC) kipo wilayani Meru ambacho hutoa huduma nafuu sana.

## 2.0 TATIZO

Kabla ya mwaka 1989, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa Kata ya Songoro katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru ulikuwa na matatizo yafuatayo. Mbali na kuboresha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, uzalishaji wa maziwa uliongezeka zaidi ya soko la eneo hilo. Kukosekana kwa soko la uhakika, kuliwalazimu wafugaji kupeleka maziwa hadi Usa-River na Arusha zaidi ya 25km kutafuta soko. Wachuuzi wa maziwa waliwapatia wafugaji bei ya chini (kama shs 180/lita) na wakati mwingine wafugaji hawakulipwa fedha taslimu na kupelekea kioato kisichkuwa na uhakika. Kulikuwa na upotevu mkubwa wa maziwa kutokana na ukosefu wa vifaa vya kupoozea katika Kata (hasa kwa maziwa yaliyokamuliwa nyakati za jioni). Ubovu wa miundombinu hasa barabara za vijiji ulikwamisha usafirishaji wa vyakula vya wanyama na maziwa. Wafugaji hawakuwa wamejipanga katika mfumo ambao ungeleta uhakika wa mnyororo wa thamani ya maziwa wenye faida. Hii ilitokana na kushindwa kwa ushirika wa zamani wa Meru kutetea maslahi ya wafugaji.

## 3.0 MALENGO

Lengo la Halmashauri lilikuwa ni kutengeneza mnyororo thabiti wa thamani ya maziwa na kuongeza pato la wafugaji wa Kata ya Songoro. Malengo mahususi yalikuwa ni:

(i) Kuwawezesha wafugaji kuunda ushirika wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa

(ii) Kuongeza uzalishaji wa maziwa kupitia kuboresha ng'ombe kwa kutumia njia ya uhamilishaji

(iii) Kuchakata maziwa ili kuongeza thamani kwa kupata bidhaaa zaidi kama siagi, samli, jibini, mtindi n.k

(iv) Kupata uhakika wa soko la maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa

(v) Kuboresha miundo mbinu kwa ajili ya ukusanyaji, kupooza na urahisi wa kusafirisha maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa kwenda kwa wateja

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Kuanzisha chama cha Meru cha wafugaji wa ng’ombe wa maziwa mwaka 1998: Ushirika wa Wafugaji wa Ng’ome wa Meru (Meru Dairy Farmers Association - MEDAFA) ulianzishwa kwa usajili RG namba 9570. Lengo la Ushirika lilikuwa ni kuwaunganisha wafugaji wa ng’ombe wa maziwa na kulinda maslahi yao katika mnyororo wa thamani. Vyama vya Ushirika ni muhimu kwa kuwa huwawezesha wazalishaji wa maziwa kupata faida zote za uzalishaji ili waweze kupunguza umaskini baada ya kuwezeshwa kiuchumi. Shughuli za vyama vya wazailishaji wa Maziwa ni kutafuta soko la maziwa, kukusanya maziwa, kuchakata maziwa, kuwezesha wafugaji kupata huduma (mfano afya, mbegu bora, fedha), kusimamia kupata vyakula vya mifugo na mikopo. Vyama vya wafugaji ni ufunguo wa mafanikio kwa wafugaji wadogo wa ng’ombe wa maziwa kwa kuwa vinaleta manufaa kama kuboresha upatikanaji wa soko la mjini, kukabili kwa pamoja ajali za kibiashara, na kutumia rasilimali zilizopo, uboreshaji wa mawasiliano na elimu.

Kununua eneo la kituo cha kukusanyia maziwa: Kupitia ushirika, wafugaji walinunua eneo na kujenga kituo cha kukusanyia maziwa. Ujenzi ulifadhiliwa na USAID kupitia LAND O’LAKES.




***Kituo cha kusanyia maziwa  cha MEDAFA***

Pipa la kuhifadhia maziwa: Kukosekana kwa miundombinu ya kuhifadhia maziwa ni kikwazo kwa kuanzisha na kupanua shughuli za ufugaji wa ng’ombe wa maziwa. Ushirika ulileta pipa la kupoozea maziwa lenye ukubwa wa lita 1,200. Ununuzi wa pipa la kupoozea maziwa lilifadhiliwa na LAND O’LAKES. Huduma za kuhifadha maziwa ni ghali sana kwa wazalisha wadogo wa maziwa. Katika nchi zinazoendelea kwenye eneo lenye wafugaji wengi wadogo wa ng’ombe wa maziwa, vituo vya kukusanyia maziwa ni jibu la vyama vya wafugaji wadogo katika kuhifadhi na kudhibiti ubora wa maziwa.

Mafunzo kwa maafisa ugani: Halmashauri kwa kushirikiana na MEDAFA iliandaa utaratibu wa mafunzo yauhamilishaji kwenye kituo cha Uhamilishaji cha taifa. Uhamilishaji ni njia nzuri ya kuongeza ubora wa ng’ombe ili kuboresha uzalishaji na kuongeza faida ya biashara za ufugaji wa ng’ombe wa maziwa. Halmashauri ina kikundi cha wataaamu cha uhamilishaji wa ng’ombe kwa njia za kisasa ambao wanaweza kutambua wanyama wanapokuwa kwenye joto na kufanya uhamilishaji. Wahudumu wote wamepatiwa vifaa kwa ajili ya kazi hii. Faida za kuhamilisha ng’ombe ni kupata mifugo bora zaidi, kuongeza sifa za uzalishaji za ng’ombe na kupunguza idadi ya madume wanaohitajika.

Kununua pikipiki kwa ajili ya shughuli ya uhamilishaji: Halmashauri kwa kushirikiana na MEDAFA imenunua pikipiki mbili kwa ajili ya maafisa ugani wa uhamilishaji wa ng’ombe.



***Afisa mifugo kwenye pikipiki akiwa na zana za uhamilishaji***

Ziara za mafunzo: Halmashauri kwa kushirikiana na MEDAFA iliandaa ziara za mafunzo za wafugaji kwenda kituo cha taifa cha uhamilishaji wa ng'ombe, mkoani wa Tanga, Kenya (KCC), Tengeru-LITI na kikundi cha wanawake Nronga mkoani wa Kilimanjaro. Kupitia ziara hizi wakulima walipanua fikra na ujuzi juu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Kuboresha barabara vijijini na kununua trekta la mkono (Power tiller). Halmashauri ilishirikiana na MEDAFA kuboresha barabara zenye urefu 3km na kutengeneza mkokoteni wa kubebea maziwa. Nyenzo kuu za kusafirisha maziwa na chakula cha mifugo ni pikipiki na trekta la mkono (power tiller). Ununuzi wa trekta ulifadhiliwa kwa ushirikiano wa MEDAFA na Halmashauri. Hii iliimarisha usafirishaji kwa kiwango kikubwa cha maziwa kutoka vituo sitiri hadi sehemu yakuchakata maziwa.






***Barabara zilizoboreshwa*** ***Trekta la mkono***

Kujenga vituo sitiri vya maziwa na ununuzi wa mashine ya kufua umeme: Kwa kushirikiana na MEDAFA Halmashauri ilijenga vituo sitiri viwili vya kukusanya maziwa. Pia kwa msaada wa DADPs Halalmshauri ilinunua mashine ya kufua umeme ili kusaidia pindi umeme wa Tanesco unapokatika.

Kushiriki katika maonesho ya kitaifa na kimataifa: Kila mwaka Halmashauri huwasaidia wakulima kushiriki maonesho ya "Nanenane". Kupitia maonesho haya wakulima hutangaza bidhaa za maziwa. Wazalishaji wadogo wa maziwa na wanashirikiana na MEDAFA. Ushirikiano huu umehamasisha uzalishaji wa maziwa katika eneo hili. Wachakataji wawili wa maziwa hupata msaada wa kiufundi na pesa kutoka kwa CARMATEC iliyokuwa ikisaidia upatikanaji wa nishaji ya biogas huko nyuma. Mchakataji mmoja, "The Mountain Green" aliandaa andiko la mradi wa kujenga kituo cha kuchakata maziwa. Aliliwakilisha na kulitetea vizuri katika kikao kijulikanacho kama "The Great Horn of Africa Round Table Initiative" mwaka 1989 kilichodhaminiwa na mpango wa "*kuondoa baa la njaa kupitia mchakato wa mnyororo wa thamani ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa*". Baadaye mradi huu ulifadhiliwa na USAID kwa kuanzisha

kituo cha uchakataji wa maziwa. Kwa hatua hii, ilionekana ni muhimu kuwa na ushirikiano wa wafugaji kupitia MEDAFA na sekta binafsi ya uchakataji maziwa (Public Private Partnership-PPP)

Mbinu bora hizi zimetumia ushirikiano miongoni mwao (mfumo wa utatu) ambao una pande tatu (wafugaji, MEDAFA na wachakataji) kama mchoro unavyoonesha hapa chini. Kila mdau kati ya hawa watatu anafanya kazi muhimu katika mnyororo wa thamani ya maziwa.




Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa ni wanachama wa MEDAFA. Kazi ya wafugaji ni kuzalisha maziwa bora kwa kuzingatia ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa na wanawajibika kuuza maziwa angalau 80% kwa MEDAFA. Wakulima wanawajibika pia kununua bidhaa na huduma kutoka MEDAFA na wachakataji (bidhaa zitokanazo na maziwa). Jukumu la MEDAFA kama chama cha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa ni kuratibu uzalishaji wa maziwa. MADEFA inawajibika kusafirisha kiasi kikubwa cha maziwa hadi kwa wachakataji, kupatana na kudhibiti bei, kulinda wakulima na kuunganisha wafugaji na wachakata maziwa. Wachakata maziwa wanawajibika kuzalisha bidhaa inayokidhi mahitaji ya soko, kufanya utafiti na kuuza bidhaa zitokanayo na maziwa. Wachakataji wana wajibu pia wa kuhakikisha wafugaji wanapata vyakula vya mifugo, madawa na vifaa vya gesi kwa utaratibu wa mkopo. Mkulima hulipia vitu vyote hivi kwa kuuza maziwa. Katika mfumo huu, MEDAFA ni mdhamini na anahakikisha malipo yote yanafanyika kupitia MEDAFA. Mfumo huu wa kipekee baina ya wadau unahakikisha unasimamia mnyororo wa thamani ambapo kila mdau anawajibika na unatoa fursa ya kukua kwa kutegemeana.

## 5.0 RASILIMALI

Zifuatazo ni rasilimali fedha zilizotumika katika kufikia malengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Meru na MADEFA.

**Jedwali 1: Fedha Zilizotumika Kata ya Songoro**

| Shughuli | Kiasi (TZS) | Chanzo |
|---|---|---|
| Ununuzi wa eneo la kituo cha kusitiri maziwa | 4,500,000 | MEDAFA |
| Ununuzi wa vifaa vya kituo cha kusitiri maziwa na kituo chakuchakata maziwa | 25,000,000 | Land O'Lakes |
| Mafunzo, ziara, maonesho, pikipiki, trekta la mkono, na ujenzi wa barabara | 59,000,000 | DADPs |

Pia shughuli zilihusisha rasilimali watu kama maafisa ugani wa Kata na Vijiji na madaktari binafsi wa mifugo.

**6.0 MATOKEO**

Kwa takwimu za ukusanyaji wa maziwa wa MEDAFA, wastani wa uzalishaji maziwa umeongezeka kutoka 100lita hadi 1200lita kwa siku. Wastani wa uzalishaji kwa ng'ombe ni lita 5 kwa siku na kuna ongezeko la bei ya maziwa kutoka TZS 180 hadi 810 kwa lita kwenye vituo vya MEDAFA. Kuna kituo kimoja na vituo sitiri viwili vya kukusanyia maziwa vilivyojengwa kwenye maeneo yanayomilikiwayo na MEDAFA. Kuna vifaa vya kukusanyia na kutunzia maziwa kama mapipa ya kupoozea, trekta la mkono, na vifaa vya kupimia ubora wa maziwa. Barabara zimeboreshwa na zinapitika majira yote ya mwaka. Wafugaji wengi wanatumia nishati ya biogas.

Kituo cha kuchakata maziwa cha Mountain Green ni soko la uhakika kwa wazalishaji wa maziwa. Kiwanda hiki huzalisha bidhaa kama samli, siagi, na mtindi ambavyo huviuza Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Arusha mjini, na kwingineko.




***Bidhaa za maziwa zinazozalishwa na Mount Green***

Kuna Ushirika imara wa wafugaji (MEDAFA) unaolinda maslahi ya wakulima na kuwaunganisha na wachakataji wa maziwa. MEDAFA pia inadhamini wanachama kupata mikopo midogo kwa ajili ya ng'ombe wa maziwa. Kwa sasa wafugaji wanaamua bei sio kuamuliwa bei kama zamani. Hakuna hofu kwa wafugaji kwa kuwa MEDAFA na wachakata maziwa huwalinda dhidi ya mabadiliko ya bei za bidhaa za maziwa sokoni.

Pato la wafugaji limeongezeka kutoka TZS 120,000 kwa mwezi kwa ng'ombe mmoja hadi kadirio la chini la TZS 260,000 kwa mwezi kwa ng'ombe wawili. Hii imesaidia kuboresha hali ya maisha kwa kujenga nyumba bora, kununua nishaji, kumiliki vyombo vya usafiri kama pikipiki n.k.



***Nyumba ya kisasa na chombo cha usafiri***

Kuna ajira ya wazi na isiyo kuwa wazi kutokana na uzalishaji, kukusanya na kuchakata maziwa. Kwa mfano MEDAFA huwahudumia wanachama 42 na wasio wanachama 150 lakini wafugaji wa ng'ombe wa maziwa wametengeneza fursa za ajira kama kuangalia ng'ombe wa maziwa, kukusanya maziwa kwenye vituo, kusafirisha maziwa, kuchakata maziwa, wakata wa nyasi na wasafirishaji.



***Wabeba chakula cha mifugo***

Biashara ya mitamba: Wapo vijana ambao hununua mitamba ya ziada kutoka kwa wafugaji na kuuza kwa faida. Mtamba uliotayari kupandishwa huuzwa kati ya TZS 1.2milioni hadi TZS 1.5 (kwa bei za 2015).

Mwisho, mahusiano ya UTATU wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, MADEFA, na wachakata maziwa umezaa huduma za uhakika, motisha kwa wakulima na ushindani wa mnyororo wa thamani ya maziwa. Mahusiano haya ni faida kwa kuwa yameleta uwezo wa kusimamia, ufundi, kuuza bidhaa, usalama wa fedha, na kununua vitendea kazi.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Kwa kushirikiana na MEDAFA Halmashauri inaendelea kuwafahamisha wafugaji faida za vyama vya wakulima na kuboresha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Huduma za ugani zinaimarishwA, barabara za vijijini na barabara kuu zinaendelea kuboreshwa. Jitihada zaidi zinaelekezwa katika kupata soko la maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa na kuhamasisha unywaji wa maziwa shuleni.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa: Wakazi wa Meru wana utamaduni wa kuthamini ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Pia wana utamaduni wa kusaidia kaya maskini kwa kuwapa ng'ombe kwa masharti ya kuwatunza, kupata maziwa na samadi kwa ajili ya shamba. Kupitia utaratibu huu, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na uzalishaji wa maziwa umeongezeka. Hatimaye familia maskini zinaweza kununua ng'ombe kutokana na uuzaji wa maziwa na hupunguza hali ya umaskini katika Halmashauri.

Ushirikiano wa UTATU: Ushirikiano wa taasisi tatu katika Kata ya Songoro umeimarisha ufanisi wa utoaji huduma kati ya pande tatu kwa maeneo maalum. Mahusiano haya yameunganisha ngazi zote za mnyororo wa thamani ambapo wazalishaji hujulishwa mahitaji/vigezo vya soko, uhakika wa zana na uhamilishaji. Pia wakulima huwekewa kinga dhidi ya kuporomoka kwa bei ya bidhaa zao. Wachakataji wa maziwa wana uhakika wa kupata kiasi cha kukidhi soka la bidhaa wanazozalisha. MEDAFA kama chama cha ushirika kinaaminika kwa wachakataji wa maziwa, wakulima na wadau wengine.

Uaminifu kwa Ushirika wa wakulima: Wanachama ni waaminifu na wanajitoa kwa ajili ya chama chao. Mahusiano ya UTATU; wakulima, MEDAFA, na wachakataji yamejenga imani ya dhati kati yao. Kwa kuwa wakulima na wachakataji ni wanachama wa MEDAFA, hali hii imetengeneza mfumo wa kusimamia na kudhibiti shughuli zote.

Siri nyingine ya mafanikio ni kuwepo kwa wadau wanaosaidia Halmashauri kama NAIC, USAID, Land O'lakes, Chuo cha Mfunzo na Utafiti (Research and Training Institutes), CARMETEC n.k, kwa kutoa misaada ya kiufundi na fedha. Pia kuna wataalam wa Halmashauri wanaosimamia shughuli zote kwa karibu sana.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

**MNYORORO WA THAMANI YA MAZIWA KATIKA JAMII**






***Uzoefu wa Kikundi cha Wanawake wa Nronga***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Hai ni moja katia ya Halmashauri saba za mkoa wa Kilimanjaro. Halmashauri inapakana na Mkoa wa Arusha upande wa Kusini, Halmashauri ya Siha upande wa Mgharibi, Nchi ya Kenya upandewa wa Kaskazini na Halmashauri za Wilaya za Moshi na Rombo upande wa Mashariki. Halmashauri ina eneo la 1,011km$^2$. Kwa mujibu na sensa ya 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ina watu 210,533. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 3, Kata 10, Vijiji 55 na Vitongoji 260. Halmashauri ina sehemu kuu tatu za uoto wa sili; nyanda za chini kati ya 600m - 900m juu ya usawa wa bahari ambazo hupata mvua kiasi cha 700mm kwa mwaka. Nyanda za kati zipo kati ya 900m -1660m juu ya usawa wa bahari na mvua hunyesha kati ya 750m - 1,250mm kwa mwaka. Nyanda za juu zipo juu ya 1,700m juu ya usawa wa bahari na mvua henyesha kuanzia 1,250mm - 1750mm kwa mwaka. Takribani 46590Ha (46%) hutumika kwa kilimo, 14,154Ha (14%) ni eneo la misitu na 13,143 Ha (13%) ni miamba. Takribani 27,297Ha (27%) ni kwa ajili ya ufugaji wa ng'ombe.

**2.0 TATIZO**

Eneo kubwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai lipo kwenye eneo la mfumo wa kilimo mseto cha kahawa, ndizi na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Kuanzia miaka ya 1960 hadi 1970 wakulima wa Halmaashauri ya Wilaya ya Hai walikuwa wanapata bei nzuri ya kahawa huku wakiendelea na ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji kama shughuli ya ziada. Kuanzia miaka ya 1970 bei ya kahawa ilianza kuporomoka kwenye soko la dunia. Mwaka 1983 hali ya uchumi ilikuwa mbaya kwa sababu ya mdororo wa mafuta duniani uliosababisha kushuka kwa pato la kaya, wakulima wakaanza kuacha uzalishaji wa kahawa, na baadhi yao walianza kung'oa mibuni kwa kuwa haikuwa na faida tena. Wanawake walianza kupata shida kutokana na pato la kaya kushuka. Shughuli mbadala ya kuongeza au kujipatia fedha ilikuwa ni kufuga ng'ombe wa kienyeji (Zebu) ambao huzalisha maziwa kidogo. Wanawake walifugia ngo'mbe ndani na maziwa yalikuwa ni kwa matumizi ya familia na pale ziada ilipopatikana basi maziwa yaliuzwa mitaani kwa bei ya chini kwa kuwa soko la maziwa lilikuwa duni sana.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu lilikuwa ni kutengeneza mnyororo wa thamani wa ufugaji wa ng'ombe wa mziwa. Malengo mahsusi ya wanawake wa Nronga yalikuwa ni;

(i) Kumiliki na kufuga mbegu bora ya ng'ombe wa maziwa ili kuongeza uzalishaji wa maziwa.
(ii) Kuanzisha ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa
(iii) Kutafuta soko la uhakika la maziwa hasa Moshi mjini
(iv) Kuongeza thamani kwa kuchakata maziwa ili kupata bidhaa nyingine zitokanazo na maziwa.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kuanzia miaka ya 1950 wanawake wa Nronga walikuwa kwenye kikundi cha kijamii chini ya mwavuli wa Kanisa la Kilutheri kilichopewa jina la "SAA" maana yake "MWANGA". Wanachama walijishughulisha na kazi za maendeleo ya kikundi kama vile kushona, kupika, kutunza nyumba n.k. Mtikisiko wa uchumi wa miaka ya 1980 ulisababisha kukosekana kwa mahitaji muhimu katika kaya. Ili kukabiliana na makali ya maisha wanawake walianza kutumia maziwa ya ziada kutengeneza siagi, jibini na samli kwa njia za kienyeji na kuuza katika mnada wa kanisa siku za Jumapili. Baadaye, juhudi hizi ziliungwa mkono na Umoja Wa Wanawake Tanzania (UWT) ambalo ni tawi la wanawake wa chama Tawala (CCM) lililowaunganisha wanawake wa Nronga na wadau wa maziwa.

Uanzishaji wa ufugaji wa mbegu bora ya ng'ombe wa maziwa na Uhamilishaji: Kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1970, wananchi wa Nronga walianza kufunga ng'ombe bora wa maziwa (Friesian, Ayshire, Jersey Guernsey, Mpwapwa, machotara) kwa imani kwamba uzalishaji maziwa utaongezeka na hatimaye kipato cha kaya kuongezekae. Ng'ombe bora waliletwa kutoka nchini Kenya, Chuo cha utafiti Mpwapwa, Kilimanjaro Magharibi, na kwa kuchanganya aina tofauti. Kwa nyongeza, wakulima walikubali kutumia uhamilishaji wa ng'ombe kama njia mbadala ya kuboresha ng'ombe wa maziwa. Jitihada hizi zilizaa matunda na zilifanikisha uzalishaji wa maziwa mwingi na kusababisha kupanuka kwa masoko na ufundi wa kuchakata maziwa.

Ununuzi wa mashine ya kuchakata maziwa: Mwaka 1983 wanawake wa Nronga walichanga jumla ya TZS 21,000 ili kununua mashine tatu (TZS 7,000 kila moja) za kuchakata maziwa. Kuzalisha jibini, siagi na samli tu hakukuweza kuongeza pato la kaya hivyo wanawake waliamua kuuza maziwa Moshi mjini bila kuyachakata. Kwa nchi zilizoendelea maziwa kama kimiminika hutumiwa kwa wingi sana kila siku. Kawaida, maziwa hutumiwa sehemu za mijini na mtindi maeneo ya vijijini lakini bidhaa itokanayo na maziwa inazidi kupata soko katika nchi nyingi hasa kipindi utalii unaposhamiri.

Utafutaji wa soko la maziwa: Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa walikuwa wanawake waliojipanga katika vikundi vya uzalishaji. Mwaka 1987, wanawake wa Nronga walijipanga katika vikundi vya wanachama 6 ili wakusanye maziwa kutoka kwa wafugaji na kuyauza Moshi mjini. Mwaka 1998, idadi ya wanawake iliongezeka na kufikia 75. Hii iliwavutia FAO na DANIDA na wakatoa msaada wa lori la tani 3 kwa ajili ya kusafirisha maziwa alfajiri kwenda Moshi mjini. Kwa siku za kwanza, lita 200 zilikusanywa na kusafirishwa kwenda Moshi mjini. Mwaka 1990, kikundi la wanawake wa Nronga kilinunua lori jingine la tani 3. Mfuko wa Rais (The Presidential Trust Fund) uliwasaidia kupata gari hilo bila kulipitia ushuru bandarini. Wanawake wengi walihamasika kuzalisha na kuuza maziwa kwa kikundi hiki cha wanawake na maziwa yakawa mengi kuzidi soko la Moshi mjini.




*Kwa nini msaada ulitoka FAO & DANIDA?*
*FAO na DANIDA waliguswa na watoto waliotumwa kuuza maziwa katika vijiji vilivyoko ng'ambo ya mto jambo hili lilikuwa hatari sana kwa biashara. Ukweli ni kuwa siku moja mto Nronga ulifurika na watoto watatu waliokuwa wanavuka baada ya kuuza maziwa walizama na kufariki. Janga hili lilifanya FAO na DANIDA kutoa msaada wa lori la tani 3 kwa ajili ya kusafirishia maziwa.*

***Gari la tani 3-ufadhili wa FAO & DANIDA***

Kwanini wanawake na sio wanaume?
----tulipoanza wanaume hawakukubali kama tungeweza shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Lakini tulipopata msaada wa gari la tani 3 na baadaye tukanunua jingine, waliamini na kusema wanawake wana nguvu!...
Hellen Ushiri, Mkuu wa kikundi cha wanawake wa Nronga

Usajili na kujipanga upya: Mwaka 1994 kikundi cha wanawake wa Nronga kilijisajiliwa rasmi kama chama cha ushirika kwa usajili namba KLR 476. Mwaka 1996 bodi ya chama ilianzishwa (kwa sasa ipo bodi ya awamu ya nne). Kikundi pia kimeajiri wafanyakazi wanaowajibika kwa meneja wa chama.

Uamuzi wa kuongeza thamani ya maziwa: Kuongezeka kwa ng'ombe wa maziwa kuliongeza uzalishaji wa maziwa katika Kijiji cha Nronga na ushindani katika soko la Moshi mjini. Kikundi kiliacha kuuza maziwa yasiyochakatwa Moshi mjini na kuanza kutengeneza bidhaa zitokanayo na maziwa kama mtindi, siagi, jibini, samli n.k. Uchakataji wa maziwa huwapatia wazalishaji wadogo kipato kikubwa kuliko kuuza maziwa na ni rahisi kufikishwa mijini na vijijini. Kuongeza thamani ya maziwa kwa kuzalisha bidhaa zitokanayo na maziwa hunufaisha jamii yote kwa kuwa huzalisha ajira kama kukusanya, kusafirisha, kuchakata na kutafuta soko bidhaa za maziwa.

Kujenga ofisi ya Ushirika na kiwanda cha maziwa: Mwaka 1991 kikundi kilipata mkopo kutoka kwa mfuko wa rais (The Presidential Trust Fund) kiasi cha TZS 750,000. Pesa zilitumika kujenga ofisi na kiwanda kidogo ndani ya eneo la kanisa lililotolewa bila malipo yoyote kwa kikundi na kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Nronga. Ndani ya ofisi, chumba kimoja kulitumika kwa shughuli za kuchakata maziwa.



***Ofisi na kiwanda cha wanawake wa Nronga***

Mafunzo: Mafunzo juu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa yalitolewa kwa wafugaji wote kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Chuo cha Mifugo Tengeru, na kituo cha Taifa uhamilishaji (NAIC). Mafunzo ya kuongeza thamani ya maziwa yalitolewa kwa baadhi ya wanachama wa vikundi waliohudhuria mafunzo ya kuongeza thamani kama yalivyo fadhiliwa na Halmashauri, SIDO, ADF na chuo cha mifugo chaTengeru kati ya mwaka 1980 hadi 2000.

Misaada ya kiufundi: Mwaka 1997, Benki ya maendeleo Africa (Africa development bank - AfDB) iliamua kusaidia kikundi kwa kuwapa mtaalam wa kuchakata maziwa kwa kipindi cha miezi tisa. Lengo lilikuwa ni kuwajengea uwezo wanawake kupata ujuzi zaidi wa kutengeneza bidhaa na kuwafundisha wenzao. Baadaye kikundi cha wanawake wa Nronga waliamua kumwajiri mtalam huyo kama mfanyakazi wa kudumu.

Mpango wa lishe Mashuleni: Mwaka 2001 kikundi cha wanawake wa Nronga kilianzisha mpango wa kutoa chakula kwa shule tatu katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na shule tatu za Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Jitihada hizi zililenga kupanua soko. Wanafunzi hupatiwa maziwa mara mbili kwa wiki chini ya mpango wa kuchangia gharama kati ya wazazi (50%). Hii iliongezea hamasa ya unywaji wa maziwa na kuongeza lishe kwa jamii.

Kupanua shughuli za kikundi: Kikundi cha wanawake wa Nronga kimefanikiwa kulea vikundi vingine vya kufunga ng'ombe wa maziwa ndani na nje ya nchi. Hatahivyo, kikundi hakikupanua shughuli zake kwa kutumia fursa za maendeleo ya kiuchumi kutoka sekta nyingine. Mwaka 2012, baada ya kuona vikwazo vya utaratibu unaotumika, uwezo mdogo wa kiwanda cha kuchakata maziwa, uwezo mdogo na ugumu wa kusafirisha bidhaa za maziwa, kikundi kilipanga kuanzisha shughuli za uzalishaji eneo jingine na kwa kutumia mitambo mikubwa zaidi. Ili kufanikisha lengo hili, serikali ya Australia kupitia Bw. Steve Pitch ilitoa msaada kwa kununua mtambo mkubwa wenye uwezo wa kuchakata lita 2,000 hadi lita 10,000 za maziwa kwa siku. Halmashauri ilichangia kwa kutoa ardhi mjini Boma Ng'ombe na kikundi kilijenga jengo na kufunga mtambo.



***Kiwanda cha kuchakata maziwa cha Boma Ng'ombe***

Kuanzishwa kwa chama cha ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS): Chama hiki kilianzishwa ili kutoa mikopo midogo kwa ajili ya kuboresha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, kulipa ada za shule, kulipa gharama za matibabu na kuboresha nyumba. Kikundi kilihamasisha wanachama kuunda vikundi vya benki za jamii vijijini (village community Bank –VICOBA) kwa ajili ya huduma zaidi za mkopo.

Kutafuta Masoko: Baada ya kufanikiwa katika uchakataji wa maziwa, kikundi kilianza kutafuta masoko mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Dar es salaam. Mkakati wa kupata masoko uliunga mkono uuzaji moja kwa moja kwenye maduka ya kawaida na maduka makubwa (supermarket) kwa kupitia wakala na maduka ndani na nje ya kijiji cha Nronga. Mkakati huu ulilenga kuongeza utumiaji wa bidhaa za maziwa katika eneo husika.

## 5.0 RASILIMALI

Kikundi cha wanawake wa Nronga kilitumia fedha kama jedwali Namba 1 linavyoonesha.

**Jedwali 1: Fedha zilizotumiwa na Kikundi cha Wanawake Nronga**

| Shughuli | Kiasi (TZS) | Chanzo |
|---|---:|---|
| Ununuzi wa mitambo 3 | 21,000 | Kikundi cha wanawake |
| Ununuzi gari la tani 3 | 9,200,000 | Kikundi cha wanawake |
| Ujenzi ofisi na mashine | 750,000 | Mkopo toka PTF |
| Mafunzo ya wanachama wa kikundi | - | SIDO ADF, Chuo cha Tangeru |
| Ujenzi wa jengo jipya | - | Kikundi la wanawake / Halmashauri |
| Ununuzi wa mitambo mikubwa | - | Serikali ya Australia |

**6.0 MATOKEO**

Kuongezeka kwa wanachama: Wanachama waliongezeka kutoka 75 mwaka 1994 hadi 462 mwaka 2015. Mtaji wa chama umeongezeka kwa kuongezeka kwa wanachama. Kikundi kinajitegemea kwa kuwa na uongozi, usafiri na ofisi. Jitihada hizi zimetokana na wanawake kuwezeshwa. Kikundi kimetengeneza ajira kupitia ufugaji wa ng’ombe wa maziwa, kuna watu 12 wenye ajira ya moja kwa moja na maelfu wanaojishughulisha na kuangalia ng’ombe, kukata nyasi, kuchakata maziwa, kusambaza maziwa n.k.

Kuboreshwa kwa hali ya maisha: Hali ya maisha ya wanachama na wananchi wa Nronga imebadilika haraka, mfano wamejenga nyumba za kisasa na kuboresha lishe. Wanachama wote wana nyumba za kisasa zenye umeme, maji ya bomba na vyoo bora.



***Nyumba za kisasa za wanachama wa kikundi cha wanawake wa Nronga***

Kutumia nishati ya biogas; Wafugaji wamefunga mitambo ya kufua gesi kwa ajili ya kupikia na kuwasha taa. Wakati wa kutoa chapisho hili la mbinu bora, wanachama 42 walikuwa wanatumia gesi. Picha hapa chini inaonesha mmoja wa wanachama akiongezea samadi kwenye shimo la mtambo wa gesi na jiko linatumia nishati ya gesi.



***Mazizi yaliyounganishwa na mashimo ya kufua gesi ya kupikia jikoni***

Uboreshaji wa ufugaji wa ng’ombe wa maziwa: Kwa sasa hivi wanachama wote wanafuga ng’ombe wa maziwa wenye ubora wa hali ya juu, wamejenga mazizi ya kisasa, hulisha ng’ombe kwa kufuata taratibu za kisasa, na ng’ombe wanapatiwa huduma za matibaabu.



***Zizi bora na ng'ombe wa kisasa***

Kuongezeka kwa pato la kaya: Wastani wa pato la kaya ni kati ya TZS. 200,000 hadi 400,000 kwa mwezi. Kutokana na kuongezeka kwa pato na lishe watoto wote wanahudhuria na kumaliza elimu ya msingi na na wote wanendelea na elimu ya sekondari. Takribani 85% ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne wanajiunga na kidata cha tano na 40% wanajiunga na elimu ya juu.

Huduma zimeimalika kijijini: Wanachama watano wamenunua vyombo vya usafiri (magari) na wengine wengi wamenunua pikipiki ambazo hutumika kwa shughuli mbalimbali. Kutokana na ongezeko la kipato, wanawake wa Nronga wamechangia fedha kuboresha barabara yenye urefu wa 10km kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya TZS 123 milioni.



***Barabara iliyotengenezwa kwa nguvu za wanawake wa Nronga***

Kikundi cha wanawake wa Nronga ni jukwaa la mafunzo: Kikundi kimeimarika na kuwa chama cha ushirika imara na kinajulikana nje na ndani ya nchi. Kikundi kimekuwa ni jukwaa la kujifunzia vikundi na vyama vingine, pamoja na SACCOS na VICOBA. Kikundi kina mtandao ulioimarika sana. Kinashirikiana na mashirika kama PTF, Techno Safe, TDA, TBS, TFDA, Land  O'Lakes, wachakataji wa maziwa Nairobi na SUA. Wanachama wa kikundi hiki wanapanua mawazo kwa kushiriki maonyesho ya kilimo.

Kuongezeka kwa aina ya bidhaa ya maziwa: kikundi kimeongeza idadi ya bidhaa kutoak moja hadi nne, ambazo ni maizwa, mtindi, jibini, siagi na samli.



***Bidhaa za kikundi cha wanawake wa Nronga***

Kuimarika kwa mahusiano ya Kijamii: Matoketo ya wanawake kupata heshima, kuongezeka kwa kipato, mahusiano mazuri ya kijamii, na mshikamano kati ya wanawake na waume zao umeimarika kwa kiasi kikubwa.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Changamoto kubwa iliyopo kwa kikundi hiki ni kuwa, ukuaji wa shughuli za kikundi umebakia ndani ya jamii ya Nronga tu. Shughuli zote za mnyororo wa thamani (malighafi, uzalishaji wa maziwa, ukusanyaji, uchakataji, usafirishaji, mauzo ya jumla na rejareja) zinafanywa na taasisi moja; Kikundi cha wanawake wa Nronga (uratibu sambamba). Ili kukabiliana na changamoto hii, kikundi kipo kwenye mchakato wa kuunganisha shughuli zake na vikundi vingine 16 vya Halmashauri ya Wilaya ya Hai chini wa mwanvuli mmoja imara ili kuimarisha biashara ya maziwa na bidhaa zake. Pia, jitihada zinafanywa ili kuongeza ushirikiano na tasisi za utafiti ili kutoa bidhaa za maziwa zenye ubora wa hali ya juu. Kikundi kinapanga kuanzisha kituo cha kuuzia dawa na vyakula vya mifugo.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kwa kiasi kikubwa mafanikio ya kikundi yanatokana na kuungwa mkono kwa hali na mali kutoka kanisa la kilutheri, usharika wa Nronga . Kanisa lilitoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na kiwanda cha kuchakata maziwa. Zaidi ya kutiwa moyo, siri ya mafanikio imetokana na kujizaatiti na utayari wa wanawake kutumia njia za kisasa za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Wanawake wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai wanajulikana kwa umakini wao wa kupanga na ujasiriamali. Zaidi ya yote, Kikundi huendesha shughuli zake kwa uwazi na kufanya maamuzi kwa kutumia demokrasia.



***Kiongozi wa kikundi cha wanawake wa Nronga akishiriki katika kufanya maamuzi***

Kikundi cha wanawake cha Nronga kinatamani na kupigania maendeleo ya wanachama wote. Pia wanachama wamejijengea tabia ya kutafuta habari kutoka wadau wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kama NIC, SUA, Tengeru LITI n.k. Wanachama wamejijengea utamaduni wa kupashana habari, kubadilishana ujuzi, uzoefu, na elimu kati yao na wengine. Tabia hii imekuwa ni mlango wa mafanikio wa kuvutia wafadhili wa nje. Zaidi ya yote, upo utamaduni wa kusaidiana wao kwa wao uliojengeka katika jamii kwa muda mrefu.

# Marejeo


Abiona, A. I. and Bello, W. N. (2013). Grassroots Participation in Decision-Making Process and Development Programmes as Correlate of Sustainability of Community Development Programmes in Nigeria, *Journal of Sustainable Development; Vol.* 6 (3):47-57.Canadian Centre of Science and Education, [www.ccsenet.org/jsd] site visited on 19 /03/ 2013.

Apolo, Kansiime (2013). The Impact of Public Procurement Reforms on Service Delivery in Uganda; Bishop Stuart University.

Chibehe, M.M. (2004). Factors Affecting Sustainability of Farmer Groups: the case of Twikinde Malimbichi Cooperative Society. MA Dissertation, SUA, Unpublished, 90pp.

Helene Bie Lielleor and Ulrik Lund-Sorensen (2013). FARMERS' CHOICE evaluating an approach to agricultural technology and adoption in Tanzania, Rockwool Foundation research Unit, PRACTICAL ACTION Publishing, pp. 154.

Helmsing, A. H. J. (1995). *Local Government Central Finance.*An Introduction: NewYork USA

Howlett. D and J. Nagu. (1997). *Agricultural Project Planning in Tanzania, A handbook on cycles and sequences, participation, identification, planning and design, economic and financial analysis, and environmental assessment of agricultural projects.* ISBN 1898828261. pp 89.

Kusago, Takayoshi. (2008). *Sustainable Livelihood and Happy Generation in Minamata-City Japan*: A Model for Endogenous Community Development.

Makonda, K.S.C. (2003). Partnership and sustainability of water supply systems in Bukombe District, Tanzania. *MA Dissertation*, Sokoine University of Agriculture, Morogoro, Tanzania. Unpublished. pp.154

Mwanga, J.N. (2011). Empowerment of Local Society in Tanzania –the Nucleus for Development- With Experience from Indonesia and Japan, *Rare Series Policy Paper*, Local Government Training Institute, Dodoma Tanzania. 100 pp.

Ohama, Y. (2002). Basic Framework and viewpoints of Participatory Local Social Development (PLSD) and construction of its evaluation framework.

Porter, Michael E. (1998). *Competitive Advantage: Creating and Sustaining Superior Performance*, 397 pp, Amazon.

Pretty, J.N. (1995). Participatory learning for sustainable agriculture. *World Development* 23(8): 1247-1263.

Scoones, I. and John Thompson (1994). *BEYOND FARMER FIRST: Rural people's knowledge, agricultural research and extension practice*. Intermediate Technology Publications LTD, London, UK, pp.301.

Sharma, P.N. and Ohama, Y. (2007*). Participatory Local Social Development-An Emerging Discipline*, Bharat Book Centre Publishers & Distributors, Lucknow India. pp. 467.

Shikuku, O.M. (2012). Community related Variables influencing sustainability of water projects in Nyando District a case. *MA Dissertation*, University of Nairobi, Digital Repository

URT (1998). Local Government Reform Agenda

URT, (2010). Public private partnership (PPP) *Act*, no 18 of 2010, pp 21

URT (2011). Millennium Development Goals, Tanzania country report. Ministry of Finance and Economic Affairs, Dar es Salaam – Tanzania.

Zadeh, B.S. and Nobaya, A. (2010). Participation and Community Development. *Current Research Journal of Social Sciences* 2(1): 13-14, 2010. [http://maxwellsci.com/print/crjss/v2-13-14.pdf] site visited on 22/07/2014